Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA NANE

**Kikao cha Thelathini na Sita – Tarehe 30 Julai, 2012**

*(Mkutano Ulianza SaaTatu Asubuhi)*

## D U A

*Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai ) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

**Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-**

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII):-**

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa Mwaka 2011/2012

Pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha, 2012/2013.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WA WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII)**:-

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani juu ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa Mwaka wa fedha 2012/2013.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 280

### Mpango wa Kulinda Mazingira ya Pwani

**MHE. LETICIA M. NYERERE** aliuliza:-

Mkutano wa *Rio +20* wa mwaka 2012 utaweka msisitizo katika kulinda mazingira ya Pwani kwa kuzingatia mabadiliko ya hali ya hewa kupitia mpango wa *Blue Carbon*:-

(a) Je, Serikali imeandaa mazingira gani ya kutekeleza mpango huo bila kuathiri faida zitokanazo na matumizi ya Bahari na Maziwa nchini?

(b) Je, Serikali imeandaa mpango wa kazi gani utakaoendena na matakwa *Rio + 20* ya 2012?

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA MAKAMU WA RAIS - MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Leticia Mageni Nyerere, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mfumo – Ikolojia wa bahari na ukanda wa pwani (mfano mikoko, matumbawe, mwani nk) unatoa mchango mkubwa katika kupunguza hewa ukaa ambapo mfumo huu una uwezo wa kunyonya zaidi ya asilimia 50 ya hewa ukaa kutoka angani iliyosababishwa na uharibifu wa mazingira.

Hewa ukaa iliyonyonywa na iliyotunzwa katika Mfumo huu unajulikana kama *Blue Carbon.* Mkutano wa *Rio +20* uliweka msingi ya jumla ya kuhifadhi mazingira ya mfumo – Ikolojia ya bahari na pwani ili kuongeza kiwango cha upunguzaji wa hewa ukaa angani. Aidha, majadiliano ya msingi kuhusu suala hili yanaendelea pia chini ya Mkataba wa Mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa ukanda wa pwani, bahari na maziwa, mwaka 2008, Serikali iliandaa na kupitisha Mkakati maalum unaojulikana kama mkakati wa hatua za haraka za kuhifadhi mazingira ya bahari, ukanda wa pwani, maziwa, mito na mabwawa.

Mkakati huu umeainisha hatua mbalimbali za kukabiliana na mikoko, ujenzi holela, uchafuzi na uharibitu wa maeneo ya ukanda wa pwani na bahari,

uharibifu wa bionuai za bahari utokanao na uvuvi usio endelevu, mmomonyoko wa fukwe za bahari na uchafuzi wa maji utokanao na maji taka, taka zenye sumu na matumizi yasiyoendelevu ya dawa na mbolea.

Matokeo ya utekelezaji wa mkakati huu kuongezeka kwa upatikanaji endelevu wa mazao ya bahari, ukanda wa pwani na maziwa, kupungua kwa hewa ukaa angani inayosababisha ongezeko la joto duniani na mabadiliko ya tabia nchi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutekeleza maazimio ya *Rio + 20* Ofisi ya Makamu wa Rai iko katika hatua za mwisho za kukamilisha mkakati wa mabadiliko ya tabianchi. Mkakati huu umeandaa mpango kazi wa utekelezaji ambapo umeanisha hatua zinazotakiwa kuchukuliwa katika kukabiliana na changamoto za uharibifu wa mazingira, hatua za utekelezaji na muda wa utekelezaji. Wahusika wa utekelezaji ni pamoja na Serikali Kuu, Serikali za Mitaa, Mashirika yasiyo ya Kiserikali na wadau wengine wakiwemo watu binafsi.

Tunatarajia kuwa utekelezaji wa mkakati wa kupambana na uharibifu wa mazingira ya ukanda wa pwani utaenda na maazimio ya mkutao wa *RIO +20* ya kuhifadhi mazingira ya Bahari, Ukanda wa pwani, maziwa, mito na mabwawa pamoja na hatua zilizoainishwa katika mkakati wa mabadiliko ya tabia nchi.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake. Kwa kuzingatia ripoti ya *United Nations Environment Program* ya mwaka 2009 inayoweka msisitizo katika kuzingatia uharibifu utokanao na tabia nchi.

Je, Serikali inatoa tahadhari gani kwa wananchi waishio pwani?

Swali la pili. Kwa kuwa Tanzania ni moja ya mataifa 135 duniani ambayo yapo pwani na kwa kuwa asilimia kubwa ya wakazi hawa hutegemea uchumi wao hutegemea bahari. Kwa kuzingatia madhara yatokanayo na tabia nchi ikiwemo kimbunga na *tsunami.*

Je, Serikali inatoa tamko gani kuhusu *blue carbon?*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS - (MAZINGIRA)**: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa napenda kumpongeaza Mheshimiwa Leticia Nyerere kwa kuwa makini sana na kufuatilia kwa karibu sana masuala ya mazingira na pia kufuatilia mikutano mikuu ya kimataifa. Tahadhari tumeshaanza kuzichukua na nyie ni mashahidi mliona kabisa mwezi uliopita tumebomoa nyumba ambazo zipo karibu sana na pwani. Hiyo ni kuchukua tahadhari kwa sababu majanga yanapotokea lawama kubwa inakuwa kwa Serikali.

Kwa hiyo ninachosisitiza zaidi tuendelee kutekeleza Sheria ya mazingira ya mwaka 2004 na

kuhakikisha kwamba watu wote wanaofanya shughuli za mifugo za kilimo na ujenzi katika mita zile 60 kutoka kwenye kina cha misho ambacho bahari inapiga. Usipime kuanzia kwenye bahari kabisa lakini tunaangalia mahali ambapo bahari inapopiga.

Kwa hiyo mwisho wa mapigo yale ya bahari ndipo tunapima mita 60. Kwa hiyo wale wote waliojenga wanaofanya shughuli katika mita hizo 60 tunaomba waache shughuli wahame ili kuacha hizi bahari ziwe endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu masuala ya *tsunami* na vipunga ni kwamba maeneo oevu yote kazi yake kubwa ni kunyonya hiyo *carbon* lakini vilevile inasaidia kupunguza hizo hatari zinapotokea. Kwa hiyo napenda kusisitiza kwamba wale wote ambao wanafanya shughuli katika hizo sehemu ni lazima watoe.

Kwa hiyo kwa kupitia kwenye Bunge lako Tukufu napenda kutoa tamko rasmi kwamba wananchi watii Sheria hiyo, wahame na napenda kuwaambia zoezi hili ni endelevu na tumewasiliana na Mawaziri wenzangu, Waziri wa Ardhi, Waziri wa Maliasili na Utalii tukimaliza tu Bunge tutatembea fukwe zote kuanzia Tanga mpaka Mtwara na kuhakikisha watu wote wanahama.

Na. 281

## Ahadi ya Kupeleka Umeme Tarafa ya Ndagalu – Magu

**MHE. RICHARD M. NDASSA (K.n.y. MHE. DKT. FESTUS B. LIMBU)** aliuliza:-

Serikali imeahidi kupeleka umeme wa *grid* Makao Makuu ya Tarafr ya Ndagalu, Jimbo la Magu katika Mji Mdogo wa Kabila, kutoka kijiji cha Tallo kupitia vijiji vya kadashi, Nyashana na Maligusu.

Je, ni hatua gani zimefikiwa kuhusiana na ahadi hiyo hadi sasa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Festus Bulugu, Limbu Mbunge wa Magu Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa kupeleka umeme wa gridi ya Taifa Makao Makuu ya Tarafa ya Ndagalu, Jimbo la Magu katika Mji mdogo wa Kabila pamoja na vijiji vya jirani utahusisha ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa *KV 33* yenye urefu wa kilometa 29 kutokea Magu Mjini.

Mradi huu pia utahusisha ufungwaji wa *transfoma 5* zenye uwezo wa *KVA 50, transfoma* 2 za KVA 100 na transfoma 2 za KVA 200. Maeneo yanayotarajiwa

kunufaika na mradi huu ni pamoja na maeneo ya Itumbili Sekondari, Kitongo, Sukuma Sekondari, Lumeji, *Busalaga Dispensary,* Ng'haya Sekondari, *Ng'haya Centre,* Mwashepi na Kabila. Gharama za mradi huu zinakadiriwa kuwa shilingi bilioni 1.7.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa kufikisha umeme vijiji vya Kadashi, Nyashana na Maligisu kutokea kijiji cha Tallo utahusisha ujenzi wa kilometa 27 za njia ya umeme wa msongo wa *KV 33,* pamoja na ufungwaji wa *transfoma 3* zenye uwezo wa *KVA 200* na moja ya KVA 100. Gharama za mradi huu zinakadiriwa kuwa shilingi bilioni 1.44. Miradi yote hii itatekelezwa kupitia Mfuko wa Nishati Vijijini na kusimamiwa na Wakala wa Nishati Vijijini *REA* kwenye awamu ya pili.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Ninaomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri kwa sababu maelezo haya ni ya siku nyingi sana na tuliambiwa kwamba zabuni zingefunguliwa mwezi wa tano, wananchi wa maeneo tajwa wangependa kujua ni lini, sio maelezo tu haya. Ni lini umeme utaanza kupelekwa katika vijiji vilivyotajwa.

Lakini la pili, kwa sababu ni maeneo mengi kupitia *REA* yatapelekewa umeme. Je, Serikali imejiandaa vipi kuhusu suala zima la fidia? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Naibu Spika, hili la zabuni nimtaarifu tu Mheshimiwa Ndassa na Mheshimiwa Limbu na wananchi wote ambako miradi

ile ya awamu ya kwanza inaishia na hii mingine inaanza ni kwamba mwezi huu wa nane tunatarajia utaratibu wote wa kufungua zabuni utakuwa umekamilika.

Kwa hiyo ujenzi utaanza wakati wowote kuanzia kwenye mwezi wa tisa mwishoni au wa kumi. Lakini hili la fidia kwenye miradi ya *REA* naomba nitumie nafasi hii kuwaomba sana Watanzania na kuwaomba sana Waheshimiwa Wabunge kwamba ile miradi ambayo ni mikubwa, *line* zile kubwa ambazo mara nyingi tumekuwa tukisaidiwa na nchi marafiki ikiwemo miradi ya *MCC* ile ilikuwa na *package* za fidia kutoka huko.

Lakini napata shida kuweza kuamini kwa fedha tulizonazo sisi kupitia hii miradi ya *REA* kama kweli tutakuwa na uwezo wa kulipa fidia na miradi hiyo itatekelezeka. Mimi niwaombe kwamba kwenye miradi hii ya *REA* ambayo fedha za kwetu wenyewe kipaumbele kiwe ni kupata umeme.

Mikoa ambayo imetangulia kupata umeme kama kule Kaskazini wananchi walishiriki hata kuchimba nguzo kusaidia *TANESCO* wakapata umeme. Lazima tutambue kwamba ni nchi yenye siasa ya ujamaa na kujitegemea. Hivi kujitegemea kumeisha lini, hivi ujamaa umeisha lini?

Mimi niwaombe sana habari ya fidia kwa miradi ya kwetu kwa njia hizi ndogo ndogo ambazo si njia za misongo mikubwa na hazichukui eneo kubwa. Waheshimiwa Wabunge niwaombe tukawaelimishe wananchi wetu wapishe miradi hii kwa sababu kupata

umeme ni maendeleo makubwa kuliko kudai hicho kifidia cha mti na pengine mti wenyewe unakuta wa asili na kama mradi unapita kwenye nyumba hapo labda tunaweza kuzungumza hilo.

Lakini kwa njia hizi za kawaida kwa kweli niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge na mimi nitakuwa mfano, watu wa Jimbo langu Kibakwe kwa miradi ya *REA* nitakwenda kuelimisha kwamba jamani tupishe tupate umeme ili tupate maendeleo lakini fidia kwa kweli napata shida maana yake *batch* hii ina vijiji vingi sana.

**MHE. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Mimi nina swali dogo tu la nyongeza napenda nifahamu Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini wana mpango gani kusambaza umeme hususan baada ya ugunduzi wa gesi kule kusini kuelekea kanda ya ziwa ukitilia maanani kwamba kule kuna moja ya tatu ya Watanzania ikiwemo Wilaya ya Serengeti ambako ni kitovu kikubwa sana cha uchumi kupitia utalii?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Naibu Spika, gesi ya kusini na umeme kwenda kanda ya ziwa hususani Serengeti. Tukifikisha hii gesi Dar es Salaam, tukizalisha umeme pale, tunaingiza kwenye grid na kwa maana hiyo tayari umeme huo unaanza kufika kanda ya ziwa na tayari umeme huo unaanza kufika Serengeti.

Na. 282

## Kuanza na Kukamilika kwa Mradi wa Umeme wa Itiryo

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE** aliuliza:-

Mradi wa *REA* katika Wilaya ya Tarime maarufu kama Maradi wa Umeme wa Itiryo ukikamilika utasaidia vijiji vya Nyamwigura, Kemakorere, Rozana, Nyarero, Nyamwaga, Keisangura, Muriba, Kobori, Itiryo, Mangucha na Masanga kupata Nishati ya Umeme.

(a) Je, ni lini mradi huo utaanza na kukamilika?

(b) Je, mradi kama huo utaanza lini katika vijiji vya Tarafa za Inchungu na Inano?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)** alijibu**:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini napenda kujibu swali la Mheshimiwa Nyambari Chacha Mariba Nyangwine, Mbunge wa Tarime, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa kupeleka umeme Itiryo katika Wilaya Tarime upo katika awamu ya kwanza ya *REA* na ulianza mwishoni mwa mwaka 2011 na unatarajiwa kukamilika mwaka huu wa 2012. Mradi huu unahusisha vijiji vya Nyamwiguru,

Kemakorere, Rozana, Nyarero, Nyamwaga, Keisangura, Muriba A na B hadi Itiryo.

Hatua ya utekelezaji iliyofikiwa hadi sasa ni pamoja na ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa KV 33, ufungaji wa transfoma sita kati ya nane zinazotakiwa kufungwa katika vijiji hivyo na ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa KV 400. Gharama ya mradi huu inakadiriwa kuwa shilingi bilioni 2.

Aidha vijiji vya Mangucha na Masanga hivi sasa vinafanyiwa upembuzi yakinifu ili viweze kuingia kwenye miradi mipya ya awamu ya pili ya miradi ya wakala wa nishati vijiji *(REA)* Mradi huu unatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha 2013/2014. *(Makofi)*

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri lakini ninasikitika kwamba kipengele (b) hakikuweza kupata majibu. Hata hivyo napenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(a) Wilaya ya Tarime ina vijiji takribani 120 na hadi mradi huu unakamilika vijiji vipatavyo 20 vitakuwa vimepata umeme je, Serikali ina waambia nini wakazi wa Tarime wanaoishi katika vijiji 100 vilivyobaki?

(b) Barabara ya *Sekiti Road* inaanzia katika Wilaya ya Rolya inapita katika vijiji vya Susuni, Viterere, Remagwe, Nyabisaga, Borega, Nyanyange mpaka Nyantira na kwa upande wa Kenya kuna umeme lakini katika nchi yetu ya Tanzania kuna giza totoro.

Je, Serikali inasema nini kuhusiana na hiyo barabara ya *Sekiti Road?*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Nyangwine kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuna vijiji 120 katika Wilaya ya Tarime lakini ni vijiji 20 tu ndivyo vitakavyopata umeme kama nilivyosema mara nyingi wakati nikijibu maswali mbalimbali hapa. Dhamira ya Serikali ni kuhakikisha tunapeleka umeme katika vijiji vyote vya Tanzania.

Lakini tunajikuta kwa sababu za kifedha tunakwenda kwa awamu hata hivyo vijiji 20 ambavyo tunaanza navyo katika Wilaya yako wewe utajenga historia kuwa uliweka umeme katika vijiji ishirini, na pengine katika *batch* inayokuja tutaweza kuweka umeme katika vijiji vingine kama nilivyosema kwa hiyo nikupongeze kwa hatua hii ambayo kwa kweli tumejitahidi, lakini siyo rahisi kama ninavyosema mara nyingi kuweza kuweka umeme kwa mara moja kwa vijiji vyote hatuna hiyo fedha.

Kwa swali la pili, la barabara ya Rolya na vijiji vyote alivyovitaja ambapo inaenda kuunganisha kwa wenzetu Kenya ambapo tayari kuna umeme nadhani haya ndiyo maeneo ya *priority.* Mheshimiwa Mbunge mimi nikukaribishe sana ofisini kwangu njoo tukae tuone

kipaumbele ni wapi angalau katika awamu inayokuja tuweze kuweka umeme katika vijiji hivyo. *(Makofi)*

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi kwa kuwa utekelezaji wa mradi wa umeme Makao Makuu ya Wilaya ya Namtumbo uko mwishoni kukamilika. Kwa kuwa, Serikali iko katika mchakato wa kutuletea umeme wa gridi ambapo Tarafa za Mkongo na vijiji vyake baadhi vitafaidika

Je, Serikali inaweza kuiomba Tarafa ya Sasawala iweze kuipatia Mji mdogo wa Lusewa umeme?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE.GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kawawa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, dhamira ya Serikali ni kuhakikisha maeneo mengi ambayo Kiuchumi yanaweza kuwa ni muhimu kupatiwa umeme yanapitiwa umeme. Nimwombe Mheshimiwa Kawawa tuwasiliane baada ya hapa tuone nini tunaweza kufanya katika kusaidia eneo la Lusewa kuweza kupata umeme. *(Makofi)*

Na. 283

## Uzalishaji wa Mitamba – Kituo cha Mpwapwa

**MHE. SLYVESTER M. KASULAMBAYI** aliuliza:-

Serikali imefanya juhudi kubwa kuzalisha Mitamba ya kisasa katika kituo chake cha Mpwapwa na kuiuza kwa wafugaji wengi ili kubadilisha ng'ombe wa asili *genetically:-*

(a) Je, wafugaji wangapi kutoka maeneo yapi ya nchi wamepatiwa mitamba hiyo?

(b) Je, Mitamba itasambazwa vipi kwenda kwenye maeneo yale ambayo hayapati ili nao wawe kwenye mfumo huo wa kubadilisha ng'ombe wa asili kuwa wa kisasa?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Mendeleo ya Uvuvi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sylivester Mhoja Kulumbayi, Mbunge wa Maswa Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kituo cha Mpwapwa kiko chini ya Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Mifugo, inayojihusisha na utafiti tu na siyo usambazaji mitamba nchini.

Hata hivyo katika utekelezaji wa majukumu yake huzalisha mifugo ambayo ni matunda ya utafiti na kuiuza, Kuanzia Januari 2006, hadi Desemba 2011, kituo kilisambaza ng'ombe 633 aina ya Mpwapwa, ikiwa ni madume 426 na mitamba 137 kwa vikundi 72 na wafugaji 9 binafsi katika Halmashauri 17 kwenye Mikoa 13 ambapo katika Mkoa wa Dodoma ulipata ng'ombe 265, Singida 152, Manyara 50, Shinyanga 40, Dar es salaam 21, Morogoro 15, Tabora 20, Mwanza 6, Mbeya 24, Ruvuma 4, Kilimanjaro 6, Pwani 50, na Mtwara 10. Usambazaji huu ulitegemea mahitaji yaliyotolewa na Halmashauri na wafugaji mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, vituo vinavyozalisha na kusambaza mitamba chotara ni Mabuki kilichoko Wilayani Misungwi, Nangaramo (Nanyumbu), Ngerengere (Morogoro Vijijini) na *Sao Hill* (Mufindi). Aidha, shamba la Kitulo Wilayani Makete huzalisha na kusambaza ng'ombe asili *(Pure Breed)* wa maziwa aina ya *Friesian*. Katika mwaka wa fedha wa 2011/2012, mashamba hayo kwa pamoja yalisambaza jumla ya mitamba 789 kwa vikundi 35 na wafugaji binafsi 60 katika Halmashauri 34 za Mikoa 17.

Aidha, kuanzia Julai 2007 hadi Juni 2012, ng'ombe 256,463 walihamishiwa katika Mikoa 22, na hivyo kuongeza idadi ya ng'ombe bora nchini kwa kiasi hicho kwa kutumia teknolojia hii rahisi na yenye matokeo ya haraka.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, usambazaji wa mitamba hufanyika kwa ushirikiano kati ya Wizara, Halmashauri na wafugaji kupitia mipango ya

maendeleo ya Kilimo ya Wilaya- DADPs ambapo wafugaji huibua miradi ya ufugaji bora na Halmashauri kuingiza kwenye miradi ya maendeleo na kupeleka mahitaji yao kwenye mashamba ya kuzalisha mitamba. Aidha, wafugaji binafsi wanaweza kuhudumiwa moja kwa moja kwa kupatiwa ng'ombe kulingana na mahitaji na upatikanaji wa mitamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na uzalishaji wa mitamba kuwa mdogo kuliko mahitaji, napenda kuwashauri wafugaji wote nchini kutumia teknolojia ya uhamilishaji mifugo katika kuongeza kasi ya uboreshaji wa mifugo asili.

**MHE. SLYVESTER M. KASULAMBAYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niongeze swali moja kwanza kwa kuishukuru Serikali kwa jitihada inayozifanya za kuhakikisha kuwa inapatikana mitamba iliyo bora ili kuongeza idadi ya ng'ombe.

Lakini sasa kwa nini Serikali haioni kwamba sasa Mkoa wa Simiyu ambao ndiyo Mkoa unaozalisha ng'ombe wengi zaidi kuwa ni wakati muafaka kuweka kituo cha kama hiki kwenye Wilaya ya Maswa ambayo ni *center* ya Wilaya za Meatu, Bariadi, Busega na Wilaya ya Itigi?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI**: Katika Ukanda huo wa Ziwa Mwanza kuna kituo tayari kwa ajili ya uhamilishaji kwa ajili ya ukanda huo ikiwa ni moja kati ya vituo vilivyofunguliwa na Wizara katika Kanda nne. Katika Kanda hiyo ya Ziwa

zinapatikana mbegu kwa ajili ya ng'ombe wa maziwa hasa wale aina *fresian Asian* na *Jerse*.

Lakini pia kwa wafugaji watakopenda kuboresha mifugo yao na kuzalisha nyama zinapatikana mbegu aina ya ng'ombe aina ya *boran* ambao ni wazuri sana kwa nyama lakini kwa wale ambao wanapenda kuwa na mifugo ambayo *dual purpose* kwa ajili ya maziwa na nyama kwa pamoja katika kituo hicho zinapatikana pia mbegu za *cemental, Sahwal* na hawa wa Mpwapwa, ningemwomba Mheshimiwa Kalumbayi, kupitia Bunge lako Tukufu kuwa Mwanza ni jirani tutumie kituo hicho mpaka hapo Serikali itakapokuwa na uwezo wa kujenga kituo kingine katika eneo analopendekeza Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Mwaka jana Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro ilitenga takribani Shilingi milioni 700 kwa ajili ya kuanzisha ranchi kule *Kakeshi,* sehemu za Ngerishi kwa lengo hilohilo la kubadilisha mifugo ya asili ya wenyeji wa Tarafa ya Ngorongoro kuwa wa kisasa.

Lakini kwa bahati mbaya mpaka Bajeti inakwisha tarehe 30 Juni, 2012 hakuna miundombinu yoyote iliyowekwa katika eneo hilo.

Je, Serikali kupitia Wizara ya Mifugo ina taarifa juu ya mradi huo mkubwa na je, inaweza kutoa msukumo gani ili mradi huo uweze kuanza?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza eneo la *Kakeshi* siyo mbali sana kutoka eneo lililokuwa na ranchi ya *Enduleni* ambayo ilijulikana na ilikuwa na mifugo mingi.

Taarifa hizi tunazo na mara Mamlaka itakapojipanga na kuweka miundombinu maana ni mipango ya Mamlaka kama sehemu ya kuwahudumia wafugaji wanaoishi ndani ya eneo hilo,Wizara tutakuwa radhi kushirikiana na Mamlaka pamoja na wenyeji wa pale na kuwapa kila aina ya huduma inayotakiwa inapatikana na ukizingatia kuwa kituo chetu cha *Naike* chenye uwezo wa kuzalisha mbegu kati ya laki nne na themanini hadi laki sita na arobaini kwa mwaka kitaweza kuwahudumia wafugaji wa eneo hilo ili kuboresha mifugo yao.

Na. 284

**Hitaji la Minara ya Simu- Lyabukande**

**MHE. JOELSON L. MPINA (K.n.y. MHE. AHMED A. SALUM)** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka mnara wa mawasiliano ya simu za mikononi katika Kata ya Lyabukande kama ilivyoaihidiwa na Mheshimiwa Rais?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, Mbunge wa Solwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia mfuko wa mawasiliano kwa wote *( UCAF)* tayari imehakiki mahitaji ya huduma za mawasiliano katika maeneo mbalimbali nchini na kubainisha zaidi ya vijiji 2175 na maeneo mengine visivyo na mawasiliano mazuri au kutokuwa na mawasiliano kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hatua zaidi, mnamo mwezi Novemba 2011, Mfuko ulitangaza zabuni kwa ajili ya utekelezaji wa awamu ya kwanza iliyojumuisha vijiji 140 nchi nzima ambapo uchambuzi wa zabuni hiyo ulikamilika, mwezi Machi, 2012.

Aidha, kwa mzabuni aliyewasilisha maombi hakushinda zabuni hiyo kutokana na gharama kubwa na fedha halisi zilizotengwa na Mfuko kwa kazi hiyo. Kufuatia hilo utafiti zaidi unaendelea kufanywa na mtaalam mwelekezi ili kufanya tathmini ya kitaalam ya mahitaji ya fedha na mbinu bora zenye gharama nafuu za kufikisha mawasiliano katika maeneo yote yenye matatizo ya mawasiliano nchini.

Tathmini hiyo inatarajiwa kukamilia mwezi Agosti, 2012 na zabuni mpya zinatarajiwa kutangazwa mwezi Septemba, 2012 kwa kuzingatia mapendekezo ya mtaalam na kwa ajili ya hatua zaidi za utekelezaji.

Ni matumaini yangu kuwa baada ya zoezi hilo, huduma za mawasiliano zitaboreshwa katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo Kata ya Lyabukande na maeneo mbalimbali ambayo Rais alitoa ahadi na Waheshimiwa Wabunge walitoa ahadi kwa wananchi.

**MHE. JOELSON L. MPINA:** Mheshimiwa Naibu Spika ninashukuru sana ninayo maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwanza kuipongeza Seriakali kwa kukubali kuweka mnara katika kijiji cha Lyabukande na kwa kuwa, Serikali imekubali na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba kuanzia Septemba 2012, zabuni hizo zitakuwa zimetangazwa. Je, mnara utakaokuwa umejengwa pale Lyabukande utakuwa na nguvu ya ku - *cover at least* kilomita kumi ili vijiji vilivyoko njiani kama Ilola, Nzoza na Mwakitolya viwe vimefikiwa?

(b) Kwa kuwa katika Jimbo la Kisesa kuna vijiji vingi ambavyo havijafikiwa na mnara kama kijiji cha Sakasaka, Mwanduichinge, Mwasengera na Semi. Je, vijiji vinavyotangazwa na ambavyo vitatangazwa katika zabuni yake Septemba 2012 na vijiji hivi navyo vitakuwepo ili wananchi wa Kisesa nao wapate mtandao wa mawasiliano?

**NAIBU SPIKA:** Sasa hivyo vijiji vya ndani vya Usukumani atavijuaje Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia? Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, imani yetu ni kwamba katika kazi iliyofanyika na mtaalam mwelekezi safari hii ni pamoja na kutafuta teknolojia mpya zaidi itakayowezesha kupunguza gharama za kufikisha mawasiliano ikiwemo minara na antena zenye nguvu kubwa zaidi.

Kwa hiyo, ni imani yetu kuwa antena zitakazowekwa Lyabukande zitawezesha ku- *cover* maeneo ambayo ameyataja lakini hili ni suala la kitaalam zaidi na tutawasiliana mara ambapo itakapokuwa imejulikana ni kampuni gani zimepangiwa kujenga mnara wa Lyabukande ili tujue kama antena hizo zitafika kwenye vijiji vya jirani.

Kuhusu maeneo ya Sakasaka na Mwasengele na maeneo mengine ambayo ameyataja katika Jimbo la Kisesa ningependa tuwasiliane na Mheshimiwa Luhaga Mpina, itakapofika Septemba tuone kama vijiji hivi kwenye maeneo ya Jimbo la Kisesa yamepangiwa kwenye awamu ya kwanza au awamu ya pili ya kupelekewa mawasiliano.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii niulize swali la nyongeza. Kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri kuwa baadhi ya maeneo ya Tanzania zina mawasiliano mazuri lakini baadhi mawasiliano yake ni ya shida mpaka upande juu ya miti au juu ya milima kupata mawasiliano kama ilivyo katika jimbo langu la Chambani.

Je Serikali inatumia mifumo gani kupeleka mawasiliano katika sehemu mbalimbali zenye shida na kama ahadi za Rais ni miongoni mwa tatizo hili.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kuna maeneo mengi nchini ambayo yana mawasiliano na mengine hayana mawasiliano ya kuridhisha kama tulivyosema wakati tunawasilisha hotuba ya Bajeti yetu ni kwamba kwenye ramani tuliyonayo sisi kule Serikalini kuna maeneo ambayo yanaonyesha kuwa yana mawasiliano lakini hali halisi inaonyesha hakuna mawasiliano.

Kwa kuwa, Mheshimiwa Mbunge wa Chambani ameleta orodha ya maeneo ya Jimboni kwake ambayo yanahitaji mawasiliano, ni imani yetu kuwa tutayafanyia kazi haraka iwezekavyo na maeneo ambayo yatapata mawasiliano na hata yale ambayo Rais hakufika, kwa sababu sisi kazi yetu ni kupeleka mawasiliano kwenye maeneo yote yanayohitaji mawasiliano, siyo maeneo ambayo ameahidi Mheshimiwa Rais.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge tuwasiliane niweze kujua kama itakapofika Septemba kama maeneo uliyotaja Jimboni kwako yatakuweko katika awamu ya kwanza, ya pili au ya tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tulivyosema katika hotuba yetu dhamira yetu hasa ni kupeleka mawasiliano kwenye maeneo yote ambayo yanahitaji mawasiliano.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Ninakushukuru Mheshimiwa Naibu Spika kwa kunipatia nafasi hii.

Kwa kuwa suala hili la mawasiliano tumekuwa tukilichukulia kwa upande ambao ni chanya zaidi kwa ajili ya kupata maendeleo endelevu, na vilevile ni jambo lililo wazi kwamba suala hili la mawasiliano lina upande hasi kama kutokujitambua wakati daktari anatibu huku anapokea simu, dereva anaendesha gari huku anapokea simu na Jaji anatoa hukumu huku anapokea simu.

Je, Serikali au Wizara yake ina sera gani ya kutuelimisha kwa kuwa waandaaji wa teknolojia hii wanaweza kuitawala na imeandaliwa na binadamu. Je, sisi ulimwengu wa tatu ambayo tunaikumbatia zaidi kwa kufanya zaidi upande wa hasi ukoje katika kuhakikisha mwanadamu huyu anadhibiti teknolojia hii ya mawasiliano?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli yapo matumizi hasi ya teknolojia, wakati mwingine unaweza kuwa unaongea na familia yako, badala ya kuongea nao, uko kwenye simu kwa hiyo pia ni namna moja.

Lakini Serikali yapo matumizi ambayo yanahatarisha maisha ya watu wengine kama mfano ulioutoa wa kuendesha gari huku unaongea na simu. Na ni kweli ajali nyingi siku hizi zinasababishwa na dereva anaendesha gari huku yupo kwenye simu anatuma meseji.

Kwa hiyo, tutashirikiana na taasisi zinazohusika, kama ni *traffic* na Polisi kuhusu kuelimisha Umma kuhusu hatari zinazotokana na kuendesha gari au kufanya vitendo ambavyo vitahatarisha maisha ya watu wengine. Mambo mengine kwa kweli ni mambo ya hulka tu na mambo ya ustaarabu ambapo Serikali kwa kweli haina mkono wake.

Na. 285

**Kampuni za Simu za Mkononi Kutoa Huduma za Kibenki**

**MHE. AMINA ABDULLA AMOUR** aliuliza:-

Kampuni za Simu za Mikononi nchini hupata leseni zao kutoka Mamlaka ya Mawasiliano nchini (*TCRA*) kwa ajili ya mawasiliano na huduma za *internet*, lakini kampuni hizi zimekuwa zikijishughulisha na utoaji wa huduma za kibenki kama vile kutuma na kupokea pesa, shughuli ambazo leseni zake hutolewa na Benki Kuu (BoT):-

Je, kampuni hizo zimepata leseni kutoka Benki Kuu kwa ajili ya huduma za kibenki au zinatumia leseni ya *TCRA* pekee?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Amina Abdulla Amour, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Maendeleo ya teknolojia nchini yanayoendelea nchini na huduma kote yamewezesha urahisi wa upatikanaji wa huduma mbalimbali za kijamii kwa kutumia vifaa vya mawasiliano. Mojawapo ya huduma hizi ni pamoja na zile za kutunza, kutuma na kupokea fedha ambazo hivi sasa hutolewa na makampuni ya simu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuweza kutoa huduma hizo za fedha makampuni haya yamepewa leseni ya ziada inaitwa *application service* kutoka Mamlaka ya Mawasiliano Nchini *(TCRA)* ambayo huwezesha makampuni haya kutumia miundombinu ya teknolojia ya mawasiliano kwa ajili ya huduma nyinginezo ikiwemo huduma za kibenki.

Hata hivyo, kutokana na shughuli za huduma za fedha nchini kusimamiwa na Benki Kuu ya Tanzania (BoT) makampuni haya pia yamepewa leseni nyingine ya kutoa huduma ya fedha kutoka Benki Kuu. Hivi sasa kuna kampuni nne (4) za simu zinazotoa huduma za kibenki kupitia mtandao wa huduma za mawasiliano.

**MHE. AMINA ABDULLA AMOUR:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Waziri kwa majibu yake mazuri. Hata hivyo nina maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa wizi wa mitandao umejaa hapa nchini. Je, Serikali ina mikakati gani kwa makampuni hayo yanayofanya shughuli hizi ili kuhakikisha usalama wa fedha za wananchi?

(b) Je, Serikali inapata mapato kiasi gani kwa kila mwaka kuhusu shughuli hizi?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba huduma hizi za kuhamisha na kupeleka fedha, kutunza kwa kutumia mitandao imewasaidia Watanzania wengi sana na kusogeza huduma za kibenki karibu na maeneo wanayoishi, wastani wa umbali kwenye benki ni kilomita 50.

Lakini siku hizi kutokana na huduma hizi wastani wa umbali kwenye huduma ya kifedha ni chini ya kilomita moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kumekuwepo na matatizo ikiwemo, wizi na udanganyifu Serikali kupitia Wizara yetu kwa maana ya *TCRA* na Wizara ya Fedha(Benki Kuu) imeanza kufanya vikao kwa wadhibiti hawa wawili. Mdhibiti wa fedha (*BOT*) na mdhibiti wa mawasiliano(*TCRA*) wamekutana na wamewekeana makubaliano (*MOU*).

Kinachofanyika sasa hivi ni kupitia upya kanuni za sheria ya Benki Kuu kwa sababu sheria ya benki kuu ndiyo inadhibiti fedha. Kanuni Na. 70 ili kuongeza ulinzi kwa mtumiaji wa huduma hii ya fedha. Kwa hiyo, tuna imani kwamba kikao kilichofanyika cha wadau siku chache zilizopita tarehe 20 Julai, 2012 maoni yamekusanywa ili kuweza kuimarisha ulinzi kwa wateja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili kwamba Serikali inapata kiasi gani kwenye huduma hii. Kwa sasa siwezi kuwa na takwimu za moja kwa moja, ninachofahamu ni kwamba mwaka jana peke yake kiasi cha fedha kilichopitia kwenye mtandao huu ni shilingi trilioni 6.2. Ni karibia asilimia 20 ya pato la Taifa. Shilingi trilioni sita nukta sita ndiyo fedha zilizozungushwa kupitia mitandao ya simu.

Kwa hiyo, hii ni biashara kubwa na Serikali inapata kodi kwenye mapato ya makampuni ya simu kutokana na huduma hii. Lakini vile vile kuna mapato kwa wale ma-*agent* na wengine ambao wanajihusisha na huduma hii. *(Makofi)*

Na. 286

**Kusambaza Maji Katika Wilaya zote za Mkoa wa Shinyanga**

**MHE. RACHEL R. MASISHANGA** aliuliza:-

Pamoja na Manispaa ya Shinyanga kuondokana na kero ya maji kupitia Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria, bado Wilaya nyingine za Mkoa huo ukiondoa Wilaya ya Kahama zinakabiliwa na ukame mkubwa na tatizo kubwa la majisafi na salama:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kusambaza maji hayo ya Ziwa Victoria katika Wilaya zote za Mkoa wa Shinyanga ili kuwaondolea wananchi hao adha ya kufuata maji kwa mwendo mrefu?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rachel Mashishanga Robert, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi wa maji wa Kahama - Shinyanga ambao chanzo chake ni ziwa Victoria ulianza rasmi kutoa huduma ya maji mwezi Februari, 2009.

Mradi huo kwa sasa unahudumia Miji ya Shinyanga na Kahama Vijiji 19 vya Wilaya ya Shinyanga na 15 vya Wilaya ya Kahama vilivyo ndani ya kilomita tano kutoka bomba kuu. Katika awamu ya pili ya mradi huduma ya maji itapanuliwa hadi kwenye vijiji vilivyopo ndani ya kilomita 12 kutoka kwenye bomba kuu ambapo Wilaya ya Kahama itakuwa na vijiji vipya 14 na Wilaya ya Shinyanga itakuwa na vijiji vipya 46.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo mengine ndani ya Mkoa wa Shinyanga yaliyopo kwenye awamu ya pili ya mradi ni miji midogo ya Tinde, Kagongwa, Muhunze, Kakola, Ilogi, Bugarama na Isaka. Wilaya nyingine itakayonufaika na maji ya Ziwa Victoria ni Kishapu ambapo upimaji, usanifu na uandaaji wa makabrasha ya zabuni za ujenzi umekamilika. Hatua inayofuata ni kutangaza zabuni za kuwapata wakandarasi wa ujenzi wa miundombinu ya maji.

Mheshimiwa Spika, kwa vijiji ambavyo havipo kwenye awamu ya pili ya mradi wa maji ya kutoka

Ziwa Victoria nazishauri Halmashauri za Mkoa wa Shinyanga ziweke vijiji hivyo katika mipango yake ili utekelezaji wake uwe kwenye awamu zinazofuata za *program* ya maendeleo ya maji (*WSDP*).

**MHE. RACHEL M. ROBERT:** Mheshimiwa Naibu Spika ahsante sana. Kwa kuwa hii ni ahadi ya Serikali kuvipatia vijiji maji ambavyo vipo kilomita 12 kutoka kwenye bomba kuu na imekuwa ni mazoea ya vijiji au maeneo ambapo mabomba makubwa au ngozo za umeme zinapita kuishia kuwa watazamaji tu.

(a) Nataka kujua ni lini sasa huu mradi wa awamu ya pili utaanza?

(b) Kwa kuwa kumekuwa na kero kubwa sana ya bei ya maji katika Mji wa Shinyanga na maeneo yanayotumia mradi huu, hii ni kwa sababu ya kuwa na Mamlaka mbili za maji KASHWASA na SHIWASA. Je, Serikali haioni sasa kuna haja ya kubakiza moja ili iwapunguzie mzigo watumiaji wa maji?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ahadi ya Serikali ya kupeleka maji katika vijiji vinavyopita kwenye bomba la kutoa maji kutoka Ziwa Victoria mpaka Kahama na Shinyanga, kama tulivyoeleza ni kwamba huu mpango umeanza kutekelezwa kwa sababu awamu ya kwanza ya vijiji 54 vilivyokuwa vimetazamiwa leo hii vijiji 19 vinapata maji. Na awamu ya pili sasa hivi inatazamiwa vijiji 96 vitapata maji. Kati ya hivyo vijiji 96 vijiji 46 vipo Shinyanga mjini. Mradi huu ukikamilika utakuwa na vijiji 135 na kati ya hivyo 65 vitakuwa ni vya Shinyanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nataka kumhakikishia kwamba katika Bajeti yetu ambayo tuliipitisha juzi tayari tumetenga fedha za utekelezaji awamu ya pili kwa kuanza na usanifu. Kwa hiyo, ni suala la uhakika kwamba hili linatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusu bei kuwa tofauti kwa sababu kuna mamlaka mbili, niseme tu kwamba hili nilichukue tukaliangalie kwa undani na kwa sababu wanaopanga bei siyo Wizara ni watumiaji au wakisimamiwa na *EWURA*. Tunallichukua tukaliangalie madhara yake na kama itaonekana hivyo ndiyo hatua muhimu zitachukuwa. *(Makofi)*

**MHE. MWIGULU L. N. MADELU:** Mheshimiwa Naibu Spika ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Vijiji vya Mseko, Malendi, Kizonzo, Ulemo, Kinampanda na Maluga ni miongoni mwa vijiji vyenye shida kubwa sana ya maji Wilayani Iramba, lengo na ramani ya awali ya Bomba hilo la maji kutoka Ziwa Victoria ilikuwa maji yavutwe yapitie Iramba, yapitie Mkoa wa Singida yaje hadi Dodoma mpaka Kongwa.

Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu kurejea ramani ile ya mjerumani ili ilete maji kupitia Iramba hado Dodoma mpaka Kongwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, jibu hilo muhimu sana tafadhali. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Nchemba kwa sababu amekuwa akifuatilia sana shughuli za maji hasa

matatizo ya maji katika Jimbo lake la Iramba na Singida kwa ujumla.

Ni kweli kwamba ramani za awali zilitengenezwa na Wajerumani wakati wa Ukoloni ambapo waliainisha kwamba wangetoa maji Ziwa Victoria na kuyafikisha mpaka Mikoa ya Singida na Dodoma. Ni wazo zuri lakini Serikali imethubutu. Kwa sababu katika kutekeleza ndoto hiyo tumeshafikisha maji katika Miji ya Kahama na Shinyanga.

Kwa hiyo, nadhani kwamba katika awamu zinazokuja tutalifikiria na kuona kama linauwezekano lakini tujue kwamba sasa hivi na wakati ule ni tofauti. Wakati ule idadi ya watu ilikuwa ni kidogo kwa hiyo iliangaliwa kwa maana hiyo. Leo idadi ya watu ni kubwa ni lazima tuangalie kwa mapana zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa Mji wa Dodoma tunao mpango wa kujenga Bwawa la Farkwa ambalo litasaidia kuongeza huduma ya maji kwa Mji wa Dodoma. Kwa hiyo, tutakachoangalia zaidi hapa pengine ni Mji wa Singida kwa maana ya kuboresha huduma za maji pale.

Na. 287

## Fidia Kutokana na Uharibifu Unaosababishwa na Wanyamapori

**MHE. CECIALIA D. PARESSO** aliuliza:-

Wananchi wanaoishi jirani na Msitu wa Hifadhi ya Mamlaka ya Ngorongoro Wilayani Karatu, wamekuwa wakipata usumbufu mkubwa kutokana na wanyamapori kuvamia na kuharibu mazao yaliyopo mashambani mwao na fidia wanayolipwa ni ndogo sana ukilinganisha na uharibifu unaotokea:-

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwalipa wananchi hao fidia inayolingana na uhalisia?

(b) Je, Serikali ipo tayari kuainisha mipaka halisi kati ya Wilaya ya Karatu, hususan Vijiji vinavyopakana na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro ili kuondoa tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu inatambua madhara yanayosababishwa na wanyamapori wakali na waharibifu dhidi ya maisha na mali za wananchi.

Hata hivyo, kulingana na kifungu cha 71 cha sheria ya kuhifadhi wanyamapori Na. 5 ya mwaka 2009, malipo yanayotolewa ni kama kifutajasho na siyo fidia. Serikali haitoi fidia kutokana na mazao yanayoharibiwa kwa kuzingatia bei ya soko au kiasi cha mazao yanayotarajiwa kuvunwa kutokana na ukweli kwamba tatizo hili ni kubwa na siyo rahisi kwa Serikali kumudu kulipa fidia halisi.

Aidha siyo rahisi kufidia uhai endapo kifo kimetokea. Vigezo vinavyotumiwa katika malipo ya kifutajasho ni ukubwa na umbali wa shamba lililoharibiwa kutoka eneo la hifadhi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ilishirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Karatu kutatua utata wa mpaka uliokuwepo kati ya vijiji vya Wilaya ya Karatu na eneo la hifadhi ya Ngorongoro. Mapema mwaka huu, timu ya wapima ardhi wa Wilaya na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro pamoja na Kamati ya Ulinzi na Usalama chini ya Uenyekiti wa Mkuu wa Wilaya ilibaini chanzo cha tatizo husika siyo mpaka bali ni wananchi wahamiaji kutaka kunywesha mifugo yao ndani ya hifadhi.

Katika kumaliza tatizo hilo, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro imetenga fedha katika Bajeti ya mwaka 2012/2013 kwa ajili ya ujenzi wa bwawa katika kijiji cha Endamaga. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Hili swali maarufu ehe, Mheshimiwa Cecilia Paresso, swali la nyongeza.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa, kifutajasho hicho hutolewa na Serikali. Je, Wizara haioni sasa kwamba ni wakati muafaka kifutajasho hicho kitolewe na Mamlaka husika kwa maana ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro?

(b) Kama mamlaka hiyo itaachiwa kutoa fidia hii. Je, Serikali kwa maana ya Wizara iko tayari kutoa mwongozo kuondokana na hii dhana ya kifutajasho na kutoa fidia yenye uhalisia kulingana na uharibifu uliotokea?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Cecilia Paresso, na baada ya mimi na yeye kuzungumza hata kabla ya leo tulikubaliana kwamba itakuwa muhimu kwa sababu suala kubwa hapa ni migogoro inayoendelea.

Kuna migogoro ambayo haiishi. Tuhakikishe kwamba tunapata nafasi ya kutembelea Karatu na tutafika vilevile Kijiji cha Endamaga ambacho Serikali kupitia Hifadhi ya Taifa ya Ngorongoro tutachimba bwawa kwa ajili ya kurahisisha wananchi waweze kunywesha mifugo yao. Ni kweli kwamba kifutajasho ambacho kinatolewa ni kidogo, lakini kama nilivyojibu katika swali la msingi Serikali haitoi fidia. Katika hali ya

kawaida itakuwa ni vigumu sana katika madhara yeyote yanayosababishwa na wanyamapori nchini kuweza kufidiwa hali halisi ikiwa ni pamoja na wananchi ambao wanapoteza maisha yao endapo watakuwa wanavamiwa na wnayama hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachotakiwa ni Serikali kuzingatia vigezo ambavyo vimewekwa chini ya kanuni ya sheria niliyoitaja kuweza kutoa kifutajasho kwa kuhakikisha kwamba wananchi wanaendelea kuwa sehemu ya uhifadhi. Kama Hifadhi ya Ngorongoro itahusika na wanyama waharibifu wanaotoka nje ya hifadhi, utaratibu huu na sheria hiyo ipo chini ya sheria ya wanyamapori.

**NAIBU SPIKA:** Nimemwona Kiongozi wa Kambi ya Upinzania kwa siku ya leo. (*Kicheko*)

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika nashukuru sana kwa kuniona na kunipa cheo kikubwa.

Kwa kuwa, tatizo hili la wanyama kuleta madhara kwa wanadamu linaathiri wananchi wengi ambao wako karibu na maeneo ya hifadhi ya Taifa, na kwa kuwa wanadamu wanazidi kuongezeka ni ukweli usipingika na maeneo ya hifadhi ni yale yale.

Je, Serikali ina mpango gani wa kudumu wa kutatua tatizo hili ambalo linaleta shida kwa wananchi wa Tanzania?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kama tulivyosema kwenye jibu letu la msingi, hifadhi ni zile zile na idadi ya watu kama anavyosema Mchungaji inazidi kuongezeka, lakini Serikali chini ya sheria ambazo zimewekwa tutahakikisha kwanza mipaka ya hifadhi zote nchini inaendelea kubaki pale pale haitabadilika kwa vyovyote vile.

Tunapojadili suala la migogoro ya mipaka kati ya wananchi na hifadhi zetu zote nchini ni vema Bunge lako Tukufu tukalijulisha kwamba mipaka hiyo kama ilivyowekwa na wakoloni, kama vile ambavyo ramani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haibadiliki, mipaka ile inayolinda hifadhi zetu itaendelea kulindwa na haitabadilika kabisa.

Mheshimiwa Spika, tunafanya mambo mawili kwanza kuendelea kuwaelimisha wananchi kuheshimu mipaka hii kwa sababu ni urithi mkubwa sana wa Taifa letu.

Pili; tunaendelea kuongeza juhudi za Serikali za kuhakikisha kwamba tunaendelea kushirikiana na wananchi wa maeneo yanayozunguka hifadhi zetu zote na tunaendelea kuongeza viwango vya fedha ambavyo tutakuwa tunaendelea kutoa kwa shughuli mbalimbali za maendeleo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ya muda, kama mnavyoona umebaki kidogo na nina maswali mawili naomba tuvumiliane.

Na. 288

**Kilimo cha Umwagiliaji Tabora**

**MHE. SHAFFIN AHMEDALI SUMAR** aliuliza:-

(a) Je, Serikali imetumia kiasi gani cha fedha kwenye kilimo cha umwagiliaji katika mwaka wa fedha 2009/2010, 2010/2011 na 2011/2012 Wilaya Uyui?

(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kutenga fedha za kutosha kwenye Bajeti ijayo ili jimbo la Tabora Kaskazini linufaike na mradi wa kilimo cha umwagiliaji?

**NAIBU WAZIRI WA KIILMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, kwanza naomba kwa ridhaa yako naomba nitume salama za pongezi kwa mke wangu kipenzi, barafu ya moyo wabgu, Naima kwa kujifungua mtoto wa Kike Akila. Kwa hiyo, kwenye ile orodha ndefu ya watoto wangu nimepata mtoto mwingine *Alhamdullilah Rabi l-alamiin.*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge katika ile orodha ameongeza mmoja. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Ila nimekataa wanaume wa Kisukuma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Shaffin Ahmedali Sumar, Mbunge wa Tabora Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Uyui mwaka 2009/2010 Wilaya ya Uyui imepata milioni 138.8. Mwaka 2010/2011 imepata kama milioni 39.6 na mwaka 2011 imepata milioni 58 kwa mgao wa *DADPs* na *TASAF.*

Fedha hizi zilizotolewa kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya *(DADPs – DADG),* Mfuko ya *DIDF na TASAF* zilitumika kuendeleza miundombinu ya umwagiliaji katika skimu za Miswaki (300 ha) na kufanya upembuzi yakinifu katika maeneo ya Shitage (400 ha) na eneo la kujenga bwawa Goweko (400 ha).

Katika utekelezaji Skimu ya Miswaki umefanyika ujenzi wa mifereji mikubwa yenye urefu wa mita 2700 na midogo yenye urefu wa mita 3200 pamoja na vigawa maji. Skimu ya Goweko utafiti wa kina wa jamii na mazingira unaendelea ili kupata *clearance certificate* kutoka Baraza la Taifa la Mazingira *(NEMC)* itakayoruhusu kuendelea na hatua za ujenzi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaona umuhimu wa kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kuendeleza kilimo cha umwagiliaji katika Wilaya ya

Uyui na Wilaya nyingine hapa nchini. Aidha, kwa kupitia program ya *ASDP* upo utaratibu uliowekwa na miongozo kutolewa inayoelekeza namna ya kuibua miradi kupitia *DADPs* na kufanya utekelezaji wake baada ya kutengewa fedha.

Kupitia utaratibu huo wananchi wanatakiwa kubaini mahitaji yao na kuyaweka katika mipango yao ya vijiji, kata na hatimaye Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia haya yote kama nilivyoeleza hapo awali Serikali imetenga fedha kiasi cha shilingi 466,000,000 kwa ajili ya miradi ya umwagiliaji ya Wilaya ya Uyui kwa mwaka huu wa fedha. Fedha hizo zinatarajiwa kufanya kazi katika miradi ya umwagiliaji ya Miswaki na Shitage, ununuzi wa kinu kikubwa cha kukoboa mpunga na ununuzi wa trekta moja na pamoja na vifaa vyake.

**MHE. SHAFFIN AHMEDALI SUMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize maswali madogo. Lakini kabla ya maswali naomba nimpongeze kwa kuongeza idadi ya watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jimbo langu la Tabora Kaskazini kuna eneo moja tu la Shitage limetajwa kuwa na mradi wa umwagiliaji ambapo hatua ya upembuzi yakinifu bado inaendelea. Lakini kuna maeneo mengi. Kwa mfano Kata ya Ufuluma, Kata ya Ibili na Kata Mabana, ambapo kuna maeneo mazuri ya kuweza kuanzisha kilimo cha umwagiliaji.

(a) Je, Waziri yuko tayari kuja na mimi kuja kuhakikisha maeneo yalivyo mazuri na hatimaye kuwachukulia hatua wale watendaji wa Halmashauri ambao hawawajibiki ipasavyo katika kuibua miradi?

(b) Je, Wizara imejipangia muda gani (*timeframe*) kwa ajili ya kuhakikisha zoezi zima la upembuzi yakinifu unakamilika na kuanzisha mradi huo hususan kata ya Shitage Jimbo la Tabora Kaskazini?

**NAIBU WAZIRI, KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali ya Mheshimiwa Shaffin kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimesema kwenye mradi wa Shitage, mradi wa Shitage ulikuwa na upembuzi yakinifu, upembuzi yakinifu umekamilika. Kwa hiyo, kwa mwaka huu kuna milioni 313 kwa sababu kuna milioni 253 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa banio na mifereji na mradi wa umwagiliaji wa Shitage Mingihu ni ujenzi wa mifereji ambao una kama milioni 60. Kwa hiyo, kuna milioni 313 ambazo zimejengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niridhie pia kwamba amenialika twende kwake tukazungumze kwanza tukaangalie maeneo, lakini pia tukazungumze na watendaji ili waweze kubuni na kuibua miradi hii.

Mimi nasema kwa sababu miradi hii yote inaonekana inakwama kwenye ngazi ya Halmashauri kwa sababu ya taaluma na matumizi mabaya ya fedha. Wacha twende tukaangalie lakini kwanza mimi ningefurahi sana kama tungeweza kuhakikisha

kwamba tunakamilisha huu mradi Miswaki ambao una hatua ya miundombinu tunaweza tukamalizia kwa mwaka huu wa fedha na huu mradi wa Shitage ambao tumeshatenga milioni 313 kwa awamu ya kwanza kuhakikisha kwamba fedha hizi zinapata matumizi mazuri. (*Makofi*)

**MHE. SAID AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa umwagiliaji ni hatua mojawapo ya kuleta mapinduzi katika kilimo. Je, ni kwa nini miradi ya umwagiliaji inachukua muda mrefu kukamilika ikiwemo mradi wa Mwamamakulu na Ugala kule Mpanda? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI, KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Arfi, Mbunge wa Mpanda Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba miradi ya umwagiliaji imekumbwa na matatizo mengi. Matatizo yako aina mbalimbali. Kwa mfano kama kule Wilaya ya Rungwe kuna tatizo la fedha kwamba ilikwenda ikapata matumizi mabaya, *DALDO* tumemsimamisha kazi.

Kuna miradi mingine ambayo tumepeleka fedha watalaam wenyewe inaonekana utalaam wao ni mdogo. Kuna miradi mingine imeanza utekelezaji yamekuja mafuriko yamesafisha kama kule maeneo ya Itilima Shinyanga na kadhalika. Kwa hiyo, miradi ya

umwagiliaji kusema kweli iko *complicated* kidogo kwa sababu ina matatizo mengi.

Lakini tulichojipanga sasa hivi ni kwamba kwanza kabisa wakati tunaongeza matumizi ya fedha lakini tuongeze pia na taaluma kwa sababu inaonekana kwamba hata zile fedha zinazokwenda kwenye Halmashauri hazipati matumizi kama yaliyotarajiwa. Kwa hiyo, nimepokea hili na lile la Mheshimiwa Shaffin nadhani kwenye miradi ya umwagiliaji ni vema kujipanga vizuri zaidi ili fedha inayokwenda ipate *value for money.* (*Makofi*)

Na. 289

**Mpango Mkubwa wa Kilimo cha Umwagiliaji Bonde la Ziwa Victoria**

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI** aliuliza:-

Bonde la Ziwa Victoria hasa katika Kata za Kiloleni, Mwamanyili, Kabita, Kalemela, Lamadi na Mwambao wa Mto Duma katika Kata za Ngasomo, Badugu, Nyaluhande na Mbuga ya Shigala ni maeneo yanayofaa sana kwa kilimo cha umwagiliaji hasa ikizingatiwa kuwa mvua mara nyingi si za uhakika na hivyo mara nyingi mazao ya wakulima yamekuwa yakiathirika na ukosefu wa mvua ya kutosha na hivyo kusababisha njaa mara kwa mara kwa wananchi wa maeneo hayo:-

(a) Je, ni lini Serikali itaanzisha mpango mkubwa wa kilimo cha umwagiliaji katika maeneo hayo?

(b) Je, ni lini Serikali itajenga bwawa la maji la Lwangwe katika kata ya Shigala kwa ajili ya umwagiliaji katika mbuga ya Busega?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Titus Mlengeya Kamati, Mbunge wa Busega, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia mradi unaogharimiwa na nchi wanachama wa Bonde la Mto Nile *(Nile Equatorial Lake Subsidiary Action Plan (NELSAP)* ya *Nile River Basin– Tanzania Irrigation and Watershed Management Project)* inafanya upembuzi yakinifu wa eneo la hekta 22,500 katika Bonde la Ziwa Victoria hususan maeneo ya mabonde ya mito Ngono na Mara, Bugwena na mabonde ya Manonga na Isanga kwa ajili kuendeleza miradi ya umwagiliaji.

Mtaalum mwelekezi kampuni ya *Gibbs East Africa* inaendelea kufanya kazi hiyo na kutayarisha usanifu wa awali *(preliminary designs).* Kazi hii iliyoanza Oktoba, 2011 inatarajiwa kukamilika Desemba, 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha katika mwaka wa fedha 2003/2004 Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Japan na Shirika la Kilimo na Chakula Dunia (*FAO*) ilianzisha mradi wa wakulima kwenye sehemu kame nchini na mradi wa ukanda wa kijani (*Greenbelt Project*), ambapo Wilaya 29 zilinufaika kwa kupatiwa

vifaa vya umwagiliaji kwa njia ya matone *(Drip Irrigation Kits),* matenki, pampu za miguu *(Treadle pumps)* na pampu zinazotumia mafuta.

Vijiji vya Mwamanyili, Kalemela, Nyakoboja katika Wilaya ya Magu vilinufaika na mradi huo wa Japan mwaka huo. Aidha, katika mwaka 2005/2006 Serikali ilitekeleza mradi wa umwagiliaji wa Kalemela (57ha) kwa kujengo miundombinu inayojumuisha pampu ya upepo *(wind mill)* kwa ajili ya kuvuta na kusukuma maji kutoka Ziwa Victoria kwenda mashambani.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya umwagiliaji Wilaya Magu. Katika mwaka 2011/2012 Mradi wa Lutubiga (200ha) Mradi umetengewa milioni 230,000,000 na kutoka *DASIP* Shilingi 725,000,000 kwa hiyo jumla imetengewa karibu shilingi bilioni. Tayari kazi ya usanifu imekamilika na mwaka huu 2012/2013 ujenzi wa skimu hii utakamilika kwani tayari zabuni kwa ajili ya kazi hiyo imetangazwa kwa ajili kumtafuta mkandarasi. Aidha, skimu ya Shinembo/Bundilya imeainisha kufanyiwa upembezi yakinifu na usanifu kwa ajili ya kutumia teknolojia zenye usanifu katika matumizi ya maji kwa njia ya matone na kuongeza tija katika uzalishaji wa zao la pamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inafanyia tathimini uendelezaji wa mradi wa Bwawa la Lwangwe na kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Magu na wananchi kwa ujumla, kwa kutumia fursa zilizopo katika *ASDP* kutenga fedha za kuendeleza miradi ya umwagiliaji likiwemo Bwawa la Lwangwe.

**MHE. DKT. TITUS M. KAMANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ambayo kwa kweli yanatia matumaini hasa kama huu mradi wa Lutubili utatekelezwa. Lakini nilitaka kumwuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Sijui kama ana taarifa kwamba katika ule mradi wa *Windmill* pale Kalemela muda mchache baada ya kusimikwa ile *Windmill* iliharibika wakati ikiwa kwenye kipindi cha *guarantee* na yule fundi ambaye alitoka Kenya hajaweza kupatikana mpaka sasa kuweza kufanya ukarabati. Ningeomba Serikali kama wanafahamu basi watusaidie ili urekebishaji wa ile *windmill* iweze kukamilika na wananchi wanufaike?

(b) Kwanza baada ya kuwasiliana kuhusiana na hili bwawa la Lwangwe kwa ajili ya mboga ya Busega Serikali imewaelekeza watalaam walioko Mwanza waweze kufuatilia. Lakini hadi sasa hawajafika kule kwa sababu ya upungufu wa rasilimali. Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kuwaambia nini wananchi wale kwamba rasilimali kwa ajili ya kituo cha Mwanza cha umwagiliaji kitapatikana lini ili maafisa husika waweze kufanya tathimini na hatimaye mradi kutekelezwa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Kamani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la Kalemela nashukuru ameniambia kwamba kuna tatizo pamoja na *windmill* pale kuwekwa lakini baada ya muda mfupi tu likasimama pamoja na kwamba iko kwenye *guarantee*.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ndio matatizo tuliyokuwa tunasema kwamba tumeona kuna udhaifu kidogo wa mawasiliano baina ya watalaam wetu na Serikali Kuu. Lakini hili tutalifanyia kazi kwa sababu hata huo utalaam wa *windmill* hata *REA* tu pake kwenye nishati mbadala wanatumia utalaam wa *windmill.* Kwa hiyo, linawezekana kufanya hata kwa nguvu wenyewe. Tutamfuatilia mkandarasi tujue palikwama nini na *what is the problem* tufufue mradi huu. *(Makofi)*

Hili la pili la Lwangwe na upungufu wa rasilimali kutoka Ofisi Kuu ya *irrigation* pale Mwanza hili halitakiwa kutokea. Kama kulikuwa na *program* ya kwenda Lwangwe na kufanya tathimini pamoja na kushirikiana na Halmashauri kufanya tathimini ya mradi huu haitakiwi kutokea kwa sababu ya upungufu wa rasilimali.

Namwomba Mheshimiwa Mbunge kwamba nitalifuatilia na nitarejea kwake na majibu na kwamba kazi hii ya kufuatilia mradi wa Lwangwe utafanyika mwaka huu wa fedha. (*Makofi*)

**MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali fupi sana la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wakulima wa *scheme* ya umwagiliaji ya Chalinze katika Bwawa la Ikoa wameitikia adhima ya Serikali ya kuendeleza kilimo cha umwagiliaji. Je, Serikali itakuwa tayari kutenga fedha zaidi kwa ajili ya kuendeleza mradi huu wa umwagiliaji ambao ni *scheme* ya siku nyingi sana?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mzee Ezekiah Chibulunje, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba hii *scheme* ya Chalinze ni *scheme* ya muda mrefu. Nadhani kwa sasa hivi watalaam wanaifanyia tathimini kwa sababu inaonekana *scheme* hii ina tatizo la *hydrology* kwa maana ya maji yanayoingia na kutoka kwenye *scheme* ile.

Kwa hiyo, nadhani pale watalaam wameomba kutafakari kidogo kuhusu njia bora ya kuendelea na *scheme* hiyo, hasa kwa kuwa kwenye upande wa pili huku Chinangali wanatoa maji yanayoonekana kwamba chini ya ardhi pana maji mengi sana.

Kwa hiyo, inawezekana kwa maana ya *irrigation* ambayo inafanya pale kwenye *scheme* ya Chalinze huenda ikabidi tuangalie tutafute teknolojia hii inayotokana na mradi wa kutoa maji chini ya ardhini ambayo maji yako mengi kama pale Chinangali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini namwomba nimhakikishie Mheshimiwa Chibulunje kwamba hii *scheme* ya Chalinze kwa sababu ya ni *scheme* ya muda mrefu haijaja tu isipokuwa inafanyiwa tathimini kuangalia kama tuangalie twende na teknolojia mpya kama hii ya Chinangali ama tuangalie kuboresha mabwawa ili kupata hifadhi kubwa zaidi ya maji kwa maji yanayotokana na mito. Hili tunalifanyia kazi nitarejea kwake na majibu baadaye. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana, maswali sasa muda wake umekwisha, naomba niende kwenye matangazo kama ifuatavyo:-

Kwanza wageni waliopo katika *Speakers Galley* au Gallery ya Mheshimiwa Spika, ni wageni wa Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi, Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, ambaye ni mkewe Bi. Mariam Hussein Mwinyi.

Naomba usimame. Karibu sana hapa Bungeni. Wageni wengine ni kutoka Wizara ya Afya ambao ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi Bi. Regina Kikuli karibu ni Kaimu Kaitbu Mkuu. Kaimu Mganga Mkuu wa Serikali Dkt. Donan Mbando, karibu sana Doctor. Wawakilishi na wadau mbalimbali wa maendeleo ya Afya waliopo tunawakaribisha. Wenyeviti wa Bodi na

Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Afya, Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo, Wakurugenzi Wasaidizi na Maafisa wengine kutoka Wizara ya Afya nyote mnakaribishwa sana, leo na kesho ni siku yenu hapa Bungeni. (*Makofi*)

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, ni pamoja na wageni wa Mheshimiwa Margaret S. Sitta, Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, ambao ni Mkurugenzi wa Taasisi ya Sikika Iren Kiria, Patrick Nemo na Hope Lyimo. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Vita Rashid Mfaume Kawawa, ambao ni wageni kutoka Israel, wenye nia ya kuwekeza katika Kilimo cha Tanzania, ni Salim Nuru Sigala na Menahenza Free, ahsante sana wako hapa pamoja na Minihaji Litumi. (*Makofi*)

Tunaye mgeni ambaye ni Mbunge Mstaafu na Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Utawala Bora Ndugu Thomas Ngawaiya. Karibu sana pale ulipo. Wageni kwa ajili mafunzo ni wanafunzi 128 pamoja na walimu wao kutoka Shule ya Msingi ya Mbwanga ya hapa hapa Dodoma. Wageni kutoka Mbwanga Shule ya Msdingi msimame pale mlipo, karibuni sana wanafunzi na walimu kutoka Mbwanga. *(Makofi)*

Tuna mhadhiri kutoka Chuo Kikuu cha *Saint John's* cha hapa hapa Dodoma, anaitwa Neema Senkondo karibu. Tuna wanafunzi 70 pamoja na walimu kutoka Shule ya Sekondari ya Dodoma. Wanafunzi kutoka *Dodoma Secondary,* simameni. Karibuni sana na wengine wako pale. Hii shule ya Dodoma, ni shule jirani

yetu kabisa na majengo yetu ya Bunge na ni shule ya zamani sana hapa. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wanakwaya 39 wa Kwaya ya Mtakatifu Maria Goreti kutoka Mbezi Beach, Dar es Salaam, karibu sana wanakwaya, karibuni hapa Dodoma. *(Makofi)*

Pia tuna wageni watano kutoka *Under the Same Sun* wakiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji Bi. Vicky Mtetema, karibuni sana hapa Dodoma. *(Makofi)*

Vile vile tuna wageni watatu kutoka *PSI*-Tanzania wakiongozwa na John Wanyancha, Mkurugenzi wa Mahusiano, Shirika la PSI-Tanzania, karibuni sana. (*Makofi*)

Matangazo ya vikao ni kama ifuatavyo:-

Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, Peter Serukamba anaomba Wajumbe wa Kamati yake wakutane saa saba mchana ukumbi 231.

Waheshimiwa Wabunge pia tuna tangazo la tanzia, naomba kuwataarifu Waheshimiwa Wabunge kwamba, Ofisi ya Bunge imepata msiba wa kufiwa na mfanyakazi Ndugu Peter Mazengo ambaye alikuwa akifanya kazi Idara ya Uhasibu. Kifo hicho kimetokana na ajali ya gari, majira ya saa tatu, jana usiku na kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge naomba tusimame kwa dakika chache kwa kumbukumbu ya Marehemu.

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge walisimama*

*dakika chache kuomboleza kifo cha Ndugu Peter Mazengo)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, taarifa zingine zinazohusiana na msiba huo tutaendelea kupeana kadri muda unavyokwenda.

Tunaye Diwani Mfudi Mihayo anayetoka Ilolo Wilaya mpya kule Isimani karibu sana Mheshimiwa Diwani, huyu ni mgeni wa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa William Lukuvi. *(Makofi)*

Tuna tangazo kutoka kwa Mwenyekiti wa *APNAC*, Daktari Mary Mwanjelwa anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati ya Utendaji wa Chama cha *APNAC* kwamba wakutane saa saba mchana katika Jengo la Utawala, Chumba 227. Bado matangazo yanaendelea kidogo, Waheshimiwa Wabunge naomba kuwafahamisha kwamba Daktari Faustine Ndugulile, Mbunge wa Kigamboni ambaye pia ni Katibu Mkuu wa *TAPAC* hivi karibuni amechaguliwa na wataalam wa masuala ya UKIMWI kuwa mwakilishi wa Bara la Afrika kwenye Taasisi ya Kimataifa ya masuala ya UKIMWI *International Aids Society* kwa kipindi cha miaka minne 2012-2016. (*Makofi*)

Katika kuwania nafasi hiyo Mheshimiwa Ndugulile alichuana na wagombea wengine kutoka nchi 13 Ethiopia, Nigeria, Afrika Kusini, Rwanda, Kenya, Morocco, Sudan na Misri. Kwa niaba ya Bunge naomba kukupongeza sana Mheshimiwa Ndugulile na

nakutakia kila la kheri katika uwakilishi wako katika chombo hicho kwa niaba yetu. (*Makofi*)

Kulikuwa na zoezi la kulenga shabaha jana tarehe 29 kwenye Kambi ya Jeshi la Kujenga Taifa, Makutupora, Dodoma na Mwenyekiti wa *Club* ya kulenga shabaha Mheshimiwa Juma Nkumba ndiyo ananitaarifu hapa kwamba, kulikuwa na mashindano ya kutumia *pistol, light machine gun LMG* na *SMG*. Katika mashindano hayo, mabingwa katika *pistol* bingwa kabisa alikuwa Mheshimiwa Ally Mohamed Keissy, akifuatiwa na Mheshimiwa Modestus Kilufi, Mheshimiwa Vincent Nyerere alikuwa wa tatu, Mheshimiwa Said Nkumba wa nne na Mheshimiwa David Matayo David wa tano.

Kwa kutumia *LMG*, Mheshimiwa Said Nkumba alikuwa wa kwanza; Matayo David, alikuwa wa pili; Martha Mlata, alikuwa wa tatu; Vincent Nyerere, wa nne na Shaffin Sumar, wa tano.

*Machine gun SMG*, Mheshimiwa Matayo David alikuwa wa kwanza; Said Nkumba, wa pili; Shafin Sumar, wa tatu; Vincent Nyerere wa nne na David Silinde wa tano.

Sasa tunaendelea kumalizia Waheshimiwa Wabunge; kuna tangazo limeletwa kwangu na Mheshimiwa Leticia Nyerere, Mratibu wa mashindano ya kumtafuta Madame Bunge, anaomba saa saba wakutane wafuatao ili wapewe taratibu za,kufanya mazoezi. (*Kicheko/Makofi)*

Wanaotakiwa huko ni Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Margareth Sita, Mheshimiwa Maria Hewa ambaye ndiye Bingwa mtetezi, Mheshimiwa Daktari Terezya Huvisa, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Mchungaji Assumpter Mshama, Mheshimiwa Rita Kabati, Mheshimiwa Rita Mlaki, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Esther Matiko, Mheshimiwa Susan Kiwanga, Mheshimiwa Vicky Kamati, Mheshimiwa Joyce Mukya, Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mheshimiwa Lolensia Bukwimba, Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, Mheshimiwa Rebecca Mngodo na Mheshimiwa Gaudensia Kabaka. Mshindi wetu hapo tutamwaisha London kwenye *Olympic*. (*Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, katika mashindano ya mechi za Jumamosi kati ya Bunge *Sports Club* na *NMB Bank*, katika mpira wa miguu *NMB Bank* walitoka suluhu na Bunge *Sports Club* kwa mpira wa miguu sifuri kwa sifuri, mpira wa pete Bunge *Sports Club* walipata 11, *NMB Bank* sita. *(Makofi)*

Lakini vile vile Mwenyekiti Bunge *Sports Club*, Mheshimiwa Idd Azzan na kwa niaba ya Wanayanga humu ndani anaomba kuwapongeza sana timu ya Yanga kwa kuchukua ubingwa wa Afrika Mashariki na Kati siku ya Jumamosi.  (*Makofi*)

Nafahamu kwa nini Waheshimiwa mnapiga makofi kwa unyonge ni kwa sababu pamoja na kuwapongeza Yanga, lakini lazima tuwakumbushe madeni ya magoli kama matano lazima wajiandae kuyarekebisha. *(Kicheko/Makofi)*

Tunawatakia kila la kheri huko wanakoelekea. Waheshimiwa Wabunge, mwisho kabisa natumaini mnafuatilia mashindano ya *Olympic* yanayoendelea kule London na mimi niliangalia kidogo jana nikawa nashangaa kweli kwa nini Tanzania hatupeleki timu za kutosha. Niliangalia mchezo wa kunyanyua uzito wakawepo Mabinti wa Kijapani, Wakorea wadogowadogo kabisa wananyanyua kilo 97, 95.

Sasa nikasema sisi hapa tuna shida gani, tuna akinamama wa Kinyamwezi, wa Kisukuma wale yaani yale mauzito yale wanayanyanyua mara moja tu, tungerudi hapa na nishani ya dhahabu chapu chapu. Kwa hiyo, natoa wito kwa Mheshimiwa Waziri wa Michezo kutembelea Tabora, Shinyanga na Mwanza. Mashindano kama yale ya kuogelea wale akinamama wanaweza kabisa tukapata dhahabu hapa. (*Kicheko/Makofi)*

Ahsanteni Waheshimiwa Wabunge, hapo ndiyo mwisho wa matangazo yetu. Nimekuona Mheshimiwa Waziri wa Nchi, halafu Waheshimiwa baadaye kidogo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 54(4), naomba kutoa hoja ya kubadilisha uamuzi wa Bunge kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa, tarehe 17 Julai 2012, Mheshimiwa Emmanuel Nchimbi, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi aliwasilisha Bungeni hoja ya makadirio ya mapato

na matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani kwa Mwaka 2012/2013;

Na kwa kuwa, tarehe 18 Julai, 2012 Bunge lilitaarifiwa kuhusu ajali ya meli ya *MV. Skagit* kuzama, iliyotokea katika eneo la Kisiwa cha Chumbe, huko Tanzania Zanzibar na kusababisha vifo vya wasafiri wengi;

Na kwa kuwa, kutokana na ajali hiyo, Mheshimiwa Waziri aliamua kutoa hoja ya kuiondoa Bungeni hoja hiyo ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara yake ya Mambo ya Ndani ya Nchi ili kuwawezesha Waheshimiwa Wabunge kushughulikia msiba huo mzito;

Na kwa kuwa, Bunge lako Tukufu kwa mujibu wa Kanuni ya 58(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, lilikubali kuwa hoja hiyo iondolewe Bungeni;

Na kwa kuwa, kilichokusudiwa siyo kuiondoa hoja ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, isipokuwa kuihairisha;

Na kwa kuwa, Kanuni ya 53(8) inazuia Mbunge yeyote kufufua jambo lolote ambalo Bunge lilikwisha kulitolea uamuzi katika mkutano unaoendelea au uliotangulia isipokuwa kwa kufuata masharti ya Kanuni za Kudumu za Bunge;

Na kwa kuwa masharti ya Kanuni ile ya 54(4) yanaruhusu hoja ya kutaka uamuzi wa Bunge uliokwishafanywa ubadilishwe;

Kwa hiyo basi, kutokana na mazingira hayo na kwa kuzingatia Kanuni ya 54(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu libadilishe uamuzi wake wa kuiondoa hoja ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2012/2013 na badala yake kuwa uamuzi wa kuiahirisha hoja hiyo ili ipate nafasi ya kurejeshwa Bungeni kwa lengo la kuhitimisha na hatimaye kupitishwa na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Bunge liliafiki na kukubaliana kuhusu kurejeshwa kwa Hoja ya Wizara ya Mambo ya Ndani Bungeni)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Kwa hiyo, rekebisho hilo limefanyika, lilikuwa ni rekebisho muhimu sana. Tunaendelea. Jamani hii hatari kubwa, sasa Katibu nisaidie majina, nitajie Katibu. Haijapata kutokea.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Napenda kutumia Kanuni ya 47(1); Baada ya muda wa maswali kwisha, Mbunge yeyote anaweza kutoa hoja kuwa shughuli za Bunge kama zilivyooneshwa kwenye orodha ya shughuli ziahirishwe

ili Bunge lijadili jambo halisi la dharura na muhimu kwa Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa leo vyombo vya habari vimetangaza kuwa Rais wa Chama cha Walimu ameitisha mgomo rasmi wa walimu nchi nzima tena wasiende kabisa kufundisha mpaka pale ambapo watakapoelewana na Serikali kuhusu suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili ni hatari kubwa kwa Taifa na hii leo pia wako watoto niliwaona wanarejea kutokana na ukosefu wa walimu katika mashule. Kwa hivyo, naomba kutoa hoja Bunge hili lijadili suala hili kuokoa watoto wetu walioko shule.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (Makofi)

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, nimewaona Waheshimiwa Wabunge. Ahsante sana. Sasa kama katika baadhi yenu kuna waliokuwa na *issue* hiyo hiyo ya kuhusiana na mgomo wa walimu basi mtakuwa mmekwishawasilishwa, kama ni mengine basi tuendelee. Sasa nitakutaja jina kama ilikuwa ni *issue* hiyo unajitoa, kama ni jambo jipya unaendelea. Mheshimiwa Mbatia?

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ilikuwa ni *issue* hiyo hiyo, nimejitoa.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Mnyika?

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni suala hilo hilo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Machali?

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni *issue* hiyo hiyo.

**NAIBU SPIKA**: Mheshimiwa Nassari?

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Naomba nisimame kwa kufuata Kanuni ya 68(7): "Halikadhalika Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba Mwongozo wa Spika, kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema ili Spika atoe ufafanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni na taratibu za Bunge na majibu ya Spika yatatolewa papo hapo au baadaye kadri anavyoona inafaa".

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi siku ya Jumamosi wakati tunaendelea na majadiliano, ilitolewa hoja hapa na Mheshimiwa Vita Kawawa ya kumwomba Mheshimiwa Spika, aivunje Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini kwa sababu ya tuhuma ambayo Kamati hii imekumbwa nayo ya rushwa. Kwa mujibu wa vyombo vya habari na mitandao ya kijamii, zipo Kamati kadhaa

ambazo zinatuhumiwa kwa masuala ya rushwa na sio Kamati ya Nishati na Madini pekee yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Mwongozo wako kwamba kwa nini sasa Ofisi yako isiamue kuzivuruga Kamati kadhaa ambazo zinatuhumiwa kwa rushwa ikiwemo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Serikali za Mitaa inayoongwa na Mheshimiwa Mrema, ikiwemo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mashirika Umma inayoongozwa na Mheshimiwa Zitto Kabwe na hii ni kwa sababu Waheshimiwa Wabunge wengi wamekuwa wakizikimbilia zile Kamati ambazo zina mikataba, lakini zile Kamati kwa mfano Kamati ya Maendeleo na Huduma za Jamii ambazo zina umuhimu mkubwa kwenye nchi kwa sababu hazina mikataba au Kamati ya Sheria Ndogo zinakimbiwa.

Kwa hiyo, naomba Mwongozo wako kwamba kwa nini sasa meza yako isiamue kuzivuruga hizi Kamati na hawa Wajumbe wa hizi Kamati wapelekwe kwenye zile Kamati ambazo zinadharaulika ili na wao waweze kujionea hali na wale Waheshimiwa Wabunge ambao wameonekana kwamba wanasimama kupinga rushwa wawekwe kwenye hizi Kamati zenye mikataba ili tuiokoe nchi na janga kubwa la rushwa ambalo imeikumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimwa Silinde?

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ilikuwa ni suala la walimu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Barwany?

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Mimi narudi katika Kifungu cha 68 fasili ya 7, nisome?

**NAIBU SPIKA**: Endelea Mheshimiwa.

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bunge lako Tukufu katika hoja ya Waziri wa Nishati na Madini, Wabunge kadhaa katika mchango wao ndani ya Bunge letu ilikuwa ni shutuma dhidi ya Wabunge ambao wanasemekana wamepokea rushwa kutoka katika kampuni ya Umma ya *TANESCO*. Watanzania kwa jumla huko nje pamoja na Wabunge wana sintofahamu juu ya hilo kwamba Wabunge kadhaa wameshutumiwa juu ya hilo na hapa tayari Kamati ya Maadili imepelekewa hoja juu ya kufanya uchunguzi kuhusu tuhuma hiyo, lakini mpaka sasa Watanzania na Wabunge hatujafahamu hasa ni Wabunge gani ambao wamepelekwa katika Tume hiyo na kufanyiwa uchunguzi huo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Watanzania wana hamu ya kutaka kuwajua Wabunge hawa ambao tayari wana shutuma juu ya jambo hilo. Naomba Mwongozo wako juu ya hilo, Watanzania wanasubiri kwa hamu kujua kinachoendelea. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Keissy!

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nilikuwa pamoja na mawazo ya Mheshimiwa Nassari na Mheshimiwa Baruwany, kwa kuongezea tu. Maana kila tukipita mitaani, hatuna raha Wabunge, tunanyanyaswa na wananchi. Kwa hiyo, naomba na majina yatajwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mawazo yangu pamoja na Mheshimiwa Nassari na Baruwany, lakini naomba na majina yatajwe. Maana kila tukipita barabarani sisi, tunakuwa hatuna raha, tunanyanyaswa, tunadhalilishwa, Bunge lote kwa sababu ya watu wachache. Naomba kuwataja majina hadharani, ili kila mtu afahamu. Wajulikane hao Wabunge wapenda rushwa na ikiwezekana wafukuzwe Bungeni moja kwa moja. *(Makofi)*

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nami natumia Kanuni ya 68(7) kwamba, naomba Mwongozo wako Mheshimiwa Naibu Spika, ni utaratibu gani ambao unaweza kutumika na ambao umekuwa ukitumika kuileta Timu ya Yanga hapa ndani Bungeni, ili tuweze kuipongeza kwa ushindi mkubwa, ulioipatia na sifa nchi yetu. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Najua Mheshimiwa Martha, alitaka kunigusa tu. Mheshimiwa Peter Serukamba!

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuomba tujadili tatizo la Walimu ama kuiomba Serikali, ilete Kauli hapa Bungeni.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Taarifa ambayo nimeipata hivi punde inaeleza kwamba, suala hili la mgogoro wa Walimu, lilipelekwa kwenye kile Chombo cha Usuluhishi *(CMA),* siku ya Ijumaa na wakashindwa kuelewana. Kwa hiyo, Serikali, imepeleka suala la Walimu Mahakamani na leo pande zote zinapeleka *submission* zake na kesho saa 7.00 suala hilo litasikilizwa Mahakamani. Hiyo ndio Taarifa niliyonayo kwa haraka haraka.

Kwa hili la pili, la kuhusiana na masuala ya rushwa, kuhusishwa kwa baadhi ya Wabunge. Hili ni suala zito pia, ni suala kubwa na Wabunge wengi mmelisemea hapa kwa uchungu mkubwa sana kuonesha jinsi ambavyo hamkubaliani kabisa na suala zima la rushwa katika Chombo hiki muhimu sana cha wananchi wa Tanzania. Naiomba Kamati ya Uongozi, Wenyeviti wa Kamati za Bunge, mko hapa wote; naomba mwelekee kule Ukumbi wa Spika, Mheshimiwa Spika, yuko kule. Muweze kulizungumza, halafu baadaye mtanipa maelekezo ya ushauri gani mnatoa kuhusu twende vipi kuhusiana na suala hili la rushwa. Naomba Wenyeviti, muanze kuelekea huko. Ahsante. Katibu!

## HOJA ZA SERIKALI

## Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2012/2013 – Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii

## MWONGOZO WA SPIKA

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mnyaa, ulichelewa rafiki yangu. Haya, Mheshimiwa Mnyaa.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, umeagiza Kamati ya Uongozi kukutana na kwa kuwa, Bunge lako hili, ratiba iliyopo imepangiwa kumalizika tarehe 18 Agosti na kwa kuwa, tarehe 18 Agosti, ndio siku ya kutazama mwezi. kwa hivyo, tunategemea tarehe 19 ndio itakuwa Sikukuu, ambapo Wabunge Waislamu, ndio itakuwa siku waondoke kwenda nyumbani na wengine wanahitaji siku mbili kufika. Kwa kuwa, kuna Jumamosi ya terehe 7 na Jumamosi ya tarehe 14 mwezi wa 8 hazijapangiwa kazi. Kwa hivyo, ningeomba Mwongozo wako kwamba, kwa nini Jumamosi mbili hizo zisitumiwe kikazi, ili Bunge, likaahirishwa mapema, ili Waislam wakapata kuhudhuria Sikukuu?

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Naiomba Kamati ya Uongozi, vile vile itazame ratiba yake kuhusiana na ushauri tulioupata kutoka kwa Mheshimiwa Mnyaa.

Sasa, naomba nimwite Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii. Mheshimiwa Dokta Hussein Mwinyi, Mheshimiwa Waziri wa Afya!

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii iliyochambua Bajeti ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Kazi za Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2011/2012 na Mipango ya

Utekelezaji ya Wizara katika Bajeti ya mwaka 2012/2013. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na ya Mipango ya Maendeleo ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Daktari Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuendelea kutuongoza na kutupatia maelekezo katika utekelezaji wa kazi za Sekta ya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nampongeza kwa kuchukua hatua ya kuhamasisha jamii katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa Malaria na kuiwezesha Tanzania kupata tuzo ya heshima ya *ALMA (African Leaders Malaria Alliance)* ya Umoja wa Viongozi wa Afrika katika kupambana na Malaria.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwa kupitia juhudi za Mheshimiwa Rais, Taasisi ya Mifupa Muhimbili iliwezeshwa na Kundi la Madaktari wa Afrika kupata vifaa vyenye thamani ya Shilingi bilioni tatu (3,000,000,000.00) vilivyoiwezesha Taasisi kuboresha huduma za matibabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais amekuwa mstari wa mbele katika kuhamasisha upimaji wa virusi vya UKIMWI kwa hiari na matumizi ya vyandarua kama njia mojawapo ya kupambana na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI na ugonjwa wa *Malaria*. Pia, namshukuru kwa kuendelea kuiunganisha

Wizara na Taasisi za Kitaifa na Kimataifa ambazo zinasaidia Serikali kuboresha huduma za afya na ustawi wa jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuongoza Tume ya Umoja wa Mataifa ya Taarifa na Uwajibikaji kwa Afya ya Wanawake na Watoto kwa umahiri mkubwa akiwa Mwenyekiti Mwenza, jambo ambalo limeiletea sifa kubwa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ripoti ya Tume hiyo iliyotoa mapendekezo kumi yenye lengo la kupunguza vifo vya wanawake vinavyotokana na uzazi na vifo vya watoto ilizinduliwa Septemba 2011 kwenye Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa. Pia, nampongeza kwa Tuzo tatu alizopokea kipindi cha mkutano huo kutoka kwa wadau mbalimbali kutokana na juhudi zake katika afya ya jamii na afya ya wanawake na watoto kitaifa na Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwapongeze Mheshimiwa Stephen Masato Wasira, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu, kwa Taarifa ya Hali ya Uchumi kwa mwaka 2011 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2012/2013, Mheshimiwa Daktari William Mgimwa, kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Fedha na kuwasilisha Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu kwa hotuba yake inayotoa dira ya jinsi Serikali itakavyotekeleza majukumu yake katika mwaka wa fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niwapongeze pia Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ambaye tunashirikiana kwa karibu katika kutoa huduma za afya na ustawi wa jamii; Mheshimiwa Celina Ompeshi Kombani, kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na kwa hotuba yake nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nawapongeza Mawaziri wapya walioteuliwa na nawashukuru Mawaziri wa Wizara nyingine zote kwa kushirikiana na Wizara yangu na kuchangia katika utoaji wa huduma za afya na ustawi wa jamii. Nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wapya waliochaguliwa na walioteuliwa kuingia katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Pia, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuchangia hotuba zilizotangulia. Michango yao imesaidia kuboresha hotuba yangu. Nawaahidi kwamba, Wizara yangu itazingatia ushauri wao katika kutekeleza majukumu na kazi zilizopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa rambirambi na salamu za pole kwa familia, ndugu na jamaa kwa vifo na majeruhi wa ajali ya meli ya *MV Spice Islander*, iliyotokea katikati ya Visiwa vya Pemba na Unguja tarehe 10 Septemba 2011, mafuriko yaliyotokea Dar es Salaam mwezi Desemba 2011 na ajali ya meli ya *MV. Skagit* iliyotokea tarehe 18 Julai, 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, natoa salamu za pole kwa familia zote zilizopoteza ndugu zao kutokana na ajali za vyombo vya usafiri na ajali nyingine nchini. Namwomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema peponi, Amina. Vile vile, napenda kutoa pole kwa wagonjwa wote waliopo hospitalini na nyumbani, namwomba Mwenyezi Mungu awaponye haraka ili waweze kuendelea kulitumikia Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee napenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii, chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Margareth Simwanza Sitta, kwa ushauri na maelekezo waliyoyatoa wakati wa maandalizi ya Bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba yangu imegawanyika katika maeneo makuu mawili kama ifuatavyo:-

Kwanza ni utekelezaji wa majukumu na malengo kama ilivyoainishwa katika bajeti ya mwaka 2011/12.

Pili ni mipango ya utekelezaji na maombi ya fedha ya bajeti ya Wizara kwa mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utekelezaji wa majukumu na malengo ya Wizara. Majukumu ya Wizara ni:-

(a) Kusimamia utekelezaji wa sera, miongozo, sheria, mipango na mikakati ya utoaji wa huduma za afya na ustawi wa jamii.

(b) Kusimamia na kudhibiti ubora na usalama wa dawa, vifaa, vifaa tiba, vitendanishi, vipodozi na chakula.

(c) Kusimamia utoaji wa huduma za ustawi wa jamii, kinga, tiba na utengamao.

(d) Kusimamia na kuboresha utendaji na kuongeza upatikanaji wa wataalam wa afya na ustawi wa jamii wenye sifa na ujuzi katika ngazi mbalimbali.

(e) Kusimamia huduma za uzazi, mama na mtoto.

(f) Kuongoza na kusimamia Wakala, Taasisi na Miradi iliyo chini ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

(g) Kulinda haki za makundi maalum yanayojumuisha watu wenye ulemavu, watoto yatima na walio katika mazingira hatarishi, wazee wasiojiweza, familia zenye dhiki na watoto walio katika mkinzano na sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya Wizara ni haya yafuatayo:-

(a) Kuboresha huduma, kuzuia na kudhibiti maambukizi ya virusi vya UKIMWI.

(b) Kupunguza magonjwa na idadi ya vifo hasa kwa watoto wachanga na wenye umri chini ya miaka mitano, vijana, watu wenye ulemavu, wanawake walio katika umri wa uzazi na wazee.

(c) Kupanga, kutoa mafunzo na kuongeza idadi ya wataalam wa afya na ustawi wa jamii wenye sifa na ujuzi stahiki kwa kuzingatia usawa wa kijinsia ili kutoa huduma za afya na ustawi wa jamii katika ngazi zote.

(d) Kufuatilia na kudhibiti ubora na usalama wa vyakula, dawa, vifaa tiba, vitendanishi, kemikali na vipodozi ili kulinda afya ya jamii na mazingira.

(e) Kukinga na kudhibiti magonjwa ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza kwa kutoa kipaumbele katika kudhibiti maambukizi ya Virusi vya UKIMWI (VVU) na UKIMWI, Malaria, Kifua Kikuu, magonjwa yatokanayo na lishe duni, na yale yasiyopewa kipaumbele, usafi na afya mazingira.

(f) Kuboresha huduma za ustawi wa jamii kwa makundi yaliyo katika mazingira hatarishi kwa kuhamasisha, kuboresha na kulinda haki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapato na matumizi kwa mwaka 2011/2012. Katika mwaka 2011/2012, Wizara ilikadiria kukusanya kiasi cha sh. 2,965,120,000.00 kutoka katika vyanzo mbalimbali vikiwemo makusanyo yatokanayo na uchangiaji wa gharama kutoka kwenye vyuo vya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, usajili wa hospitali na maabara binafsi. Hadi mwezi Juni 2012, Wizara iliweza kukusanya kiasi cha sh.

3,405,750,813.39 sawa na asilimia 105 ya makadirio ya mwaka. Fedha hizi zilitumika kulingana na taratibu zilizopo ikiwemo kuboresha utoaji wa huduma katika maeneo zilipokusanywa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara ilitengewa kiasi cha sh. 219,367,376,000.00 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, sh. 121,208,124,100.00 zilitengwa kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Taasisi zilizo chini yake na kiasi cha shilingi 98,159,251,900.00 kilitengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi tarehe 30 Juni, 2012, Wizara ilikuwa imeongezewa jumla ya shilingi 28,380,826,709.00 kwa ajili ya mishahara.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, kuongeza fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida kuwa sh. 247,748,202,709.00 ambapo sh. 149,588,950,809.00 zilikuwa kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Taasisi zilizo chini yake, na sh. 98,159,251,900.00 kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi tarehe 30 Juni, 2012, Wizara ilipokea toka Hazina sh. 243,342,754,261.00 kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ambapo kati ya fedha hizo, sh. 149,558,950,809.00 zilitumika kulipa mishahara ya wafanyakazi na sh. 93,753,803,452.00 zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu matumizi kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Katika mwaka 2011/12, Wizara iliomba kiasi cha sh. 364,794,487,000.00 kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha

hizo sh. 9,873,761,000.00 zilikuwa ni fedha za ndani na sh. 354,920,726,000 00 ni kutoka kwa Taasisi za Kimataifa na Wadau wa Maendeleo wanaochangia Mfuko wa Pamoja wa Afya na wale walioko nje ya Mfuko. Kati ya fedha kati ya fedha kutoka vyanzo vya nje, shilingi 72,622,982,000.00 zilitoka kwa wadau wa maendeleo wa Mfuko wa Pamoja na sh. 282,297,744,000.00 zilitoka kwa wadau wa maendeleo walio nje ya Mfuko wa Pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi tarehe 30 Juni, 2012 Wizara ilipokea kiasi cha sh. 289,386,641,872.00 kutoka Hazina kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo kiasi cha sh. 274,610,141,872.00 ni kutoka vyanzo vya nje na kiasi kilichobaki cha sh. 14,776,500,000.00 kutoka vyanzo vya ndani. Kiasi cha sh. bilioni 4.9 kilichoongezeka kilitolewa na Serikali kwa ajili ya kukamilisha jengo la Taasisi ya Saratani *Ocean Road* na ununuzi wa vifaa kwa ajili ya upasuaji wa moyo katika Hospitali ya Taifa Muhimbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2011/2012. Katika mwaka 2011/2012, Wizara yangu imetekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025), Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12 – 2015/16), Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini II (2010), Sera ya Afya (2007), Mpango Mkakati wa III wa Sekta ya Afya (2009 – 2015), Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (2007 – 2017) na Malengo ya Milenia. Aidha, katika kipindi hiki, Wizara imeendelea kutekeleza mipango na majukumu pamoja na

malengo yaliyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala ya mwaka 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo yaliyotekelezwa ni haya yafuatayo:-

Utawala na Rasilimali Watu. Katika mwaka 2011/2012, Wizara iliendelea kutekeleza Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM) 2007 - 2017 kwa kuongeza idadi ya wanafunzi watarajali waliodahiliwa katika vyuo vya afya kutoka 4,296 mwaka 2008 hadi 7,458 mwaka 2011. Hili ni ongezeko la wanafunzi 3,162 sawa na asilimia 57.6. Lengo ni kudahili wastani wa wanafunzi 10,000 kwa mwaka ifikapo mwaka 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kupitia fedha za Mfuko wa Dunia *(Global Fund)* kampasi za Waganga Wasaidizi Mtwara, Chuo cha Uuguzi Bagamoyo, St Bhakita na Hurbert Kairuki zilifanyiwa ukarabati wa miundombinu na kupanuliwa ili kuongeza idadi ya wanafunzi wanaodahiliwa. Vile vile, magari 16 yalinunuliwa na kusambazwa katika Vyuo vya Uuguzi Mbozi, Mtwara, Same, Mirembe, Mpanda, Nachingwea, Kibondo, Bagamoyo, Mkomaindo na Vyuo vya Sayansi Shiriki Kigoma, Mbeya, Ifakara, Muheza, Tanga pamoja na Chuo cha Ustawi wa Jamii Kisangara na Chuo cha Mafunzo ya Masafa – Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikiongeza idadi ya wahitimu katika sekta ya afya ili kukidhi mahitaji ya watumishi kama yalivyoainishwa katika MMAM. Katika kipindi cha 2008 hadi 2011, idadi

ya wahitimu imeongezeka kutoka wahitimu 3,744 hadi 5,173, kwa ngazi mbalimbali za afya zikiwemo cheti, stashahada na shahada, ongezeko ambalo ni sawa na asilimia 27.6.

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi la kuajiri watumishi pamoja na kuwapanga kwenye mamlaka mbalimbali za ajira ikijumuisha Halmashauri, Tawala za Mikoa na Wizara kwa ajili ya ajira mpya lilifanyika. Hii ilisababisha kuwa na ongezeko la nafasi zilizoidhinishwa kutoka 5,241 (2008/09) hadi 9,391 (2011/12). Aidha, idadi ya wataalam waliopangwa iliongezeka kutoka 3,010 (2008/09) hadi 7,028 (2011/12).

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na idadi tajwa, idadi ya watumishi waliopangwa katika mamlaka mbalimbali imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka. Idadi halisi ya waliopangwa inaonekana kuwa ndogo ikilinganishwa na kibali kilichotolewa, hii inatokana na tatizo la upatikanaji wa wataalam katika soko la ajira. Wizara inaendelea na jitihada za kuongeza idadi ya wanafunzi katika vyuo vya mafunzo ya afya kwa lengo la kupata wataalam wa afya wengi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara ilipata kibali cha kuajiri watumishi 260 wa kada ya afya kwa ajili ya kufanya kazi katika vituo mbalimbali vilivyo chini ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Hadi Juni, 2012 jumla ya watumishi 198 waliajiriwa na kupangiwa vituo vya kazi. Aidha, katika kuboresha na kusimamia maslahi na haki za watumishi wake, Wizara iliwaingiza kwenye orodha ya malipo ya

mshahara watumishi 113 wa ajira mpya. Vile vile, watumishi 282 walirekebishiwa mishahara yao. Wizara pia, ilifanyia kazi majalada 62 ya wastaafu, majalada 195 ya malimbikizo ya mishahara ya watumishi na majalada 25 ya watumishi ambao walikuwa hawajalipwa mishahara na taarifa kuwasilishwa Hazina kwa ajili ya malipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/12, Wizara iliandaa moduli 46 kwa lengo la kuboresha mafunzo ya nadharia na vitendo. Kati ya moduli hizo 23 ni kwa ajili ya mafunzo ya nadharia, 14 ni kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo na tisa ni kwa ajili ya mafunzo kwa njia ya masafa. Aidha, vyuo vya afya 37 kati ya 135 vipo katika hatua mbalimbali za kupata ithibati kutoka Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, Wizara ilikamilisha mapitio ya mitaala mitano ya kada za Watunza Kumbukumbu za Magonjwa ya Binadamu, Tabibu Kinywa na Meno, Fiziotherapia katika ngazi ya stashahada na Uuguzi- Afya ya Jamii na Watoto katika ngazi ya shahada. Mapitio hayo yalifanyika ili kuendana na vigezo vinavyohitajika na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi vinavyolenga kuinua umahiri wa mwanafunzi awapo mafunzoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara iliimarisha Mfumo wa kukusanya takwimu za rasilimali watu katika Sekta ya Afya katika mikoa. Aidha, Kiwango cha taarifa za watumishi wa sekta ya Afya na Ustawi wa Jamii kutoka ngazi zote zilizokwishaingizwa katika mfumo ni asilimia 75. Vile vile,

taarifa kutoka katika Vyuo vya Mafunzo ya Afya zimeingizwa katika mfumo wa taarifa za vyuo kwa kiwango cha asilimia 84. Wizara pia, iliandaa Mwongozo wa matumizi bora ya takwimu zitokanazo na mfumo huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara ilikamilisha rasimu ya ikama ya watumishi wa afya na ustawi wa jamii. Ikama hiyo imehuishwa na Mwongozo wa utoaji wa huduma muhimu za afya na ustawi wa jamii kwa lengo la kuoanisha huduma zinazotolewa na idadi ya wataalam wanaohitajika kutoa huduma husika. Aidha, Mwongozo wa utekelezaji wa elimu ya masafa katika ngazi zote za utekelezaji uliandaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, mtaala wa mafunzo ya muda mfupi ya kuwawezesha Waganga Wasaidizi Vijijini *(Rural Medical Aid)* kujiendeleza kuwa Maafisa Tabibu uliandaliwa pamoja na moduli za kufundishia masomo kwa njia ya masafa. Pia, Wizara ilitoa mafunzo kwa wakufunzi 45 wanaoratibu na kusimamia mafunzo ya masafa vyuoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara ilikasimu utaratibu wa kupokea maombi ya kujiunga na vyuo vya mafunzo ya afya katika Kanda zote nane za Mafunzo. Lengo la kukasimu utaratibu huo ni kusogeza fursa kwa waombaji kutoka sehemu mbalimbali nchini kujiunga na vyuo. Aidha, matangazo ya kujiunga na mafunzo yalitolewa katika ofisi za Waganga Wakuu wa Mikoa na Wilaya, vyombo vya habari na katika tovuti ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Sera na Mipango. Katika mwaka 2011/2012, Wizara iliandaa rasimu ya Sera ya Taifa ya Huduma za Ustawi wa Jamii na kuiwasilisha Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri. Aidha, Wizara iliendelea kuandaa Mpango Mkakati wa Ugharamiaji Huduma za Afya. Uandaaji wa Mpango huo ulihusisha kufanya tafiti mbalimbali zinazolenga kujua gharama halisi za huduma ya afya. Tafiti hizo zilifanyika katika mikoa ya Kilimanjaro, Iringa, Mbeya, na Shinyanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, Wizara ilifanya na kukamilisha uchambuzi wa vyanzo na matumizi mbalimbali ya fedha katika Sekta ya Afya *(National Health Accounts* - 2009/2010). Matokeo ya uchambuzi huo yanaonesha kuwepo kwa ongezeko kubwa la matumizi ya fedha kwa ajili ya huduma za afya kwa mtu binafsi *(out of pocket expenditure)* kutoka asilimia 25 mwaka 2005/06 hadi 32 kwa mwaka 2009/2010. Hii inaonesha umuhimu wa Serikali kuwa na ajenda ya kudumu ya uhamasishaji wananchi kujiunga na bima ya afya na mifuko ya afya ya jamii ili kupunguza matumizi ya fedha taslimu mtu anapohitaji huduma za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti ya Sekta ya Afya imekuwa ikiongezeka mwaka hadi mwaka, kutoka shilingi bilioni 520 mwaka 2006/2007 hadi trilioni 1.2 mwaka 2012/2013. Kulingana na kielelezo tajwa, kiasi kilichotengwa kwa ajili ya Sekta ya Afya kwa mwaka 2012/2013 ni sawa na asilimia 10.4 ya bajeti kuu ya Serikali. Aidha, katika kutekeleza Sera ya ugatuaji wa

madaraka kwenda ngazi ya Mikoa na Halmashauri, kumekuwa na ongezeko la uwiano wa rasilimali fedha zinazotengwa chini ya Mikoa na Halmashauri ikilinganishwa na fedha zinazotengwa chini ya Wizara Makao Makuu. Katika mwaka 2012/2013, asilimia 55 ya fedha zimetengwa chini ya Mikoa na Halmashauri, ikilinganishwa na asilimia 36 zilizotengwa mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ufuatiliaji na tathmini. Katika mwaka 2011/2012, Wizara iliendelea kuboresha Mfumo wa Takwimu na uendeshaji wa Huduma za Afya nchini (MTUHA), kwa kufanya mapitio ya vitabu vya ukusanyaji wa taarifa za afya *(health registers)* na kuanzisha programu ya kielektroniki inayojulikana kama *District Health Information Software (DHIS)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la kuboresha mfumo huu ni kurahisisha upatikanaji wa takwimu sahihi za afya na kwa wakati. Aidha, zoezi la kupeleka mfumo huu kwenye mikoa mingine ulianza kwa kusambaza vitabu na kufunga mfumo wa kielektroniki katika Mikoa ya Mtwara, Lindi, Dar es Salaam, Shinyanga na Dodoma kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na wadau wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara iliendelea na uraghibishi wa jamii kuhusu Sera ya Afya ya mwaka 2007 hususan Mabadiliko katika Sekta ya Afya na Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi-MMAM (2007 – 2017) kupitia vipindi 42 vya redio na runinga kuhusu

Mabadiliko katika Sekta ya Afya. Vipindi hivyo vinaendelea kutangazwa kupitia kipindi cha Afya Mambo Mapya kinachotangazwa na *TBC* Taifa kila wiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara iliendelea na usambazaji wa nakala za vitabu vinavyoelezea na kuhamasisha kuhusu Sera ya Afya, Mpango Mkakati wa Tatu *(HSSP III)* na MMAM katika Halmashauri kwa lengo la utoaji elimu na uhamasishaji wa ushiriki wa wananchi katika Halmashauri zao. Wizara pia, imetoa muhtasari wa kitabu cha MMAM, kilichofanyiwa tafsiri kwa lugha rahisi ya Kiswahili kwa wananchi katika wilaya, mikutano na maonesho mbalimbali ambapo vitabu 2,500 vilisambazwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara iliendelea kutoa elimu kuhusu mabadiliko katika Sekta ya Afya na utekelezaji wa MMAM kwa wadau wa Halmashauri za Wilaya za Longido, Siha, Rorya, Nanyumbu na Halmashauri ya Mji wa Kibaha. Hii itawawezesha kuandaa na kuridhia Hati Rasmi na Sheria ndogo ya uundaji wa Bodi za Afya za Halmashauri na Kamati za Vituo vya kutolea huduma za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/12, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, iliendelea kusimamia, kufuatilia na kutoa ushauri wa kupanga na kutekeleza Mipango Kabambe ya Afya ya Halmashauri katika Halmashauri 132 nchini. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi hiyo pamoja na Wataalam kutoka *University Computing Center (UCC)*

ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Halmashauri zenyewe ilifanya mafunzo ya matumizi ya Mfumo wa kutumia *PlanRep3* na Mwongozo wa Uandaaji Mipango Kabambe ya Afya ya Halmashauri nchini. Kila Halmashauri ilitoa wataalam sita (6) kutoka Timu ya Uendeshaji ya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na wadau wengine ilifanya mapitio ya 12 ya Sekta ya Afya. Mkutano huo ulijadili mafanikio yaliyopatikana kwa mwaka 2010/2011. Changamoto zilizojitokeza ni pamoja na upungufu wa rasilimali watu; upatikanaji wa dawa, upungufu wa rasilimali fedha kulingana na mahitaji. Kupitia mkutano huo wadau kwa pamoja walikubaliana mikakati ya kukabiliana na changamoto hizo, ipewe kipaumbele katika bajeti ya mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara ilifuatilia utekelezaji wa majukumu ya Bodi na Kamati za Afya katika Halmashauri 60 zilizoanzisha vyombo hivyo. Matokeo yake ilionekana kuwa vyombo hivyo vinatekeleza majukumu yake kulingana na Hati Rasmi na wananchi wamehamasika katika kuchangia huduma za afya ambapo hadi mwezi Machi 2012 kaya 614,328 zilikuwa zimejiunga na Mifuko ya Afya ya Jamii ikilinganishwa na kaya 457,731 zilizokuwa zimejiunga mwaka 2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano. Katika mwaka 2011/2012, Wizara ilianzisha

mfumo wa huduma za tiba kwa njia ya mtandao *(Telemedicine)* katika Taasisi ya Saratani ya *Ocean Road*. Mfumo huu umeunganisha Taasisi na baadhi ya hospitali za nchini India na kuwezesha wataalam wa hapa nchini kuwasiliana na wataalam bingwa wa tiba nchini India na kupata miongozo kuhusu uchunguzi, tiba na mafunzo ya magonjwa mbalimbali. Mipango ya kupanua wigo wa huduma hii katika hospitali nyingine umeanza na vifaa kwa ajili ya mfumo huu vimepelekwa katika baadhi ya hospitali ikiwemo Hospitali ya Taifa Muhimbili, Tumbi, Temeke, Amana na Bagamoyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara iliandaa Mpango wa Ununuzi na Ugavi wa mwaka, ambao ulitekelezwa kwa kukamilisha taratibu mbalimbali za ununuzi, ikiwemo kuingia mikataba 75 ya vifaa *(goods)*, mitatu ya ujenzi *(works)*, 15 ya huduma za ushauri *(consultancy)* na 36 ya huduma nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Usimamizi wa Fedha. Katika mwaka 2011/2012, Wizara ilianzisha mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji wa taarifa za mapato na matumizi ya fedha kwa miradi misonge ambayo ni Mradi wa Kifua Kikuu, UKIMWI na Malaria. Mfumo huu unawezesha kutoa ripoti kwa wakati kulingana na mahitaji, hivyo utatumika pia kwenye miradi mingine. Aidha, Hospitali za Rufaa Mbeya na *KCMC* zimeanza kutumia mifumo ya aina hiyo katika shughuli mbalimbali za ukusanyaji wa taarifa za hospitali; zikiwemo taarifa za fedha, huduma za wagonjwa pamoja na za kiutawala.

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi hili litaendelea hatua kwa hatua katika hospitali nyingine kulingana na upatikanaji wa fedha. Vile vile, Wizara iliendelea kuimarisha mifumo ya ndani ya udhibiti katika usimamizi wa rasilimali watu, fedha na usalama wa mali za Serikali kwa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo mbalimbali. Pia, Wizara imeendelea kuboresha Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani kwa kutoa mafunzo kwa wataalam na kununua vitendea kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/12, Wizara iliendelea kushirikiana na vyombo vya habari vyote nchini katika kutoa taarifa na kuelimisha wananchi kuhusu masuala ya afya na ustawi wa jamii kupitia radio, magazeti, televisheni pamoja na mitandao ya habari ya kijamii. Aidha, Wizara ilitoa tahadhari na taarifa za magonjwa ya mlipuko kila yalipojitokeza ikiwemo ugonjwa wa Kipindupindu, kuharisha kwa watoto wadogo na Surua. Wananchi walihamasishwa kuhusu umuhimu wa kuwapeleka watoto kupata chanjo ya Surua na dawa ya minyoo kwenye kampeni iliyoendeshwa nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuelimisha wananchi kuelewa masuala mbalimbali yanayohusu huduma za afya na ustawi wa jamii, Wizara iliandaa vipindi na kutoa ufafanuzi kwenye vyombo vya habari kuhusu matumizi ya njia za uzazi wa mpango na maambukizi ya virusi vya UKIMWI, chanjo, Malaria, Kifua Kikuu na Ukoma, usafi wa mazingira, sheria ya mtoto na huduma ya malezi ya kambo na kuasili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Huduma za Kisheria. Katika mwaka 2011/2012, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, iliandaa Kanuni za Sheria mbalimbali zinazosimamiwa na Wizara ambazo ni Kanuni za Sheria ya Afya ya Jamii ya Mwaka 2009, Kanuni za Sheria ya Famasia ya Mwaka 2010, Kanuni za Sheria ya Mtoto ya Mwaka 2009 na Kanuni za Sheria ya Usajili wa Wataalam wa Afya Mazingira ya mwaka 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliandaa mikataba mbalimbali ya ushirikiano na taasisi mbalimbali za Kitaifa na Kimataifa na ilisimamia utekelezaji wake katika sekta ya afya na Ustawi wa Jamii. Vile vile, Wizara ilitoa nakala za Sheria za Afya na Ustawi wa jamii ambazo katika mwaka wa Fedha 2012/2013 zitasambazwa kwa watendaji husika kwa lengo la kuwapa uwezo wa kuzisimamia na kuzitekeleza sheria hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Maabara ya Kitaaluma. Katika mwaka 2011/2012, Wizara kwa kushirikiana na Baraza la Madaktari iliandaa Mfumo wa Taarifa wa Kompyuta ambao utatumika katika kuingiza taarifa za Madaktari wote nchini. Aidha, Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania liliendesha mafunzo ya maadili kwa Wauguzi na Wakunga 286 na kuwajengea uwezo pamoja na kuwakumbusha masuala ya uadilifu katika taaluma.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, Baraza la Wauguzi na Wakunga limekamilisha maandalizi ya

kuanzisha mtihani wa usajili utakaosaidia kujiridhisha na ubora wa wahitimu wa taaluma wanaotoka katika vyuo mbalimbali. Pia, Baraza lilihakiki vyeti vya taaluma vya wauguzi pamoja na vyeti vya elimu ya sekondari kwa wanafunzi wanaojiunga na mafunzo ya uuguzi na ukunga ili kujiridhisha na uhalali wa vyeti hivyo. Vyeti 7,746 vilihakikiwa na kati ya hivyo 1,209 sawa na asilimia 13.5 vilibainika kuwa ni vyeti vya kughushi, ambapo wahusika wote waliondolewa vyuoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara kwa kushirikiana na Baraza la Famasi lilifanya ukaguzi wa vituo vyote vinavyotoa mafunzo kwa vitendo katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mbeya, Mwanza, Tanga, Arusha na Kilimanjaro. Aidha, Baraza liliendelea kusajili wafamasia waliohitimu masomo yao nje na ndani ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Baraza lilifanya ukaguzi wa maduka ya dawa na famasi za hospitali katika mikoa ya Mbeya, Manyara, Dar es Salaam kwa lengo la kuhakikisha kuwa huduma zitolewazo zinakidhi matakwa ya kitaalamu. Katika ukaguzi huu maduka 24 kati ya 106 yaliyokaguliwa yalifungwa kutokana na kukiuka taratibu za uendeshaji huduma hii, ikiwepo uchafu wa kukithiri, watoa huduma kutovaa sare ya kazi, kutokuwa na wataalam na kutokuwa na vitabu vya kutunza kumbukumbu za dawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wamiliki waliagizwa kurekebisha mapungufu haya kabla ya kuruhusiwa kuendelea kutoa huduma. Wizara pia, ilitoa elimu kwa wadau na asasi mbalimbali kuhusu Sheria ya Famasi

Namba 1 ya mwaka 2011 ili ieleweke na kutekelezwa kwa ufanisi. Uhamasishaji kwa wafamasia ulifanyika ngazi ya mkoa katika kanda zote na katika Wilaya za mikoa ya Mbeya, Ruvuma, Iringa, Tabora, Rukwa, Mtwara, Pwani, Kigoma, Singida, Dodoma, Lindi na Mwanza ili wajisali. Jumla ya Wafamasia 267 wa hospitali za Wilaya na Mikoa walipata mafunzo kuhusu majukumu ya Baraza kama yalivyoainishwa kwenye sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara ilikamilisha Mwongozo wa Viwango vya Elimu kwa Vyuo vya Famasi pamoja na kuusambaza kwa wadau mbalimbali ikiwa ni njia ya kuwahamasisha ili waweze kushiriki katika kuanzisha vyuo vipya vya famasi kwa lengo la kuongeza idadi ya wataalam.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo huo ulisambazwa vyuo vya Bugando, *KCMC*, Iringa, Dar es Salaam na vyuo vinavyomilikiwa na watu binafsi. Aidha, Baraza lilikamilisha tovuti ya Baraza pamoja na mfumo wa kuhifadhi takwimu kielektroniki na hivi sasa unafanya kazi vizuri. Tovuti ya Baraza ni *www.pharmacycouncil.go.tz*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara kupitia Baraza la Radiolojia ilisajili Wataalam wa Radiolojia 229, kati ya maombi 250. Katika hao 157 walipata usajili kamili *(full registration)*, 37 waliandikishwa *(enrolled)* na *interns* 20 walipata usajili kwa ajili ya kuwawezesha kufanya mafunzo kwa vitendo *(provisional registration - internship)*. Aidha,

wataalam sita walipata usajili wa 27 muda *(Temporary Registration)* unaotolewa kwa wataalam wageni na wataalam tisa waliorodheshwa kama wataalam wa *ultrasound.*

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, Baraza kwa kushirikiana na Mabaraza ya Radiolojia katikannchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, liliandaa mwongozo wa pamoja wa kukagua vyuo vya Radiolojia. Pia, Baraza kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Mionzi linaendelea kuandaa mwongozo wa ubora wa huduma za Radiolojia na usalama wa mionzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/12, Wizara kupitia Baraza la *Optometria* ilikamilisha rasimu ya Mwongozo wa Wataalam wa Kurekebisha Upeo wa Macho Kuona. Aidha, Baraza lilitayarisha vijarida vilivyojumuisha Sheria, Kanuni, Maadili na Miiko ya Wataalam wa Kurekebisha Upeo wa Macho Kuona na kusajili Wataalam 271 na kuorodhesha wasaidizi 26 kwa mujibu wa Sheria ya *Optometria* Na. 12 ya mwaka 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Wizara kupitia Baraza la Kusajili Wataalam wa Afya Mazingira iliandaa Kanuni za Usajili wataalam wa Afya Mazingira ambazo zilitangazwa katika Gazeti la Serikali Na. 388 la tarehe 25 Novemba, 2011. Pia, Baraza lilisajili Watalaam wa Afya Mazingira 26 waliotimiza vigezo kati ya 36 walioomba 28.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/12, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ilisajili waganga na

wakunga wa tiba asili 1,570, wasaidizi wao 84 na waganga wa tiba mbadala saba. Aidha, waratibu ngazi ya Halmashauri na Mikoa wa Mikoa ya Ruvuma, Iringa, Mbeya, Rukwa, Arusha, Manyara, Kilimanjaro na Tanga walipata mafunzo kuhusu usajili, sheria, kanuni na miongozo ya tiba asili na tiba mbadala. Vile vile, Bodi ya Ushauri ya Hospitali Binafsi iliendelea kusajili vituo binafsi vya kutolea huduma za afya. Pia, Bodi ilifanya ukaguzi katika vituo 70 vya kutolea huduma za afya ya kinywa katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara kupitia Bodi ya Maabara Binafsi za Afya ilitoa vibali vya kufungua maabara mpya 30 na maduka yanayouza vifaa vya maabara 27. Aidha, Bodi ilikagua Jumla ya Maduka 38 yanayouza vifaa na Vitendanishi vya Maabara katika Mkoa wa Dar es Salaam na Maabara binafsi 116 katika mikoa mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, Bodi ilikagua maduka 38 yanayouza vifaa na vitendanishi vya maabara katika Mkoa wa Dar es Salaam. Matokeo yake maduka 14 yalibainika kuwa na kasoro ndogo ndogo ambazo Wamiliki 29 wake walipewa ushauri kuzirekebisha. Pia, Bodi ilikagua mizigo 572 ya vifaa na vitendanishi vya Maabara na Bodi ilifanya tathmini ya ubora wa Vifaa na Vitendanishi ambapo vyote vilikidhi viwango vinavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma za kinga, Epidemiolojia na Udhibiti wa Magonjwa katika mwaka 2011/2012, Wizara ilifuatilia mwenendo na viashiria vya

milipuko ya magonjwa pamoja na kudhibiti magonjwa ya milipuko kwa kufanya ufuatiliaji wa karibu wa magonjwa ya kuambukiza na yale yasiyoambukiza katika maeneo mbalimbali nchini. Aidha, Wizara iliendelea kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa wataalam 11 na muda mfupi kwa wataalam 80 juu ya kukabiliana na magonjwa ya kuambukiza na yasiyoambukiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, Wizara iliendelea kushikiriana na wadau mbalimbali pamoja na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi katika kufuatilia na kukabiliana na magonjwa yanayohusisha sekta zaidi ya moja kama vile Kichaa cha Mbwa, Mafua ya Ndege, Tauni na Kimeta kwa kuzingatia utekelezaji wa kanuni za afya za Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Malaria Wizara iliendelea kutekeleza Mpango Mkakati wa Kudhibiti Malaria 2008 – 2013 kwa kununua na kusambaza dawa ya mseto ya malaria nchini na kutoa huduma ya upimaji wa vimelea vya malaria kwa kutumia vipimo vinavyotoa majibu haraka *(rapid diagnostic test)* katika mikoa 15. Jumla ya dozi 9,196,080 za dawa ya mseto na vitendanishi 7,379,225 vilinunuliwa na kusambazwa nchini. Aidha, mafunzo ya kutumia vipimo vinavyotoa majibu haraka yalifanyika katika mikoa iliyobaki ya Shinyanga, Kigoma, Tabora, Tanga, Kilimanjaro na Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipimo hiki kimechangia kwa kiasi kikubwa kupunguza matumizi ya dawa za kutibu Malaria hususan kwa wale waliokuwa

wanatumia dawa bila kupima. Vile vile, kupitia mpango wa Hati Punguzo kwa akina mama wajawazito na watoto wachanga, Kampeni ya Kusambaza Vyandarua katika Malazi na Kampeni ya Kusambaza Vyandarua kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano, jumla ya vyandarua 34,477,173 vimewafikia wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/12, Wizara iliendesha kampeni ya ugawaji vyandarua kwa wote *(universal coverage*) ambayo ilikamilika 31 mwezi Oktoba mwaka 2011. Katika kampeni hiyo jumla ya vyandarua 17,617,891 viligawiwa katika sehemu za malazi kwa kila kaya katika mikoa yote Tanzania Bara, bila malipo. Aidha, Wizara ilisambaza jumla ya vyandarua vya hati punguzo vyenye viuatilifu 5,412,579 kwa wanawake wajawazito na vyandarua 2,693,265 kwa watoto wenye umri chini ya mwaka mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, dawa ya ukoko *(Indoor Residual Spray)* yenye viuatilifu ya kuua mbu ndani ya nyumba iliendelea kupulizwa katika wilaya 18 za Mikoa ya Kagera, Mara na Mwanza, ambapo jumla ya kaya 1,175,792 zenye jumla ya watu 7,252,914 zimenyunyiziwa viuatilifukwa ajili ya kuzuia maambukizi ya ugonjwa wa malaria katika mikoa hiyo. Unyunyiziaji huo umeweza kuzuia milipuko ya malaria iliyokuwa inatokea katika wilaya hizo siku za nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara iliendelea kutekeleza Mpango wa kuangamiza viluwiluwi vya mbu waenezao malaria

katika mazalio yao *(larviciding)*, kwa kushirikiana na Wataalam kutoka nchi ya Cuba. Mpango huo unatekelezwa katika kata zote 90 za Mkoa wa Dar es Salaam na 32 utaendelezwa katika mikoa mingine kwa awamu. Aidha, iliendelea kusambaza na kutoa huduma ya upimaji wa vimelea vya malaria kwa kutumia vipimo vinavyotoa majibu haraka *(rapid diagnostic test)* katika mikoa 18. Mafunzo kwa ajili ya Mikoa 3 iliyobaki ya Tanga, Kilimanjaro na Morogoro yatafanyika kupitia fedha za *Global Fund*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara iliendeleza mradi wa upatikanaji wa dawa mseto ya kutibu malaria kwa bei punguzo *(Affordable Medicine Facility – Malaria – AMFm)* isiyozidi shilingi 500.00 kwa dozi ya mtoto na shilingi 1,000.00 kwa dozi ya mtu mzima, katika sekta binafsi. Hadi mwezi Mei, 2012 jumla ya dozi milioni 27.1 za dawa, ziliagizwa na kati ya hizo, dozi milioni 20.1 ziliingizwa nchini, chini ya mradi huo. Mradi huu ambao ulikuwa ni wa majaribio, utakamilika ifikapo Desemba 2012. Mpango wa Kudhibiti Kifua Kikuu na Ukoma

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/12, Wizara iliimarisha hatua mbalimbali za kudhibiti maambukizi shirikishi ya Kifua Kikuu na UKIMWI. Hii ni pamoja na kuchunguza asilimia 90 ya wagonjwa wa kifua 33 kikuu nchini kote kama wanayo maambukizi ya VVU na kuanza kutoa dawa ya kuzuia Kifua Kikuu kwa watu wanaoishi na VVU katika wilaya 18 za awali. Vifo vitokanavyo na Kifua Kikuu vimepungua kutoka asilimia 8 mwaka 2006 hadi asilimia 4.9 mwaka 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara iliimarisha huduma za maabara kwa kuongeza idadi ya vituo vya maabara za uchunguzi kutoka 720 hadi 900 kwa kushirikisha sekta binafsi. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ilisambaza aina mpya za hadubini kutoka 82 hadi 133 za kugundua Kifua Kikuu katika ngazi ya wilaya na mkoa. Wizara iliimarisha mafunzo ya Fundi Sanifu Maabara kwa kuwafundisha wataalam wa maabara 95 kutoka mikoa yote jinsi ya kugundua vimelea sugu vya Kifua Kikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, Wizara iliendelea kuimairisha huduma za uchunguzi wa Kifua Kikuu sugu kwa njia ya maabara katika hospitali maalum ya Kifua Kikuu Kibong'oto. Hadi mwezi Machi 2012, jumla ya wagonjwa 45 waligundulika kuwa Kifua Kikuu sugu na kuanza matibabu na hivyo kufikisha idadi ya wagonjwa wote waliokwisha kutibiwa kufika 87 tangu mwaka 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara ilianza utafiti wa kwanza wa kitaifa wa kutathmini kiwango cha Kifua Kikuu nchini katika mikoa yote ya Tanzania Bara na miwili ya Zanzibar. Utafiti ulianza rasmi Desemba 2011 na hadi mwishoni mwa Mei 2012, utafiti huu umekamilika katika mikoa 10 ya Arusha, Dar es Salaam, Kagera, Kilimanjaro, Manyara, Mara, Morogoro, Mwanza, Pwani na Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara ilitibu wagonjwa wa Ukoma 2,361 kati yao watoto chini ya miaka 14 walikuwa ni 124

sawa na asilimia tano. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali iliendelea kufanya kampeni za kuhamasisha wananchi wanaoishi kwenye maeneo yenye uambikizo mkubwa kujitokeza kufanyiwa uchunguzi. Katika mkoa wa Dar es Salaaam watu 13 walipatikana kuwa na ugonjwa wa Ukoma. Vilevile, Wizara iliendelea kutoa huduma za uraghibishi kwa watu wenye ulemavu utokanao na Ukoma ambapo waathirika 59 walipatiwa huduma za upasuaji, viatu maalum jozi 3,036 na miguu bandia 57 ilitolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI, idadi ya wananchi waliojitokeza kupima virusi vya UKIMWI imeongezeka kutoka watu milioni 16,626,830 mwezi Desemba 2011 hadi 17,008,475 mwezi Machi 2012. Aidha, idadi ya wagonjwa wanaopata dawa za UKIMWI iliongezeka kutoka 412,108 mwezi Desemba 2011 hadi 564,723 mwezi Machi 2012, ambapo asilimia 7.6 kati yao ni watoto chini ya miaka 15. Vilevile, vituo vya kutolea huduma za Afya 1,100 vilitoa huduma ya matunzo na tiba kwa watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, idadi ya wagonjwa wanaopata dawa za UKIMWI iliongezeka kutoka wagonjwa 388,947 Machi 2011 hadi 564,723 mwezi Machi 2012, ikilinganishwa na lengo la wagonjwa 478,000. Pia, katika kipindi hicho Wizara ilisambaza mashine 232 kwa ajili ya kupima *CD4*. Wizara ilisambaza vitabu 1,500 vya miongozo ya kufundishia masuala ya UKIMWI mahali pa kazi kwa wafanyakazi

wa sekta ya afya, wadau na Halmashauri zote nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu afua ya tohara kwa wanaume ilipoanzishwa na Wizara mwaka 2009, jumla ya wanaume waliopatiwa tohara ilifikia 164,599 mwezi Machi 2012 katika mikoa iliyokuwa imetambulika kuwa na kiwango kikubwa cha maambukizi ya VVU na kiwango cha chini cha tohara kwa wanaume. Mikoa hiyo ni Shinyanga, Tabora, Rukwa, Mbeya, Kagera, Iringa, Mara (Rorya) na Mwanza. Aidha, Wizara ilifanya kampeni za kuhamasisha tohara kwa wanaume ambayo inakadiriwa kupunguza maambukizi ya VVU kwa asilimia 60.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, mafunzo ya namna ya kufanya tohara kwa wanaume yalitolewa kwa watoa huduma 213 na kufanya idadi hiyo kufikia 591 mwezi Machi 2012. Vituo vya kutolea huduma viliongezeka kufikia 42 katika mikoa hiyo minane. Lengo ni kutoa huduma ya tohara kwa wanaume milioni 2.8 itakapofika mwaka 2015 kwa kuzingatia Mkakati wa Taifa wa Kuongeza Huduma za Tohara kwa Wanaume kwa ajili ya kuzuia maambukizi ya VVU wa mwaka 2010 -2015. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Huduma ya Afya ya Uzazi na Mtoto, Wizara iliendelea kutekeleza Mkakati wa Kuongeza Kasi ya Kupunguza Vifo vya Watoto na vya Akinamama Vinavyotokana na Matatizo ya Uzazi 2008-2015 ili kufikia Malengo ya Maendeleo ya Milenia. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na kupungua kwa vifo vya watoto wenye umri chini ya miaka mitano

kutoka 91 mwaka 2007/08 hadi 81 kwa kila vizazi hai 1,000 mwaka 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo ni kufikia vifo 54 kwa kila vizazi hai 1,000 ifikapo mwaka 2015. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau ilinunua na kusambaza dawa na vifaa vya uzazi wa mpango ikiwa ni vidonge mizunguko 2,196,000 sindano chupa 3,116,043, vipandikizi 288,801 na vitanzi 55,222. Vifaa hivyo vilinunuliwa na kusambazwa kwenye vituo vya kutolea huduma za afya katika ngazi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara ilikamilisha na kuzindua Mpango Mkakati wa Taifa wa Kinga na Udhibiti wa Saratani ya Shingo ya Kizazi. Aidha, Wizara ilipanua vituo vya huduma ya uchunguzi wa saratani ya shingo ya kizazi kutoka 14 hadi vituo 96 katika mikoa minane ya Morogoro, Kigoma, Iringa, Pwani, Ruvuma, Kilimanjaro, Dar es Salaam na Mbeya. Vile vile katika kipindi hicho, mafunzo ya uchunguzi wa saratani ya shingo ya kizazi yalitolewa kwa watoa huduma za afya 180 kutoka vituo 84. Lengo ni kuongeza vituo vya uchunguzi ili kusogeza huduma karibu na wananchi na kubaini mapema matatizo yatokanayo na saratani na jinsi ya kuidhibiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/12, Wizara ilisambaza kwa majaribio jumla ya vifaa muhimu 128,700 vinavyotumika wakati wa kujifungua *(delivery pack)* katika Mikoa ya Dodoma (vifaa 88,000) na Pwani (vifaa 40,700). Uzoefu utakaopatikana katika mikoa hii, utatumika kusambaza vifaa hivi nchi nzima.

Aidha, kupitia Mpango Kabambe wa Afya wa Halmashauri, mwongozo umetolewa kuwa Halmashauri zote zitenge fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa hivyo ili vitumike katika vituo vyote vinavyotoa huduma za uzazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu *(NIMR)* na Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shiriki Muhimbili *(MUHAS)* ilifanya uchunguzi ili kubaini idadi ya vifaa vya kutolea huduma wakati wa dharura kwa wanawake wajawazito na watoto wachanga. Matokeo ya utafiti huu yalitumika kuandaa orodha ya ugawaji wa vifaa vilivyonunuliwa kwa ajili ya kuboresha huduma ya afya ya uzazi na mtoto. Awamu ya kwanza ya kusambaza vifaa tiba kwa hospitali zote za mikoa na Wilaya imekamilika na awamu ya pili inaendelea kwa vituo vya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara iliendelea na juhudi za kupunguza vifo vya akina mama vitokanavyo na uzazi. Wizara ilisambaza pikipiki 372 za magurudumu matatu kwa ajili ya kurahisisha rufaa ya akinamama wajawazito wenye matatizo, kufika katika vituo vya kutolea huduma za afya. Pikipiki hizo zilisambazwa katika Mikoa yote Tanzania Bara, isipokuwa Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, juhudi zinaendelea kuwezesha vituo vya afya kutoa huduma ya upasuaji wakati wa kujifungua, kwa kuhakikisha kuwa na chumba maalum cha upasuaji, vifaa pamoja na kuwapanga wataalam wenye sifa na ujuzi stahiki.

Kwa sasa vituo vya afya 16 vimeanza kutoa huduma hii na 100 viko kwenye hatua mbalimbali za kuanzisha huduma hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi Machi 2012, vituo 4,603 ambayo ni asilimia 93 ya vituo vyote vinavyotoa huduma ya Afya ya Uzazi na Mtoto vilitoa huduma za kupunguza maambukizi ya VVU toka kwa mama kwenda kwa mtoto. Aidha, jumla ya watoa huduma 130 walipata mafunzo mapya, juu ya kupima VVU kwa watoto wanaozaliwa na mama wenye VVU katika mikoa ya Rukwa, Dodoma na Mwanza. Mafunzo haya yataendelea kutolewa katika mikoa iliyobakia kwa awamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Afya Duniani ilipitia upya mwongozo na mitaala ya kufundishia namna ya kupima VVU kwa watoto wanaozaliwa na mama wenye VVU kwa kutoa mafunzo rejea kwa watoa huduma 100 katika mikoa ya Arusha, Iringa na Tanga. Katika kipindi hicho jumla ya kinamama wajawazito 93,770 waligundulika kuwa na maambukizi ya VVU na kati yao asilimia 92.6 na watoto asilimia 56 walipatiwa dawa za *ARV* kuzuia maambukizi toka kwa mama kwenda kwa mtoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iliandaa na kukamilisha Mpango wa Kutokomeza Maambukizi Mapya ya VVU kwa watoto na kupunguza vifo vya mama zao ifikapo 2015 (*Tanzania Elimination of Mother to Child Transmission of HIV Plan, 2011-2015*) ikiwa ni

utekelezaji wa Mpango wa Dunia wa kutokomeza maambukizi mapya ya VVU.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu udhibiti wa magonjwa ya watoto kwa wwiano; katika mwaka 2011/12, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ilitoa mafunzo ya kumhudumia mtoto mgonjwa sana kwa wahudumu wa afya na kufanya tathmini ya ubora wa huduma za afya kwa watoto ili kupunguza vifo vinavyotokea katika hospitali katika Mikoa sita ya Mara, Tanga, Arusha, Dar es Salaam, Singida na Manyara. Aidha, Wizara ilitoa mafunzo kwa wawezeshaji wa mafunzo 124 wa ngazi ya Wilaya kutoka katika Mikoa ya Shinyanga,Tabora na Mwanza juu ya namna ya kumsaidia mtoto mchanga kupumua.

Mheshimiwa Naibu Spika, watoa huduma 446 kutoka Wilaya za Sengerema, Nyamagana na Geita walipatiwa mafunzo hayo. Vile vile, Wizara kwa kushirikiana na wadau, ilitoa mafunzo kwa watoa huduma 135 na kuanzisha huduma ya matunzo ya mtoto aliyezaliwa na uzito pungufu (chini ya kilo 2.5) katika hospitali za Mikoa ya Tanga, Kagera, Shinyanga, Singida, Mara, Mwanza na Rukwa ili kupunguza vifo vya watoto wenye umri chini ya mwezi mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mpango wa Taifa wa Chanjo; Wizara iliweza kuinua kiwango cha chanjo kutoka asilimia 90 mwaka 2010/2011 hadi asilimia 95 mwaka 2011/2012, ambayo ilifikiwa kwa kutumia mkakati maalum wa fika kila Wilaya mfikie kila mtoto (*Reach Every District/ Reach Every Child*) ili apate haki yake ya chanjo. Wilaya 70 na vituo vya

huduma 700 vilivyokuwa na kiwango kidogo cha chanjo vilitekeleza mkakati huu na viliweza kuongeza kiwango cha chanjo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara ilifanya kampeni ya chanjo ya surua kwa nchi nzima (*Intergrated Measles Campaign*), ambapo watoto wote wenye umri chini ya miaka mitano walipatiwa chanjo ya Surua, *Polio, vitamin A* na dawa za minyoo, ili kudhibiti milipuko ya magonjwa ya Surua nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara ilifanya maandalizi ya awali ya uanzishwaji wa chanjo mpya kwa ajili ya kinga za magonjwa ya kichomi na homa ya uti wa mgongo; magonjwa ya kuharisha kwa watoto walio na umri chini ya miaka miwili (*rotavirus)* na saratani ya shingo ya kizazi kwa wasichana wenye umri wa miaka 10 (*Human papiloma Virus*).

Mheshimiwa Naibu Spika, maandalizi yaliyofanyika ni pamoja na kuongeza uwezo wa kuhifadhi chanjo katika ngazi ya Taifa na mikoa kwa kununua na kuanza kufunga yumba maalum kwa ajili ya mnyororo baridi (*walk in cold rooms*) pamoja na jenereta katika vyumba thelathini na nne (34). Aidha, miongozo, mabango na vipeperushi kwa ajili ya uhamasishaji wa utoaji wa chanjo hizi mpya iliandaliwa ikiwa ni juhudi maalum za kuwawezesha watumishi kutoa chanjo hizo mpya katika kiwango na ubora unaotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma za chanjo ziliendelea kuboreshwa ambapo vituo vya kutolea

huduma viliongezeka kutoka 4,406 mwaka 2010 hadi 5,300 mwezi Machi, 2012. Chanjo zilizotolewa zinakinga watoto dhidi ya magonjwa ya kifua kikuu, polio, kifaduro, pepopunda, donda koo, homa ya ini, na surua. Idadi ya watoto waliopata chanjo iliongezeka kutoka 1,479,321 mwaka 2010 hadi 1,581,919 mwaka 2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara inaendelea kutoa chanjo aina ya *DPT-HB-Hib (Diphtheria, Pertussis, Tetanus, Hepatitis-B, Haemophilus Influenza* B) yenye mchanganyiko wa chanjo tano. Chanjo hiyo inakinga watoto dhidi ya kifaduro, pepopunda, dondakoo, homa ya ini na kichomi pamoja na homa ya uti wa mgongo. Idadi ya watoto waliopata chanjo hii imeongezeka kutoka 1,479,321 mwaka 2010 hadi 1,534,583 mwaka 2011 ambayo ni sawa na asilimia 92.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele katika mwaka 2011/2012, Wizara ilifanya tathmini ya ugonjwa wa usubi katika Wilaya za Muheza, Korogwe na Lushoto kuangalia hali ya uambukizo wa vimelea vya ugonjwa huo. Matokeo yalionyesha kupungua kwa uwepo wanavimelea vya ugonjwa wa usubi kwa binadamu yamepungua kutoka asilimia 40 mwaka 1999 hadi chini ya asilimia moja mwaka 2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu afya mashuleni, katika mwaka 2011/2012, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ilitoa mafunzo kwa waratibu 88 na watendaji wa afya 6,800, wagawa

dawa wa jamii 67,900 na walimu 15,000 ambao walishiriki katika zoezi zima la ugawaji dawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, usafi wa mazingira, Wizara iliendesha mashindano ya Afya na Usafi wa Mazingira kwa kuhusisha Halmashauri zote nchini. Mashindano haya yalikuwa na lengo la kuinua kiwango cha usafi nchini sambamba na kuhamasisha ushiriki wa jamii katika uboreshaji afya kwa njia ya usafi.

Mheshimiwa Naibu Spika,Washindi katika ngazi ya Halmashauri za majiji mshindi mmoja (Halmashauri ya Jiji la Mwanza), Ngazi ya Halmashauri za Manispaa washindi watatu (Halmashauri ya Manispaa ya Moshi), Arusha na Bukoba, ngazi ya Halmashauri za Miji washindi wawili (Mji wa Mpanda na Njombe).

Mheshimiwa Naibu Spika, washindi ngazi ya Halmashauri za Wilaya washindi watatu (Wilaya ya Meru, Njombe na Rungwe). Aidha, Wizara iliandaa Mpango wa Sekta ya Afya wa Utekelezaji wa Shughuli za Mazingira pamoja na Kanuni za Utekelezaji wa Sheria ya Afya ya Jamii ili kudhibiti uchafuzi wa mazingira na kuboresha huduma za usafi na afya ya jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchafuzi wa mazingira, katika mwaka 2011/2012, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo imeanza kuandaa mpango wa utekelezaji wa Mkataba wa Libreville unaounganisha sekta ya afya na mazingira kwa kufanya uhakiki bainifu kuhusu hali halisi ya uchafuzi wa mazingira na mahitaji katika kuboresha mazingira. Aidha, Wizara ilitoa

mafunzo kwa Maafisa Afya wa Mikoa 21, Majiji matano na Manispaa 18 juu ya masuala ya afya mazingira, mabadiliko ya tabia nchi, kemikali na udhibiti wa taka ngumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, Wizara iliandaa vielelezo vya kuelimisha jamii kuhusu udhibiti taka ngumu. Wizara pia, ilifanya tathmini ya matumizi na udhibiti wa taka za kemikali na kuwezesha mafunzo kwa maafisa afya wa Mikoa 21 na Majiji 5 kuhusu tathmini ya athari za afya zitokanazo na miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu afya Bandarini, Viwanja vya ndege na Mipakani, katika mwaka 2011/12, Wizara iliendelea kudhibiti magonjwa yanayotolewa taarifa Kimataifa ili yasiingie nchini, kwa kuviimarisha vituo vya afya bandarini, viwanja vya ndege na mipakani kwa kuvipatia chanjo 18,000 za kudhibiti homa ya manjano na kadi 8,000 za chanjo ya homa ya manjano kwa ajili ya wasafiri wanaotoka katika nchi ambazo zina ugonjwa huo. Aidha, Wizara iliandaa rasimu za Kanuni za utekelezaji wa Sheria ya Afya ya Jamii ya mwaka 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ya afya kwa umma, katika mwaka 2011/2012, Wizara kwa kushirikiana na wadau, iliendelea kuhamasisha na kuelimisha jamii ili iweze kubadili tabia hatarishi kwa afya na kujikinga na maradhi kupitia vyombo mbalimbali vya habari. Aidha, Wizara iliandaa rasimu ya Mpango Mkakati wa Kuboresha na Kudumisha Afya ya Jamii wa mwaka 2011- 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, Wizara ilishirikiana na wadau kuandaa rasimu ya Mwongozo wa sera wa Kuboresha na Kudumisha Afya ya Jamii wa mwaka 2012. Rasimu hizo zinajumuisha masuala ya kinga kwa maradhi ya kuambukiza, maradhi yasiyo ya kuambukiza, ajali, majanga na matukio ya dharura. Pia, Wizara imeanzisha mfumo wa kuhifadhi vielelezo vya uelimishaji wa afya kwa jamii na kazi ya kukusanya na kuhakiki vielelezo kwa kuhakikisha upatikanaji wa vifaa ikiwemo kompyuta maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu huduma za tiba, Vituo vya kutolea Huduma za Afya; katika mwaka 2011/2012, Wizara iliendelea kuboresha huduma zinazotolewa katika hospitali za rufaa kwa kuzipatia vifaa na watumishi wenye sifa. Wizara iliendeleza ujenzi wa miundombinu katika Taasisi ya Saratani *Ocean Road* na Bugando ili kuboresha huduma kwa wagonjwa wa saratani. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China ilikamilisha ujenzi wa jengo la kuhudumia wagonjwa wa moyo katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na kutoa mafunzo kwa wataalam wa moyo 39.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma zitakazotolewa, zitapunguza idadi ya wagonjwa na gharama za kupeleka wagonjwa nje ya nchi. Vilevile, Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi pamoja na mashirika ya dini imekuwa ikiongeza idadi ya vituo vya kutolea huduma za afya ili kukidhi mahitaji ya ya huduma za afya kwa wananchi wake kama ilivyoainishwa katika MMAM.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya Taifa, Rufaa za Kanda na Maalum Hospitali ya Taifa Muhimbili katika mwaka 2011/12, Hospitali ya Taifa Muhimbili ilihudumia jumla ya wagonjwa 205,730. Kati yao 125,102 walitibiwa na kuondoka na wagonjwa waliolazwa walikuwa 80,628. Jumla ya wagonjwa 10,745 walifanyiwa upasuaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Hospitali ya Taifa Muhimbili iliimarisha utoaji wa huduma za ubingwa na ubingwa wa juu kwa kufanya upasuaji wa moyo, usafishaji wa damu kwa wagonjwa wa figo, upasuaji kwa kutumia *endoscope* na kufanya uchunguzi wa magonjwa kwa kutumia mashine za kisasa kama vile, *fluoroscopy*, *CT Scan* na *MRI*. Tangu huduma ya upasuaji mkubwa wa moyo ilipoanzishwa mwaka 2008, jumla ya wagonjwa 340 wamefanyiwa upasuaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya hao, wagonjwa 75 walifanyiwa upasuaji katika kipindi hiki. Vile vile, taratibu za kuanzisha upasuaji kupitia tundu dogo (laparascopic surgery) ziliendelea ambapo baadhi ya vifaa vinavyohitajika tayari viliishafungwa kwenye vyumba viwili katika Jengo la Watoto. Huduma ya kuchuja damu (*renal dialysis*) iliyoanzishwa Mei 2011, ilitolewa kwa wagonjwa 30 wa figo katika mizunguko *(sessions)* 540. Pia, hospitali ilitoa tiba kwa waathirika 500 wa dawa za kulevya wanaojidunga sindano *(methadone assisted therapy)* ili kupunguza tabia hatarishi ya kujidunga sindano ambayo inachangia kuongeza kasi ya maambukizi ya virusi vya UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa kituo cha Tibana Mafunzo ya Upasuaji wa Moyo ulikamilika na kukabidhiwa kwa Serikali tarehe 6 Februari, 2012 na kitafunguliwa rasmi baada ya kukamilisha uwekaji wa vifaa. Kwa sasa tayari fedha za kununua vifaa zimekwisha tolewa na taratibu za ugavi na ununuzi zinaendelea. Kituo hicho kitakuwa na uwezo wa kuhudumia wagonjwa 100. Aidha, ujenzi wa kitengo cha uchunguzi na matibabu ya maradhi ya mfumo wa chakula umekamilika kwa asilimia 90 na kitatumika kufundishia madaktari na wafanyakazi wengine katika fani ya ubingwa wa juu wa magonjwa ya matumbo, ini na saratani ya tumbo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya Taifa Muhimbili ilikamilisha ujenzi wa maabara ya kutengeneza vifaa vya usikivu *(hearing mould laboratory)* kwa ajili ya kusaidia viziwi na iko katika hatua ya kupata vifaa vitakavyotumika kutengeneza shimesikio ili huduma hii iweze kuanza. Aidha, Hospitali ilianzisha tiba ya mazoezi ya kuongea (*speech therapy*) kwa wagonjwa wenye matatizo ya kuongea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/12, Hospitali ya Rufaa ya Bugando ilihudumia jumla ya wagonjwa 147,091. Kati yao 108,106 walitibiwa na kuondoka na wagonjwa waliolazwa walikuwa 38,985. Jumla ya wagonjwa 6,775 walifanyiwa upasuaji. Aidha, Hospitali ilifanya upasuaji wa moyo kwa wagonjwa 53 kati ya hao wagonjwa 16 walifanyiwa upasuaji mkubwa wa moyo. Wagonjwa 252 walifanyiwa upasuaji wa mishipa ya fahamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, idadi ya wagonjwa wanaopata huduma zatiba ya VVU, iliongezeka kutoka 25,000 hadi 51,297. Pia, hospitali ilipokea jumla ya madaktari, mafamasiana wauguzi 74 kwa ajili ya mafunzo ya vitendo nailiendelea na ujenzi wa awamu ya kwanza wa jengo la wagonjwa wa saratani inayotarajia kukamilikaifikapo mwezi Agosti, 2012.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/12, Hospitali ya Rufaa ya *KCMC* ilihudumia jumla ya wagonjwa 186,189. Kati ya hao, wagonjwa 160,944 walikuwa wagonjwa wa nje na wagonjwa waliolazwa walikuwa 25,245. Wagonjwa 7,437 walifanyiwa upasuaji katika idara mbalimbali. Aidha, Hospitali ilianza kutoa huduma za upasuaji kwa kupitia tundu dogo kwa kutumia kifaa kiitwacho *endoscope* ambapo wagonjwa 63 walitibiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, Hospitali ilitoa mafunzo ya kutumia njia hii ya upasuaji kwa Madaktari 45 kutoka katika Hospitali za *KCMC*, Hospitali ya Taifa Muhimbili, Bugando, na Arusha *Lutheran Medical Centre*. Pia, Ujenzi wa jengo la watu wenye magonjwa ya ngozi na walioungua umekamilika, na michoro na usanifu wa majengo mapya ya wodi yenye uwezo wa kulaza wagonjwa 300 ulikamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya Rufaa ya Mbeya, katika mwaka 2011/12, Hospitali ya Rufaa ya Mbeya ilihudumia jumla ya wagonjwa 267, 285. Kati yao, 153,798 ni wagonjwa wa nje na wagonjwa waliolazwa walikuwa 113,487.

Aidha, Hospitali ilianzisha uchunguzi wa saratani ya shingo ya kizazi baada ya kutoa mafunzo kwa wataalam 16 kuhusu kufanya uchunguzi huo kwa njia rahisi (*Acetic Acid -VIA)* ambapo wanawake 803 walifanyiwa uchunguzi. Kati ya hao, wanawake 29 waligundulika kuwa na saratani ya shingo ya kizazi na kupatiwa ushauri na maelekezo ya matibabu yanayostahili. Vilevile, watoto 1,686 wanaoishi na VVU/UKIMWI walianza kupewa dawa za UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Mifupa Muhimbili katika mwaka 2011/2012, Taasisi ya Mifupa Muhimbili ilihudumia jumla ya wagonjwa 60,422. Kati yao 44,533 walitibiwa na kuondoka na wagonjwa waliolazwa walikuwa 15,889. Jumla ya wagonjwa 4,367 walifanyiwa upasuaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Taasisi ya Mifupa Muhimbili iliboresha utoaji wa huduma za ubingwa wa juu katika upasuaji wa ubongo, uti wa mgongo na mifupa. Wagonjwa 54 walifanyiwa upasuaji wa uti wa mgongo, wagonjwa 112 walifanyiwa upasuaji wa kubadilisha mifupa ya nyonga, wagonjwa 54 walifanyiwa upasuaji wa saratani ya ubongo na wagonjwa 48 walifanyiwa upasuaji wa kubadilisha mifupa ya goti. Upasuaji huu uliokoa shilingi za kitanzania bilioni 4.47 endapo wagonjwa wangepata rufaa ya matibabu hayo nje ya nchi. Vilevile, Taasisi ilitoa huduma za mkoba katika Hospitali ya mkoa wa Iringa na hospitali ya Mbalizi (Mbeya). *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Taasisi ya Mifupa Muhimbili ilikamilisha taratibu za kumpata mkandarasi wa ujenzi wa awamu ya tatu ya hospitali. Aidha, ilikamilisha upatikanaji wa mkopo wa fedha za ujenzi kutoka Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya *(NHIF)*. Ujenzi huo utakapokamilika utaongeza uwezo wa kutoa huduma ya tiba ya upasuaji wa ubongo na uti wa mgongo pamoja na utoaji wamafunzo katika fani hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, hospitali iliwapatia mafunzo watumishi 82; katika fani za uuguzi (41), utunzaji kumbukumbu za kitabibu (4), fiziotherapia (2), radiolojia (1), famasia (2) shahada ya uzamili ya tiba (*MMed*) (29) na ubingwa maalum *(super specialization)* (3). Aidha, Taasisi iliendelea kushirikiana na wadau wa maendeleo katika masuala ya taaluma na utoaji huduma. Ushirikiano kati ya Taasisi na wadau wa maendeleo ulinufaishawagonjwa zaidi ya 2,000. Vilevile, Taasisi ilinunua mashine ya *ultra sound* na mashine mbili za kutolea dawa ya usingizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya *Ocean Road*, katika mwaka 2011/12, Taasisi ya *Ocean Road* ilihudumia jumla ya wagonjwa wapya wa Saratani 5,102, wanaume wakiwa 1,708 na wanawake 3,394. Hili ni ongezeko la wagonjwa 966 ukilinganisha na mwaka 2010/2011. Wagonjwa 1,632 walitibiwa kama wagonjwa wa nje, kati yao wanaume walikuwa ni 461 na wanawake 1,171.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya wagonjwa 3,853 waliolazwa, wanaume walikuwa ni 1,247 na wanawake 2,606. Hospitali ilihudumia wagonjwa 19,143 wa marudio katika Kliniki ambao wanaume walikuwa ni 6,928 na wanawake 12,215. Aidha, Jumla ya wanawake 11,899 walifanyiwa uchunguzi wa Saratani ya shingo ya kizazi na matiti. Kati yao 952 waligundulika na dalili za awali za Saratani ya Shingo ya Kizazi na 86 walikutwa na Saratani ya Matiti. Hawa wote walianza kupatiwa matibabu ya awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/12, Taasisi ilikamilisha ujenzi wa jengo jipya lenye uwezo wa kulaza wagonjwa 150 na hivyo kuongeza uwezo wa hospitali ya kulaza jumla ya wagonjwa 270. Kazi inayoendelea ni kufunga mitambo mbalimbali ya matibabu na uwekaji wa vifaa anuai vya kihospitali. Aidha, huduma za matibabu ya mionzi imeendelea kuimarishwa zaidi kwa kutumia mashine zilizopatikana za kutibu Saratani, yaani *high-dose rate intracavitary machine* na *Simulator*.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, Mashine za digitali za Telemedicine zimeshafungwa katika Taasisi ya Saratani ya *Ocean Road*, na zimeshaanza kufanya kazi kwa mawasiliano kati ya Taasisi ya Saratani ya *Ocean Road* na Vyuo pamoja na Hospitali za nchini India. Wanafunzi na madakatari wananufaika kwa huduma hii kwa kuongeza ujuzi na uwezo wa kutoa tiba kwa wagonjwa wa Saratani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Taasisi kwa kushirikiana na wadau wengine

ilitoa mafunzo ya uchunguzi wa saratani ya shingo ya kizazi katika hospitali za Mikoa ya Pwani, Morogoro, Tabora, Kigoma, Iringa na Mbeya. Hii itasaidia wagonjwa wa Saratani katika mikoa hii kupata uchunguzi mapema na kuwahi kupata tiba mapema. Aidha, Taasisi kwa kushirikiana na wadau wengine ilitoa elimu kwa wananchi kupitia vyombo mbalimbali vya habari, tovuti, warsha, maonyesho na semina kuhusu kinga na matibabu ya saratani.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, Taasisi kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Muhimbili imeendelea na kutoa mafunzo ya kozi ya uzamili ya Onkolojia *(MMED Clinical Oncology)* na Shahada ya matibabu ya Mionzi *(BSc Radiation Therapy Technology)*. Kozi hii itasaidia kupata wataalam wengi zaidi wa kutibu Saratani. Tayari wanafunzi madaktari 19 wapo mafunzoni katika kozi ya Uzamili na 16 katika kozi ya Shahada. Pia, Taasisi ilishirikiana na wadau wa ndani na nje ya nchi katika kuimarisha huduma na tafiti za saratani kwa kuboresha huduma na matibabu kwa wagonjwa wanaofika kupata matibabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/12, Hospitali ya Mirembe ilihudumia jumla ya wagonjwa 40,492. Kati ya hao, 36,858 walikuwa wagonjwa wa nje na waliolazwa walikuwa 3,634. Kati ya wagonjwa wa nje, wagonjwa 7,544 walikuwa wagonjwa wa akili na 29,314 walikuwa wagonjwa wa kawaida. Aidha, kati ya wagonjwa wote waliolazwa, wagonjwa 2,110 walikuwa wagonjwa wa akili wa kawaida, wagonjwa 219 walikuwa wagonjwa wa akili wahalifu na waliobaki 1,305 walikuwa wagonjwa waliolazwa kwa magonjwa

yasiyo ya akili. Vile vile, Hospitali iliwapatia watumishi 103 mafunzo rejea yanayohusu utoaji wa huduma bora kwa wagonjwa wa akili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/12, Taasisi ilipokea jumla ya wagonjwa wa akili wahalifu 219. Kati ya hao, wagonjwa 199 walikuwa wanaume na wagonjwa 20 walikuwa wanawake. Aidha, Hospitali ilifanya uchunguzi wa akili kwa watuhumiwa 100 ambapo kati ya hao, wanaume walikuwa 87 na wanawake 13 na kutoa maoni ya kitaalam kuhusu mashauri yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Hospitali ya Kibong'oto iliwahudumia jumla ya wagonjwa wa Kifua Kikuu 600; kati ya hao kifua kikuu cha kawaida 573 na Kifua Kikuu sugu 27. Aidha, Hospitali iliwahudumia wagonjwa wengine wa nje 11,953, waliolazwa ni 946, wenye VVU 379, walianzishiwa ART 244. Vile vile, Hospitali ilitoa mafunzo ya njia za kujikinga na Kifua Kikuu sugu kwa watumishi 42 wa hospitali na mafunzo ya matibabu ya Kifua Kikuu sugu kwa watumishi wa afya 65 kutoka Wilaya mbalimbali ambazo wagonjwa waliruhusiwa baada ya kumaliza matibabu ya awali ya Kifua Kikuu sugu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, Hospitali iliendelea kushirikiana na taasisi za utafiti kufanya tafiti za kufupisha matibabu ya Kifua Kikuu na uchunguzi wa vifaa tiba vya kutambua usugu wa dawa za Kifua Kikuu za daraja la pili. Hospitali ilisajili wagonjwa wa Kifua Kikuu sugu 87. Wagonjwa 48 kati ya wagonjwa hao, waliruhusiwa na kuendelea na dawa wakiwa

majumbani, wagonjwa 18 wako wodini na wagonjwa 6 wamepona kabisa. Hospitali ilifanya usimamizi wa wagonjwa *(supportive supervision and mentoring)* wilayani mara 89 kwa wagonjwa 38 wa Kifua Kikuu sugu waliokwisharuhusiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Huduma za Hospitali za Mashirika ya Kujitolea, Makampuni na Watu Binafsi katika mwaka 2011/2012, Wizara iliendelea kuimarisha mazingira ya kuifanya sekta binafsi ishiriki katika utoaji wa huduma za afya hapa nchini. Hospitali 10 za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, zilizopandishwa hadhi na kuwa Hospitali za Rufaa, ngazi ya Mkoa zilianza kupatiwa dawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Hai, Manispaa ya Shinyanga na Jiji la Arusha ziliingia makubaliano na wamiliki wa Hospitali ya Machame (Hai), Hospitali ya Kolandoto (Manispaa ya Shinyanga) na Hospitali ya St. Elizabeth (Jiji la Arusha) ili hospitali hizo zitoe huduma kwa niaba ya Halmashauri husika. Makubaliano haya yanafanya idadi ya Hospitali zinazotumika kama Teule za Hamashauri kufikia 37, hii ni pamoja na Hospitali nne (Ilembula - Njombe, Nyangao - Lindi, Peramiho Songea na St.Francis - Kilombero) ambazo zimepandishwa daraja na kuwa Hospitali za rufaa ngazi ya mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo, Wizara iliandaa Mkutano wa Kanda wa Kimataifa kujadili uhusishwaji wa sekta binafsi katika utoaji wa huduma za afya. Mkutano huo uliohudhuriwa na washiriki 250 kutoka nchi 19, uliibua

masuala kadhaa muhimu yakiwemo ya nchi za Afrika kuimarisha juhudi za ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi ili kuleta maendeleo ya huduma za afya, kuzijengea uwezo Wizara za Afya za nchi za Afrika katika utekelezaji wa ushirikiano kati ya sekta ta umma na binafsi na kuongeza kuaminiana kati ya sekta hizo mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/12, Wizara iliboresha huduma za kinywa kwa kununua na kusambaza dawa za tiba ya meno katika mikoa yote nchini. Aidha, Wizara ilisambaza viti 82 vya kutibia meno katika mikoa 17 kama ifuatavyo:-

Shinyanga (16), Kagera (10), Tanga (10), Morogoro (7), Rukwa (6), Tabora (6), Mara (6), Arusha (5), Mbeya (4), Pwani (3), Iringa (2), Lindi (2), Dodoma (1), Manyara (1), Ruvuma (1), Mtwara (1) na Mwanza (1). Vilevile, matengenezo kinga na matengenezo ya kawaida ya mashine na vifaa vya kutibia kinywa yalifanyika katika Hospitali ya Mkoa wa Dodoma, Hospitali ya Wilaya Kondoa, Hospitali ya Wilaya Karatu, Kituo cha Afya Kibaha, Hospitali ya Mkoa Morogoro, Kituo cha Afya Ngome na Ipogolo (Iringa) na Hospitali ya Mkoa Ruvuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, magonjwa yasiyo ya kuambukiza na dawa za kulevya katika mwaka 2011/2012, Wizara ilisambaza nakala za Sheria mpya ya Afya ya Akili na Dawa za Kulevya katika hospitali za rufaa za mikoa yote. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau ilikamilisha Mpango Kazi wa Kuboresha

Huduma ya Magonjwa yasiyo ya kuambukiza katika Hospitali za Rufaa za Kanda na Hospitali za Rufaa za Mikoa yote. Vile vile, Wizara iliandaa rasimu ya Mkakati wa Taifa wa Kudhibiti Madhara ya Matumizi Mabaya ya Pombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara iliandaa Mpango Mkakati wa Taifa wa kuzuia magonjwa yasiyo ya kuambukiza na Mpango Mkakati wa Taifa wa Kuzuia Magonjwa ya Saratani. Aidha, Wizara ilifanya utafiti wa tabia hatarishi zinazochangia kuenea kwa magonjwa yasiyo ya kuambukiza, matokeo ya awali yamebainisha kuwa tabia hatarishi zinazochangia kuongezeka kwa magonjwa yasiyo ya kuambukiza ni; uvutaji wa sigara na bidhaa za tumbaku, unywaji pombe wa kupindukia, kutokufanya mazoezi na ukosefu wa lishe bora. Vile vile, Wizara iliandaa Mwongozo wa Kuzuia Utumiaji Hatarishi wa Pombe *(National Alcohol Prevention Guideline).*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara kwa kushirikiana na wadau ilielimisha na kuhamasisha wananchi juu ya huduma za macho kwa kupitia maadhimisho ya Siku ya Afya ya Macho Duniani yaliyofanyika mwezi Oktoba 2011. Aidha, Wizara iliendesha kambi za Macho katika mikoa ya Dar es Salaam, Manyara, Iringa, Mwanza na Kilimanjaro, ambapo wagonjwa wa macho 4,000 walipata huduma mbalimbali. Miongoni mwao, wagonjwa 378 walifanyiwa upasuaji wa macho ambapo kati ya hao 300 waligundulika kuwa na tatizo la mtoto wa jicho.

Vile vile, jozi 1,300 za miwani zilitolewa kwa wananchi bila malipo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara kwa kushirikiana na wadau ilikamilisha na kuzindua rasmi Mpango Mkakati wa Pili wa miaka mitano wa Huduma za Macho (2011 -2016). Mpango mkakati huu unalenga kuboresha huduma za macho hapa nchini ili kuchangia kufanikisha malengo ya Dira 2020 ya Kimataifa ya Kutokomeza Upofu Unaozuilika Duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa huduma za afya ya macho katika Hospitali za Rufaa za Mikoa ya Dodoma, Mwanza, Iringa, Singida, Ruvuma na Mbeya ziliweza kuboreshwa kwa kupatiwa vifaa tiba vya kisasa kwa ajili ya kupima wagonjwa. Aidha, hospitali hizo zilipewa miwani ya kuuzwa kwa bei nafuu kwa lengo la kupata fedha ili huduma hizo ziwe endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma ya matibabu nje ya nchi. Katika mwaka 2011/2012, Wizara ilipeleka nje ya nchi wagonjwa 502 wenye matatizo mbalimbali kwa ajili ya kupata matibabu baada ya kushindikana kutibiwa hapa nchini. Kati yao, watoto walikuwa ni 225 na watu wazima walikuwa 277. Kati ya wagonjwa wote 502, wagonjwa wa moyo walikuwa 326, saratani walikuwa 52, figo walikuwa 44 na magonjwa mengine walikuwa 80. Kati ya wagonjwa wote waliopelekwa nje ya nchi asilimia 8.7 walikuwa viongozi wa ngazi mbalimbali. Aidha, Wizara ilileta Madaktari Bingwa 16 kutoka India kwa lengo la kutoa huduma kwa

wagonjwa hapa nchini na kutoa mafunzo kwa Madaktari wazalendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma na mafunzo hayo yalitolewa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, Taasisi ya Mifupa Muhimbili na Taasisi ya Saratani *Ocean Road* na jumla ya wagonjwa 612 walinufaika na huduma hii. Kati ya wagonjwa hao 513 sawa na asilimia 84 walionekana kuwa wanaweza kupatiwa matibabu hapa nchini. Wagonjwa 22 sawa na asilimia 3.5 walifanyiwa upasuaji wa moyo, ubongo, mishipa 63 ya damu pamoja na mifupa. Wagonjwa 77 sawa na asilimia 12.5 walitakiwa kupata rufaa ya kwenda India kwa matibabu zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uchunguzi wa Magonjwa katika mwaka 2011/12, Wizara ilifanya matengenezo kinga ya vifaa tiba ikiwa ni pamoja na vifaa vya radiolojia katika hospitali zote nchini. Aidha, Wizara kupitia Sehemu ya Uchunguzi wa Magonjwa iliendelea kusimamia na kuboresha huduma za uchunguzi wa magonjwa ikiwa ni pamoja na matengenezo kinga ya vifaa vya maabara na radiolojia katika hospitali zote za wilaya, rufaa mikoa, rufaa kanda, maalum na Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo, ilikamilisha tathmini ya mahitaji halisi ya vifaa vya radiolojia, vyumba vya upasuaji na huduma za uzazi na mtoto katika awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mradi wa *ORIO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini hiyo ilifanyika katika Hospitali ya Taifa Muhimbili; Hospitali Maalum za *MOI*, Kibong'oto na Mirembe; Hospitali za Rufaa za Kanda za Bugando, *KCMC* na Mbeya na Hospitali za Wilaya za Tandahimba, Rungwe, Kilolo, Misungwi, Chato na Bukombe. Serikali, kwa kupitia Hazina, iliwasilisha taarifa ya tathmini hiyo, kwa Serikali ya Uholanzi mwezi Desemba 2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, maabara (7) kati ya 12 za Hospitali za Rufaa za Mikoa sita ya Dar es Salaam (Amana, Temeke na Mwananyamala), Morogoro, Arusha, Tanga, Iringa na Mtwara na Hospitali za Wilaya sita za Lushoto, Kisarawe, Kahama, Mafinga, Tukuyu na Newala zilizoingizwa kwenye mchakato wa ithibati kwa viwango vya kimataifa vya ubora wa huduma za maabara, kwa utaratibu wa hatua kwa hatua wa nyota wa Shirika la Afya Duniani, Ukanda wa Afrika *(WHO Afro Stepwise Laboratory Accreditation),* zilifanikiwa kufikia nyota moja hadi tatu za viwango vya ubora wa Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maabara iliyofikia ngazi ya nyota tatu ni ya Hospitali ya Amana (Dar es Salaam), nyota mbili ni za Hospitali za Rufaa za Mkoa wa Morogoro, Mt. Meru (Arusha) na za Wilaya za Lushoto na Newala na nyota moja ni kwa Hospitali za Bombo (Tanga) na Mafinga (Mufindi). Maabara hizi zipo kwenye hatua za kufanyiwa tathmini na wakaguzi wa nje ili ziweze kupewa nyota kulingana na viwango vilivyofikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/12, Maabara ya Taifa ya Mafunzo na Uhakiki wa Ubora wa Huduma za Maabara *(National Health Laboratory, Quality Assurance and Training Centre)* iliendelea kuimarishwa na kuboreshwa kwa kujenga uwezo wa kuchunguza magonjwa ya milipuko ya Mafua ya Nguruwe, Mafua ya Mdege, Homa ya Bonde la Ufa, Kuhara Damu, na *Dengue fever*. Aidha, wigo wa uhakiki wa vipimo vya maabara uliimarishwa na kupanuliwa toka vipimo vya aina mbili tu vya chembe chembe za kinga mwilini (*CD4*) na upimaji haraka wa *VVU (HIV Rapid Test)* hadi vipimo vya aina saba kwa kuongeza vipimo vya haematology, *clinical chemistry*, *DNA PCR,* mikrobiolojia na parasitolojia hususan vipimo vya malaria.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara kupitia Mpango wa Taifa wa Damu Salama ilikusanya chupa 155,000 ambayo ni sawa na asilimia 86 ya matarajio ya chupa 180,000. Aidha, chupa hizo zilisambazwa katika hospitali 209 kati ya 261 ambapo hospitali 75 zilipata asilimia 80 ya mahitaji yao. Vile vile, kiwango cha VVU toka kwa wachangia damu wa hiari kilishuka toka asilimia 1.2 kwa mwaka 2010 hadi asilimia 1.0 kwa mwaka 2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/12, Mpango wa Damu Salama uliongeza vituo vya ukusanyaji damu kutoka vituo viwili vya Dar-es-Salaam na Dodoma hadi vituo sita. Vituo vilivyoongezeka viko katika mikoa ya Kagera, Kigoma, Morogoro na kituo kipya cha Lindi kilizinduliwa tarehe 14 Juni 2012 wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wachangia Damu Duniani.

Aidha, Wizara iliongeza upatikanaji wa mazao ya damu *(Blood products)* toka asilimia saba hadi asilimia 12.5. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara iliendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kuchangia damu kwa hiari kwa kutumia njia mbalimbali ikwemo vyombo vya habari, vipeperushi pamoja na kutumia viongozi wa dini, siasa pamoja na jamii. Aidha, Mpango ulitumia mfumo mpya wa kielektroniki ili kupata taarifa na takwimu mbalimbali kuanzia kwa mchangiaji damu hadi kwa mgonjwa anayepewa damu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara ilitumia shilingi 189,746,367,762.00 kununua na kusambaza dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika vituo vya kutolea huduma za afya vya umma. Aidha, Wizara kupitia Bohari ya Dawa ilisambaza dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika zahanati 4,190, vituo vya afya 494, hospitali za wilaya na teule 111, hospitali za rufaa za Mikoa 24, hospitali za rufaa ngazi ya Mkoa 10, hospitali za rufaa za kanda 4, hospitali maalum *(Super Speciality)* 4, hospitali ya Taifa moja, hospitali za jeshi la wananchi mbili na hospitali ya jeshi la polisi moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa kutumia mfumo mpya wa usambazaji hadi ngazi ya zahanati, ilisambaza dawa na vifaa tiba katika Mikoa 10 ya Tanzania Bara. Mikoa hiyo ni: Tanga, Manyara, Dodoma, Dar es Salaam, Pwani, Shinyanga, Kigoma, Rukwa, Ruvuma na Lindi.

Mfumo huo wa usambazaji dawa, vifaa na vifaa tiba utaendelea kutekelezwa katika mikoa yote iliyobakia katika mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara iliboresha utaratibu wa kugawa fedha za dawa, vifaa tiba na vitendanishi zinazotolewa kwa Bohari ya Dawa kwa kuzingatia ukubwa wa huduma na idadi ya walengwa wanaohudumiwa na kituo husika tofauti na awali ambapo fedha zilikuwa zikigawiwa kwa kulingana na ngazi ya utoaji wa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu huduma za Tiba Asili na Tiba Mbadala katika mwaka 2011/2012, Wizara ilitoa elimu kwa umma kwa kupitia vipindi 12 vya radio na semina ya viongozi 48 wa Vyama vya Waganga wa Tiba Asili na Tiba Mbadala kuhusu huduma za tiba asili zinazozingatia sheria, kanuni na miongozo iliyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara iliwashirikisha waganga 261 katika maadhimisho ya Siku ya Tiba Asili ya Mwafrika na waganga nane katika kusherehekea miaka 50 ya Uhuru wa Tanzania Bara. Vile vile, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa iliteua Waratibu wa Tiba Asili na Tiba Mbadala katika ngazi za Mikoa na Halmashauri zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Bohari ya Dawa iliboresha ununuzi wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi kwa kuingia katika mikataba ya muda wa kati na wazabuni

*(Suppliers)*. Mikataba hiyo ilisaidia kupunguza mlolongo mrefu wa manunuzi na hivyo kuboresha upatikanaji endelevu wa dawa na vifaa katika vituo vya kutolea huduma za afya. Aidha, ujenzi wa maghala ya kisasa ya kuhifadhia dawa, vifaa tiba na vitendanishi unaendelea katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mbeya na Dodoma. Ujenzi huo utakapokamilika utaongeza uwezo wa utunzaji dawa kwa zaidi ya mita za mraba 12,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Bohari ya Dawa ilikamilisha kwa kiwango kikubwa usimikaji wa mfumo mpya wa kielektroniki wa *EPICOR* na kuanza kutoa mafunzo kwa watumishi juu wa mfumo huo mpya. Mfumo huu utasaidia kuboresha upatikanaji wa taarifa sahihi na kwa wakati katika ngazi zote. Aidha, Bohari ya Dawa ilifanya mabadiliko ya muundo wa utendaji katika safu ya menejimenti, kwa lengo la kuelekeza nguvu zaidi katika shughuli za kanda ili kuongeza ufanisi katika uagizaji na usambazaji wa dawa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukaguzi na Uhakiki wa Ubora wa Huduma za Afya na Ustawi wa Jamii. Ukaguzi wa Huduma za Afya. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2011/12, Wizara ilikagua vituo 36 vya kutolea huduma za afya katika ngazi ya hospitali ya Taifa (1), hospitali za rufaa (3), maalum (4), mikoa (23) na hospitali za wilaya (5) zilizopata mafunzo ya kukinga na kudhibiti maambukizo ya magonjwa wakati wa kutoa huduma ili kusimamia na kufuatilia kuona kama vituo hivyo vinazingatia utekelezaji wa viwango vya ubora wa

kukinga na kudhibiti maambukizo katika utoaji wa huduma za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara ilitoa mafunzo ya ukufunzi kuhusu kukinga na kudhibiti maambukizo katika utoaji wa huduma za afya kwa Timu za Uendeshaji za Afya za Halmashauri 30 za Mikoa ya Dodoma, Morogoro, Mtwara, Singida na Pwani. Halmashauri hizo ni za Wilaya za Bahi, Chamwino, Kondoa, Kongwa, Mpwapwa, Morogoro, Mvomero, Kilosa, Kilombero, Ulanga, Mtwara, Tandahimba, Masasi, Newala, Nanyumbu, Singida, Manyoni, Iramba, Bagamoyo, Kibaha, Kisarawe, Mafia, Mkuranga na Rufiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri 71 nyinginezo za Mji wa Kibaha na za Manispaa za Dodoma, Morogoro, Singida na Mtwara Mikindani. Aidha, Wizara ilitoa mafunzo ya ukufunzi kuhusu kukinga na kudhibiti maambukizo katika uboreshaji wa huduma za afya kwa wajumbe wapya 36 kutoka Timu za Uendeshaji za Afya za Mikoa na wajumbe washirikishwa *(co-opted members)* 101 na pia, maafisa wa Wizara 28 ambao wanahusika na ukaguzi na ufuatiliaji wa huduma za afya katika vituo vya kutolea huduma za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/12, Wizara kwa kushirikiana na wadau iliendelea kujiweka tayari kukabiliana na dharura na maafa pindi yatakapotokea. Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kitengo cha Maafa, kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu na Mkoa wa Dar es Salaam ilikabiliana na maafa

yaliyotokana na mafuriko ya mvua mjini Dar es Salaam kwa kutoa huduma za afya na ustawi wa Jamii kwa waathirika. Timu ya wataalam wa afya wa fani mbalimbali wakiwa na dawa, vifaa na vifaa tiba walikwenda Zanzibar kushiriki katika kuokoa na kutoa tiba kwa waathirika wa meli ya *MV. Spice Islander* iliyozama tarehe 10 Septemba, 2011 na meli ya *MV. Skagit* iliyotokea tarehe 18 Julai, 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara ilishiriki katika kuchunguza miili 43 ya wahamiaji haramu waliotelekezwa katika msitu wa Chitepo katika Halmashauri ya Kongwa na ilisimamia maziko kwa kuzingatia sheria na kanuni za afya. Taarifa za awali za uchunguzi zimebaini kuwa sababu ya vifo hivyo ni kutokana na kukosa hewa na chakula. Vile vile, Mpango wa kukabiliana na dharura kwa kutoa huduma za Afya kwa waathirika uliendelea kuboreshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ushirikiano katika masuala ya Sekta ya Afya na Ustawi wa Jamii katika Jumuiya za Afrika *(SADC, EAC, ECSA-HC)* na Kimataifa; katika mwaka 2011/2012, Wizara iliendelea kuratibu na kushiriki kwenye mikutano na kutekeleza maamuzi yenye manufaa kwa Taifa yaliyofikiwa katika Jumuiya zote za kanda ambazo ni *SADC, EAC, ECSA-HC* na Mashirika mengine ya Kimataifa ikiwa ni pamoja na kuwianisha usajili wa dawa za binadamu, kuwa na mkakati wa pamoja wa kuboresha uzalishaji wa dawa katika nchi wanachama.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara iliratibu huduma za ustawi wa jamii zilizotolewa na wadau mbalimbali zikiwemo asasi zisizokuwa za Kiserikali. Aidha, Wizara iliendelea kusimamia utekelezaji wa sheria, sera na miongozo inayolenga kupatikana kwa huduma na ulinzi kwa watu walio katika mazingira hatarishi kama vile wazee wasiojiweza, watu wenye ulemavu, familia zenye dhiki, watoto walio katika mazingira hatarishi na watoto walio katika mkinzano na sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu huduma kwa familia, watoto na malezi ya awali ya mtoto; katika mwaka 2011/2012, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri pamoja na wadau wa maendeleo kupitia mradi wa “Pamoja Tuwalee” imefanya utambuzi wa watoto walio katika mazingira hatarishi katika halmashauri mpya nne (4) za Liwale, Kilwa, Lindi na Manispaa ya Lindi na kufanya idadi ya halmashauri zilizofikiwa kuwa 95.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii imefanya idadi ya watoto waliotambuliwa kufikia 867,041 wakiwemo wavulana 500,946 sawa na asilimia 57.78 na wasichana 366,095 sawa na asilimia 42.22. Aidha, Wizara ilikamilisha uandaaji wa kanuni zinazohusu uanzishaji na uendeshaji wa vituo vya kulelea watoto wadogo na wachanga mchana, uanzishaji na uendeshaji wa mahabusi za watoto na shule ya maadilisho, malezi ya kambo na kuasili, uanzishaji na uendeshaji wa makao ya watoto, ajira mbaya kwa watoto na ufundi kazi (*apprenticeship*) kwa watoto ili kuwezesha utekelezaji wa Sheria ya Mtoto Na. 21 ya 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Wizara ilifanya tathmini ya kina kuhusu huduma zinazotolewa katika makao ya kulelea watoto walio katika mazingira hatarishi katika mikoa 21 ya Tanzania bara. Matokeo ya tathmini hii, yanaonyesha kuwepo kwa makao 282. Kati ya makao hayo, 87 yalisajiliwa na 195 hayajasajiliwa. Jumla ya watoto 11,216 wanalelewa katika makao hayo, wakiwemo wavulana 5,127 na wasichana 6,089.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara ilipokea jumla ya maombi 151 ya msaada wa Rais kwa kina mama waliojifungua watoto zaidi ya wawili kwa mara moja kwa ajili ya matunzo ya awali kwa watoto hao. Kati ya maombi hayo jumla ya kina mama 29 walipatiwa msaada huo. Aidha, Wizara ililipia gharama za shule kwa watoto wenye shida walio katika vituo vya ustawi wa jamii vikiwemo; 75 makao ya Taifa ya watoto Kurasini watoto 98; ambapo wavulana 56 na wasichana 42.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara ilikamilisha tathmini ya Mpango Kazi wa Kitaifa wa Huduma kwa Watoto walio katika Mazingira Hatarishi 2007 – 2010. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri imeanzisha na kuimarisha mifumo ya ulinzi wa mtoto kwa kuunda Timu za Ulinzi na Usalama wa Mtoto katika Halmashauri sita za Temeke, Hai, Magu, Kasulu, Bukoba na Musoma kwa kuanzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, timu hizo zimejengewa uwezo juu ya namna ya kushughulikia

masuala yanayohusiana na ulinzi na usalama wa mtoto dhidi ya ukatili, unyanyasaji, utumikishwaji na ukandamizaji. Wizara pia, imeandaa zana za kukusanyia taarifa za matukio ya ukatili, unyanyasaji, utumikishwaji, ukandamizaji na vitendo vingine vinavyokiuka ulinzi wa mtoto ngazi ya Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma za haki za mtoto na marekebisho ya tabia. Katika mwaka 2011/2012, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ilitoa mafunzo ya Uwezeshaji Haki Jamii ngazi ya Wilaya kwa washiriki 198 kutoka katika Halmashauri tano ambazo 76 ni Halmashauri za Wilaya za Kilombero, Kilosa, Kibaha, Korogwe na Halmashauri ya Manispaa Singida na ngazi ya Kata katika Halmashauri nne ambazo ni Halmashauri ya Iramba (Kata ya Kisiriri), Geita (Kata ya Katoro) Songea Manispaa (Kata ya Lizaboni) na Jiji la Arusha (Kata ya Levolosi, Ngarenaro na Kati). Lengo kuu la mafunzo hayo ni kuiwezesha jamii kutambua haki na wajibu kulingana na sheria zilizopo. Huduma kwa wazee na watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012 Wizara iliendelea na juhudi za kuboresha huduma za afya kwa wazee nchini kote. Kupitia kwa Waziri Mkuu vituo vyote vya kutolea huduma za afya vilielekezwa kutenga dirisha maalum kwa ajili ya kutoa huduma kwa wazee. Mpango huu una lengo la kupunguza muda wa kusubiri katika kituo cha afya ili kupata huduma hivyo kupunguza kero kwa wazee. Vile vile, Wizara iliendelea kusisitiza kwamba wazee wote zaidi ya miaka 60 wapewe huduma bila malipo bila kujali

uwezo wao kiuchumi. Nia ni kuhakikisha kuwa wazee wanapata huduma yenye ubora na wanapewa kipaumbele katika vituo vya kutolea huduma za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara iliandaa Mpango wa Utekelezaji wa Sheria ya Watu Wenye Ulemavu Na.9 ya mwaka 2010 kwa lengo la kutetea haki, maslahi na ustawi wa watu wenye ulemavu. Aidha, Wizara ilitoa mafunzo kwa watu 94 wenye ulemavu katika vyuo vya Singida na Yombo kwa kutoa vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Vilevile, Wizara iliendelea kusimamia na kuratibu utoaji wa huduma na shughuli zinazofanywa na wakala za hiari zinazohudumia wazee na watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara iliunda Baraza la Taifa la Ushauri la Watu Wenye Ulemavu hatua ambayo itasaidia usimamizi na utoaji wa haki. Aidha, Wizara iliendelea kuratibu vikao vya Kamati Elekezi ya Taifa ya Muongo kwa Watu Wenye Ulemavu ili kuboresha utoaji wa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, katika jitihada za kuboresha utoaji wa huduma za kinga ya jamii ikijumuisha nyenzo za kujimudu, Wizara kwa kushirikiana na wadau iliwezesha viziwi 549 kupata shimesikio na iliwatengamanisha katika jamii watu wenye ulemavu 20 kutoka katika makazi kwa kuwawezesha kujenga nyumba nje ya makazi. Pia, Wizara iliendelea kutoa matunzo kwa wazee na wasiojiweza kwenye makazi 17 ya Serikali ambapo 78 jumla ya wahudumiwa 1,196 wanapatiwa mahitaji yote ya msingi na inaratibu

huduma hizo katika makazi 24 mengine ya wakala za hiari.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara ilitafsiri Sheria ya Watu Wenye Ulemavu Na. 9 ya 2010 katika lugha ya Kiswahili. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau ilitoa mafunzo kwa washiriki 25 kuhusu marekebisho ya watu wenye ulemavu mahali walipo kwa mameneja wa miradi midogo midogo kutoka kwenye makazi yanayosimamiwa na Serikali na wakala za hiari. Vile vile, Wizara ilitoa ruzuku kwa vyama saba vya Watu Wenye Ulemavu pamoja na Shirikisho lao ili kuvijengea uwezo wa kujiendesha. Pia, Wizara kwa kushirikiana na wadau ilifanya ufuatiliaji wa mradi wa kuzuia ulemavu utokanao na ukoma katika wilaya za Kilosa, Shinyanga na Rorya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la kuhudumia watoto *UNICEF* ilifanya upembuzi wa hali ya huduma zinazotolewa kwa watoto walio katika mazingira hatarishi wanaolelewa katika Taasisi. Upembuzi huo ulifanyika katika mikoa yote 21 ya Tanzania Bara na utawezesha kuandaliwa kwa mkakati wa utekelezaji utakaosaidia kuboresha utoaji wa huduma kwa watoto walio katika mazingira hatarishi katika makao.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara iliendesha mafunzo kwa Maafisa Ustawi wa Jamii kutoka Ofisi za Makatibu Tawala wa Mikoa yote 21 pamoja na Maafisa Ustawi wa Jamii 10

kutoka Makao Makuu ya Idara ya Ustawi wa Jamii. Mafunzo hayo yalilenga kuwajengea uwezo washiriki juu ya stadi za kupanga na kuandaa bajeti *(Planning and Budgeting Skills)* katika eneo la huduma za Ustawi wa Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo ni kuwezesha Maafisa Ustawi wa Jamii Washauri katika Sekretarieti za Mikoa kuhakikisha kuwa huduma za Ustawi wa Jamii zinatengewa fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kama ilivyoelekezwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara kwa kushirikiana na wadau iliendesha zoezi la uchambuzi yakinifu wa nguvu kazi ya wataalam wa taaluma ya Ustawi wa Jamii. Lengo la zoezi hilo lilikuwa ni kuangalia idadi ya Maafisa Ustawi wa Jamii waliopo, huduma wanazozitoa, mazingira ya kazi, taaluma walizonazo pamoja na changamoto 80 wanazokabiliana nazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi yakinifu ulifanyika katika Ofisi za Halmashauri, Ustawi wa Jamii Makao Makuu, Taasisi za Serikali, Kidini na Taasisi zisizokuwa za Kiserikali ambazo zinatoa huduma za ustawi wa jamii nchini. Taarifa itatumika kuandaa mkakati wa kuongeza na kuimarisha nguvu kazi ya Maafisa Ustawi wa Jamii nchini. Matokeo ya tathmini hiyo, yanaonyesha upungufu mkubwa wa maafisa ustawi wa jamii katika Halmashauri na Taasisi za Serikali. Kati ya Maafisa Ustawi 3,367 wanaohitajika, waliopo ni 437 tu sawa na asilimia13.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Wakala na Taasisi zilizo chini ya Wizara. Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali. Katika mwaka 2011/2012, Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ilinunua vitendanishi vya kutosha, mitambo ya kisasa na kufanya matengenezo ya mitambo ambayo ilisaidia kutoa matokeo ya uchunguzi kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, jumla ya sampuli 6,944 zilichunguzwa, ambapo kati ya hizo sampuli 572 zilihusu chakula, dawa, mitidawa, majitaka, kemikali, bidhaa mbalimbali za viwandani na mali ghafi na sampuli 5,372 zilihusu makosa ya jinai kama ujambazi, ubakaji, mauaji, dawa za kulevya, vinasaba na toksikolojia. Matokeo ya uchunguzi yalichangia katika kulinda afya ya jamii, mazingira na kuharakisha usikilizwaji wa kesi zilizoko Mahakamani na kuleta utengamano katika jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara kupitia Wakala iliandaa kanuni za utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Vinasaba vya Binadamu, Sura ya 73 na rasimu za Waraka wa Baraza la Mawaziri kuhusu utungwaji wa Sheria ya Mkemia Mkuu wa Serikali na Sheria ya Kusimamia Taaluma ya wa Kemia. Aidha, Wakala iliandaa Mpango Mkakati wa Muda wa Kati (2012 – 2017) kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa Miaka Mitano ya Maendeleo ya Taifa (2011/2012 – 2015/2016).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara kupitia Wakala iliendelea kusimamia

na kutekeleza Sheria ya Udhibiti wa kemikali za Viwandani na Majumbani, Sura Na.182, kwa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara katika viwanda na maghala 280, vituo 12 vya bandari kavu, vituo vyote 18 vya mipakani, bandarini, viwanja vya ndege, migodi ya dhahabu ya North Mara, Geita, Kahama, Nzega na maeneo yanayozunguka migodi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya viwanda, maghala na migodi iliyokaguliwa, asilimia 56 ilikidhi matakwa ya sheria na kupatiwa hati za usajili na maeneo ambayo hayakukidhi matakwa ya sheria wahusika walipatiwa ushauri wa kurekebisha upungufu uliojitokeza ili hatimaye yaweze kupata usajili. Aidha, Wakala iliendesha mafunzo, kusambaza vipeperushi kwa wadau, na kutumia vyombo vya habari kuelimisha umma kuhusu matumizi sahihi na salama ya kemikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara kupitia Wakala ilitoa elimu kwa wataalamu wa afya wanaohusika na ufuatiliaji wa usafirishaji wa kemikali kwenda migodini na nje ya mipaka ya nchi kwa mujibu wa sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali Sura Na. 182, katika barabara kuu za Mikoa ya Pwani, Morogoro, Dodoma, Shinyanga, Mwanza, Kagera na Mara. Aidha, mchakato wa kufungua Ofisi ya Kanda ya Kati katika Manispaa ya Dodoma unaendelea baada ya Katibu Tawala Mkoa kuipatia Wakala majengo ya kukarabati katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, Wakala ilitoa mafunzo kwa Maafisa Afya wa mikoa 18 Tanzania Bara

ambao waliteuliwa kuwa Waratibu wa Kemikali wa Mikoa yao. Pia, mafunzo ya usimamizi wa kemikali yalitolewa kwa Maafisa Afya 16 wa Halmashauri za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wakala iliandaa nyaraka na kuziwasilishwa katika Taasisi ya Kusimamia Ithibati ya nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (*SADCAS*), ili kupata hati ya ithibati. Mafunzo ya ISO 9001:2008 yalitolewa kwa kushirikiana na Kampuni ya Ithibati ya Bureau Veritas na mpango wa kazi kuandaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Mamlaka ya Chakula na Dawa kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa iliende1ea kudhibiti usalama na ubora wa vyaku1a, dawa, vipodozi na vifaa tiba kwa kukagua maeneo 6,726 na ilisajili maeneo mapya 3,031 ya biashara hizo. Aidha, Mamlaka ilifanya tathmini ya maombi 1,036 ya kusajili dawa, 1,505 chakula, 866 vipodozi na 50 vifaa tiba. Vilevile, Mamlaka imekamilisha uundaji wa mfumo wa kusajili majaribio ya dawa kwa mtandao ili kurahisisha utumaji maombi ya usajili wa majaribio ya dawa na utambuzi wa majaribio ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Mamlaka iliendelea kudhibiti uingizaji nchini wa bidhaa za vyakula, dawa, vipodozi, na vifaa tiba ambapo ilikagua mizigo 2,116 katika vituo vya forodha ili kuhakiki usalama na ubora wa bidhaa hizo. Aidha, Mamlaka iliendelea kufanya uchunguzi wa kimaabara

wa vyakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba ili kuhakiki usalama, ubora na ufanisi wake kwa kuchunguza sampuli 965 katika maabara ambapo sampuli 859 sawa na asilimia 89 zilikidhi vigezo. Sampuli ambazo hazikukidhi vigezo bidhaa husika zilizuiliwa kuingizwa nchini au kusambazwa kwa matumizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Mamlaka iliendelea kukusanya na kutathmini taarifa za madhara ya matumizi ya dawa. Aidha, Mamlaka iliendelea kutekeleza Mpango wa Ufuatiliaji wa Usalama wa Dawa Mseto ya Malaria ya *Artemether/ Lumefantrine (ALu)* na *Dihydroartemisinin/ Piperaquine* ambapo jumla ya taarifa 7,840 zilikusanywa kati ya lengo la kukusanya taarifa 10,000. Vilevile, Mamlaka ilikusanya na kutathmini taarifa 143 za magonjwa yatokanayo na kula chakula na kutoa elimu kuhusu utayarishaji wa chakula salama na namna ya kupambana na milipuko ya magonjwa yatokanayo na vyakula visivyo salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Mamlaka iliendelea na utekelezaji wa Mpango wa Maduka ya Dawa Muhimu ambapo hadi sasa imetoa mafunzo kwa Watoa Dawa 10,109 na kusajili Maduka ya Dawa Muhimu 3,873. Aidha, Mamlaka ilitoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa watumishi 45 ili kuwajengea uwezo wa kukabiliana na changamoto mbalimbali za kiutendaji ikiwa ni pamoja na mabadiliko ya teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/12, Taasisi ya Chakula na Lishe ilitoa mafunzo ya uokaji

bidhaa zinazotokana na unga wa muhogo kwa wajasiriamali 90 katika Halmashauri za Mtwara na Masasi. Mafunzo hayo yamesaidia wasindikaji kuongeza nguvu ya soko, hasa katika kutoa ushawishi wa bei, hivyo kufanya kilimo cha zao hili kuwa cha manufaa kwa wakulima kwa kuwaongezea kipato. Aidha, wakulima 36 wa Mikoa ya Pwani na Mtwara walipatiwa mafunzo ya uendeshaji biashara ya zao la muhogo. Vilevile, vikundi 25 vya wasindikaji 86 vimeunganishwa katika mitandao 16 kwa kushirikiana na Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Tanzania (MVIWATA).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Taasisi iliratibu ugawaji wa matone ya vitamini A na dawa za minyoo zinazotolewa mara mbili kwa mwaka, mwezi Juni na Desemba. Jumla ya watoto 6,899,474 sawa na asilimia 100 ya walengwa walipata matone ya vitamini A na watoto 6,009,678 sawa na asilimia 99 ya walengwa walipata dawa za minyoo mwezi Novemba 2011, wakati wa zoezi lililojumuisha chanjo ya Surua, matone ya Polio, vitamini A na dawa za minyoo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Taasisi ilifanya uchambuzi kuhusu viwango vya upungufu wa vitamini A kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano na akina mama wanaonyonyesha na kubaini kuwa asilimia 33 ya watoto wenye umri chini ya miaka mitano na asilimia 37 ya wanawake walio kwenye umri wa kuzaa (miaka 15-49) wana upungufu wa vitamini A.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Taasisi iliendesha semina kwa viwanda vikubwa 10 ambavyo vinasindika unga wa mahindi, unga wa ngano na mafuta ya kula kuhusu umuhimu wa virutubishi nyongeza vinavyotokana na vyakula hivyo. Aidha, Taasisi iliendesha zoezi la utambuzi wa viwanda vidogo vidogo vya usindikaji ngazi ya kijiji katika Mikoa ya Iringa na Arusha ili viweze kupewa stadi za kuongeza virutubishi kwenye vyakula vya asili vya unga wa ngano, unga wa mahindi na mafuta ya kula.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Taasisi ilifanya utafiti wa kuboresha vyakula vya kulikiza na vinavyofaa kwa wanaoishi na virusi vya UKIMWI na wenye UKIMWI kwa kutumia mazao yanayopatikana hapa nchini. Matokeo ya awali yanaonesha kuwa matumizi ya unga mchanganyiko wa mahindi na soya huboresha afya na lishe ya watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI na wenye UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Taasisi ilitoa mafunzo kwa wataalam 29 kutoka maabara nane, kuhusu namna ya kupima viwango vya madini joto katika chumvi katika Mikoa ya Lindi, Mtwara Ruvuma, Iringa, Njombe na Mbeya. Aidha, Taasisi kwa kushirikiana na Wakala wa Takwimu wa Taifa ilizindua ripoti ya maendeleo ya matumizi ya chumvi yenye madini joto mwilini, mwezi Februari 2012. Ripoti hiyo ilionesha kwamba matumizi ya chumvi yenye madini joto kwa viwango mbalimbali katika kaya ni asilimia 82.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, ni asilimia 47 tu ya chumvi hizo ilikuwa na viwango madini joto vinavyotosheleza mahitaji ya mwili. Ripoti hiyo pia, imeonesha kuwa asilimia 55 ya wanawake walio kwenye umri wa kuzaa hususan mama wajawazito na asilimia 60 ya wanaonyonyesha bado wana upungufu mkubwa wa madini joto mwilini. Pia, ilitoa mafunzo ya utaalam wa kuchanganya chumvi na madini joto kwa wazalishaji chumvi 120 kutoka Pemba na Unguja.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Taasisi ilichapisha na kusambaza mwongozo, vijitabu na vipeperushi 5,000 na kuelimisha jamii kuhusu tabia bora ya kula na mtindo bora wa maisha. Aidha, Taasisi iligawa chakula dawa chenye virutubisho vya nishati kwa wingi kijulikanacho kama *Plumpy Nut* kwa watoto, watu wenye VVU na wenye utapiamlo katika Wilaya 16 za Mikoa ya Arusha, Dodoma na Singida.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, ilihamasisha viongozi 228 na kutoa mafunzo kwa watoa huduma za afya 384 wa wilaya hizo kuhusu matibabu ya utapiamlo kwa kutumia chakula dawa. Pia, Taasisi iliendelea kuimarisha tiba ya watoto wenye utapiamlo mkali kwa kutoa mafunzo kwa watoa huduma 300 kwenye Hospitali za Mikoa ya Tanga, Morogoro, Shinyanga, Arusha, Dodoma, Lindi, Mtwara, Ruvuma, Dar es Salaam, Mbeya, Pwani na Iringa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Taasisi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ilikamilisha Mkakati wa Taifa wa Lishe 2011 –

2016. Mkakati huo ambao ulizinduliwa tarehe 20 Septemba 2011 na Waziri Mkuu Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda unalenga kuharakisha na kupanua huduma za lishe nchini na hivyo kuboresha hali ya lishe ya wananchi ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa msukumo wa Kimataifa wa kupanua huduma za lishe duniani *(Scaling up Nutrition-SUN-Movement).* Mkakati huo umeshaanza kutekelezwa kwa kuhamasisha viongozi watendaji katika mikoa na wilaya zote nchini ili waweze kuingiza masuala ya lishe katika mipango na bajeti zao kwa mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/12, Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu iliendelea na utafiti wa awamu ya tatu wa chanjo ya malaria iitwayo *RTS,S/AS01E*. Utafiti huu umehusisha Vijiji 34 vya Wilaya za Handeni na Korogwe, ambapo jumla ya watoto 1,505 chini ya umri wa miezi 17 walipatiwa chanjo au chanjo kilinganishi. Ufuatiliaji unaendelea na watoto hao wanaendelea kupatiwa dozi ya *booster*.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo rasmi ya awali ya utafiti huu kwa watoto wa rika la miezi 5-17 yalitolewa mwezi Oktoba 2011 ambapo chanjo ilionekana kuwa ina ubora sawa na chanjo zitolewazo kwa watoto na inazalisha viini kinga vya kiwango cha juu. Aidha, chanjo hii inazuia malaria kwa kiwango cha asilimia 50 yaani nusu ya waliopatiwa chanjo walikingwa ugonjwa wa malaria kwa kipindi cha mwaka mmoja walichofuatiliwa. Utafiti unaendelea kuboresha ufanisi wa chanjo hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Taasisi ilikamilisha utafiti wa tathmini ya njia bora na rahisi ya kutoa chanjo dhidi ya virusi vya aina ya *Human Pappiloma* vinavyosababisha saratani ya shingo ya kizazi, kwa wanafunzi waliopo katika shule za msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utafiti ulionesha kwamba kutoa chanjo kwa watoto walioko katika darasa moja unawafikia walengwa wengi zaidi na ni nafuu kuliko kutoa chanjo kwa watoto walio na umri mmoja lakini wako katika madarasa tofauti. Utafiti ulionyesha chanjo hii inakubalika na jamii. Matokeo haya sasa yanatumiwa katika kutayarisha Mpango Mkakati wa Kitaifa wa utoaji wa chanjo dhidi ya virusi aina ya *Human Pappiloma*.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Taasisi iliendelea na majaribio ya chanjo mbalimbali za Virusi Vya UKIMWI (VVU) ili kutathmini usalama na uzalishaji wa kinga (*immunogenecity*) kwa kutumia chanjo ya vinasaba *(DNA)* iongezwayo nguvu na chanjo ya *Modified Vaccinia Ankara* (MVA). Utafiti huo wa awali ulifanikiwa kuonesha kiwango cha mwili wa binadamu kuweza kutengeneza kinga dhidi ya virusi vya UKIMWI na haina madhara kwa watumiaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Taasisi iliendelea kutekeleza mradi wa Utafiti wa Kutathmini Faida na Athari za Kutumia Dawa za Kifua Kikuu na Dawa za UKIMWI kwa pamoja kwa mgonjwa wa Kifua Kikuu na UKIMWI. Matokeo ya utafiti huo yataelekeza kama mgonjwa aanze kutumia *ARVs* wakati mmoja na tiba

ya Kifua Kikuu ama atumie *ARVs* baada ya tiba ya Kifua Kikuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Mpango wa Taifa wa Udhibiti wa Magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele uligawa dawa za kudhibiti magonjwa ya Matende na Mabusha, Usubi, Kichocho, Vikope na minyoo ya tumbo katika Wilaya 92 za Mikoa kumi na moja (11) ya Rukwa, Singida, Dodoma, Mtwara, Lindi, Pwani, Morogoro, Iringa, Mbeya, Ruvuma na Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya dozi milioni 25 zilitolewa kwa watu milioni 11 na kingatiba ya ugonjwa wa kichocho ilitolewa kwa watoto 1,600,000 walio shuleni. Aidha, Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Matende ulifanya utafiti katika Wilaya ya Tandahimba (Mtwara) kuangalia hali ya uambukizo wa vimelea vya Matende na Mabusha na kugundua kuwa uambukizo umepungua kufikia asilimia 0.96. Hii inaonesha kuwa maambukizi yamedhibitiwa katika Wilaya hii ya Tandahimba.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Taasisi iliendelea na utafiti ili kubaini ukubwa wa tatizo la magonjwa yasiyoyakuambukiza kwa lengo la kuyadhibiti. Taarifa za awali zinaonesha kuwa magonjwa haya yana sababisha vifo vya watu 134 kwa kila watu 100,000 na baadhi ya sababu hatarishi ni pamoja na utumiaji wa pombe kwa asilimia 33, uvutaji was sigara kila siku kwa asilimia 11.1. Aidha, ajali za barabarani zinachangia asilimia 43.7 ya vifo kutokana na magonjwa yasiyo ya kuambukiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Taasisi ilianza kufanya utafiti wa kubaini uwezo wa dawa inayotolewa na Mchungaji Mstaafu Ambilikile Mbetwa Mwaisapile katika kutibu UKIMWI na kisukari  kati ya magonjwa ambayo yalisemekana kutibiwa na mchungaji huyo. Utafiti wa kulinganisha wagonjwa wa UKIMWI na Kisukari waliokunywa na ambao hawakunywa dawa ya Mchungaji wanaoendelea kuhudhuria kiliniki za magonjwa hayo katika hospitali mbalimbali za rufaa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti huo ulianza mwezi Machi, 2012 unahusisha wagonjwa 200 wanaofuatiliwa kwa kupima vipimo vya maabara pamoja na damu, *CD4*, uzito wa wagonjwa na kuona ubora wa afya ya wagonjwa *(Quality of life)* ili kuona mabadiliko yoyote. Taarifa zao za awali zilizopo katika kiliniki kuanzia walipokunywa dawa hadi utafiti ulipoanza zilifuatiliwa na kujumuishwa katika taarifa ya utafiti. Matokeo ya awali ya utafiti yameonesha kuwa hakuna utofauti katika vipimo vya kimaabara pamoja na damu, *CD4*, uzito na ubora wa afya ya wagonjwa kati ya waliokunywa na wale ambao hawakunywa dawa ya Mchungaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Taasisi inafanya tathmini ya usalama na uwezo wa dawa ya *TASHACK* inayotumika kama tiba asili ya UKIMWI na Asasi ya Tanga *AIDS Working Group* (*TAWG*) inafanyiwa majaribio kubaini uwezo na usalama wake katika kudhibiti UKIMWI na kuboresha

afya za wagonjwa wa UKIMWI. Utafiti huo unahusisha wagonjwa 90 wanaoishi na virusi vya UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara kupitia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya iliendelea kusimamia jitihada za kupanua wigo wa Watanzania hasa maeneo ya vijijini kujiunga na utaratibu wa Bima ya Afya kupitia *NHIF* na Mfuko wa Afya ya Jamii. Aidha, hadi mwezi Machi 2012, Mfuko umeongeza wanufaika kutoka 5,198,545 waliokuwepo mwezi Juni, 2011 hadi wanufaika 6,269,163 sawa na asilimia 18.2 ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, Mfuko unakamilisha utaratibu wa kisheria wa kujumuisha wanachama kutoka katika vikundi vya watu binafsi na kumruhusu mwanachama anayetaka kuongeza wategemezi *(mPlus membership)* kuweza kufanya hivyo kwa kuzingatia kanuni zitakazowekwa. Pia, uboreshaji wa huduma za wanachama wa Mifuko hiyo uliendelea kufanyika kwa kuzingatia maoni ya wadau na tathmini ya uhai wa Mfuko.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ilifanya utafiti unaolenga kujua gharama za huduma za matibabu na wastani wa bei za dawa katika soko ili ziweze kuwa kigezo cha uhakika cha upangaji bei za dawa na huduma mbalimbali za matibabu kwa watoa huduma nchini ukiwemo Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, ujenzi wa kituo cha matibabu cha mfano katika Hospitali ya Mkoa wa Dodoma umefikia asilimia 82 ya utekelezaji na unatarajiwa kukamilika na kukabidhiwa mwezi Agosti 2012. Aidha, mradi wa ujenzi wa Kituo cha Matibabu cha Mfano katika Chuo Kikuu cha Dodoma uliotarajiwa kukamilika mwezi Septemba 2011 umefikia asilimia 55 ya utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni kutokana na mahitaji mapya ya kuwa na kitivo cha kufundishia madaktari. Vilevile, Mfuko umefungua ofisi tano katika Mikoa ya Mara, Ruvuma, Kigoma, Tanga na Rukwa na hivyo kufanya idadi ya ofisi zake kuwa katika mikoa 19. Pia, Mfuko ulifungua ofisi ya uratibu wa shughuli zake Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Mfuko ulifanya mikutano na wadau wake yenye lengo la kutoa elimu ili waweze kutambua umuhimu wa kutumia kadi wakati wa matibabu lakini pia, watoa huduma kutambua wajibu na haki zao. Mikutano hiyo ilifanyika katika mikoa yote ambapo wadau waliazimia kwa pamoja kulifanya suala la Mfuko wa *NHIF* na *CHF* kuwa ajenda ya kudumu ngazi ya Mkoa, Wilaya na Halmashauri. Hatua hii ni muhimu katika kutekeleza jukumu la Serikali la kufikia afya bora kwa wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Mfuko ulitimiza miaka 10 tangu kuanzishwa kwake ambapo ulitumia fursa hiyo kuwaenzi mashujaa wake akiwemo Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu,

Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, aliyekuwa Waziri wa Afya, Mheshimiwa Anna Abdallah na aliyekuwa Naibu Waziri wa Afya wa wakati ule, Mheshimiwa Daktari Hussein Ali Mwinyi, viongozi waandamizi, wanachama, watoa huduma na waandishi wa habari waliojitolea bila kuchoka ili kufanikisha malengo ya kuanzishwa kwa Mfuko huu. Hii ni hatua kubwa iliyofikiwa, kwani hata jumuiya ya Kimataifa kupitia Shirika la Taasisi ya Hifadhi ya Jamii Duniani *(International Social Security Association)* imeupatia tuzo Mfuko na kuutangaza kuwa Mfuko wa mfano Barani Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Ustawi wa Jamii. Katika mwaka 2011/2012, Taasisi iliendelea kufundisha na ilidahili wanafunzi 2,698. Aidha, Taasisi ilifanya mapitio ya Mitaala yote kuanzia ngazi ya Cheti hadi Shahada na kuiwasilisha Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (*NACTE*) ambalo limeipitia na kuiridhia itumike kuanzia mwaka wa masomo 2011/2012 hadi 2015/2016 na tarehe 7 Desemba, 2011 Taasisi ilipewa ithibati mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, kwa kushirikiana na Chuo cha Illinois kutoka Marekani Taasisi ilianza kukusanya taarifa ili kubaini uhitaji wa mafunzo ya Shahada ya Uzamili ya Ustawi wa Jamii na rasimu ya awali ya mtaala wa mafunzo haya itawasilishwa kwenye Baraza kwa ajili ya kuridhiwa na hivyo kuanza kutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Taasisi ya Ustawi wa Jamii kwa kushirikiana

na Idara ya Ustawi wa Jamii na *UNICEF* iliendelea kutoa ushauri elekezi katika masuala ya ulinzi wa mtoto katika Halmashauri za Wilaya ya Temeke, Hai na Magu. Aidha, Taasisi ilifanya utafiti wa malezi mbadala kwa watoto chini ya miaka 18 na hali halisi ya ukiukwaji wa haki za watoto Tanzania Bara na Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti huo ambao ulifanyika katika mikoa 14 umebaini kuwa kulikuwa na watoto takribani 3,000,000 ambao walikuwa na malezi mbadala wakilelewa na ndugu wengine ambao si wazazi wao, vikongwe na watoto wenzao. Licha ya kukosa malezi ya msingi, mambo mengine yaliyogundulika ambayo watoto hawa huyakosa ni pamoja na ulinzi, elimu na chakula. Matokeo yake watoto hawa hupata manyanyaso na kukosa matumaini katika maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Taasisi ya Ustawi wa Jamii kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, ilitoa mafunzo ya muda mfupi kwa Maafisa Ustawi Wasaidizi 250. Aidha, Taasisi kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Kwa Zulu Natal na *African Center for Children* ya Afrika ya Kusini ilitoa mafunzo ya cheti kwa mtindo wa elimu ya masafa *(distance learning)* katika kuwahudumia watoto, familia na jamii zilizoathirika na Virusi Vya UKIMWI (*VVU*) na UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo hayo yalifadhiliwa na Shirika la *Psychosocial Wellbeing For All Children.* Wanafunzi waliohitimu mafunzo hayo kwa mwaka 2011/2012 walikuwa 106. Vile vile, Taasisi ya

Ustawi wa Jamii kwa kushirikiana na *UNICEF* ilitoa mafunzo kuhusu ulinzi wa mtoto na jinsi ya kujumuisha masuala hayo ya ulinzi wa mtoto katika mitaala ya kufundishia ya Taasisi ya Ustawi wa Jamii, Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini Dodoma na Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Miradi ya Maendeleo; katika mwaka 2011/2012, Wizara ilikamilisha ujenzi wa wodi za wagonjwa katika Taasisi ya Saratani *Ocean Road* na iliendelea na ukamilishaji wa Jengo la matibabu ya Saratani Bugando ambapo awamu ya kwanza ya ujenzi huo unatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2012. Aidha, ujenzi wa maktaba ya Taasisi ya Ustawi wa Jamii unaendelea na umekamilika kwa asilimia 60.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ilikamilisha ujenzi wa kituo cha Tiba na Mafunzo ya Upasuaji wa Moyo katika hospitali ya Taifa Muhimbili na taratibu za ununuzi wa vifaa na vifaa tiba unaendelea. Aidha, Wizara ilinunua na kusambaza vifaa na vitendanishi vya Mradi wa Taifa wa Damu Salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012 Wizara iliendelea kutekeleza mradi unaofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika wa Kupunguza Vifo vya Mama na Mtoto katika Mikoa ya Mara, Mtwara na Tabora ambapo ukarabati na upanuzi wa majengo umeendelea. Aidha, ukarabati na upanuzi wa zahanati 76 unaendelea ambapo kati ya hizo 44, zilikamilika na kukabidhiwa, 14 ziko katika hatua za mwisho kukamilika na 18 bado ujenzi haujaanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, vituo vya afya vya Nyasho, Murangi, Kiagata, Ikizu, Kasahunga, Nata, Iramba, Kinesi, Muriba, Nyarwana, Likombe, Kitere, Nanguruwe, Mahurunga, Chiwale, Michiga, Chihangu, Mahuta, Namikupa, Kitunda, Ipuge na Choma vipo katika hatua ya mwisho za kufungiwa vifaa vya kutolea huduma na nyumba 19 za watumishi katika vituo hivi tayari zimekabidhiwa. Pia, Majengo ya upasuaji katika hospitali za Musoma, Mugumu, Tarime, Kitete na Mazinge zipo katika hatua za mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2011/2012, Wizara ilifanya ukarabati wa bweni la wasichana katika kambi ya watoto watukutu Irambo (Mbeya) na kujenga chuo cha watu wenye ulemavu cha Masiwani (Tanga) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 70. Aidha, ujenzi wa kambi ya Wazee Fungafunga (Morogoro) ulifikia asilimia 80 ya utekelezaji. Vile vile, ujenzi wa kambi ya watoto watukutu Mtwara awamu ya kwanza umekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mgomo wa Madaktari nchini; katika utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2011/2012, Wizara yangu imekuwa ikikabiliana na changamoto mbalimbali, ikiwemo migomo ya Madaktari iliyotokea kati ya Januari na Juni, 2012. Chimbuko la migomo hii ni kucheleweshwa kwa posho ya Madaktari walio katika mazoezi kwa vitendo (*interns*) na madai ya Madaktari.

Mheshimiwa Naibu Spika, madai hayo ni pamoja na kuongezewa kiwango cha mshahara wa Madaktari

wanaoanza kazi kutoka sh. 957,700.00 hadi kufikia sh. 3,500,000.00, posho ya kuitwa kazini baada ya saa za kazi *(On call allowance)* kuwa asilimia 10 ya mshahara, posho ya Mazingira Hatarishi *(Risk Allowance)* kuwa asilimia 30 ya mshahara; Madaktari kupewa nyumba au posho ya nyumba sawa na asilimia 30 ya mshahara na posho ya mazingira magumu *(Hardship Allowance)* ya asilimia 40 ya mshahara.

Mheshimiwa Naibu Spika, madai mengine ni posho ya usafiri ya asilimia 10 ya mshahara, au kukopeshwa magari; kupewa *Green Card* za Bima ya Afya; kurekebisha malipo ya posho ya kuchunguza maiti; kuchukua hatua dhidi ya viongozi Wakuu wa Wizara; kupatiwa chanjo ya *Hepatitis B;* kuboresha huduma zinazotolewa kwa wananchi; kurudishwa kazini kwa *interns* waliopangiwa vituo vingine na Viongozi kulazimisha rufaa ya matibabu nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilichukua hatua mbalimbali za kushughulikia madai hayo, ikiwa ni pamoja na kuunda Kamati chini ya Uenyekiti wa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Kamati ilifanya mazungumzo na wawakilishi wa Madaktari kuhusu madai 12 yaliyowasilishwa Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, yafuatayo yalitekelezwa na Serikali:-

- Kuongeza kiwango cha posho ya kuitwa kazini baada ya saa za kazi na kuanza kulipa rasmi mwezi Februari 2012;

- Kutenga fedha katika bajeti ya mwaka 2012/13 kwa ajili ya utoaji wa chanjo dhidi ya maambukizi ya *Hepatitis B;*

- Kutoa *green card* ya Bima ya Afya kwa Madaktari wote;

- Madaktari kukopeshwa fedha kwa ajili ya ununuzi wa magari kwa kuzingatia taratibu zilizopo za utumishi wa umma;

- Kuboresha huduma za afya nchini kwa kuongeza bajeti ya Sekta ya afya kwa ajili ya kuboresha miundombinu, ununuzi wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi na kuboresha maslahi ya watumishi;

- Kuongeza posho ya kuchunguza maiti kutoka sh. 10,000.00 hadi sh. 100,000.00; kurudishwa Muhimbili kwa Madaktari *interns* waliokuwa wamerudishwa Wizarani katika mgomo wa awamu ya kwanza mwezi Februari 2012;

- Uboreshaji wa bajeti kwa ajili ya miundombinu ya hospitali zetu na ununuzi wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi utawezesha wagonjwa wengi zaidi kupata huduma za afya ndani ya nchi wakiwemo viongozi wa nchi na kuondolewa kwa viongozi wakuu wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hatua hizo zilizochukuliwa na Serikali ili kushughulikia madai yao, madaktari hawakuridhia na waligoma tena kwa mara

ya tatu kuanzia tarehe 23/06/2012 hadi Mheshimiwa Rais alipoagiza kuwa madaktari ambao hawakubaliani na mshahara unaolipwa sasa na Serikali wawe huru kuacha kazi kwa hiari yao kwa sababu Serikali haina uwezo wa kulipa mshahara wanaotaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa agizo hili ulisababisha jumla ya Madaktari (*interns*) 372 kati 763 waliopo kurudishwa Wizarani kwa Katibu Mkuu ili achukue hatua nyingine kwa mujibu wa taratibu za kisheria kupitia Baraza la Madaktari na Madaktari wa Meno – Tanganyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulithibitishia Bunge lako Tukufu kwamba Serikali ina nia thabiti ya kuendelea kuboresha hali ya utoaji huduma za afya nchini kote. Aidha, itaendelea kuboresha maslahi ya watumishi wote wa kada za afya na ustawi wa jamii nchini. Vile vile napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza watumishi wote ambao waliendelea kutoa huduma za afya wakati wa mgomo, shukrani za pekee ziwaendee wafanyakazi wote wa sekta ya afya wa vituo vya kutolea huduma vya Serikali, Mashirika ya Dini na binafsi ambao hawakushiriki katika mgomo kwa kuonesha moyo wa uzalendo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Serikali natoa masikitiko kwa kitendo alichofanyiwa Daktari Stephen Ulimboka, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Madaktari kwa kupigwa na kuumizwa. Natoa pole na kumuombea apone haraka ili aungane na familia yake na Watanzania wenzake katika ujenzi wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mipango na Maombi ya Fedha ya Bajeti kwa mwaka 2012/13. Maeneo yaliyopewa kipaumbele katika Bajeti ya Mwaka 2012/13. Wizara itaendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia vipaumbele vifuatavyo:-

(a) Kuhakikisha upatikanaji wa vifaa pamoja na dawa katika vituo vya afya na ustawi wa jamii kwa kufanya ukarabati na ujenzi wa majengo ya kutolea huduma, kuhakikisha upatikanaji wa huduma za damu salama katika ngazi zote na vifaa tiba na vitendanishi vyenye viwango stahiki;

(b) Kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za uzazi, watoto pamoja  na watoto wachanga, ikiwa ni pamoja na huduma za uzazi salama wakatiwa ujauzito, kujifungua na baada ya kujifungua, huduma za chanjo na mnyororo baridi na huduma rafiki za uzazi kwa vijana katika vituo vya kutolea huduma;

(c) Kuimarisha udhibiti wa magonjwa yakuambukiza, yasiyo ya kuambukiza pamoja na yale yaliyokuwa hayapewi kipaumbele. Katika kutekeleza hili, Wizara itaendeleza utoaji wa elimuya afya, itaimarisha mikakati iliyopo inayolengakatika kuimarisha mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI, Malaria, Kifua Kikuu, Magonjwa yasiyo ya kuambukiza na yale yaliyosahaulika;

Hii inajumuisha kuhakikisha upatikanaji wa huduma za uchunguzi pamoja na matibabu kwa magonjwa haya pamoja na kubuni mbinu mpya za udhibiti. Aidha, Wizara itaratibu, itasimamia na itafuatilia afua

mbalimbali za afya ya mazingira; itamarisha shughuli zinazolenga katika utoaji wa huduma za lishe ikiwemo kuongeza virutubishi katika vyakula na itaimarisha udhibiti wa usalama na ubora wa vyakula, dawa, vipodozi, vifaa tiba na vitendanishi; na

(d) Kuhakikisha upatikanaji na usawa wa huduma za afya na ustawi wa jamii kwa kuimarisha utoaji wa huduma kwa makundi maalum wakiwemo watoto walio katika mazingira hatarishi, watu wenye ulemavu na wazee; ukarabati na ujenzi katika Taasisi zinazotoa huduma za Ustawi wa Jamii; kuwezesha upatikanaji wa haki kwa watoto walio katika mkinzano na sheria na kuhamasisha wananchi kujiunga na huduma za bima ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/13, Wizara inaomba kiasi cha sh. 298,228,037,000.00 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, sh. 188,464,956,408.00 zinaombwa kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Taasisi zilizo chini yake. Kiasi cha sh. 109,763,080,592.00 kinaombwa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Fedha hizi zitatumika kutekeleza kazi zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utawala na rasilimali watu; katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea na utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM) kwa kupanua na kukarabati vyuo ili kuongeza idadi ya wanafunzi watakaodahiliwa na vyuo. Aidha, jitihada za kuimarisha ubora wa mafunzo vyuoni zitafanyika kwa kuongeza idadi ya wakufunzi na vifaa vya kufundishia.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, Wizara chini ya fungu 52, itaajiri wataalam 89 wa kada mbalimbali na kuwapandisha vyeo watumishi 724. Pia, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma itaendelea kuwapanga wataalam waliomaliza mafunzo ili kuboresha huduma katika vituo vya kutolea huduma za afya na ustawi wa jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara itaandaa Mwongozo wa Sera ya Watumishi wa Sekta ya Afya na Ustawi Jamii kwa lengo la kuweka mikakati itakayoboresha upangaji, uendelezaji na matumizi bora ya rasilimali watu. Aidha, mwongozo huo utatumika katika uandaaji wa Mpango Mkakati wa Watumishi wa Afya na Ustawi wa Jamii wa miaka mitano (2014 - 2019).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara itaweka mfumo wa takwimu za watumishi wa afya na ustawi wa jamii katika mikoa minne mipya ya Geita, Katavi, Njombe na Simiyu na jukumu hili litakamilika ifikapo Septemba 2012. Aidha, jitihada za kuimarisha mifumo zitaendelea ikiwemo mfumo wa taarifa za vyuo kwa kutoa mafunzo ya uendeshaji mifumo hiyo na matumizi bora ya takwimu. Mafunzo haya yatatolewa kwa Maafisa katika ngazi za Wilaya, Mikoa na Makao Makuu ya Wizara na Taasisi zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara itapitia mitaala ya Mafundi Sanifu Meno na Mafundi Sanifu Mionzi katika ngazi ya

stashahada. Aidha, Wizara itaandaa moduli za utekelezaji wa mitaala sita ya Shahada za Ualimu wa Uuguzi, uuguzi wa magonjwa ya akili, watoto, macho, afya ya jamii pamoja na menejimenti katika chumba cha upasuaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu sera na mipango; mwaka 2012, Serikali imejiunga na mpango wa uendeshaji wa shughuli za serikali kwa uwazi. Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ni moja kati ya Wizara zilizochaguliwa kwa ajili ya kufanyiwa majaribio ya mpango huu. Katika utekelezaji wa mpango huu, dhana ya uwazi itaimarishwa kwa kuhakikisha kuwa taarifa za kiutendaji za Wizara ikiwemo taarifa zinazohusu maombi na upatikanaji wa dawa zinapatikana kwa wananchi katika ngazi za kutolea huduma. Aidha, Wizara itaendelea kuimarisha mahusiano baina yake na Asasi za kiraia kupita mikutano mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo ni kupata maoni na kutoa mrejesho wa masuala mbalimbali kwa nia ya kuboresha utoaji huduma. Vilevile, katika kutekeleza dhana ya uwajibikaji, Wizara itasimamia utekelezaji wa mkataba wa kutoa huduma katika ngazi zote pamoja na kuimarisha mfumo wa kupokea na kushughulikia malalamiko kwa wakati. Vile vile, Wizara itaimarisha Mfumo wa Ukusanyaji Takwimu (MTUHA) ili kupata takwimu sahihi na kusimbaza kwa walengwa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara itafuatilia utekelezaji wa majukumu ya Bodi na Kamati za Afya katika Halmashauri 60 kati ya

Halmashauri 127 zilizoanzisha vyombo hivyo. Aidha itahimiza Halmashauri za Wilaya za Nanyumbu, Longido, Rorya, Siha na Halmashauri ya Mji wa Kibaha kukamilisha taratibu za kuwa na hati rasmiili kuunda Bodi za Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inashiriki kikamilifu katika maandalizi ya Sensa ya Watu na Makazi, itakayofanyika tarehe 26 Agosti, 2012. Hii ni kwa kutambua umuhimu wa takwimu na viashiria mbalimbali ambavyo hutumika katika kuandaa mipango na mikakati mbalimbali ya kisekta.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Sensa tutapata mambo mengi kama kutambua idadi ya walengwa mbalimbali, kasi ya kuongezeka watu na ya vifo kwa watoto wachanga, watu wazima na akina mama kutokana na uzazi pamoja na umri wa kuishi. Matokeo ya Sensa yatawezesha uboreshaji wa Sera, Mipango na Mikakati kwa lengo la kuimarisha huduma za afya nchini. Hivyo, nawaomba wananchi kwa ujumla kushiriki kikamilifu katika zoezi la Sensa kwa manufaa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu teknolojia ya habari na mawasiliano; katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kuboresha na kuimarisha mtandao wake wa mawasiliano wa intaneti ili kufanikisha utoaji na upokeaji wa taarifa kwa wakati. Aidha, Wizara itaanzisha mtandao wa mawasiliano kwa njia ya simu *(telemedicine)* kwa Madaktari na Matabibu wa hospitali za rufaa nchini wakati wa utoaji wa huduma za afya bila gharama yoyote. Mpango huu

unatarajiwa kuanza kutekelezwa kuanzia mwezi Oktoba 2012. Matarajio ni kuendeleza huduma hizi kikanda kuendana na mfumo uliopo wa rufaa za wagonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu usimamizi wa Fedha zinazoelekezwa katika Sekta ya Afya na Ustawi wa Jamii; katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kutekeleza Sera ya Serikali ya kuboresha mfumo wa utunzaji kumbukumbu za watumishi, ununuzi, mikataba na malipo. Aidha, itaendelea kuweka mitandao ya malipo kwa miradi ya Wizara na Mabaraza ya Kitaaluma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ukaguzi wa ndani; mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kufanya ukaguzi wa usambazaji wa dawa, uhakiki wa mishahara ya watumishi, matumizi ya fedha na ukaguzi wa miradi iliyoko chini ya Wizara. Aidha, itaendelea kuchukua hatua kulingana na matokeo ya ukaguzi kwa lengo la kuimarisha mifumo ya udhibiti wa ndani na usimamizi wa rasilimali za Serikali ili kuongeza tija na ufanisi katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na baada ya kupata maamuzi katika ngazi husika Serikalini, inatarajia kuwasilisha Bungeni kwa mara ya kwanza Muswada wa kutunga Sheria ya Kuanzisha Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, muswada wa mapendekezo ya kutunga Sheria ya Kusimamia Taaluma ya Kemia, Muswada wa Sheria mpya ya Kudhibiti Matumizi ya

Bidhaa za Tumbaku na Sheria ya Kusimamia Huduma za Afya Nchini (*The National Health Services Act*).

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara itaandaa nyaraka mbalimbali za Baraza la Mawaziri ili kuwasilisha Serikalini katika ngazi husika kwa ajili ya maamuzi, mapendekezo ya Miswada ya kutunga Sheria Mpya ya Madaktari na Madaktari wa Meno, kutunga Sheria Mpya ya Wazee, Mabadiliko ya Sheria ya Hospitali ya Taifa Muhimbili, Sura ya 150, mapendekezo ya Sheria ya kuwianisha Mifuko ya *CHF* na *NHIF*, mapendekezo ya Marekebisho ya Sheria iliyoanzisha Taasisi ya Chakula na Lishe na mapendekezo ya mabadiliko ya Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi, Sura ya 219.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kuandaa Kanuni za Sheria mbalimbali katika sekta ya Afya na Ustawi wa Jamii na kutoa mafunzo kuhusu Sheria na Kanuni mbalimbali kwa watumishi wa kada ya afya na ustawi wa jamii. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, itaandaa mikataba mbalimbali ya ushirikiano na taasisi mbalimbali za Kitaifa na Kimataifa, kulingana na mahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, kusimamia utekelezaji wa mikataba hiyo katika sekta ya Afya na Ustawi wa Jamii. Pia, Wizara itaandaa vipeperushi na nakala za sheria za afya na ustawi wa jamii kwa ajili ya kusambaza kwa watendaji na wananchi kwa ujumla ili kujenga zaidi uelewa na utekelezaji wa sheria hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mabaraza ya Kitaaluma, katika mwaka 2012/2013, Wizara kwa kushirikiana na Baraza la Madaktari Tanganyika litafanya ukaguzi wa hospitali zinazofundisha mafunzo kwa vitendo pamoja na kukagua hospitali za rufaa za mikoa ili kuangalia ubora wake kwa ajili ya kutumika katika kutoa mafunzo kwa vitendo kwa Madaktari.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la ukaguzi huo ni kuongeza idadi ya hospitali zinazoweza kuhimili idadi ya Madaktari wanaohitimu katika vyuo vikuu. Aidha, Baraza litatengeneza kanuni za kuwasilisha malalamiko dhidi ya wanataaluma pamoja na kupitia na kusambaza miiko na maadili ya taaluma ya Udaktari.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara kupitia Baraza la Uuguzi na Ukunga itaendelea na ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Maadili kwa Wauguzi na Wakunga. Aidha, Baraza litaanzisha mpango wa kuhakiki ubora wa kitaaluma kwa Muuguzi na Mkunga kupitia utaratibu wa kufuatilia mafunzo ya kujiendeleza kazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara itatayarisha Kanuni za Utendaji Kazi za Famasi (*Pharmacy Practice Regulations*), mwongozo wa Kusajili Sehemu za Kutolea Huduma ya Dawa na Mwongozo wa Viwango vya Famasi za Hospitali. Aidha, kanuni mpya za maduka ya dawa muhimu zitatayarishwa na Wizara itafanya ukaguzi katika sehemu za kutolea huduma ya dawa ili kuhakikisha kuwa huduma inayotolewa ni sahihi. Vile vile, Wizara

itaendelea kuelimisha wadau kuhusu Sheria ya Famasi ya mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara kupitia Baraza la Maabara litakamilisha Mpango Mkakati wa Baraza na Mwongozo wa Miiko na Maadili ya Wataalam wa Maabara. Aidha, Baraza litaandaa Mwongozo wa Uanzishwaji wa Vyuo vya Maabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara kupitia Baraza litaendelea kupitia mitaala ya vyuo vya kufundisha wataalam wa radiolojia nchini na kukagua vyuo hivyo. Aidha, Baraza litatayarisha Mpango Mkakati wa Baraza kwa kipindi cha miaka mitano (2012/2013 – 2016/2017) na Kanuni za Huduma za Radiolojia (*Medical Radiology and Imaging Practice Regulations*). Vile vile, Baraza litaendelea kushirikiana na Tume ya Taifa ya Mionzi ili kuhakikisha kuwa huduma za radiolojia zinazotolewa ni salama na zenye ubora unaokubalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara kupitia Baraza la Optometria itaendelea kusajili Wataalam wa Kurekebisha Upeo wa Macho Kuona kwa mujibu wa Sheria ya Optometria Na. 12 ya mwaka 2007. Aidha, Wizara kupitia Baraza la Wataalam wa Afya ya Mazingira litakamilisha kazi ya kutengeneza Mpango Mkakati wa Baraza 2012- 2017 na kuendelea na Usajili wa wataalam wa Afya ya Mazingira nchini kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa itaendelea na usajili wa Waganga na Wakunga wa tiba asili na tiba mbadala na wasaidizi wao na pia, vituo vya tiba asili na tiba mbadala. Aidha, Wizara itaanzisha usajili wa wauza dawa na maduka ya dawa asili katika Halmashauri za Miji, Manispaa na Majiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, Wizara itatoa mafunzo kwa waratibu wa Halmashauri na Mikoa ya Tabora, Kigoma, Shinyanga, Kagera, Mwanza, Simiyu na Mara kuhusu usajili, sheria, kanuni na miongozo ya tiba asili na tiba mbadala. Pia, Wizara itaelimisha jamii kuhusu umuhimu wa kuzingatia matumizi ya dawa asili kupitia waganga wanaotambulika katika maeneo yao kwa usalama wa afya zao.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Bodi ya Ushauri ya Hospitali Binafsi itaendelea kusajili vituo binafsi vya kutolea huduma za afya. Aidha, Bodi itaendelea na ukaguzi wa vituo vya kutolea huduma vya afya vya umma na binafsi ili kuhakikisha kuwa wananchi wanapata huduma za afya zenye ubora na viwango vinavyokubalika nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, Wizara kupitia Bodi ya Maabara Binafsi za Afya itaendelea kusajili maabara mpya na maduka yanayouza vifaa vya maabara, kuratibu na kukagua maabara na maduka hayo. Bodi itaendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa ofisi yake huko Buyuni-Chanika katika Manispaa ya Ilala.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma za kinga, Epidemiolojia na Udhibiti wa Magonjwa, katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kufuatilia mwenendo na viashiria vya milipuko ya magonjwa pamoja na kudhibiti magonjwa kwa kutumia mbinu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuimarisha ushirikishwaji wa jamii. Aidha, Wizara itaendelea kutoa chanjo za kukabiliana na magonjwa ya homa ya uti wa mgongo pamoja na kichaa cha mbwa. Chanjo ya kichaa cha mbwa itatolewa kwa ushirikiano na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, Wizara itatoa chanjo kwa awamu dhidi ya ugonjwa wa homa ya ini *(Hepatitis B)* kwa wafanyakazi wa sekta ya afya na itaendelea kufanya ufuatiliaji wa ugonjwa wa mafua makali ya ndege katika vituo maalum vilivyopo sehemu mbalimbali nchini (*sentinel surveillance sites*). Pia, Wizara itaendelea kutoa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi kuhusu kukabiliana na magonjwa ya milipuko ili kuweza kuimarisha uwezo wa wataalam kukabiliana na magonjwa hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Malaria; katika mwaka 2012/2013, Wizara itaandaa Mpango Mkakati mpya wa kudhibiti malaria (2014–2020) ambao utalenga zaidi katika namna ya kuishirikisha jamii katika Kinga ya Malaria, hususan kuondoa mazalio ya mbu katika sehemu za makazi, kushiriki katika upulizaji wa viuatilifu majumbani pamoja na kwenye mazalio. Aidha, upuliziaji wa viuatilifu majumbani na katika mazalio ya mbu

utatekelezwa katika mikoa ya Mtwara, Lindi na Ruvuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika mwaka 2012/2013, Wizara itaandaa utaratibu wa kudumisha mafanikio yaliyofikiwa *Keep-up Strategy* ya kuwepo kwa vyandarua majumbani katika kila kaya kwa zaidi ya asilimia 80, ili kuhakikisha kuwa kiwango hicho hakishuki na kuinua kiwango cha matumizi ya vyandarua, hapa nchini. Utaratibu utakaotumika utahusu mchanganyiko wa kugawa vyandarua vyenye dawa *(LLINs)* kupitia shule za msingi na sekondari pamoja na kuendelea na Hati Punguzo, ili kupata njia mbadala yenye ufanisi katika ugawaji wa vyandarua.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kupulizia dawa ya ukoko kwenye kuta za nyumba katika wilaya 18 za mikoa mitatu ya Kanda ya Ziwa: Mwanza, Kagera na Mara. Aidha, Wizara itaendelea kutekeleza Mpango wa kuangamiza viluwiluwi vya mbu waenezao malaria katika mazalio yao (*larviciding*) katika kata zote 90 za Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, katika kuhakikisha Mpango wa kuangamiza viluwiluwi wa mbu, unakuwa endelevu, Serikali kupitia Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) na kwa kushirikiana na Serikali ya Cuba, inajenga kiwanda cha kuzalisha viuadudu (*biolarvicide*) vinavyotumika kuua viluwiluwi vya mbu katika mazalio. Gharama za mradi huu zinalipwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa asilimia 100. Kiwanda hicho kinajengwa

Wilayani Kibaha, Mkoa wa Pwani. Pia, Wizara itaendelea kuhakikisha kuwa tiba sahihi ya malaria inapatikana na inatolewa katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya na kukamilisha mwongozo mpya wa matibabu ya malaria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mpango wa Kudhibiti Kifua Kikuu na Ukoma; katika mwaka 2012/2013, Wizara itaandaa Mwongozo wa Kuchunguza na Kutibu Kifua Kikuu pamoja na Maambukizi ya VVU kwa Watoto ili kuimarisha huduma hizi nchini. Aidha, Wizara itashirikiana na wadau kutoa mafunzo kwa watumishi wa afya 500 ili kuboresha huduma hizi kwa watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, Wizara itaanda Mwongozo wa Kuanzisha Utoaji Huduma za Kifua Kikuu katika Maeneo ya Kazi kwa nia ya kupunguza maambukizi na vifo vitokanavyo na kifua kikuu katika maeneo ya kazi. Pia, Wizara itaandaa mwongozo wa kisera wa kushirikisha Asasi zisizo za Kiserikali kuweka mikakati na kusimamia utekelezaji wake ili kuboresha ushiriki wa jamii katika udhibiti wa kifua kikuu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kutoa huduma kwa wagonjwa wa kifua kikuu sugu wapya 50 katika hospitali maalum ya Kibong'oto. Aidha, Wizara itashirikisha watoa huduma ya afya katika ngazi ya jamii katika mikoa mitano ya Dar es Salaam, Mwanza, Mara, Manyara na Arusha katika kutoa huduma ya kifua kikuu sugu kwa lengo la kupanua wigo wa huduma hizi baada ya wagonjwa

kumaliza matibabu ya awali katika hospitali ya Kibong'oto.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara itaandaa mpango kazi wa miaka mitano wa kuimarisha uchunguzi wa kifua kikuu katika maabara ili kuboresha huduma hizi katika hospitali za mikoa na wilaya. Aidha, Wizara inatarajia kutoa mafunzo ya teknolojia mpya (*Gene expert*) ya kugundua vimelea sugu ya kifua kikuu kwa wataalam wa maabara wapatao 100 katika ngazi za Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, Wizara itaendelea kuimarisha huduma za ugunduzi na tiba kwa watu wenye ugonjwa wa ukoma hasa katika mikoa mitano ya Morogoro, Mtwara, Lindi, Dar es Salaam na Rukwa ambayo bado kuna wagonjwa wengi. Pia, Wizara itaimarisha uraghibishi kwa watu walioathirika na kupata ulemavu wa kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mpango wa Kudhibiti UKIMWI; katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kupanua huduma za kinga, matunzo na tiba kwa ajili ya UKIMWI, kwa kuzingatia makundi maalum. Lengo ni kuhakikisha huduma zote zinapatikana kwa wote ifikapo mwaka 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango Mkakati wa Kudhibiti UKIMWI wa Sekta ya Afya (*Health Sector HIV Strategic Plan II (*2008 – 2012)) utapitiwa na mkakati mpya wa tatu utaandaliwa kwa kipindi (2013 – 2018). Wizara itapanua huduma za matunzo na tiba kwa kujenga uwezo wa Kamati za Afya za Mikoa na Wilaya

kutekeleza hatua za kuwezesha utoaji wa huduma hizi. Idadi ya wagonjwa wanaotumia dawa za UKIMWI itaongezeka zaidi ya 564,723 waliopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, Wizara itaendelea kusambaza mashine zipatazo 150 kwa ajili ya kupimia *CD4* kwa watu wanaoishi na VVU. Huduma za ushauri nasaha na kupima uambukuzi wa VVU zitapanuliwa na kufikishwa katika maeneo ya vijijini. Wizara itaendelea kufanya uhamasishaji wa jamii na kutoa elimu juu ya mambo mbalimbali yanayohusu VVU na UKIMWI na magonjwa yanayoambukizwa kwa njia ya ngono.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendeleza juhudi za kupunguza ugonjwa wa kifua kikuu kwa wagonjwa wenye uambukizo wa VVU kwa kuwafanyia uchunguzi na kuwapa dawa ya kukinga maambukizi ya ugonjwa huo (*isoniazid preventive therapy*). Aidha, huduma ya tohara kwa wanaume itapanuliwa kupitia kampeni maalum katika Mikoa ya Mwanza, Tabora, Kagera, Iringa, Shinyanga, Rukwa, Mara na Mbeya katika lengo la kuzuia ongezeko la maambukizi. Vile vile, Wizara itapanua huduma za matunzo kwa wanaoishi na virusi vya UKIMWI na wagonjwa wa UKIMWI katika ngazi ya jamii (*home based care).*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara kwa kushirikiana na wadau itaendelea kuimarisha huduma ya afya ya uzazi na mtoto nchini kwa kununua na kusambaza dawa na vifaa vya uzazi wa mpango, vikiwemo; vidonge,

sindano, vipandikizi, vitanzi na kondomu. Aidha, katika juhudi za kuboresha huduma ya afya ya uzazi na mtoto, Wizara itaendelea kujenga uwezo wa watoa huduma ya afya ya uzazi na mtoto katika ngazi ya vituo vya kutolea huduma na ngazi ya jamii. Mafunzo yatatolewa katika nyanja za uzazi, stadi za kuokoa maisha, uzazi wa mpango, huduma ya mama aliyepata matatizo ya kuharibika mimba na huduma rafiki kwa vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kufanya upanuzi wa huduma ya uchunguzi wa saratani ya shingo ya kizazi na kutoa mafunzo kwa watoa huduma. Aidha, Wizara itaendelea kununua na kusambaza vifaa vya uzazi (*delivery pack*) na kuzihimiza Halmashauri zote kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya ununzi wa vifaa hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara itanunua na kusambaza virutubishi kwa ajili ya kuongezwa katika vyakula vikuu kwa kuanzia na mikoa ya Iringa na Arusha katika Halmashauri za Wilaya za Kilolo, Njombe, Iringa, Karatu, Monduli na Meru. Lengo ni kudhibiti upungufu wa vitamin na madini katika jamii hasa unaoathiri watoto chini ya miaka mitano na akinamama walio katika umri wa kuzaa. Aidha, Wizara itatafuta Mshauri Elekezi kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Uongezaji wa Virutubishi katika Vyakula Vikuu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali

itaendeleza kampeni ya kutokomeza maambukizi mapya ya VVU kwa watoto na kupunguza vifo vya mama zao ifikapo 2015. Aidha, Wizara itaendelea kuboresha huduma ya matunzo ya mtoto aliyezaliwa na uzito pungufu katika hospitali za mikoa yote nchini kwa kuzifanyia ufuatiliaji na usimamizi shirikishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango wa Taifa wa Chanjo, katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea na kudumisha kiwango cha chanjo kuwa zaidi ya asilimia 90 kwa kutekeleza Mkakati wa Fikia kila Wilaya Fikia kila Mtoto hususan katika wilaya zilizo na kiwango kidogo cha chanjo. Aidha, Wizara itaanzisha chanjo ya *pneumococcal* na *rotavirus* ambazo zitatoa kinga kwa magonjwa ya *pneumonia* na kuharisha kwa watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, chanjo ya *Human Papilloma Virus (HPV)* itaanzishwa kwa wasichana wenye umri wa kubalehe kwa ajili ya kuzuia saratani ya shingo ya kizazi. Utoaji wa chanjo hii utaanza na Mikoa ya Dodoma, Dar- es – Salaam na Kilimanjaro baada ya kupata uzoefu wa utekelezaji katika Mkoa wa Mwanza. Pia, Wizara itaendelea kuimarisha mfumo wa utoaji wa huduma za chanjo ikiwa ni pamoja na kupanua wigo wa walengwa kwa kujumuisha rika zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara itahakikisha chanjo na vifaa vya kutolea chanjo vinanunuliwa na kusambazwa katika mikoa yote nchini. Aidha, Wizara itaimarisha huduma za mnyororo baridi katika ngazi ya Taifa na mikoa kwa kufunga vyumba vya mnyororo baridi (*Walk in Cold*

*Rooms*) na kangavule (*Generator*), ili kuhakikisha kuwepo kwa utunzaji mzuri wa chanjo. Vile vile, Wizara itaendelea kuzijengea uwezo Halmashauri kwa kutoa na kusimamia huduma za chanjo na kuendesha mafunzo ya chanjo ili kuhakikisha kuwa huduma za chanjo zinatolewa katika ubora unaotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara itahamasisha Viongozi na watendaji wa mikoa ya Mtwara, Lindi, Tanga na Morogoro ili kutoa kipaumbele kwa huduma za afya shuleni. Aidha, Wizara itafanya ufuatiliaji katika mikoa ya Iringa, Pwani, Rukwa na Mbeya juu ya huduma za afya shuleni na kutoa mafunzo kwa waratibu 40 juu ya mbinu shirikishi za kuboresha maji, usafi na mazingira shuleni. Vilevile, Wizara itapitia upya na kuandaa mwongozo wa utoaji wa huduma za afya shuleni.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/13, Wizara kwa kushirikiana na wadau itaandaa Mwongozo wa Afya na Usalama Kazini utakaosaidia kuwaelekeza wadau wote nchini juu ya utoaji huduma za afya na usalama mahala pa kazi. Aidha, Wizara itafanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa shughuli za afya na usalama kazini katika halmashauri mbalimbali na kutoa maelekezo ya kuboresha huduma za afya na usalama kazini katika maeneo ya uzalishaji mali.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, Wizara itakamilisha mapitio ya Mkakati wa Kudhibiti VVU na UKIMWI kwa wafanyakazi wa sekta ya afya,

kuuchapisha na kuusambaza kwa wadau husika katika ngazi zote za utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kuratibu zoezi la Mashindano ya Afya na Usafi wa Mazingira ili kuzidi kuinua mwamko wa kuthamini usafi wa mazingira katika jamii na usafi binafsi. Aidha, Wizara itasimamia utekelezaji wa Kampeni ya Kitaifa ya Usafi wa Mazingira ambayo inaanza kutekelezwa katika mwaka huu wa fedha kwenye Mikoa ya Rukwa, Iringa, Mtwara, Pwani, Dodoma, Tanga, Arusha, Manyara, Tabora, Kigoma, Kagera na Mara. Pia, Wizara itakamilisha maandalizi ya Sera ya Usafi na Afya Mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kuwajengea uwezo wataalam wa usafi na afya mazingira juu ya usimamizi wa mazingira. Aidha, Wizara itaandaa Mwongozo wa kufanya tathmini ya athari za afya zitokanazo na miradi ya maendeleo. Vile vile, Wizara itahamasisha mikoa, majiji na manispaa juu ya udhibiti wa taka ngumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Afya Bandarini, Viwanja vya ndege na Mipakani, katika mwaka 2012/13, Wizara itaendelea kudhibiti magonjwa yanayotolewa taarifa kimataifa yasiingie nchini kwa kufanya ufuatiliaji. Aidha, Wizara itaendelea kutoa chanjo ya kudhibiti homa ya manjano kwa wasafiri wanaotoka katika nchi ambazo zina ugonjwa huo. Vile vile, Wizara itaandaa Kanuni nyingine tatu za utekelezaji wa Sheria ya Afya ya Jamii ya mwaka 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/13, Mpango wa Taifa wa Udhibiti wa Magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele utaendelea kugawa dawa za kudhibiti magonjwa ya Matende na Mabusha, Usubi, Kichocho, Vikope na minyoo ya tumbo katika mikoa ya Rukwa, Singida, Dodoma, Mtwara, Lindi, Pwani, Morogoro, Iringa, Mbeya, Ruvuma, Tanga na Tabora.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, mpango huu utafanya utafiti wa kufahamu kiwango cha maambukizi ya magonjwa ya matende na mabusha na kichocho katika mkoa wa Mwanza na kugawa dawa za kudhibiti magonjwa hayo katika Mkoa wa Dar es Salaam. Vile vile, mpango huu utaendelea kufanya utafiti ili kufahamu ukubwa wa magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele kwa lengo la kuyadhibiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu ya afya kwa umma, katika mwaka 2012/2013, Wizara itaimarisha ushirikiano na wadau na kuendelea kuhamasisha na kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa kubadili tabia hatarishi kwa afya na kujikinga na maradhi; na kuhimiza utumiaji wa huduma za afya kwenye vituo vya kutolea huduma za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau, itachapisha na kusambaza nakala za Mpango Mkakati wa Kuboresha na Kudumisha Afya ya Jamii wa 2012- 2015 (*National Strategic Framework for Health Promotion and Disease Prevention,* 2012 - 2015) na Mwongozo wa kisera wa Kuboresha na Kudumisha Afya ya Jamii wa 2012, katika

mikoa na halmashauri zote. Vile vile, Wizara itaendelea kukusanya, kuhakiki na kuhifadhi vielelezo vya uelimishaji kutoka kwa wadau mbalimbali na kuimarisha mfumo wa kuhifadhi vielelezo hivyo kwa nia ya kuvitunza na kuvitumia wakati vitakapohitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Huduma za Tiba, Vituo vya kutolea Huduma za Afya, katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kuboresha huduma zinazotolewa katika vituo na zile za mkoba ili wananchi wengi waweze kuhudumiwa na vituo hivyo hususan upatikanaji wa dawa. Aidha, Wizara itaendelea kuvipatia vituo hivyo watumishi, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi kulingana na mahitaji na upatikanaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Hospitali ya Taifa Rufaa za Kanda na Maalum, Hospitali ya Taifa Muhimbili; katika mwaka 2012/2013, Hospitali ya Taifa Muhimbili itaendelea kuboresha huduma za rufaa ngazi za juu kwa kuboresha upasuaji kwa kutumia hadubini (*endoscopic surgery*), upasuaji mkubwa wa moyo na huduma za kusafisha damu kwa wagonjwa wa figo. Aidha, Hospitali itakamilisha ujenzi wa kitengo cha uchunguzi na matibabu ya maradhi ya mfumo wa chakula. Vile vile, Hospitali itaendelea kuboresha huduma za ubingwa wa juu kwa kukamilisha ujenzi wa kituo cha Tiba na Mafunzo ya Upasuaji wa Moyo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2012/2013, Hospitali ya Rufaa ya Bugando itaendelea kuimarisha huduma za upasuaji wa moyo na mishipa ya fahamu na itaendelea na ujenzi wa awamu ya pili ya jengo la wagonjwa wa saratani na kuanza kutoa tiba ya mionzi

kwa wagonjwa wa saratani. Pia, Hospitali itajenga mtambo wa kuteketeza taka.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Hospitali ya Rufaa ya *KCMC* itaendelea kuboresha huduma za matibabu, mafunzo na utafiti. Aidha, Hospitali itakamilisha ujenzi wa jengo la huduma kwa wagonjwa wenye matatizo ya ngozi. Vile vile, Hospitali itaanza ujenzi wa jengo kwa ajili ya huduma za binafsi (*private wards*) kwa watakaokuwa na uwezo wa kulipia zaidi. Hatua hii itaiongezea hospitali fedha zitakazotumika kuboresha huduma kwa wagonjwa wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Hospitali ya Rufaa ya Mbeya itaendelea kuboresha huduma za rufaa za uchunguzi na tiba kwa wagonjwa. Aidha, Hospitali itaanza kutekeleza mradi wa *Care 2X* wa mfumo wa utunzaji wa taarifa za wagonjwa kwenye kompyuta na hivyo kurahisisha upatikanaji wa taarifa zao kwa urahisi na haraka zaidi. Vile vile, Hospitali itaendelea na uchunguzi wa saratani ya shingo ya kizazi kwa wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Mifupa Muhimbili, katika mwaka 2012/2013, Taasisi ya Mifupa Muhimbili itaanza ujenzi wa jengo jipya kwa ajili ya kutoa huduma za matibabu katika fani za mifupa na magonjwa ya mishipa ya fahamu. Ujenzi unatarajiwa kuchukua kipindi cha miezi 18.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi huo utakapokamilika utaimarisha uwezo wa Taasisi katika

kutoa huduma za matibabu, utapunguza kwa kiasi kikubwa idadi ya wagonjwa watakaopata rufaa ya kwenda kutibiwa nchi za nje na utatatua kwa kiwango kikubwa tatizo la msongamano wa wagonjwa wodini. Aidha, ujenzi utakapokamilika utaongeza idadi ya vitanda katika Taasisi hii kutoka 136 vya sasa hadi 336. Vilevile, Taasisi inatarajia kuanzisha mafunzo ya shahada ya uzamili ya upasuaji wa ubongo na uti wa mgongo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/13, Taasisi ya Saratani *Ocean Road* itaendelea kutoa huduma za kinga, uchunguzi na matibabu ya Saratani. Aidha, itatoa mafunzo ya uchunguzi wa Saratani kwa Wataalam wa afya katika hospitali za mikoa ili kuweza kubaini Saratani katika hatua za awali na kutoa rufaa mapema. Vilevile, kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, Taasisi itaendelea na utoaji wa tiba shufaa katika Mikoa ya Morogoro, Pwani, Dar es Salaam, Mwanza, Kagera, Mbeya, Mtwara na Kilimanjaro.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Taasisi inatarajia kununua mashine za kutibu Saratani kwa ufanisi zaidi ziitwazo *CT Simulator na Linear Accelerator*. Aidha, huduma za matibabu ya dawa za Saratani zitaimarishwa ili wagonjwa wote wanaotegemea kupata matibabu hayo wayapate. Vilevile, Taasisi itaanzisha huduma ya upasuaji wa Saratani. Pia, Taasisi katika mpango wa muda mrefu, itaendelea na utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Kupambana na Saratani kwa kushirikiana na wadau wa ndani na nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Taasisi itawaelimisha wadau na wananchi kwa ujumla kwa kutoa elimu endelevu kupitia vyombo mbalimbali vya habari, tovuti, warsha na semina kuhusu kinga na matibabu ya saratani. Aidha, Taasisi itaendelea kushirikiana na Taasisi za ndani na nje ya nchi katika kuimarisha huduma na tafiti za saratani. Vile vile, Taasisi itaendelea na utoaji wa mafunzo ya Shahada ya BSc RTT na ya Uzamili ya *MMED Clinical Oncology* kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Sayansi za Afya Shiriki Muhimbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka 2012/2013, Taasisi itaanza kutumia mfumo wa kielektroniki katika utoaji wa huduma za kliniki, matibabu na utawala. Mfumo huu utasaidia kufuatilia kwa karibu wagonjwa wanaopata matibabu, tafiti na kuboresha utunzaji wa takwimu na taarifa mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Hospitali ya Mirembe itaendelea kuboresha huduma za rufaa na itatoa mafunzo maalum kwa Madaktari mawili na Maafisa Wauguzi wanne kuhusu jinsi ya kuhudumia waathirika wa dawa za kulevya. Aidha, Hospitali itaanza ujenzi wa jengo la kuhifadhi maiti. Vile vile, Taasisi ya Isanga itaendelea kuboresha huduma zinazotolewa kwa wagonjwa wa akili wahalifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Hospitali ya Kibong'oto itaendelea kutoa huduma kwa magonjwa ya kuambukiza ikitilia mkazo huduma za magonjwa ya kifua kikuu na maambukizi

ya virusi vya UKIMWI (VVU). Aidha, Hospitali itapanua wodi za kifua kikuu sugu na maabara ya ugunduzi wa vimelea vya kifua kikuu sugu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, Hospitali itaendelea kutoa mafunzo kwa wafanyakazi na kwa watoa huduma za kifua kikuu sugu katika wilaya ambazo baada ya wagonjwa kuruhusiwa, wataendelea kupata huduma hizo. Pia, Hospitali itaendelea kufuatilia wagonjwa wa kifua kikuu sugu na kuendelea kutoa elimu kwa jamii wanakotoka ili kubaini kama kutakuwa na uambukizo wa mwanafamilia au jamaa wa karibu ili wanaogundulika waweze kutibiwa mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu huduma za Hospitali za Mashirika ya Kujitolea na Makampuni Binafsi; katika mwaka 2012/2013, Wizara itaimarisha huduma za hospitali za mashirika ya kujitolea, makampuni na watu binafsi zinazochangia kupunguza idadi ya wagonjwa wanaolazimika kupelekwa nje ya nchi kwa uchunguzi na matibabu. Huduma hizo ni pamoja na huduma za upasuaji mkubwa wa moyo, kuweka viungo bandia vya nyonga na goti na upasuaji kwa kutumia *endoscope*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara itaboresha huduma za afya ya kinywa kwa kununua na kusambaza vifaa na dawa katika vituo vyote vya umma vyenye kliniki za afya ya kinywa. Aidha, Wizara itasambaza viti vya kutolea huduma za afya ya kinywa katika kliniki 30. Vile vile, Wizara itachapisha na kusambaza nakala za Mpango

Mkakati wa Huduma za Afya ya Kinywa nchini kwa wadau mbalimbali na kuwaelimisha jinsi ya kuutekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu huduma za magonjwa yasiyo ya kuambukiza na dawa za kulevya, katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kusimamia utekelezaji wa mikataba ya Kimataifa kuhusu kuzuia magonjwa yasiyo ya kuambukiza kwa kusambaza miongozo inayohusu kukinga na kutibu magonjwa hayo; kuwaelimisha wananchi kuhusu viashiria hatari vinavyosababisha magonjwa yasiyo ya kuambukiza; kusambaza sheria ya magonjwa ya akili kwenye hospitali zote za rufaa, mikoa na wilaya; kusambaza Mwongozo wa Kitaifa wa Kuzuia Utumiaji Hatari wa Pombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara itasambaza Mkakati wa Taifa wa Kuzuia na Kukinga Magonjwa Yasiyo ya kuambukiza; itasambaza Mkakati wa Taifa wa Kuzuia na Kukinga Magonjwa ya Saratani. Pia, Wizara kwa kushirikiana na wadau itatoa mafunzo maalum kwa watumishi katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Hospitali za Rufaa za Kanda za Mbeya, Bugando, *KCMC* na Hospitali ya Rufaa Maalum ya Mirembe, juu ya kubainisha na kusaidia wanywaji wa pombe kuondokana na unywaji hatarishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara itapanua huduma za kuwahudumia waathirika wa kujidunga dawa za kulevya kwa kutumia dawa ya methadone, katika Hospitali za Rufaa za Amana, Temeke na Mwananyamala na kupata

uangalizi wa karibu kutoka kwa wataalam wa magonjwa ya afya ya akili kutoka Hospitali ya Taifa ya Muhimbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara kwa kushirikiana na wadau itaendelea kuelimisha na kuhamasisha umma wa Watanzania juu ya huduma za macho kupitia maadhimisho ya Siku ya Afya ya Macho Duniani. Maadhimisho haya yataambatana na uendeshaji wa kambi za huduma za macho. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau itafanya tathmini ya huduma za afya ya macho kwa wagonjwa wa kisukari ili kujua hali halisi na kuandaa mpango wa utekelezaji ili kukabiliana na upofu na upungufu wa kuona utokanao na ugonjwa wa kisukari.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kusimamia na kuboresha huduma za uchunguzi wa magonjwa (maabara, radiolojia na vyumba vya kutunzia maiti). Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo, itaanza kutekeleza mradi mpya wa *ORIO* wa kuboresha huduma za radiolojia, uzazi na mtoto na upasuaji kwa kufunga *x-ray* za digitali na mtandao wa elektroniki wa huduma za *x-ray* (*teleradiology*) pamoja na kuimarisha matengenezo kinga ya vifaa vya radiolojia katika hospitali 37. Mashine hizi zitawezesha kutoa huduma ya tiba kwa kutumia mfumo wa kielektroniki (*Telemedicine*).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara itaingiza maabara 18 kwenye

mpango wa urasimishaji kwa viwango vya kimataifa vya ubora wa huduma za maabara na kufanya jumla ya idadi za maabara kuwa 36. Aidha, uchunguzi wa magonjwa ya milipuko na uhakiki wa ubora wa vipimo vya maabara, kupitia Maabara ya Taifa ya Mafunzo na Uhakiki wa Ubora wa Huduma za Maabara, vitaimarishwa na kuongeza vituo vinavyoshiriki kwenye uhakiki wa ubora wa vipimo kutoka vituo 35 hadi 70 kwa vipimo vya *clinical chemistry* na *hematology*. Vile vile, Wizara itaongeza vituo vya uhakiki wa vipimo vya mikrobiolojia na parasitolojia kutoka vituo 20 hadi 50.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/13, Wizara kupitia Mpango wa Taifa wa Damu Salama itakusanya chupa za damu salama 200,000 ili wananchi wengi waweze kupata huduma ya damu salama. Katika kufanikisha hili, elimu itaendelea kutolewa kwa wananchi ili wawe na utamaduni wa kuchangia damu mara kwa mara, kuanzisha klabu za wachangia damu nje ya mashule na kuendelea kuimarisha klabu zilizoanzishwa mashuleni. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Chama cha Msalaba Mwekundu, itahamasisha jamii kuhusu umuhimu wa kuchangia damu kwa hiari, kukusanya damu na kusambaza kwenye hospitali husika za mikoa ya Kigoma, Kagera, Rukwa, Shinyanga, Pwani na Manyara.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Mpango wa Taifa wa Damu Salama utapima damu ili kuhakikisha viwango na ubora, na itaendelea kufanya kazi na Mradi wa m-Health ili kuwafikishia wachangia damu ujumbe mfupi wa

maandishi *(sms)* kuwakumbusha kuendelea kuchangia damu mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika kuhakikisha ubora na viwango, Mpango utaendelea kutumia mfumo mpya wa kielektroniki (*Blood Establishment Computer System-BECS)* ili kupata taarifa na takwimu mbalimbali kuanzia kwa mchangiaji damu hadi kwa mgonjwa anayepewa damu. Vile vile, Wizara itashirikiana na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma kuhakikisha kuwa Mpango unakuwa endelevu kwa kuajiri watumishi kwa mkataba Serikalini. Hadi sasa jumla ya wafanyakazi 85 kati ya 210 wamepata ajira Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu huduma za dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi; katika mwaka 2012/2013, sh. 253,468,765,171.00 zimetengwa kwa ajili ya kununua na kusambaza dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika zahanati, vituo vya afya na hospitali za umma. Kati ya fedha hizo, sh. 147,423,523,200.00 zitatolewa na *Global Fund* kwa ajili ya kununua na kusambaza dawa za malaria na UKIMWI. Kiasi cha shilingi 106,045,241,971.00, kitatumika kwa ajili ya ununuzi na usambazaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya fedha hizi kiasi cha sh. 84,935,841,820.00 ni kwa ajili ya ununuzi na usambazaji wa dawa na sh. 21,148,400,151.00 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa vifaa, vifaa tiba na vitendanishi. Aidha, kati ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya ununuzi wa dawa, sh. 67,698,574,800.00 zimetengwa

katika bajeti ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na sh. 17,237,267,019.00 zimetengwa katika Bajeti za Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara kupitia Bohari ya Dawa itasambaza dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika zahanati 4,190, vituo vya afya 494, hospitali za Wilaya na Teule 111, hospitali za Rufaa za Mikoa 24, hospitali za Rufaa ngazi ya Mkoa 10, hospitali za Rufaa za Kanda nne, hospitali za rufaa maalum *(Super Speciality)* nne, hospitali ya Taifa moja, hospitali za jeshi la wananchi mbili na hospitali ya Jeshi la Polisi moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara kupitia vyuo vya afya vya kanda itatoa mafunzo kwa watumishi katika zahanati, vituo vya afya na hospitali juu ya kuandaa makadirio ya mahitaji ya dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi pamoja na uagizaji sahihi. Aidha, watumishi hao watapewa mafunzo juu ya uagizaji wa dawa na vifaa tiba kulingana na mahitaji na mgao wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu huduma za Tiba Asili na Tiba Mbadala; katika, mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kuwaelimisha waganga wa tiba asili na tiba mbadala na wananchi kwa ujumla kuhusu tiba asili ili wazingatie sheria, kanuni na miongozo iliyopo. Aidha, Wizara itaandaa machapisho mbalimbali yanayohusu taaluma ya Tiba Asili kwa lengo la kuiboresha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka 2012/2013, Bohari ya Dawa kupitia Mpango Mkakati

(2007 - 2013) itaimarisha upatikanaji endelevu wa dawa, vifaa na vifaa tiba kutoka asilimia 87 hadi asilimia 95. Aidha, Bohari itaendelea kuboresha mfumo wa usambazaji dawa na vifaa tiba hadi zahanati na vituo vya kutolea huduma za afya katika Mikoa tisa ya Lindi, Pwani, Ruvuma, Rukwa, Dodoma, Kigoma, Tanga, Shinyanga na Manyara. Vile vile, Mikoa ya Iringa, Kilimanjaro, Mbeya, Pwani, Tabora, Singida, Mwanza, Mtwara na Tabora itaingizwa katika utaratibu huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka 2012/2013, Bohari ya Dawa itaanzisha na kukamilisha ujenzi na upanuzi wa maghala ya kisasa ya kuhifadhia dawa katika mikoa ya Tanga, Tabora, Dar es Salaam na Mbeya. Ujenzi huo utaongeza uwezo wa uhifadhi dawa kwa zaidi ya mita za mraba 12,000 na hivyo kuongeza upatikanaji wa dawa kwa wakati. Aidha, Bohari itaanza utaratibu wa kuweka alama maalum katika dawa zote za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu huu utasaidia kudhibiti upotevu wa dawa na kuongeza uwajibikaji katika mfumo wa usambazaji wa dawa nchini. Vile vile, Bohari itaendelea kuboresha mawasiliano na wateja kwa kujadili na kuelimishana kuhusu masuala mahsusi ya kiutendaji ikiwemo kuendelea kuboresha mfumo wa kukusanya taarifa za maoteo ya dawa na vifaa tiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ukaguzi na uhakiki wa ubora wa huduma za afya na ustawi wa jamii; huduma za Uuguzi na Ukunga; katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kusimamia na kuratibu

huduma za uuguzi na ukunga kwa kusimamia na kutathmini utekelezwaji na uzingatiwaji wa miongozo ya uuguzi na ukunga katika mikoa kumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara itaendelea kuwajengea wauguzi uwezo wa kufanya tafiti zenye kuboresha huduma za uuguzi na ukunga kwa kushirikiana na wadau wa ndani na nje ya nchi na itaandaa Mpango Mkakati wa Huduma za Uuguzi na Ukunga ambao utatoa dira na mwelekeo wa huduma za uuguzi kwa miaka mitano ijayo (2012-2017).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara itakagua vituo 48 vya kutolea huduma za afya katika ngazi ya hospitali za rufaa nne, maalum nne, mikoa 28 na hospitali za Wilaya 12 zilizopata mafunzo ya kukinga na kudhibiti maambukizo. Aidha, Wizara itatathmini ili kubaini vituo vitakavyokuwa vinazingatia viwango vya ubora katika utekelezaji wa kukinga na kudhibiti maambukizo katika utoaji wa huduma za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara itatoa mafunzo ya ukufunzi kuhusu kukinga na kudhibiti maambukizo na uboreshaji wa huduma za afya kwa Timu za Uboreshaji Huduma za Afya, ambazo zitahusisha wajumbe 210 wa hospitali 48 ili ziweze kufanya usimamizi shirikishi na mafunzo katika sehemu zao za kazi. Aidha, ili kuhakikisha mipango ya uboreshaji na uhakiki huduma za afya inafungamanishwa (*integrated and focused*), Wizara itaandaa Mpango Mkakati wa Uboreshaji Huduma za Afya wa miaka mitano (2012-2017).

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, Wizara itaanza maandalizi ya awali ya utekelezaji wa Mfumo wa Usajili wa Huduma za Afya Hatua kwa Hatua na Utoaji rasmi wa Ithibati. Pia, Wizara itapitia miongozo ya kitaifa, mkakati wa mawasiliano na viwango vya kukinga na kudhibiti maambukizo ikiwa ni pamoja na mwongozo wa kitaifa wa kufundishia, ukaguzi na utambuaji wa huduma bora za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara kwa kushirikiana na wadau itaendelea kujiweka tayari kukabiliana na dharura na maafa pindi yatakapotokea. Tathmini ya kuangalia hali ya utayari wa kukabiliana na maafa katika huduma za afya itafanywa ili kutoa nafasi nzuri ya kupanga mpango wa kukabiliana na dharura. Aidha, Wizara itaendelea kutoa mafunzo ya kukabiliana na dharura na maafa kwa Timu za Dharura za Mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ushirikiano katika Masuala ya Sekta ya Afya na Ustawi wa Jamii katika Jumuiya za Afrika *(SADC, EAC, ECSA-HC)* na Kimataifa, katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kuratibu na kushiriki kwenye mikutano na kutekeleza maazimio ya pamoja yenye manufaa kwa Taifa yaliyofikiwa katika Jumuiya zote za kanda ambazo ni *SADC, EAC, ECSA-HC* na mashirika mengine ya Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea na uratibu, utoaji na usimamizi wa huduma za ustawi wa jamii kwa watu walio katika mazingira hatarishi kama vile wazee

wasiojiweza, watu wenye ulemavu, familia zenye dhiki, watoto walio katika mazingira hatarishi na watoto walio katika mkinzano na sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu huduma kwa familia, watoto na malezi ya awali ya mtoto, katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kutoa huduma kwa watoto walio katika mkinzano na sheria katika mahabusi za watoto za Arusha, Moshi, Tanga, Mbeya, Dar es Salaam na Mtwara pamoja na Shule ya Maadilisho iliyoko Mbeya. Aidha, Wizara itaendelea kutoa mafunzo kwa watumishi wanaofanya kazi katika taasisi hizo juu ya Sheria ya Mtoto, Kanuni za Mahabusi za Watoto na Shule ya Maadilisho pamoja na Miongozo mbalimbali inayoongoza utoaji wa huduma katika taasisi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kuratibu watoa huduma kwa watoto wanaoishi mitaani. Wizara kwa kushirikiana na wadau itaendelea kuimarisha mradi wa pamoja wa kutambua na kuhudumia watoto hao katika Mkoa wa Dar es Salaam. Aidha, mafanikio yatakayopatikana yatasaidia uendelezaji wa mradi wa kusaidia watoto wanaoishi mitaani katika mikoa mingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, Wizara itaendelea kuufanyia majaribio mpango wa Marekebisho ya Tabia kwa Watoto walio katika Mkinzano na Sheria katika Jamii katika Halmashauri ya Manispaa ya Temeke na utapunguza idadi ya watoto wanaolazimika kuingizwa katika vizuizi yakiwemo magereza au mahabusi za watu wazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu huduma za Haki za Mtoto na Marekebisho ya Tabia, katika mwaka 2012/2013, Wizara kwa kushirikiana na wadau itatoa mafunzo ya uwezeshaji haki jamii katika Halmashauri za Korogwe, Lushoto, Tanga, Muheza, Same na Karatu. Lengo kuu la mafunzo hayo ni kuiwezesha jamii kutambua haki na wajibu mbalimbali, sheria zinazolinda haki hizo na mifumo mbalimbali ya utoaji haki ili hatua zichukuliwe pale ukiukwaji wa haki unapojitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu huduma kwa Wazee na Watu wenye Ulemavu; katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kusimamia utoaji wa mafunzo ya ufundi stadi katika vyuo vya watu wenye ulemavu vya Singida na Yombo kwa kugharamia vifaa vya kujifunzia na kufundishia. Aidha, Wizara itaendelea kusimamia na kuratibu huduma za matunzo kwa watu wenye ulemavu na wazee wasiojiweza katika makazi 17 yanayosimamiwa na Serikali na 24 yanayoendeshwa na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kuelimisha umma kuhusu Sheria ya Mtoto Na. 21 ya mwaka 2009 na kanuni zake katika ngazi ya Halmashauri, vituo vinavyosimamiwa na Idara ya Ustawi wa Jamii na wadau wengine. Aidha, Wizara itatoa elimu na kusambaza Mpango Kazi wa Kitaifa Awamu ya Pili wa Huduma kwa Watoto Walio katika Mazingira Hatarishi (2012 – 2016). Vile vile, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri na wadau itaendelea kuanzisha na kuimarisha mifumo ya ulinzi na usalama wa mtoto katika Halmashauri 25.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaendelea kuzijengea uwezo timu hizi za Halmashauri za ulinzi na usalama wa mtoto kwa kuzipatia mafunzo juu ya sheria, kanuni na miongozo zinazohusu huduma na ulinzi wa watoto. Pia, Wizara itaendelea kuandaa na kukamilisha Kanuni za Sheria ya Mtoto zinazohusu ulinzi na usalama wa mtoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kugharamia mahitaji ya shule kwa watoto walio katika mazingira hatarishi wanaolelewa katika Vituo vya Ustawi wa Jamii vikiwemo Makao ya Taifa ya watoto Kurasini, Makazi 17 ya Wazee Wasiojiweza na Shule ya Maadilisho Irambo Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kutoa msaada wa Rais kwa akinamama wanaojifungua watoto zaidi ya wawili mara moja na kuratibu huduma ya malezi ya kambo na kuasili, huduma za malezi, makuzi na maendeleo changamushi ya awali ya mtoto, huduma kwa watoto wanaoishi mitaani na huduma kwa familia zenye dhiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kuwezesha vikao vya Baraza la Kamishna la Usuluhishi wa Ndoa, Bodi ya Shule ya Maadilisho iliyoko Irambo Mbeya, Muongo wa Afrika kwa watu wenye ulemavu, Kamati ya Kiufundi na Kamati ya Uratibu na Usimamizi ya Kitaifa ya Watoto Wanaoishi katika Mazingira Hatarishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara kwa kushirikiana na wadau itaandaa mkakati wa wataalam wa ustawi wa jamii *(Social Welfare Workforce Strategy)* ili kuweza kuongeza idadi ya maafisa ustawi wa jamii katika Halmashauri na taasisi za Serikali. Aidha, mkakati huu utasaidia kuboresha huduma za ustawi wa jamii na mazingira ya kazi kwa maafisa hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara itaandaa mkakati wa kuwaelimisha wamiliki wa makao ya watoto walio katika mazingira hatarishi kuhusu miongozo ya uanzishaji na uendeshaji wa makao, kwa mujibu wa Sheria ya Mtoto Na. 21 ya mwaka 2009 na kanuni zinazohusu makao ya watoto. Aidha, makao ambayo hayatakidhi vigezo na viwango stahiki, Wizara italazimika kuyafunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Wakala na Taasisi zilizo chini ya Wizara; Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali; katika mwaka 2012/2013, Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali itaendeleakuimarisha utoaji huduma bora za uchunguzi wa sampuli na vielelezo mbalimbali na kutoa matokeo kwa wakati ili kulinda afya, mazingira na utoaji haki kwa kuzipatia Maabara zake mashine za kisasa, vifaa na vitendanishi vya kutosha. Aidha, Wakala utagharamia matengenezo kinga kwa mitambo ya uchunguzi ili iweze kutoa matokeo sahihi na iweze kudumu kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wakala itaendelea kukamilisha miongozo

ya utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Vinasaba vya Binadamu Sura ya 73. Aidha, Wakala itaendelea kushiriki katika kikosi kazi kinachojumuisha vyombo vya dola na kuchukua sampuli za uchunguzi kwa watuhumiwa wa mauaji ya wenye ulemavu wa ngozi, vikongwe, majambazi, wabakaji na watumiaji wa dawa za kulevya katika kanda za Ziwa na Magharibi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara kupitia Wakala itaimarisha usimamizi wa Sheria ya Udhibiti wa Kemikali kwa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara katika migodi na maeneo yanayozunguka migodi, viwanda na maghala, vituo vyote 18 vya mipakani, bandarini na viwanja vya ndege. Aidha, Wakala utaendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu matumizi salama na sahihi ya kemikali kupitia vyombo vya habari na mikutano kwa kushirikiana na Mashirika ya Kitaifa na Kimataifa katika kutekeleza mikataba ya usimamizi wa kemikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, Wakala kwa kushirikiana na Halmashauri itateua wasimamizi wa kemikali katika kila Halmashauri na kutoa elimu katika mikoa yenye migodi kwa timu ya wataalam wa afya watakaohusika na ufuatiliaji wa utekelezaji wa sheria ya usimamizi wa kemikali katika maeneo yao.

Mheshimwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wakala itaendelea kufuatilia taratibu za kupata hati ya ithibati *(ISO 9001:2008)* chini ya usimamizi wa *Bureau Veritas*, kukamilisha rasimu na kushiriki katika kuandaa miswada ya Sheria ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali na Sheria ya Kusimamia Taaluma wa Kemia.

Aidha, Wakala itaendelea kugharamia mafunzo ya muda mfupi na mrefu yenye manufaa kwa Taasisi kwa watumishi 24 katika ngazi ya uzamili, shahada, stashahada na cheti ili kuwaongezea elimu, ujuzi na ufanisi katika utoaji huduma bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/13, Mamlaka ya Chakula na Dawa kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa itaendelea kudhibiti usalama na ubora wa vyakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba kwa kukagua maeneo ya biashara hizo. Aidha, Mamlaka itaendelea kufanya tathmini ya bidhaa ili kuhakiki usalama, ubora na ufanisi wake kabla ya kusajiliwa na kuruhusiwa kutumika nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Mamlaka itaendelea kudhibiti uingizaji nchini wa bidhaa za vyakula, dawa, vipodozi, na vifaa tiba kwa kutoa vibali vya uingizaji nchini baada ya kukidhi vigezo. Aidha, Mamlaka itaendelea kukagua shehena za bidhaa hizo katika vituo vya forodha. Vilevile, Mamlaka itaendelea kufanya uchunguzi wa kimaabara wa vyakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba ili kuhakiki usalama, ufanisi na ubora wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Mamlaka itaendelea kukusanya na kutathmini taarifa za madhara ya matumizi ya dawa ikiwa ni pamoja na kutekeleza Mpango wa Ufuatiliaji wa Usalama wa Dawa Mseto ya Malaria ya *Artemether /Lumefantrine (ALu)* na *Dihydroartemisinin/ Piperaquine*.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Mamlaka itaendelea kukusanya na kutathmini taarifa za magonjwa yatokanayo na kula chakula na kutoa elimu kwa umma kuhusu utayarishaji wa chakula salama na namna ya kupambana na milipuko ya magonjwa yatokanayo na vyakula visivyo salama. Vile vile, Mamlaka itaendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa watumishi wake ili kuwajengea uwezo wa kukabiliana na changamoto mbalimbali za kiutendaji ikiwa ni pamoja na mabadiliko ya teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/13, Taasisi ya Chakula na Lishe kwa kushirikiana na wadau itakamilisha Mpango wa Utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Lishe na kuusambaza kwa wadau. Lengo ni kuainisha na kuratibu majukumu ya wadau mbalimbali ili kupata matokeo yaliyo bora zaidi. Aidha, Taasisi itaandaa mwongozo wa kupanga na kuandaa bajeti ya utekelezaji wa afua za lishe katika Halmashauri. Mwongozo huo utazirahisishia Halmashauri kuainisha na kutekeleza afua zinazolenga kuinua lishe ya jamii katika Halmashauri hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Taasisi itaendelea kugawa chakula maalum cha kuongeza nguvu na virutubishi kwa wingi (*Plumpy Nut*) kwa watoto, watu wenye VVU na wenye utapiamlo katika wilaya 16 za mikoa ya Arusha, Singida na Dodoma. Aidha, itafanya ufuatiliaji katika vituo vya afya vinavyotoa chakula dawa katika Wilaya hizo na itaendelea kutoa mafunzo kuhusu matibabu ya utapiamlo kwa kutumia chakula dawa kwa watoto, watu wenye VVU na utapiamlo kwa watoa huduma za

afya ambao hawajapata mafunzo kwenye Wilaya za Mikoa hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Taasisi itatoa mafunzo kwa Maafisa Afya kuhusu uchanganyaji na ufuatiliaji wa chumvi yenye madini joto na itaelimisha na kuhamasisha uongozi wa Wilaya kuhusu umuhimu wa matumizi na ufuatiliaji wa chumvi yenye madini joto. Mafunzo na uhamasishaji utafanyika katika Mikoa ya Ruvuma, Kagera, Kigoma, Rukwa, Lindi na Mtwara ambapo viwango vya matumizi ya chumvi yenye madini joto yako chini sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, itaendelea kufanya ufuatiliaji wa karibu kwa wazalishaji wa chumvi ili waweze kuzalisha chumvi yenye viwango vya madini joto vinavyokubalika kutosheleza mahitaji ya mwili wa binadamu. Vile vile, Taasisi itaendelea kuelimisha na kuhamasisha jamii kuhusu lishe na umuhimu wa matumizi ya chumvi yenye madini joto mwilini kwa kutumia njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na radio, televisheni, magazeti na machapisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Taasisi itashirikiana na sekta ya viwanda vikubwa na vidogo kuanzisha uzalishaji wa viini lishe kwa kuzingatia viwango na sheria ya uwekaji virutubisho nyongeza kwenye vyakula. Aidha, Taasisi itaendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa matumizi ya vyakula vyenye virutubisho nyongeza mwilini na itaandaa Mpango wa Utekelezaji wa Mkakati wa Kuweka Virutubisho Nyongeza kwenye

Vyakula ili kuweza kufuatilia na kutathmini maendeleo ya programu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu itaendelea na utafiti wa chanjo ya Malaria iitwayo *RTS,S/ AS01E* katika awamu ya tatu kwa kufuatilia watoto waliokwishapata chanjo zote tatu. Aidha, watoto hao watapewa chanjo ya dozi ya *booster* na watafuatiliwa tena hadi Desemba 2013 na matokeo ya ufuatiliaji huo yatatolewa mwaka 2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, Taasisi itaendelea na hatua ya pili ya chanjo dhidi ya UKIMWI, aina ya vinasaba (*DNA*) iongezwayo nguvu na chanjo ya *MVA* kuchunguza kwa kina uwezo wa mwili kutengeneza kinga dhidi ya virusi vya UKIMWI. Pia, Taasisi itaendeleza utafiti wa dawa za kudhibiti VVU *(ARVs)* ili kutathmini ubora wa matumizi ya dawa mpya zilizo katika mseto kwa wagonjwa wanaoanza dawa na wale wanaojenga usugu wa dawa za kundi la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Taasisi, itaendelea kufanya utafiti wa kutathimini faida na athari za kutumia dawa za kifua kikuu na *ARVs* kwa pamoja kwa mgonjwa wa kifua kikuu na UKIMWI anayeanza kutumia *ARVs* kwa wakati mmoja. Aidha, Taasisi itaendelea na utafiti unaolenga kufupisha tiba ya kifua kikuu kutoka miezi sita hadi nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Taasisi itaendelea na utafiti wa magonjwa

yasiyo ya kuambukiza ili kubaini ukubwa wa tatizo na itafanya utafiti wenye lengo la kuyadhibiti. Aidha, Taasisi itaendelea kuwajengea uwezo wananchi waishio vijijini namna ya kutibu na kuhifadhi maji ya kunywa kwa usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya utaimarisha mfumo wa utambuzi wa wanachama, utoaji wa vitambulisho na utaimarisha mfumo wa udhibiti madai ya watoa huduma ili kudhibiti udanganyifu na kuweza kulinda fedha za wanachama. Aidha, Mfuko utaanzisha kitengo cha ukaguzi na ubora wa huduma katika Makao Makuu ya Mfuko na Ofisi za Mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Mfuko utafungua ofisi za Mikoa ya Lindi, Manyara, Shinyanga, Singida na Kagera kwa lengo la kusogeza zaidi huduma karibu na wanachama na kuwapunguzia usumbufu wa kufuata huduma katika ofisi za Kanda. Aidha, Mfuko utaanza ujenzi wa ofisi zake katika mikoa ya Dodoma, Mbeya na Tabora ambazo licha ya kutumika kama ofisi, pia majengo hayo yatatumika kama vitegauchumi na itasaidia kupunguza gharama zinazotumika kulipa pango. Vilevile, Mfuko kwa kushirikiana na wadau wengine utaendelea kufanya utafiti ili kujua gharama sahihi za matibabu na hii inatokana na ukweli kwamba gharama za matibabu zinapanda kwa kasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Taasisi ya Ustawi wa Jamii itaanzisha

mafunzo ya Shahada ya Uzamili na lengo ni kudahili wanafunzi 50 kwa mwaka. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi itaanzisha mafunzo ya ngazi ya cheti katika Chuo cha Ustawi wa Jamii Kisangara mkoani Kilimanjaro. Mafunzo hayo yanalenga kupata kada ya Wasaidizi wa Ustawi wa Jamii ili waweze kuajiriwa katika ngazi za vijiji na kata. Wanafunzi 35 wa awamu ya kwanza 161 wamedahiliwa na idadi itakuwa inaongezeka kadri hali ya miundo mbinu itakavyoendelea kuboreshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Taasisi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itatoa mafunzo ya muda mfupi kwa wasaidizi wa ustawi wa jamii 250 wa Mikoa ya Manyara, Singida, Kigoma na Katavi. Aidha, Taasisi itawasilisha *NACTE* mtaala wa mafunzo ya masafa ya kuhudumia watoto, familia na jamii zilizoathirika na VVU na UKIMWI ili ukiridhiwa Taasisi itoe tuzo ya mafunzo hayo badala ya kupitia Chuo Kikuu cha Kwa Zulu Natal cha Afrika ya Kusini kama ilivyo sasa. Vile vile, Taasisi kwa kushirikiana na Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini Dodoma na Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru watajumuisha masuala ya ulinzi wa mtoto katika mitaala ya kufundishia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara inaomba kiasi cha sh. 283,446,029,000.00 kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo sh. 19,142,638,000.00 ni fedha za ndani na sh. 264,303,391,000.00 zinatoka kwa Taasisi za Kimataifa na Wadau wa Maendeleo wanaochangia Mfuko wa Pamoja wa Afya na wale

walioko nje ya Mfuko. Kati ya fedha hizo sh. 64,285,624,800.00 zinatoka kwa wadau wa maendeleo wa Mfuko wa pamoja na sh. 200,017,766,200.00 zinatoka kwa wadau wa maendeleo walio nje ya Mfuko. Fedha hizo zitatumika kutekeleza kazi zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kuboresha miundombinu ya utoaji wa huduma za saratani nchini kwa kuendelea na ujenzi wa Kituo cha Tiba ya Saratani katika Hospitali ya Bugando. Kukamilika kwa kituo hicho kutaboresha utoaji wa huduma hii kwa wananchi waishio Kanda ya Ziwa na mikoa ya jirani na hivyo kupunguza msongamano katika Taasisi ya Saratani ya *Ocean Road*.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara itafunga vifaa kwenye jengo jipya la kulaza wagonjwa katika Taasisi ya Saratani ya *Ocean Road*, ambapo uwezo wa Taasisi kulaza wagonjwa utaongezeka hadi vitanda 270 ikilinganishwa na vitanda 120 vilivyopo hivi sasa. Vile vile, Wizara itaendelea na ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mtwara, lengo likiwa ni kuimarisha mfumo wa rufaa na kusogeza huduma kwa wananchi wa Kanda ya Kusini na mikoa ya jirani na itaendeleza ujenzi wa kituo kwa ajili ya waathirika wa madawa ya kulevya Itega Mkoani Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, Wizara kwa kutumia fedha kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika itaendelea na ujenzi na ukarabati wa vituo vya kutolea huduma za afya katika mikoa ya Mara, Tabora na Mtwara, ili kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara itaboresha utoaji wa huduma za afya zitolewazo na taasisi, mashirika na wakala zilizo chini yake. Katika Taasisi ya Saratani ya *Ocean Road*, Wizara itanunua mashine ya kutibu kwa kutumia mionzi *(radiotherapy)* kwa ajili ya kuboresha utoaji wa huduma kwa wagonjwa wa saratani.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Wizara itaimarisha utoaji wa huduma za kibingwa katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili kwa kuanza kutoa huduma katika Kituo cha Tiba na Mafunzo ya Moyo pamoja na ununuzi wa mashine ya kufanyia upasuaji kwa kutumia *endoscope*. Katika Taasisi ya Mifupa ya *MOI*, Wizara itanunua vifaa tiba pamoja na jenereta, na itaendelea na ujenzi wa ofisi ya Wakala wa Maabara ya Mkemia wa Serikali katika Kanda ya Kaskazini ili kuimarisha huduma za uchunguzi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo itanunua na kusambaza dawa, vifaa, vifaa tiba pamoja na vitendanishi kupitia Bohari ya Dawa. Aidha, Wizara itanunua dawa za uzazi wa mpango, vifaa vya uzazi wa mpango, chanjo, pamoja na mifuko ya vifaa vya uzazi watakavyopewa akina mama wiki chache kabla ya kujifungua pamoja na kugharamia afua mbalimbali za kudhibiti Malaria, VVU na UKIMWI.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/13, Wizara itaendelea kutoa mchango wake wa tele-kwa-tele kwa Halmashauri zilizoanzisha na kuchangia Mifuko ya Afya ya Jamii. Kwa kutumia utaratibu uliopo, Wizara

kupitia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, itaendelea kuwahamasisha wananchi kujiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii, lengo ikiwa ni kuongeza uhakika wa upatikanaji wa huduma za afya hasa kwa wananchi waishio vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendeleza ukarabati wa vituo vya ustawi wa jamii vya Masiwani Tanga, chuo cha wanawake wasioona Singida, chuo cha ufundi Luanzari, na chuo cha ufundi Mtapika na makazi ya wazee wasiojiweza Sukamahela. Aidha, Wizara itaendelea kufanya ununuzi wa vifaa mbalimbali vya kujimudu kwa watu wenye ulemavu vikiwemo baiskeli za miguu mitatu, fimbo nyeupe na vifaa vingine. Pia, Wizara itaendelea kufanya ununuzi wa mahitaji muhimu kwa wakazi kwenye Makao ya watoto Kurasini, Mahabusu za watoto, shule ya maadilisho Mbeya na Makazi ya wazee wasiojiweza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea na ukarabati wa vyuo vya mafunzo na ujenzi wa maktaba katika Taasisi ya Ustawi wa Jamii. Lengo ni kuboresha mazingira ya kujifunzia na kuongeza wataalam watakaotoa huduma za afya na ustawi wa jamii nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ushirikiano wa ndani na nje ya nchi; katika mwaka 2012/2013, Wizara itaendelea kuwa na ushirikiano mzuri na wa karibu na nchi rafiki na Mashirika ya Kimataifa yanayosaidia sekta ya afya na ustawi wa jamii. Aidha, itaendeleza ushirikiano mzuri na sekta nyingine ambazo

zinachangia katika kutoa huduma za afya na ustawi wa jamii nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2012/2013, Wizara kwa kushirikiana na mikoa na wadau wa sekta itaendelea kuadhimisha siku mbalimbali za afya na ustawi wa jamii za Kitaifa na Kimataifa. Baadhi ya siku hizo ni za Afya Duniani, UKIMWI, Ukoma, Malaria Afrika, Wazee, Watu Wenye Ulemavu, Kutotumia Tumbaku, Wachangia damu, *Albino*, Kifua Kikuu, Fimbo Nyeupe na Tiba Asili ya Mwafrika.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii ya kipekee kuzishukuru nchi za Denmark, Uswisi, Uholanzi, Norway na Ujerumani na Mashirika ya Maendeleo ya Kimataifa yakiwemo Benki ya Dunia, *UNFPA, Ireland Aid, CIDA* (Canada), Shirika la Kuhudumia Watoto *(UNICEF)* na *UN System* kwa kutoa misaada katika Mfuko wa Pamoja wa Sekta ya Afya na Ustawi wa Jamii ambao umesaidia kwa kiasi kikubwa kuboresha huduma za afya na ustawi wa jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, napenda kuzishukuru nchi nyingine za China, Cuba, Canada, Hispania, India, Ireland, Italia, Japan, Korea Kusini, Marekani, Misri, Sweden, Ufaransa na Uingereza ambazo zimeendelea kuisaidia sekta ya afya na ustawi wa jamii kwa njia mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii pia kushukuru Mashirika mengine ya Kimataifa kwa ushirikiano wao mzuri na Wizara. Mashirika haya

yanajumuisha Jumuiya ya Nchi za Ulaya *(EU)*, Shirika la Afya Duniani *(WHO)*, Shirika la Umoja wa Kimataifa la Maendeleo *(UNDP), DFID, FINIDA, GAVI*, Shirika la Umoja wa Mataifa la Kudhibiti UKIMWI *(UNAIDS)*, Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi *(UNHCR)*, Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki *(IAEA)*, Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB)*, Benki ya Nchi za Kiarabu kwa ajili ya Maendeleo ya Uchumi ya Nchi za Afrika *(BADEA), ORIO*, Umoja wa Nchi zinazotoa Mafuta kwa wingi Duniani *(OPEC)*, na Madaktari Wasio na Mipaka *(Medicins Sans Frontieres – MSF)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wengine ni *CUAMM, DANIDA, GIZ, JICA, KOICA, Baylor College of Medicine* ya Marekani, *KfW*, *MISERIOR, EED, SAREC, SDC, CDC, SIDA* (Sweden), *Abbott Fund, Engender Health* (USA), *CORDAID (Netherlands) BASIC NEED* (UK), *HelpAge International, ILO, Family Health International (FHI), Elizabeth Glaser Paediatric Aids Foundation (EGPAF),* Shirika la Upasuaji la Spain, *Good Samaritan Foundation (GSF), German TB and Leprosy Relief Association (GLRA), USAID*, Kundi la *SIGN* la Marekani, *Jane Adams School of Social Work* ya Chuo Kikuu cha 168 Illinois Marekani na Shirika la *Human Resource Capacity Project*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, tunawashukuru pia Wadau wa Maendeleo wa mradi wa kudhibiti magonjwa ya Usubi na Vikope ambao ni *African Programme for Orchorcerciasis Control, Plan International, International Eye Foundation, Sight Savers International, Merck & Company, Pfizer, Helen Keller*

*International, Christoffel Blinden Mission (CBM)* na *International Trachoma Initiative*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi nyingine za Kimataifa ni *Axios International, President's Emergency Plan for AIDS Relief (PEPFAR), Clinton Health Access Initiative, Bill and Melinda Gates Foundation, London School of Hygiene and Tropical Medicine, Johns Hopkins University, Global Fund, University of Columbia, CMB, Christian Relief Services (CRS), Citi Bank, General Electric (GE – USA), Havard University* na *Duke University za Marekani, University of Marryland, Community of Saint Egidio (DREAM). (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, taasisi nyingine ni *Supply Chain Management System (SCMS), NOVARTIS, Saint Thomas Hospital- London, Management Science for Health (MSH), Glaxo Smith Kline (GSK), Merck, Qiagen, Labiofarm Industry, URC, Futures Group, USA-Presidential Malaria Initiative (PMI), IMA, WorldVision, MEDA, Pathfinder, PATH, Jhpiego, Pharm Access International, Malaria No More, Save the Children, Research Triangle Institute (RTI), AIHA, CLSI, ASCP, ASM, APHL, PactWorld, World Education Inc, ECSA, Intrahealth, I-TECH* na *Military Advancement for Medical Research, Department of Defence* ya Marekani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kwa niaba ya Serikali kuwashukuru watu binafsi, vyama vya hiari na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya ndani ya nchi kwa kuwa mstari wa mbele katika kuchangia uimarishaji wa huduma za afya na ustawi

wa jamii. Mashirika hayo ni pamoja na Benjamin William Mkapa *HIV/AIDS Foundation, Aga Khan Foundation, AMREF, Lions Club, Rotary Club International,* BAKWATA, *CCBRT, CSSC, CCT, ELCT, TEC,* Msalaba Mwekundu, Shree Hindu Mandal, UMATI, Counsenuth, PRINMAT, *MAT, TANNA, APT, MeLSAT, AGOTA, PAT, TPHA, USADEFU, PASADA, Ifakara Health Institute, TISS, PSI, TPRI, PACT, Women Dignity Project, Tanzania Diabetic Association, MEHATA, APHFTA, TANESA, MEWATA, Regional Psychosocial Support Initiatives (REPSSI), MUKIKUTE, White Ribbon Alliance*, Mabaraza yote ya Kitaaluma, Mashirika, hospitali na vituo vya kutolea huduma za afya na ustawi wa jamii nchini pamoja na vyama vyote vya kitaaluma vya sekta ya afya na ustawi wa jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii kwa niaba ya Serikali kuvishukuru Vyuo Vikuu vya Dar es Salaam, Muhimbili, Sokoine, Ardhi, Mzumbe, Chuo Kikuu Huria, Kumbukumbu ya Hubert Kairuki, *IMTU*, Tumaini, Saint Agustino, Saint John, Aga Khan, Morogoro Muslim, Arusha pamoja na Vyuo vyote vya Sekta ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa kuwa mstari wa mbele katika kuchangia uimarishaji wa huduma. Aidha, Wizara inawashukuru wadau wengine waliotoa huduma ya elimu kwa njia za redio, televisheni, magazeti na mitandao ya kijamii katika masuala ya afya na ustawi wa jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, katika kipindi hiki kifupi cha utendaji wangu wa kazi katika Wizara hii, nimefanya kazi kwa ushirikiano mkubwa na viongozi wote wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Napenda

kumpongeza Mheshimiwa Daktari Seif Suleiman Rashid, Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais ili tusaidiane kuisimamia Wizara hii. Aidha, nachukua fursa hii kumshukuru Kaimu Katibu Mkuu Bibi Regina Lucian Kikuli kwa kunipa ushirikiano katika utekelezaji wa majukumu yangu katika kipindi hiki kifupi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, nawashukuru wafuatao: Daktari Donan Mmbando, Kaimu Mganga Mkuu wa Serikali, Bwana Dunford Daniel Makala, Kamishna wa Ustawi wa Jamii na Wakurugenzi wa Idara zote katika Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru pia, Wakurugenzi wa Hospitali za Rufaa, Maalum na Taasisi zilizo chini ya Wizara, Waganga Wakuu wa Mikoa na Wilaya, Waganga Wafawidhi wa Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati, Wakuu wa Vyuo vya Mafunzo ya Afya vilivyo chini ya Wizara na wafanyakazi wote wa Sekta ya Afya na Ustawi wa Jamii na Mashirika ya Dini, ya Kujitolea na Binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa shukrani kwa sekta nyingine ambazo tunashirikiana nazo katika kutoa huduma za afya na ustawi wa jamii pamoja na wananchi wote kwa ushirikiano wao. Nawaomba waendelee kufanya kazi kwa manufaa ya wananchi na Taifa letu kwa ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumalizia hotuba yangu kwa kuishukuru familia. Kipekee

namshukuru mke wangu mpendwa Mama Mariam Mwinyi na watoto wetu Ibrahimu Hussein Mwinyi, Jamila Hussein Mwinyi, Tariq Hussein Mwinyi, Sitti Hussein Mwinyi, kwa kunitia moyo na kwa mchango wao unaoniwezesha kutekeleza majukumu yangu ya Kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wananchi wa Jimbo la Kwahani nawashukuru kwa heshima waliyonipa kwa kunichagua kuwa mbunge wao na kwa ushirikiano wanaoendelea kunipatia katika kuendeleza jimbo na naahidi nitaendelea kuwaenzi na kuwatumikia kwa moyo mkunjufu ili kuleta mabadiliko ya haraka ya kimaendeleo katika Jimbo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, kwa upande wa shukrani, lakini kwa unyenyekevu mkubwa, napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais Daktari Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuniteua kuiongoza Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Nasema ahsante sana kwa imani aliyonayo kwangu na naahidi kufanya kazi kwa uadilifu na uwezo wangu wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 2012/2013, Wizara imekadiria kukusanya mapato ya kiasi cha sh. 30,556,448,000.00 Kati ya kiasi hiki sh. 25,000,000,000.00 zitakusanywa katika Mashirika na Taasisi zilizo chini ya Wizara na kiasi cha sh. 5,556,488,000.00 ni kutoka katika vyanzo vya Makao Makuu. Vyanzo hivyo vinatokana na makusanyo ya uchangiaji gharama kutoka kwenye vyuo vya Wizara, usajili wa hospitali binafsi, maabara binafsi na Baraza la Waatalam wa Maabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 2012/2013, Wizara inakadiria kutumia kiasi cha sh. 298,228,037,000.00 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo kati ya fedha hizo, kiasi cha sh. 109,763,080,592.00 kitatumika kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na sh. 188,464,956,408.00 ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi. Kati ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya mishahara kiasi cha sh. 34,621,632,800.00 kimetengwa kwa ajili ya watumishi wa Makao Makuu na sh. 153,843,323,608.00 ni kwa ajili ya watumishi wa Taasisi, Mashirika na Wakala zilizo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Miradi ya Maendeleo, kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara inakadiria kutumia jumla ya sh. 283,446,029,000.00 kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, Serikali ya Tanzania itachangia kiasi cha sh. 19,142,638,000.00. Fedha kutoka kwa wahisani wanaoisaidia Sekta ya Afya ni sh. 264,303,391,000.00 Kati ya fedha hizo sh. 64,285,624,800.00 zitatolewa na wahisani wanaochangia Mfuko wa Pamoja na sh. 200,017,766,200.00 zitatolewa na wahisani walio nje ya Mfuko.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuiwezesha Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kutekeleza kazi zilizopangwa mwaka 2012/13, naliomba Bunge lako Tukufu litafakari, lijadili na kuidhinisha makadirio ya matumizi ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii pamoja na Asasi zake yenye jumla ya sh. 581,674,066,000.00 Kati ya fedha hizo, sh. 298,228,037,000.00 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na sh. 283,446,029,000.00 ni kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii. Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi, tunakushukuru sana kwa kusoma hotuba yako.

Sasa naomba nimwite Msemaji wa Kamati ya Huduma za Jamii kuhusiana na Wizara ya Afya na Ustawi Dkt. Kebwe Stephen Kebwe. Karibu Mheshimiwa!

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE (K.n.y. MHE. MARGARET S. SITTA) MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII):** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote natoa pole kwa niaba ya Kamati kwa kifo cha Mtumishi wa Bunge ndugu Peter Mazengo kilichotokea jana jioni kwa ajali ya gari. Mwenyezi Mungu aipokea roho yake ipumzike mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa watani zangu wa jadi wa Yanga, mashabiki na wapenzi wote wa klabu ya Yanga kwa ushindi wao wa ujuzi dhidi ya Azam kwa kufanikiwa kuchukua Kombe la *CECAF* kwa mara ya pili mfululizo ila wasibweteke. Nawasihi ndugu zangu wa Simba kuwa wavumilivu na watulivu kwani asiyekubali kushindwa si mshindani.

Suala ni kujizatiti upya kwa kujipanga na kuipanga safu makini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana na wenzangu walionitangulia kutoa pole kwa wafiwa na majeruhi wote wa ajali ya meli *MV. Skagit* iliyotokea tarehe 18 Julai, 2012 huko Zanzibar. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inatoa pole kwa Daktari Stephen Ulimboka, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Madaktari na familia yake kutokana na tukio la kufanyiwa unyama kwa kupigwa na kutupwa maeneo ya Mabwepande. Kamati inamwombea kwa Mwenyezi Mungu apone haraka na kurejea katika afya yake ya kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nawatakia waislam wote mfungo mwema wa Ramadhani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ajili ya muda naomba taarifa yote hii iingie katika *Hansard* kama ilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (7) na Kanuni ya 114(11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2007, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012 na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na nguvu kusimama mbele ya Bunge hili kutoa Maoni na ushauri wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii. Natumia nafasi hii kuwapongeza Wabunge wenzetu waliopewa dhamana ya kuwa Mawaziri na Naibu Mawaziri kufuatia mabadiliko ya Baraza la Mawaziri; ni imani yangu kwamba tutashirikiana nao katika utendaji kazi wenye lengo la kuwaletea maendeleo Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii ina jukumu la kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Katika kutekeleza jukumu hilo kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012, Kamati ilifanya ziara kukagua utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii zikiwemo; utoaji huduma za afya katika Kitengo cha Matibabu ya Figo Muhimbili *(Neuphrology Unit)*, Taasisi ya Mifupa *MOI*, Bohari ya Dawa ya Kanda ya Ziwa, Hospitali ya Mkoa wa Mwanza ya Sekou Toure, Kituo cha Afya cha Sangabuye, Mpango wa Damu Salama - Mwanza, Makazi ya Wazee Sukamahela-Singida, Taasisi ya Saratani *Ocean Road*, Dar es Salaam na Kituo cha Afya Mlali, Kongwa-Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilitoa ushauri uliolenga kuboresha utolewaji wa huduma za afya kwa wananchi katika Taarifa ya Utekelezaji wa Shughuli za Kamati ya Mwezi Aprili 2011 mpaka Aprili 2012, iliyowasilishwa katika Mkutano wa Saba wa Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 4 Juni mpaka 5 Juni, 2012, Kamati ilikutana kupokea na kujadili Taarifa ya utekelezaji wa malengo ya bajeti ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii yenye Fungu 52, kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012 na kufikiria makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 iliyowasilishwa na Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Mheshimiwa Daktari Hussein Ali Mwinyi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inatoa masikitiko yake ya kupata muda mfupi wa kutafakari na kupitia Vitabu vya Bajeti kwa mwaka wa fedha 2012/2013, hali iliyojitokeza pia katika Mwaka wa Fedha 2011/2012. Jambo hili linasababishwa na kuchelewa kuwasilishwa kwa Vitabu hivyo katika Ofisi ya Bunge, nje ya utaratibu ulioainishwa na Kanuni ya 96(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa ya Waziri iliyowasilishwa mbele ya Kamati ilikuwa na maeneo mahsusi, ambayo ni pamoja na:-

- Utekelezaji wa maoni ya Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii kwa bajeti ya Mwaka 2011/2012;

- Utekelezaji wa Hoja za Ukaguzi kwa Hesabu za mwaka ulioishia tarehe 30 Juni 2010 za Bohari Kuu ya Dawa *(MSD)*;

- Utekelezaji wa maoni ya Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii yaliyotolewa katika Taarifa ya Utekelezaji wa Shughuli za Kamati Mwezi Aprili 2011 hadi Aprili 2012; na

- Utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwaka wa Fedha 2011/2012, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii iliidhinishiwa Jumla ya sh. 584,161,863,000.00. Kati ya fedha hizo sh. 219,367,376,000.00 zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na sh. 364,794,487,000.00 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Tarehe 30 Mei, 2012 jumla ya sh. 361,562,929,831.00 sawa na asilimia 61.8 zilipokelewa kutoka Hazina kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ilitoa Taarifa ya mrejesho wa utekelezaji wa maoni na mapendekezo ya Kamati, yaliyotolewa katika Taarifa ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012, Kamati ilibaini kuwa bado kuna maeneo yanayohitaji kufanyiwa kazi zaidi mapema iwezekanavyo. Maeneo hayo ni pamoja na:-

(a) Taasisi ya Ustawi wa Jamii Dar es Salaam kukamilisha vigezo vya *NACTE* ili kupata Ithibati ya Kudumu, sambamba na kumaliza mgogoro baina ya Menejimenti na Wakufunzi ambao ajira zao zilisitishwa mwezi Agosti 2011;

(b) Kuwezesha upatikanaji wa Mashine ya Mionzi angalau moja katika Taasisi ya Saratani ya *Ocean Road* Dar es Salaam;

(c) *MSD* kusambaza dawa na vitendanishi vyenye viwango vinavyokubalika;

(d) Serikali kusimamia usambazaji wa dawa kuzuia wizi pamoja na kuweka alama za utambuzi wa Dawa za Serikali;

(e) Uwazi wa matumizi ya fedha za Mfuko wa Pamoja wa Sekta ya Afya *Health Busket Funds;*

(f) Uwazi wa Taarifa za Fedha zinazotolewa na Serikali kwa kila Halmashauri kwa ajili ya utoaji wa huduma za Afya kwa wadau;

(g) Utendaji kazi wa Kitengo cha Tiba ya Figo katika Hospitali ya Taifa Muhimbili; na

(h) Utekelezaji wa madai ya Madaktari na Watumishi wengine wa Sekta ya Afya nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la Utekelezaji wa Madai ya Madaktari dhidi ya Serikali; Kamati imekuwa ikifuatilia kwa karibu na kutoa ushauri uliolenga kumaliza tatizo hili. Katika kupata Taarifa ya Serikali kuhusu utekelezaji wa madai ya Madaktari, Kamati ilielezwa kwamba Serikali imetekeleza madai yanayoweza kufanyiwa kazi kwa muda mfupi kama ifuatavyo:-

(a) Yamefanyika mabadiliko ya Watendaji Wakuu wa Wizara;

(b) Posho ya *Interns* imeanza kulipwa kuanzia Mwezi Februari 2012 na kupewa kipaumbele na Serikali kupitia Hazina, kwa kutolewa mapema kama mishahara. Hivyo kwa sasa fedha hizi zinatolewa na kulipwa kwa muda unaostahili;

*(c) On-call allowance* - imeanza kulipwa kwa viwango vipya kuanzia mwezi Februari 2012, viwango vipya vya sh. 15,000/= (*Interns*), sh. 20,000/= (*Registrars*) na sh. 25,000/= (*Specialists*). Aidha, malipo haya yameingizwa katika Bajeti mpya 2012/2013 na kiasi cha Shilingi Bilioni 18.9 kimetengwa kwa ajili ya Watumishi wa Sekta ya Afya. Kati ya hizo, shilingi bilioni 5.4 ni za Wafanyakazi wa Fungu 52 la Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii linalohudumia Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Hospitali za Rufaa, Kanda na Hospitali Maalum. Kiasi kilichobaki cha shilingi bilioni 13.5 ni kwa ajili ya Watumishi wa Sekta ya Afya ngazi za Mikoa na Halmashauri;

(d) Posho ya uchunguzi wa maiti (*Post mortem allowance*) imeongezwa kufikia sh. 100,000/= kwa Daktari na sh. 50,000/= kwa Wasaidizi (kutoka sh. 10,000/= ya awali);

(e) Madaktari wamepewa *Green Card* za Bima ya Afya;

(f) Katika Bajeti ya mwaka 2012/2013, fedha zimetengwa kwa ajili ya kununua chanjo ya *Hepatitis* B kwa ajili ya kuwakinga Wafanyakazi wote wa Sekta ya Afya;

(g) Mapendekezo ya Muundo kutoka kwa Wauguzi, Wafamasia na Wataalam wa Teknolojia ya Maabara kwa ajili ya kupitia na kutoa ushauri wa kitaalam kuhusu Muundo wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, hususan uanzishwaji wa Idara za maeneo haya yamewasilishwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma;

(h) Madaktari watakopeshwa magari kwa utaratibu wa Watumishi kukopeshwa magari, ambapo Watumishi wa Sekta ya Afya watapewa kipaumbele;

(i) Katika kuboresha mazingira ya kazi, Wizara katika Bajeti ya Mwaka 2012/2013, imeongeza fedha kwa ajili ya ununuzi wa dawa, vifaa na vifaa tiba. Aidha, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na TAMISEMI watasimamia vyanzo vya mapato kutoka Bima ya Afya, Mfuko wa Afya ya Jamii na malipo ya papo kwa papo ya uchangiaji wa huduma za afya ili asilimia inayotengwa kwa ajili ya kununua dawa itekelezwe ipasavyo; na

(j) Wizara imepokea na kuidhinisha fedha za mafunzo ya Shahada ya Uzamili kwa Wanafunzi 63 wa *MUHAS*, ambao hawakuwa na ufadhili na waliomba kufadhiliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kamati ilielezwa kuwa maeneo ambayo hayakuweza kufikiwa muafaka kutokana na hali ya uwezo wa Serikali ni pamoja na:-

(a) Nyongeza ya Mishahara kwa Madaktari kufikia sh. 3.5 milioni (Nyongeza iliyowekwa katika bajeti ya mwaka 2012/2013 ni asilimia 15);

(b) Nyongeza ya Posho ya mazingira hatarishi (*Risk Allowance)* ya asilimia 30;

(c) Posho ya mazingira magumu (*Hardship Allowance)* ya asilimia 40;

(d) Suala la Madaktari wote kupewa nyumba au posho ya nyumba ya asilimia 30; na

(e) Posho ya usafiri ya asilimia 10.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilielezwa pia kwamba madai ya Madaktari yaliyobaki yanazungumzika na Serikali iko tayari kuyashughulikia kwa awamu kadri uwezo utakavyoruhusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inasikitishwa na mgogoro uliopo kati ya Serikali na Madaktari nchini kwani mgogoro huu unajirudia kwa mara ya tatu tangu ulipoanza Mwezi Januari 2012 na wanaoathirika na mgogoro ni wananchi wasio na hatia.

Kamati inasisitiza kwamba pande mbili ambazo ni Wataalam katika Sekta ya Afya na Serikali warudi kwenye meza ya majadiliano yenye lengo la kufikia muafaka mapema iwezekanavyo. Kamati inaamini kwamba suluhu ya tatizo hili itapatikana katika majadiliano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kufuatilia utekelezaji wa shughuli za Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012, Kamati ilibaini changamoto zifuatazo zinazoikabili Sekta ya Afya nchini:-

(a) Tengeo la bajeti ya Sekta ya Afya nchini kutokidhi Azimio la Abuja la Mwaka 2001 linazozitaka kila nchi Mwanachama wa Umoja wa Afrika kutenga 15% ya bajeti yake kwa ajili ya Sekta ya afya. Katika Afrika ni nchi ya Rwanda pekee yake ambayo wameweza kufikia asilimia 18;

(b) Bajeti inayotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kutegemea zaidi fedha za wahisani kwa zaidi ya asilimia 90 ni jambo la hatari;

(c) Migogoro ya mara kwa mara kati ya Serikali na Watumishi wa Sekta ya Afya, ni changamoto ambayo tuliibaini;

(d) Kasi ndogo ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi MMAM 2007-2017;

(e) Deni la Serikali kwa Bohari Kuu ya Dawa *(MSD)* la sh. 41.7 bilioni (Machi 2012), pamoja na utendaji usioridhisha wa Taasisi hii;

(f) Bajeti inayotengwa kwa ajili ya ununuzi wa dawa kutokidhi mahitaji;

(g) Mazingira duni ya Utoaji wa huduma za afya katika Zahanati na Vituo vya afya nchini hasa katika

maeneo ya Vijijini, ikiwemo upungufu wa watumishi, dawa, vifaa tiba na vitendanishi;

(h) Utolewaji duni wa huduma ya afya ya Mama na Mtoto hasa katika maeneo ya Vijijini;

(i) Uwepo wa idadi kubwa ya Dawa zilizo chini ya viwango;

(j) Ongezeko la vipodozi visivyofaa kwa matumizi ya binadamu;

(k) Gharama kubwa kwa Serikali za kupeleka wagonjwa nje ya nchi kwa matibabu wakiwemo wagonjwa wa moyo; na

(l) Gharama kubwa ya matibabu ya Saratani nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa Fedha 2012/2013 Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii inatarajia kukusanya mapato yenye jumla ya sh. 44,121,810,729.58 na imeomba kuidhinishiwa jumla ya sh. 581,674,066,000.00 kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Kati ya fedha hizo sh. 298,228,037,000.00 zitatumika kwa ajili ya matumizi ya kawaida na sh. 283,446,029,000.00 kwa ajili ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilifanya uchambuzi wa mgawanyo wa fedha za Bajeti katika Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 na kubaini kuwa mgawanyo wa bajeti ya Wizara haukuzingatia

mambo muhimu katika utoaji wa huduma za afya nchini kama ifuatavyo:-

(a) Ununuzi wa dawa kulingana na uhitaji. Kiasi cha shilingi bilioni 54.08 kilitengwa kwa ajili ya ununuzi wa dawa kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013, wakati uhitaji ni jumla ya shilingi bilioni 100.3;

(b) Idara ya Ustawi wa Jamii kutopewa fedha za kutosha kuhudumia makazi ya watu wenye ulemavu, wazee na makao ya watoto waishio katika mazingira magumu;

(c) Ununuzi wa Mashine angau moja ya Mionzi na ujenzi wa chumba cha kuweka mashine hiyo katika Taasisi ya Saratani ya *Ocean Road*, Dar es Salaam;

(d) Ununuzi wa jenereta la dharura kwa ajili ya Taasisi ya Mifupa *MOI;* na

(e) Ulipaji wa deni la Serikali kwa *MSD* la shilingi 41.7 bilioni (Machi 2012) ambao haukutengewa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kutoridhika na mgawanyo wa Bajeti ya Wizara, Kamati ilielekeza kupitia upya mgawanyo wa fedha katika vifungu vya Wizara ili kupata fedha zitakazohudumia mambo muhimu yaliyobainika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 8 Juni, 2012 Dar es Salaam, Kamati ilikutana na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na kuelezwa kuwa umefanyika

uhamisho wa ndani ya vifungu vya Wizara (*Budget Reallocation*) kama ifuatavyo:-

(i) Jumla ya sh. 8,609,000,000.00 zilipatikana kwa kupunguza sh. 3,435,000,000.00 toka kasma 220404 *Dental Supplies* na sh. 5,174,000,000.00 toka kasma 220405 *Hospital Supplies*. Hivyo kasma 220402 *Drugs and Medicines* imeongezewa fedha hizo, kutoka sh. 7,630,000,000.00 zilizokuwepo hadi sh. 16,239,000,000.00 na hivyo kuvuka kiwango cha sh. 13,636,239,00.00 cha mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ushauri wa Kamati, Wizara kwa kushirikiana na TAMISEMI imepitia mpango kabambe wa kila Halmashauri kuhusu ununuzi wa dawa na kutenga jumla ya Sh. 17,237,267,019.00. Aidha, Mfuko wa Pamoja wa Sekta ya Afya (*Health Busket Fund*) umetenga jumla ya Sh. 46, 459,574,800.00 kwa ajili ya ununuzi wa dawa.

(ii) Kwa ushauri wa Kamati, jumla ya Sh.5,000,000,000.00 ziliongezwa na Serikali katika bajeti ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na kupelekwa moja kwa moja kwenye ununuzi wa dawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo bajeti halisi ya dawa kwa mwaka wa Fedha 2012/2013 ni Sh. 84, 935,841,819.00.

(iii) Aidha, Taasisi mbalimbali za Wizara ikiwemo Taasisi ya *Saratani Ocean Road,* Taasisi ya Mifupa *MOI*, Hospitali za Rufaa za Mbeya, Kibong'oto na

Mirembe, Idara ya Ustawi wa Jamii ziliongezewa fedha, kama inavyoonekana katika Jedwali I.

## JEDWALI I: MAENEO YALIYOONGEZEWA BAJETI BAADA YA MAJADILIANO NA KAMATI

## KIWANGO CHA AWALI

| | ENEO | KIWANGO CHA AWALI | | NYONGEZA | | KIWANGO |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | OC | MAENDELEO | OC | MAENDELEO | |
| **A** | **Eneo lililoongezewa toka uhamisho ndani ya kifungu** | | | | **Kutoka Health & Dental Supplies** | |
| 1 | Drugs and Medicines | 7.630,000,000 | | 8.609,000,000 | | 16.239.000.000 |
| | **Jumla** | **7,630,000,000** | | **8,609,000,000** | | **16,239,000,000** |
| | | | | | | |
| **B** | **Eneo lililoongezewa kwa uhamisho kutoka Kasma za Vifungu mbalimbali** | | | | | |
| 1 | Ocean Road Cancer Institute | 6,181,812,000 | 3,000,000,000 | | 800,000,000 | 9.981.812,000 |
| 2 | Social Welfare | 4,958,331,600 | | 300,000,000 | | 5.258.331,6000 |
| 3 | MOI | 19,710,666,000 | 1,042,638,000 | 300,000,000 | 200,000,000 | 12,263,304,000 |
| 4 | TB and LEPROSY | | | 100,000,000 | | 100,000,000 |
| 5 | ARV | | | 500,000,000 | | 500,000,000 |
| | **Jumla** | | | **1,200,000,000** | **1,000,000,000** | **28,093,447.600** |
| | **HOSPITAL** | | | | | |
| 6 | Mbeya Referral Hospital | 2,185,0240,000 | | 35,000,000 | | 1.220,024,000 |
| 7 | Mirembe and Isanga Institution | 754,104,0000 | | 20,000,000 | | 774,104,000 |
| 8 | Kibongoto Hospital | 685,416,000 | | 20,000,000 | | 705.416,000 |
| | Jumla | | | 75,000,000 | | 2,699,544,000 |
| | **JUMLA KUU YA ENEO B** | | | **1,275,000,000** | | |

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishukuru Serikali kwa kukubali ushauri wa Kamati na kufanya mabadiliko ya bajeti za vifungu vya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kukidhi mahitaji muhimu ya Wizara hiyo ikiwemo kuongeza bajeti ya ununuzi wa dawa kwa mwaka wa fedha 2012/2013, kutoka jumla ya Sh.54, 089,575,800.00 hadi Sh.84, 935,841,819.00.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuridhika na majibu ya hoja mbalimbali na kupitia kifungu kwa kifungu na kukamilisha zoezi la kujadili bajeti ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Kamati inatoa ushauri katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, Serikali kuwasilisha Vitabu vya Bajeti ya Serikali Bungeni kwa wakati. Kwa mujibu wa Kanuni ya 96(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Mwaka 2007 inasema:-

*"...kila Mbunge atapelekewa Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na ya Maendeleo ya Serikali ya Mwaka wa Fedha unaohusika, siku 21 kabla ya Mkutano ambao utashughulikia Makadirio hayo…"*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inasisitiza kwamba Kanuni hiyo izingatiwe ili kuwapa Waheshimiwa Wabunge muda, kutafakari na kusoma kwa kina Bajeti ya Serikali na kutoa ushauri wenye tija kwa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, bajeti ya Serikali katika Sekta ya Afya nchini. Tanzania imeridhia Azimio la Abuja la mwaka 2001 linaloelekeza kila nchi Mwanachama wa Umoja wa Afrika (*African Union*) kutenga 15% ya Bajeti ya Serikali katika Sekta ya Afya ifikapo mwaka 2015. Takwimu zinaonesha kwamba bajeti inayotengwa katika sekta ya Afya nchini inateremka mwaka hadi mwaka kama Jedwali II linavyoonesha:-

**JEDWALI LA II: Mwenendo wa Bajeti kwa Sekta ya Afya kwa Mwaka 2006/2007-2010/2011(000,000,000)**

| | 2006/07 | 2007/08 | 2008/09 | 2009/10 | 2010/11 | 2011/12 | 2012/13 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Bajeti Kuu ya Serikali (bila deni la Taifa) | 4,496,000 | 5,452,000 | 6,631,000 | 7,994,000 | 9,899,100 | 10,730,000 | 12,374,588 |
| Bajeti ya Sekta ya Afya | 520,000 | 616,000 | 734,000 | 925,000 | 1,009,000 | 1,209,000 | 1,288,800 |
| Asilimia | 11.6% | 11.3% | 11.1% | 11.6% | 10.2% | 10.50% | 10.40% |
| Bajeti kwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii | 286.8bil | 369.6bil | 440.2bil | 478.9bil | 584.1bil | 584.11bil | 581.7.bil |

**Chanzo: Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii Juni, 2012**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa utekelezaji wa utoaji wa huduma za afya unahusu uwezo wa Serikali katika kutenga bajeti inayokidhi mahitaji ya sekta ya afya nchini, Kamati inashauri kwamba Serikali ijizatiti kupanua wigo wa walipa kodi, kuongeza vyanzo zaidi vya mapato ya ndani na kupunguza mianya ya ukwepaji kodi. Hatua hii itawezesha Serikali kutenga 15% ya bajeti yake na kufikia malengo ya Abuja. Aidha, Sekta ya Afya ipewe kipaumbele cha kudumu kibajeti ili iweze kutoa huduma bora za afya kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, tengeo la Bajeti ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii katika Miradi ya Maendeleo. Jumla ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa mwaka 2012/2013 ni Sh.283,446,029,000.00 ambapo fedha kutoka vyanzo vya ndani vya Serikali ni Sh.19,142,638,000.00 na fedha

kutoka kwa wadau wa maendeleo wanaosaidia sekta ya afya (Wahisani) ni Sh.264,303,391,000.00. Uzoefu unaonesha kwamba Bajeti ya Wizara katika shughuli za maendeleo hutegemea kwa kiasi kikubwa fedha za wahisani, kama inavyooneshwa katika Jedwali III.

## WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII

| Bajeti ya Fedha za Miradi ya Maendeleo ya Wizara ya Afya kwa Kipindi cha kuanzia 2008 – 2013 | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka** | **Fedha za Ndani** | | **% ya zilizotolewa** | **Kiasi kilichoidhinishwa** | | **% ya zilizotolewa** |
| | Kiasi Kilichoidhi-nishwa | Kiasi kilichotolewa | | Kiasi Kilichoidhi-nishwa | Kiasi kilichotolewa | |
| 2008/2009 | 13,029,173,000 | 10,000,000,000 | 77% | 208,214,783,083 | 173,905,382,168 | 84% |
| 2009/2010 | 13,029,173,000 | 9,529,193,000 | 73% | 247,570,694,000 | 253,173,439,657 | 102% |
| 2010/2011 | 9,873,761,000 | 7,000,000,000 | 71% | 437,989,409,130 | 240,661,423,058 | 55% |
| 2011/2012 | 9,873,761,000 | 8,166,944,000 | 83% | 354,920,726,000 | 131,318,998,994 | 37% |
| 2012/2013 | 19,142,638,000 | - | - | 264,303,391,000 | - | |
| **JUMLA** | **64,948,506,000** | **34,696,137,000** | | **1,512,999,003,213** | **371,980,422,052** | |

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya shughuli za miradi ya maendeleo hushindwa kutekelezwa wafadhili wanaposhindwa kutoa fedha kwa wakati, wanapotoa kiasi kidogo kuliko walichoahidi na hata wanapojitoa. Kwa mfano, kwa mwaka wa fedha 2011/2012, tengeo la Miradi ya Maendeleo kutoka kwa wahisani lilikuwa ni Sh.354,920,726,000.00. Hadi kufikia tarehe 30 Mei, 2012, jumla ya Sh.129,517,808,846 .00 tu, sawa na asilimia 36.4 zilikuwa zimetolewa na wahisani. Kamati inashauri kwamba Serikali ipunguze utegemezi huo kwa kutenga bajeti ya maendeleo kutoka katika fedha za ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, Serikali kuimarisha vyanzo vya ndani vya mapato. Kamati imebaini kwamba kuna vyanzo mbalimbali vya mapato ambavyo vikisimamiwa kikamilifu vitaongeza mapato

ya ndani ya Wizara hii. Vyanzo hivyo ni pamoja na Mamlaka ya Chakula na Dawa *Tanzania (TFDA),* Wakala wa Mkemia Mkuu wa Serikali *(Chief Government Chemist),* Hospitali ya Taifa Muhimbili, Taasisi ya Mifupa MOI na Taasisi ya Chakula na Lishe. Kamati inashauri kwamba Serikali iweke mikakati madhubuti ya kukusanya mapato kusaidia uendeshaji wa Sekta ya Afya nchini. Aidha, Hospitali za Rufaa za Mikoa zitumie mapato yake ya ndani kugharamia baadhi ya shughuli za utoaji wa huduma za afya katika Taasisi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM) 2007 – 2017. Kupitia mpango huu, Serikali imedhamiria kuboresha huduma ya afya vijijini na kusogeza huduma za afya hususan tiba, kinga, uboreshaji na utengamano karibu na wananchi. Katika kufanikisha lengo la mpango huu Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

(i) Ni vyema Serikali iongeze kasi ya utekelezaji wa MMAM kwa kufanikisha upatikanaji wa dawa, vifaa na vifaa tiba nchini. Kasi hii iende sambamba na kuboresha miundombinu, kupata wataalamu na watumishi wengine wa afya katika ngazi zote ili kutoa huduma za afya kulingana na mahitaji.

(ii) Serikali itathimini utekelezaji wa MMAM ili kubaini ufanisi na upungufu wa mpango huu na kuyatatua mapema iwezekanavyo.

(iii) Mpango wa ujenzi wa Zahanati kwa kila Kijiji ukamilike mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sita, uboreshaji wa mazingira ya utoaji huduma za afya nchini. Huduma za afya nchini ni jambo la msingi kwa maendeleo na ustawi wa jamii. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuipandisha hadhi Hospitali ya Kijeshi ya Lugalo kuwa Hospitali ya Rufaa. Pamoja na pongezi hizo, Kamati inashauri kwamba Hospitali za Kijeshi ziimarishwe ili ziweze kutoa huduma za afya kwa wananchi wengi zaidi. Aidha, mkakati wa makusudi uchukuliwe kuboresha mazingira ya utoaji wa huduma za afya nchini utakaofanya upungufu wa vifaa, vifaa tiba na vitendanishi kuwa historia.

Mheshimiwa Naibu Spika, saba, utolewaji wa huduma za afya ya mama na mtoto. Maeneo hasa ya vijijini yanakabiliwa na changamoto nyingi zikiwemo za ukosefu wa usafiri, ukosefu wa umeme, upungufu wa watumishi na mazingira duni ya utolewaji wa huduma za afya. Hali inayosababisha kuendelea kuwepo kwa vifo vinavyotokana na uzazi. Kamati inasisitiza kwamba juhudi za makusudi zichukuliwe kupunguza vifo vya mama na mtoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, nane, Bohari Kuu ya Dawa (*Medical Stores Department*) ina jukumu la kununua, kuhifadhi na kusambaza dawa, vifaa tiba na vitendanishi katika Hospitali na Vituo vya Afya vya Serikali nchini. Uzoefu unaonesha kuwa kuna tatizo kubwa la huduma za *MSD* kutofika katika vituo vya afya kwa wakati, dawa kuhamishiwa kwenye maduka

binafsi ya dawa, hali inayosababisha ukosefu wa huduma ya dawa katika vituo vya afya nchini. Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

(i) Serikali ifanye uchambuzi yakinifu ili kutathimini mfumo mzima wa mnyororo wa ugavi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi utakaokidhi mahitaji ya nchi;

(ii) Serikali ifanye maboresho ya kimfumo na kiutendaji katika Taasisi ya *MSD*;

(iii) Kiundwe chombo maalumu kinachojitegemea cha kusambaza dawa, vifaa tiba na vitendanishi kutoka *MSD* mpaka kwenye vituo vya afya nchini. *MSD* ibaki kuwa na jukumu la ununuzi na uhifadhi dawa, vifaa tiba na vitendanishi;

(iv) Kamati za Afya za Wilaya na Kamati za mapokezi za hospitali ziimarishwe na zihusishwe katika kupokea na kuhifadhi dawa, vifaa tiba na vitendanishi katika vituo vyao vya afya;

(v) Serikali ifanye tathimini ya mahitaji halisi (*Forecasting and Quantification*) ya dawa, vifaa tiba na vitendanishi vinavyohiyajika nchini. Aidha, elimu ya kukadiria mahitaji ya dawa itolewe kwa wahusika; na

(vi) Halmashauri zihimizwe kupeleka mahitaji ya dawa, vifaa tiba na vitendanishi *MSD* mapema iwezekanavyo ili kutoa muda wa kutosha wa ununuzi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, tisa, uwepo wa idadi kubwa ya dawa na vitendanishi ambavyo muda wa matumizi yake umepita. Taarifa mbalimbali zikiwemo za Ukaguzi zinaonesha kwamba kumekuwepo idadi kubwa ya dawa na vitendanishi ambavyo muda wa matumizi yake umepita katika Bohari Kuu ya Dawa (*MSD*). Mfano Mwezi Aprili 2012, *MSD* iliiuzia Hospitali ya Taifa Muhimbili, "*cotton wool swab"* zilizotengenezwa mwezi Julai 2007 na kuisha muda wa matumizi yake mwezi Juni 2010. Kamati imebaini kwamba pamoja na mambo mengine, kwa sehemu kubwa uzembe katika mchakato wa manunuzi ya vifaa hivyo umechangia kwa kiasi kikubwa uwepo wa hali hii. Kamati inashauri ifuatavyo:-

(i) Hatua za kinidhamu zichukuliwe kwa watendaji watakaobainika kusababisha jambo hili;

(ii) Ni vyema *MSD* kuwa na '*Bonded Warehouse'* ili kulinda ubora na kuwezesha kukamilisha mchakato wa utoaji dawa, vifaa tiba na vitendanishi Bandarini;

(iii) Serikali iboreshe mfumo mzima wa kuhifadhi dawa ukilenga katika utambuzi wa muda wa matumizi ya dawa mbalimbali zilizopo katika maghala ya Bohari; na

(iv) Serikali iangalie muundo wa *MSD* kiutendaji ili kurahisisha utoaji wa huduma. Aidha, watumishi wenye utaalamu katika fani ya dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi waajiriwe na watumike katika kutoa huduma yenye tija kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumi, kuwezesha viwanda vya ndani kutengeneza dawa, vifa tiba na vitendanishi. Kwa maelezo ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, asilimia 80 ya dawa, vifaa tiba na vitendanishi zitolewazo na *MSD* huagizwa kutoka nje ya nchi. Kwa kurejea katika mgogoro wa madai ya Madaktari dhidi ya Serikali wa mwezi Januari 2012, kumekuwepo na upungufu mkubwa ukiwemo wa vifaa tiba na vitendanishi; zikiwemo "*gloves*" na "*gauze".* Kamati inashauri kwamba ni vyema Serikali kufanya mapitio ya Sera ya Viwanda vya Ndani ili kuvipa uwezo ikiwemo kutengeneza mazingira rafiki yanayovutia uwekezaji na ukuaji wa viwanda hivyo. Hatua hii itaviwezesha viwanda hivyo kutengeneza dawa, vifaa tiba na vitendanishi vinavyotumia teknolojia nyepesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumi na moja, fedha za uchangiaji wa huduma ya afya katika ngazi ya Halmashauri nchini. Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya *(NHIF),* Mifuko ya Afya ya Jamii *(CHF)*, Tele kwa Tele na Papo kwa Papo huchangia utoaji wa huduma za afya katika ngazi ya Halmashauri nchini. Kamati imebaini kwamba makusanyo ya fedha za uchangiaji hayapewi nguvu ya kutosha, taarifa za takwimu za fedha hizi hazipo wazi kwa wadau na matumizi ya fedha yake kutozingatia sheria, kanuni na taratibu zilizokusudiwa. Kamati inashauri ifuatavyo:-

(i) Sheria, Kanuni, miongozo na taratibu za matumizi ya fedha hizi katika kutoa huduma ya afya nchini zizingatiwe. Asilimia 67 ya makusanyo ya Fedha za uchangiaji *(NHIF, CHF* na Papo kwa Papo) zitumike katika ununuzi wa dawa na vifaa tiba;

(ii) Serikali ifikirie kupeleka sehemu ya makusanyo ya fedha za uchangiaji moja kwa moja *MSD* kwa ajili ya ununuzi wa dawa. Hatua hii itaongeza ufanisi katika upatikanaji wa dawa nchini;

(iii) Sera ya uchangiaji huduma za afya nchini iangaliwe upya, kutoa nafasi kwa wenye uwezo kuchangia utolewaji wa huduma za afya nchini. Hatua hii itasaidia kuongeza mapato yatakayoboresha utolewaji wa huduma za afya;

(iv) Serikali iboreshe utolewaji wa huduma za afya katika Zahanati na Vituo vya Afya hasa katika maeneo ya vijijini ili kuhamasisha wananchi kujiunga na mifuko ya uchangiaji huduma za afya nchini; na

(v) Serikali ihakikishe kwamba taarifa za fedha za uchangiaji huduma za afya nchini zinaonekana katika vitabu vya Serikali katika kila mwaka wa fedha ikiwemo kufanyiwa ukaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumi na mbili, Idara ya Ustawi wa Jamii ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, ni muhimu sana kwani inahudumia idadi kubwa ya wananchi wanaoishi katika mazingira magumu ikiwemo wazee, walemavu na yatima. Idara hii inaonekana kama imesahaulika kwani wateja wake wanakabiliwa na changamoto nyingi ikiwemo huduma ya chakula, mavazi, malazi na matibabu. Hivyo Kamati inashauri ifuatavyo:-

(i) Serikali itoe maelekezo mahsusi ya kuhakikisha kwamba huduma ya chakula, malazi, mavazi,

matibabu na usalama zinawafikia walengwa kwa wakati. Aidha, suala la matibabu kwa wazee nchini litafutiwe utaratibu maalumu wa utekelezaji wake mapema iwezekanavyo;

(ii) Serikali ihakikishe kuwa ukarabati wa miundombinu ya vituo vya ustawi wa jamii ikiwemo makazi ya wazee nchini, vituo vya watoto yatima, walemavu na mahabusu ya watoto, unatekelezwa mapema iwezekanavyo;

(iii) Ili kufanikisha utendaji kazi wa Sheria ya Watu Wenye Ulemavu ya Mwaka 2010, ni vyema kanuni na taratibu za utekelezaji wa Sheria hii zikamilike na kutumika mapema iwezekanavyo. Aidha, Baraza la Taifa la Utendaji liundwe mapema iwezekanavyo kufuatilia utekelezaji wa masuala mbalimbali yanayohusu Watu Wenye Ulemavu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumi na tatu, Serikali itoe maelezo mahususi kuhusu matumizi ya fedha za Mfuko wa Pamoja wa Sekta ya Afya (*Health Basket Funds)* ili zitumike kwa matumizi yaliyo kusudiwa ikiwemo ununuzi wa dawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumi na nne, msongamano wa wagonjwa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili. Vituo vya Afya na Zahanati zilizoko Dar es Salaam zifanye kazi kwa muda wa ziada kupunguza msongamano wa wagonjwa katika Hospitali za Manispaa zikiwemo Hospitali za Amana, Temeke na Mwananyamala. Hatua hii itazipa nafasi Hospitali za

Manispaa kupunguza msongamano wa wagonjwa katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumi na tano, gharama kubwa ya matibabu ya magonjwa ya moyo nje ya nchi. Kamati inashauri Serikali itoe fedha za kutosha kuwezesha Taasisi ya Moyo iliyojengwa kwa ufadhili wa Serikali ya China iweze kuanza kazi mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumi na sita, Serikali iandae utaratibu maalumu wa kupunguza gharama za matibabu ya Saratani kwa wagonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumi na saba, elimu itolewe kuhusu uchimbaji wa madini ya *uranium* ili kujikinga na madhara yatokanayo na uchimbaji huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumi na nane, hatua za makusudi za kupima na kuthibitisha ubora wa dawa (*quality assuarance and quality control)* zichukuliwe ili kudhibiti dawa na vipodozi vilivyo chini ya kiwango. Aidha, njia zisizo rasmi za kuingiza dawa au vipodozi visivyo na viwango zidhibitiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumi na tisa, Taasisi ya Ustawi wa Jamii, Dar es Salaam. Pamoja na maelezo ya Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii kuhusu hatua ya Serikali katika kushughulikia mgogoro uliojitokeza katika Taasisi hii mwezi Augusti 2011, Kamati inasisitiza kwamba Serikali ichukue hatua za haraka kupata Viongozi wa Juu wa Taasisi wenye sifa na vigezo vinavyotambulika na *NACTE*. Aidha, suala la

Wakufunzi waliosimamishwa ajira zao litafutiwe ufumbuzi mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho, Kamati inawashukuru Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Mheshimiwa Dkt. Hussein Hassan Mwinyi, Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Mheshimiwa Dkt. Seif Suleiman Rashid na Watendaji wote wa Wizara wakiongozwa na Kaimu Katibu Mkuu Ndugu Regina L. Kikuli kwa kushirikiana na Kamati kwa wakati kila inapohitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, nawashukuru wajumbe wenzangu wa Kamati kwa ushirikiano na umakini katika kushauri na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Kwa heshima, naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Margeret Simwanza Sitta, Mwenyekiti na Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile, Makamu Mwenyekiti. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Dkt. Maua A. Daftari, Mheshimiwa Agripina Z. Buyogera, Mheshimiwa Pauline P. Gekul, Mheshimiwa Desderius J. Mipata, Mheshimiwa Dkt. Kebwe S. Kebwe, Mheshimiwa Lameck O. Airo, Mheshimiwa Dkt. Antony G. Mbassa, Mheshimiwa Zarina S. Madabida, Mheshimiwa Ali J. Haji, Mheshimiwa Anna MaryStella J. Mallac, Mheshimiwa Martha J. Mlata, Mheshimiwa Salome D. Mwambu, Mheshimiwa Highness S. Kiwia, Mheshimiwa Mch. Luckson N. Mwanjale, Mheshimiwa Clara D. Mwatuka,

Mheshimiwa Dkt. Hamisi A. Kigwangala, Mheshimiwa Nyambari C. Nyangwine, Mheshimiwa Rashidi A. Omari, Mheshimiwa Said S. Suleimani, Mheshimiwa Stephan H. Ngonyani, Mheshimiwa Saidi R. Bwanamdogo, Mheshimiwa Albert O. Ntabaliba na Mheshimiwa Faki H. Makame. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee tunakushukuru wewe binafsi na Mheshimiwa Spika na Wenyekiti wa Bunge kwa kushirikiana na Kamati yetu wakati wote. Aidha, tunamshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas D. Kashililah, Katibu wa Kamati hii Ndugu Stella Mlambo na Ndugu Happiness Ndalu kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi taarifa hii kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge hili likubali kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Fungu 52 kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja muda mfupi uliopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Msemaji wa Kamati za Huduma za Jamii, Mheshimiwa Dkt. Kebwe Stephen Kebwe kwa kusoma vizuri sana mawasilisho na maoni ya Kamati. Sasa naomba nimwite Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA (K.n.y. MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA) - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI, WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani juu ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Napenda niseme kwamba taarifa yangu ni ndefu lakini, nasoma ufupisho kwa hiyo naomba iinginzwe yote kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe salamu za rambirambi kwako wewe, Wabunge pamoja na Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuondokewa na ndugu yetu Peter Mazengo katika ajali iliyotokea usiku wa kuamkia leo. Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi na aipe familia yake roho ya ustahimilivu katika kipindi hiki kigumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na kuweza kusimama hapa mbele yenu hivi sasa na kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusiana na bajeti ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa mwaka wa fedha 2012/2013, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge Kanuni ya 99(7), Toleo la mwaka 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nawashukuru viongozi wangu wa CHADEMA, Wilaya ya Biharamulo, Mkoa wa Kagera na Taifa kwa ujumla. Pia Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Mbowe (Mb), pamoja na Kamati nzima ya Uongozi ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwa kazi kubwa

ya kuhakikisha kuwa Kambi inafanya kazi kwa matarajio ya Watanzania wote. Pia nawashukuru wote waliotoa mchango wao katika maandalizi ya hotuba hii muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, niwashukuru wananchi wa Jimbo la Biharamulo Magharibi kwa imani yao kubwa kwangu wakati wa kipindi chote tulichokuwa tunakabiliwa na kesi ya uchaguzi na hatimaye tukashinda kama hukumu ilivyotolewa. Nasema ahsanteni sana na ninawaahidi kuwa tutaendelea kushirikiana kama ambavyo tumekuwa tukifanya kazi kwa kipindi chote kabla na baada ya kuwa mwakilishi wenu Bungeni. Pia naishukuru familia yangu kwa ushirikiano wote nilioupata kipindi chote ninapokuwa nje ya familia nikitimiza majukumu yangu ya Kichama na Kibunge; naomba iendelee kunivumilia kwani ni familia iliyokubali mimi kuchukua jukumu la kuwawakilisha wananchi wa Biharamulo Magharibi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, lakini kwa umuhimu mkubwa, niwapongeze na kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Huduma za Jamii kwa kazi kubwa ya kuhakikisha sekta ya afya inaleta tija kwa jamii pamoja na changamoto inazokumbana nazo. Naamini tutafika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatma ya afya na uhai wa Taifa. Kambi Rasmi ya Upinzani na Watanzania walio wengi tunasononeshwa sana na hali ya migogoro ya mara kwa mara inayoendelea kati ya Serikali na wafanyakazi wa afya hapa nchini. Migogoro

hii imepelekea kuyumba kwa utoaji na upatikanaji wa huduma za afya, hasa zile za rufaa. Pamoja na Mahakama kutumika kuzima haki ya watumishi kudai haki zao, pamoja na kuzuia mjadala wa kadhia hii Bungeni, Kambi Rasmi ya Upinzani inalitaka Bunge kuingilia kati mgogoro huu kwa manufaa ya wananchi. Haikukusudiwa kwame dhana ya uhuru na mamlaka ya Mahakama kutumika kukandamiza haki za wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa kipengele cha 85 (a) (i), cha Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2010 -2015, imeahidi Watanzania upatikanaji wa rasilimali watu wenye ujuzi na wa kutosha katika sekta ya afya. Pamoja na jitihada za kupanua udahili katika vyuo vya elimu vya afya na kuongeza ajira kwa wahitimu ila ukweli ni kuwa Serikali ya CCM imeenda kinyume kabisa kwani sasa inawafukuza wafanyakazi na kuwafutia leseni Madaktari wetu. Wafanyakazi wa afya wanahitaji kutiwa moyo na hamasa ikiwa ni pamoja na kupatiwa vitendea kazi ili waweze kufanya kazi zao kwa mujibu wa viapo vyao na sio kutekwa, kupigwa, kudhalilishwa na kukejeliwa kama ambavyo inafanyika sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upatikanaji wa vifaa tiba na vitendanishi, haiingii akilini kumlazimisha mtu atoe huduma bila vitendea kazi vya msingi. Ni sawa na Bunge hili kutarajiwa kutekeleza majukumu yake bila vifaa vya kazi. Nitaongelea upatikanaji wa vifaa baadaye katika hotuba hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo cha kuwadharau, kuwadanganya Madaktari na hatimaye kuwafutia leseni Madaktari 319 wa mafunzo kwa vitendo ni kujikanganya kwa Serikali. Ni uamuzi unaonekana umechukuliwa kwa kukomoa na kwa ubabe bila kujali maslahi ya Taifa na afya za wananchi. Mgogoro mzima unaashiria uwezo finyu wa Serikali kutatua migogoro kwa njia ya majadiliano na ukosefu wa dhima ya kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM. Ikumbukwe kwamba hivi sasa kuna mgomo baridi katika hospitali nyingi za rufaa unaotokana na kukandamiza uhuru wa wafanyakazi wa afya kudai haki zao na vitendea kazi ili waweze kutimiza viapo vyao.

Mheshimiwa Naibu Spika, maamuzi ya kisiasa na hatma ya sekta ya afya Tanzania. Ni kweli kwamba uratibu wa masuala ya afya hapa nchini unategemea sana utashi wa kisiasa na taratibu mbalimbali za namna nchi inavyoendeshwa. Hii ni kwa sababu sera ya afya, kwa mfano, inatokana na utekelezaji Ilani ya Uchaguzi ya CCM na kwa maana hiyo ni mchakato wa kisiasa. Hali kadhalika, uongozi wa juu wa Wizara unatokana na uamuzi wa kisiasa na hata bajeti ya Wizara inapitishwa kwa mchakato wa kisiasa pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inatambua kwamba kuna changamoto nyingi katika uongozi wa namna yoyote ile. Hata hivyo, nyakati za changamoto ndipo busara na ukomavu wa uongozi unapochukua nafasi yake ili kuweka mazingira katika hali shwari pasipo upande mmoja kuumizwa kwa kuonewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inasikitishwa na kitendo cha Serikali kushindwa kutumia busara katika kutafuta ufumbuzi wa madai ya vitendeakazi na stahili za Madaktari jambo ambalo lilisababisha migomo ya Madaktari hapa nchini. Migomo ya Madaktari hatimaye ilisababisha adha kubwa katika utoaji wa huduma ya afya hapa nchini lakini mbaya zaidi ni kwamba baadhi ya wagonjwa walipoteza maisha kwa kukosa huduma ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na migomo ya Madaktari, ni tukio la kutekwa na kupigwa hadi kukaribia kufa kwa aliyekuwa kiongozi wa Jumuiya ya Madaktari Dkt. Ulimboka Steven na kutelekezwa katika Msitu wa Pande uliopo nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Dkt. Ulimboka alitekwa na kufanyiwa unyama wakati mgogoro baina ya Serikali na Madaktari unaendelea, kuna ushahidi ambao umekuwa ukitolewa na vyombo vya habari hususan Gazeti la Mwanahalisi kuwa Watendaji wa Serikali wanahusika na tukio hilo. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe majibu Bungeni kuhusu kutajwa kwa watendaji wake na sababu za watendaji hao kutokukamatwa na kuhojiwa na vyombo vya dola mpaka hivi sasa. Aidha, kwa kuwa Serikali imetuhumiwa kuhusika, Kambi Rasmi ya Upinzani inasisitiza haja ya kuundwa kwa Tume Huru kufanya uchunguzi kuhusu tukio husika. Taarifa iliyotolewa na Polisi kuhusu kukamatwa na kufikishwa Mahakamani kwa raia wa Kenya haipaswi kutumika kama kisingizio cha kuzuia mjadala na haiwezi kuwa kizuizi cha

uchunguzi huru kuendelea kufanyika. Kama Bunge ambalo ndio chombo cha uwakilishi cha wananchi na mtetezi mkuu wa wananchi likiwekewa pingamizi za kikanuni kutojadili matatizo ya wananchi hasa ya kiafya ni nani sasa atawasemea wananchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mwongozo wake wa tarehe 3 Februari, 2012, Naibu Naibu Spika baada ya kuombwa na baadhi ya Wabunge kwa nyakati mbalimbali kuwa suala mgogoro kati ya Serikali na Madaktari lijadiliwe Bungeni alielekeza:-

*"Lakini jambo hili lina unyeti wa kipekee; na unyeti wake unatokana na kwamba ni jambo linalohusu mgogoro, kama alivyosema Mheshimiwa Waziri wa Afya, ni mgogoro wa pande mbili na sisi hapa ...tumepata maelezo ya upande mmoja. ...uwe katika nafasi ambayo wenzetu wanasema uko-informed sawasawa. Mimi ninaamua ifuatavyo; kulipeleka suala hili kwenye Kamati ya Huduma za Jamii ...ili Kamati hiyo ikae na Serikali, ikae na upande wa Madaktari bila kubagua, ikutane na Jumuiya ya Madaktari, ikutane na Chama cha Madaktari, ikutane na Madaktari Bingwa au wadau wengine itakaoyoona yenyewe Kamati wanafaa katika suala hili; kwa haraka iwezekanavyo Kamati hii ifanye kazi hii. Kamati hii itakapokuwa tayari, mimi naamini tunaweza tukafika mahali ambapo tunaweza tukaona namna ya kusonga mbele kwa jambo hili".*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka maelezo yatolewe Bungeni, ni namna gani ya

kusonga mbele iliyoamuliwa kutokana na kazi hiyo iliyofanywa na Kamati kwa kipindi chote.

Mheshimiwa Naibu Spika, izingatiwe kwamba baadhi ya Wabunge walipoomba kwamba Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii iwasilishwe na kujadiliwa Bunge uamuzi wa Naibu Naibu Spika Bungeni tarehe 27 June, 2012 ulikuwa:-

*"Kuhusu Kamati ya Huduma za Jamii, ilishalishughulikia jambo hili hili na ikatuletea taarifa hapa. Sasa Kamati irudi kufanya nini?"*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo wa Kiti unasema kuwa taarifa ilikwishaletwa hapa Bungeni, lakini kwa masikitiko makubwa ni kwamba taarifa hiyo haijawahi kuletwa hapa Bungeni kwa njia yoyote ile na hivyo jambo hili lilikuwa ni siri wakati Waheshimiwa Wabunge waliomba Mwongozo wa Kiti ili Bunge lipewe nafasi ya kuishauri na kuisimamia Serikali kuhusu mgogoro huo.

Kambi Rasmi ya Upinzani inasikitika kuwa suala hili la Madaktari, Kiti ndicho kimepelekea kufikia hatua iliyofikiwa ya Madaktari wetu hadi kufutiwa leseni, kwani kama Kiti kingetoa fursa kwa Bunge kujadili na mwisho kutoa ushauri au Maazimio kwa Serikali jambo ambalo ndio wajibu wetu kwa mujibu wa Katiba, Ibara ya 63 mgogoro huo usingeendelea kudumu kwa mrefu na kuleta athari zaidi katika sekta ya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni zinazolizuia Bunge kujadili masuala ya wananchi kwa kisingizio

kuwa masuala hayo yako Mahakamani, zinadumaza demokrasia ya nchi yetu, zinalipora Bunge haki yake ya Kikatiba ya kuisimamia Serikali na zinawakandamiza wananchi wanyonge ambao hawana pa kusemea isipokuwa kupitia Bunge lao.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Wabunge wanazuiliwa kuzungumzia suala la mgomo wa Madaktari kuwa jambo hilo lipo Mahakamani, Rais Jakaya Kikwete alipokuwa akilihutubia Taifa tarehe 1 Julai, 2012 alizungumzia suala la migomo ya Madaktari na kutoa maagizo mbalimbali. Kambi ya Upinzani inataka kujua kama kitendo cha Baraza la Madaktari Tanganyika kusitisha usajili kwa Madaktari 319 kuanzia tarehe 11 Julai, 2012, ni sahihi wakati Madaktari haohao walikuwa wameshtakiwa Mahakamani kwa shauri hilohilo la mgomo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kwamba Bunge liazimie kuwa Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma za Jamii iliyoshughulikia mgogoro kati ya Serikali na Madaktari iwasilishwe Bungeni na kujadiliwa kabla ya kupitishwa kwa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa mwaka wa fedha 2012/2013 ili maoni na mapendekezo ya Kamati husika yaweze kuzingatiwa katika bajeti. Hatua hiyo italiwezesha pia Bunge kupitisha Maazimio yenye kulenga kuishauri na kuisimamia Serikali kushughulikia vyanzo vya migogoro katika sekta ya afya nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, madai ya Madaktari na mdororo wa huduma za afya nchini. Sekta ya afya imekumbwa na mdororo wa huduma za afya ambao umeshika kasi zaidi hasa kwa mwaka jana na mwaka huu. Kuzorota kwa sekta hii ya afya kunatokana na upungufu mkubwa wa vitendea kazi kwa Madaktari, jambo ambalo linawafanya Madaktari washindwe kufanya kazi zao kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inasikitishwa na kitendo cha Serikali kuwachonganisha Madaktari na wananchi kwa kutoa taarifa kwa umma kwamba Madaktari hawawatakii mema wananchi kwa kuwa madai yao yalikuwa ni ya mishahara na posho tu badala ya kueleza pia suala la vitendeakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Jumuiya ya Madaktari ni kwamba pamoja stahili zao, madai yao mengine yalikuwa ni vitendea kazi duni ambavyo vinafanya utendaji wao kuwa mgumu. Nanukuu sehemu ya madai yao waliyoiandikia Serikali:-

*"Uboreshaji wa huduma za afya wakati viongozi wakikimbizana kwenda nchini India kwa matibabu, kumekuwa na hali ya kuzorota kwa huduma za afya katika kiwango ambacho hakivumiliki tena, na hali hii kwa kiwango kikubwa inasababishwa na ukosefu wa vifaa tiba, madawa na wataalamu wa afya katika hospitali zetu, mfano ni katika hospitali za Manispaa ya Temeke, Mwananyamala na Amana ambapo wagonjwa wanalazimika kujinunulia vifaa tiba na dawa kwa gharama kubwa licha ya wagonjwa kuchangia katika Mfuko wa Matibabu ya Kijamii.*

*Wakati huohuo, ni kitendo cha aibu na fedheha katika karne hii kwa wagonjwa kulala chini hasa katika Hospitali ya Rufaa kama Muhimbili na kwingineko. Hali hii licha ya kuwa kero kwa wagonjwa na ndugu zao lakini pia inajenga mazingira magumu kwa watumishi wa afya".* Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani tunahoji, huku ndiko kutekeleza Ilani?

Mheshimiwa Naibu Spika, dhamira hasi ya Serikali kwenye sekta ya afya. Dhamira ya Serikali kwenye sekta ya afya haina matokeo mazuri hata kidogo kwani haitilii maanani wala haitoi kipaumbele kwenye kuhakikisha kuwa wananchi wanapata huduma stahiki za kiafya na hili linathibitishwa na taarifa mbalimbali za Serikali pamoja na kiasi cha bajeti ambacho kinatengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuonyesha kuwa Serikali haijali afya ya wananchi wake, ni zaidi ya miaka kumi sasa tokea kutiwa saini kwa Azimio la Abuja linalozitaka Serikali ikiwemo ya Tanzania kutenga angalau asilimia 15 ya bajeti ya Serikali kwenye sekta ya afya. Kambi Rasmi ya Upinzani inasikitika kuona kwamba kwa kipindi chote hiki bado Serikali yetu haijaweza kufikia lengo hili, pamoja na kwamba Mpango Mkakati wa Tatu wa Sekta ya Afya *(Health Sector Strategic Plan III)* unahimiza umuhimu wa Serikali kufikia lengo la Abuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Sera ya Afya ya Taifa ikitamka kwamba Serikali itakuwa mfadhili mkuu wa sekta ya afya, mwelekeo wa sasa unaendelea

kukinzana na sera hii. Kwa mfano, kwa zaidi ya miaka mitano sasa bajeti ya maendeleo ya Wizara ya Afya imetegemea wafadhili wa nje kwa zaidi ya asilimia 90. Wakati huohuo, bajeti nzima ya Wizara ya Afya hutegemea wafadhili kwa zaidi ya asilimia 50. Mfano, bajeti ya mwaka huu wa fedha wa 2012/2013 ya Wizara ya Afya inategemea wafadhili kwa asilimia 46. Hali hii ya utegemezi ni kielelezo kwamba Serikali inakwepa majukumu yake ya msingi ya kutoa huduma kwa wananchi na kuyakabidhi kwa wafadhili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ripoti ya Hali ya Afya nchini 2011 iliyotolewa na Wizara ya Afya inaonyesha kuwa kila mwananchi anatumia jumla ya dola za Kimarekani 10.55 *(real per capital)* kwa ajili ya huduma za afya kwa mwaka. Mpango Mkakati wa sekta ya afya uliweka lengo la dola za Kimarekani 17.92 kwa kila mwananchi kwa ajili ya huduma za afya kwa mwananchi ifikapo mwaka 2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo tu kwamba tumeshindwa kufikia lengo bali tuko nyuma sana ya kiwango kilichopendekezwa na Shirika la Afya Duniani cha dola za Kimarekani 54 kwa kila mtu. Hali hii inatokana na sababu nyingi ikiwemo umaskini wa kipato wa wananchi wetu lakini kubwa zaidi ni bajeti finyu ya Serikali katika sekta ya afya, inayopungua mwaka hadi mwaka huku mahitaji na changamoto zikiongezeka mwaka hadi mwaka. Mfano mwaka 2010/2011 ilikuwa ni asilimia 10 ya bajeti ya Serikali lakini mwaka 2011/2012 ni asilimia 8.9 tu ya bajeti ya Serikali iliyoelekezwa katika sekta ya afya na mwaka huu wa fedha ni asilimia 8.3 ya bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi uliofanywa na Sikika, Shirika lisilo la Kiserikali uliochapishwa mwaka 2011, unaendelea kuthibitisha kuwa Serikali haiipi afya kipaumbele chochote. Haiingii akilini kwamba Serikali ya Tanzania ina mashine moja tu ya *"CT scan"* ambayo inapatikana katika hospitali ya Taifa ya Muhimbili. Hata hivyo, mashine hii ni mbovu tangu mwishoni mwa mwaka jana. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasikitishwa sana na kiwango cha kutojali afya za wananchi kinachofanywa na Serikali kwani wagonjwa wengi hawawezi kumudu gharama za huduma ya *"CT scan"* katika hospitali za binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na matatizo ya mashine hiyo ya *CT Scan*, kuna tatizo la mashine nyingine mbalimbali katika hospitali nyingi za Serikali hapa nchini. Ni jambo la kawaida kukuta mashine ya *X-ray* haifanyi kazi kwa sababu tofautitofauti zikiwemo kukosa filamu au uharibifu wa kawaida. Kinachopelekea tatizo hili kwa kiasi kikubwa ni utawala dhaifu katika hospitali zetu mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya madawa na vifaa tiba. Katika vituo vya huduma za afya vya Serikali, kumekuwa na tatizo sugu la upatikanaji wa dawa na vifaa tiba. Hali hii kwa kiasi kikubwa inatokana na Serikali kutotenga fedha za kutosha kwa ajili ya ununuzi wa dawa na matatizo ya utendaji katika taasisi mbalimbali zilizopewa jukumu la kuratibu mfumo wa manunuzi na usambazaji wa dawa na vifaa tiba ambayo yanapelekea hata hizi rasilimali ndogo zilizotengwa zisitumike ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2011 kulikuwa na upungufu mkubwa wa kifaa tiba muhimu kiitwacho shashi au gozi katika vituo karibia vyote vya huduma za afya nchini. Kifaa tiba hiki hutumiwa kuzuia kuvuja kwa damu kwenye vidonda na kwenye huduma za wazazi wanapojifungua. Utafiti uliofanywa kipindi hicho ulibaini kwamba asilimia 48 ya Wilaya 71 zilizofanyiwa utafiti hazikuwa na kifaa tiba hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, malaria ni ugonjwa unaosababisha vifo vingi hasa miongoni mwa watoto wadogo na kwa mujibu wa taarifa za utafiti za Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Ugonjwa wa Malaria Nchini *(NMCP)* inakadiriwa kuwa, kwa Tanzania bara pekee kuna idadi ya vifo kati ya 60,000 hadi 80,000 vinavyosababishwa na ugonjwa wa malaria kwa mwaka. Hata hivyo utafiti ulibaini, katika mwezi wa tano mwaka huu (2012) asilimia 37% ya vituo vyote vya afya vya Serikali havikuwa na aina hata moja (kati ya nne) ya dawa muhimu ya mseto ya Malaria –ALU, ilhali Bohari Kuu ya Dawa ilikuwa na kiasi kikubwa cha dawa hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Taarifa za Shirika la Afya la Dunia, Tanzania ni moja ya nchi zenye idadi ndogo ya vitanda vya wagonjwa ukilinganisha na idadi ya watu. Wastani wa dunia ni vitanda 30 kwa watu 10,000, ilhali Tanzania ina vitanda saba (7) tu kwa watu 10,000. Hali hii imesababisha adha kwa wagonjwa hasa kina mama na watoto kwa kulala zaidi ya mmoja kwenye kitanda au wengine kulazimika kulala chini kwenye wodi zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mipango ya fedha kwa ajili ya madawa na vifaa tiba bado haijaimarika. Kwa mwaka 2012/2013, kiasi cha shilingi bilioni 80.5 zimetengwa katika Wizara ya Afya kwa ajili ya manunuzi ya madawa na vifaa tiba ikiwa ni sawa na asilimia 40 tu ya mahitaji. Kama ilivyoainishwa na wataalamu Wizarani na *MSD*, mahitaji halisi yalikua shilingi bilioni 198. Vilevile fedha hizi kwa kiasi kikubwa zinategemea fedha za wahisani kwani fedha za ndani ni shilingi bilioni 34 na zile za nje ni shilingi bilioni 46.5.

Mhesimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kupendekeza yafuatayo:-

(i) Kupunguza utegemezi kutoka kwa wafadhili hasa kwenye ununuzi wa madawa na vifaa tiba muhimu, kama vile madawa ya tiba ya malaria, VVU na UKIMWI.

(ii) Kupunguza utegemezi kutoka kwa wasambazaji wa madawa wanne waliothibitishwa na Shirika la Afya Duniani na kutafuta watengenezaji na wasambazaji wengine ili kuongeza usambazaji kukidhi mahitaji ambayo yamekuwa hayafikiwi ya madawa na vifaa tiba muhimu.

(iii) Serikali iongeze kiasi cha fedha za ununuzi wa madawa kulingana na kiasi cha shilingi bilioni 198 kama ilivyokadiriwa na kuombwa na *MSD* ili kuweza kuondoa upungufu wa dawa kwenye hospitali zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahadi ya Rais kuhusu Huduma za Uzazi wa Mpango, London Uingereza.

Mpango wa Taifa wa Serikali wa Kupunguza Vifo vya Mama Wajawazito na Watoto (2008 -2015), umeeleza bayana kuwa huduma za uzazi wa mpango zinaweza kupunguza vifo vya mama wajawazito kwa zaidi ya asilimia 35, iwapo zitapatikana kwa ukamilifu. Mbali na mpango huo, mnamo tarehe 11 Julai mwaka huu, Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete akiwa katika mkutano wa Masuala ya Uzazi wa Mpango mjini London nchini Uingereza, alinukuliwa na vyombo mbalimbali vya kimataifa, likiwemo gazeti la "*The Guardian*" la hapa nchini, akitoa ahadi mbele ya Wakuu wa nchi mbalimbali duniani, kwamba Serikali ya Tanzania itahakikisha inaongeza upatikanaji na matumizi ya huduma za uzazi wa mpango kwa mara mbili zaidi ifikapo mwaka 2015, kutoka asilimia 27 ya sasa ili kuongeza kasi ya kupunguza vifo vya mama wajawazito na watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Rais akiwa ametoa ahadi hiyo, tathimini iliyofanywa na Kambi Rasmi ya Upinzani inaonyesha kuwa mwaka 2010/2011, Serikali ilichangia asilimia 17 tu ya fedha zote zilizohitajika kwa ajili ya huduma za uzazi wa mpango. Mwaka jana 2011/2012, Serikali ilitenga kutoka kwenye fedha za ndani shilingi bilioni 1.2 kwa ajili ya huduma za uzazi wa mpango, lakini cha kushangaza hadi kufikia mwisho wa mwaka wa fedha Julai mwaka huu, hakuna kiasi chochote kilichotolewa kwa ajili ya kugharamia huduma hizi, zaidi ya kutegemea fedha za wafadhili ambazo huwa hazitoshi na hazitolewi kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali ijieleze imejipanga vipi kuhakikisha huduma za uzazi wa mpango zinaongezewa pesa ili kutimiza ahadi hii ya Rais? Ni vema ikazingatiwa kuwa kutopewa kipaumbele cha bajeti kwa eneo hili sio tu kutamdhalilisha Rais wa nchi, lakini pia kutakwamisha jitihada za kupunguza vifo vya mama wajawazito na watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo wa dhamana ya ahadi katika ununuzi wa dawa. Utafiti uliofanywa na Shirika la Kimataifa la Idadi ya Watu Duniani kwa Kushirikiana na Chuo Kikuu cha Mzumbe - Mkoani Morogoro, utafiti uliofanyika mwaka 2011, unaonyesha kuwa mara kwa mara kumekuwa na uhaba mkubwa wa dawa yanayohusiana na afya ya mama na mtoto, kwa sababu fedha za bajeti kwa ajili ya ununuzi wa dawa huchelewa kutolewa na Serikali na zinapotoka mchakato wa ununuzi wa dawa huchukua miezi sita (6) hadi tisa hadi yaingie nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabiliana na tatizo hili, Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kutumia mfumo wa ununuzi wa dawa ujulikanao kama "Mfumo wa Dhamana ya Ahadi" au "*Pledge Guarantee System*". Mfumo huu uliozinduliwa na Umoja wa Mataifa mwaka 2009, utaiwezesha Serikali kuwa na uwezo wa kuagiza dawa kwa wakati mahitaji yanapotokea hata kama fedha zinazotengwa kwenye bajeti ya Wizara ya Afya kwa ajili ya ununuzi wa dawa zitakuwa zinachelewa kutolewa. Tunaitaka Serikali ijifunze hili kupitia *UNFPA Tanzania*.

Mheshimiwa Naibu Spika, rasilimali watu katika Sekta ya Afya. Kwa muda mrefu sasa kumekuwepo upungufu mkubwa sana wa wafanyakazi katika sekta ya afya. Taarifa na takwimu kuhusu rasilimaliwatu zilizotolewa katika mikutano ya kisera ya Wizara zinaoyesha upungufu wa wafanyakazi katika sekta hii wanaofikia 96,468. Upungufu huu wa watumishi wa afya mbali na kuzorotesha ubora wa huduma za afya lakini pia unawanyima wananchi haki yao ya msingi ya kupata huduma bora ya afya. Mwezi Oktoba mwaka jana kwa mfano, wananchi wa Kata ya Chase katika Wilaya ya Kondoa walilazimika kukosa huduma za afya baada ya zahanati yao kufungwa kufuatia kufariki kwa mtumishi wa afya pekee aliyekuwa akihudumia katika zahanati hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ukosefu mkubwa wa watumishi wa afya, bado idadi ya wanafunzi waliodahiliwa katika vyuo vya afya ni ndogo ukilinganisha na mahitaji halisi ya watoa huduma. Mwaka 2010/2011, wanafunzi 6,713 ndio waliweza kupata udahili katika vyuo mbalimbali vya afya. Idadi hii ya wadahiliwa ni ndogo sana kuweza kuziba pengo la watumishi wa afya lililopo nchini. Kwa mwenendo huu wa udahili, itatuchukua nchi zaidi ya miaka kumi na nne kuweza kuziba pengo iwapo idadi ya watu haitaongezeka na wafanyakazi waliopo hawatapungua kwa njia yoyote ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu zinaonyesha kuwa Tanzania inachangia kati ya asilimia tatu mpaka tano ya vifo vya kina mama duniani, ikiwa na idadi ya

vifo 450 kati ya uzazi hai 100,000. Hii ina maana kuwa, kati ya wakinamama 100 wanaofariki duniani kutokana na matatizo ya uzazi, watatu hadi watano ni Watanzania. Moja ya sababu kubwa inayochangia vifo hivi ni upungufu wa wakunga wenye utaalamu wa kutoa huduma stahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utendaji wa sekta ya afya kulingana na taarifa ya mapitio ya hali ya matumizi ya sekta ya Afya *(PER)* ya mwaka 2011, suala la ucheleweshwaji wa mishahara na posho za kujikimu hasa kwa waajiriwa wapya limeendelea kuwa tatizo kwa watumishi wa afya na linawavunja moyo watumishi wa sekta hii. Kambi Rasmi ya Upinzani inauliza ni kwa nini tatizo hili limeendelea kuwa sugu mwaka hadi mwaka na ni mkakati gani mbadala umewekwa na Serikali ili kuondokana na tatizo hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ukosefu wa watumishi wa kutosha kasi ya ajira kulingana na maombi ya vibali vya ajira imekuwa ndogo sana. Kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Serikali ilitoa vibali vya kupeleka watumishi wa afya wapatoa 9,391 katika Halmashauri, Majiji, Manispaa na hata Wizarani. Hadi kufikia mwezi Desemba 2011, Wizara iliweza kupeleka watumishi wa afya wapatao 2,127 tu. Kambi Rasmi ya Upinzani inahitaji maelezo ya Serikali, je, hadi sasa watumishi wangapi wamekwishaajiriwa kati ya vibali hivi vilivyotolewa na kupata mwelekeo wa ajira mpya kwa mwaka 2012/2013.

Mheshimkiwa Naibu Spika, tuhuma za matumizi mabaya ya madaraka katika Taasisi ya Ustawi wa

Jamii na hatma ya Wahadhiri 26 waliofukuzwa. Mwaka jana 2011/2012, Kambi Rasmi ya Upinzani katika hotuba yake iliainisha migogoro iliyokuwa ikiendelea katika Taasisi ya Ustawi wa Jamii iliyopo Dar es Salaam kati ya Menejimenti na Wahadhiri wa Taasisi hiyo. Hata hivyo, Serikali haikuchukua hatua zinazostahili kushughulikia vyanzo vya mgogoro huo hali ambayo imesababisha mgogoro huo kuendelea na sasa kuchukua sura ya tuhuma za ufisadi na matumizi mabaya ya madaraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza ilichobaini ikiwa imefanya uchunguzi kuhusu tuhuma za muda mrefu kuwa Mkurugenzi Utawala na Fedha wa Taasisi ya Ustawi wa Jamii, Bi. Mbonimpaye Mpango hana sifa za cheo hicho kwa kile kinachodaiwa kuwa elimu yake ni ya Shahada ya Uzamili *(Masters Degree*) wakati cheo hicho kinastahili Shahada ya Uzamivu *(Ph.D)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikiwa madai ya kushikilia cheo asichostahili ni sahihi, tafsiri yake ni kuwa mshahara ngazi ya PHTS 19 anaopokea Mkurugenzi huyo ambao ni sawa na mshahara wa Profesa *(Associate Professor)* wakati yeye si mwana taaluma wa kiwango hicho na anatajwa kutokuwa na Shahada ya Uzamivu *(Ph.D)*. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka maelezo kuhusu tuhuma hizo ambazo zina mwelekeo wa matumizi mabaya ya fedha za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkurugenzi huyu analalamikiwa pia kukata mishahara ya wafanyakazi wa taasisi na kutengeneza Hati za Mishahara *(Salary Slips)* ambazo zinaonesha tofauti ya mshahara unatoka

Hazina na ule unaotolewa kwa wafanyakazi wa taasisi bila maelezo ya sababu za makato hayo na fedha hiyo haijulikani inaishia wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, malalamiko mengine ni kutowapandisha vyeo au madaraja watumishi wenye sifa na kuwapandisha wengine wasio na sifa jambo ambalo linaashiria ubaguzi na upendeleo katika uendeshaji wa chuo. Aidha, Mkurugenzi huyu anaingilia utendaji wa Waandamizi wake jambo ambalo linawafanya washindwe kufanya kazi kwa ufanisi. Jambo hili linathibitishwa na barua ya kujiuzulu ya aliyekuwa Mkurugenzi wa Mafunzo ya terehe 22 Desemba 2008, Dkt. Emmanuel James Matiku, kutokana na kuingiliwa majukumu yake na Mkurugenzi wa Fedha na Utawala.

Mheshimiwa Naibu Spika, mgogoro mwingine ni kufukuzwa kazi kwa Wahadhiri 26 wa Taasisi ya Ustawi wa Jamii ambao pamoja na sababu zilizotajwa na uongozi wa taasisi hiyo kwenye vyombo vya habari yapo pia malalamiko kwamba uamuzi wa kuwafukuza ulipata msukumo baada ya Wahadhiri mbalimbali wa taasisi hiyo kuingia katika mgogoro na taasisi hiyo uliombatana na kuhoji masuala mbalimbali kuhusu uendeshaji wa taasisi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kwa kuwa masuala haya tulianza kuyahoji toka mwaka 2011, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii itoe maelezo ya kina katika Bunge hili kuhusu tuhuma hizo na hatua ambazo Serikali imechukua kumaliza mgogoro kati ya uongozi na Wahadhiri katika

Taasisi ya Ustawi wa Jamii. Aidha, Serikali ieleze hatma ya Wahadhiri 26 waliosimamishwa katika taasisi hiyo kwa kuzingatia uhaba wa watalaamu unaolikabili Taifa letu. Pamoja na maelezo yatayotolewa na Serikali, Kambi Rasmi ya Upinzani inatoa mwito kwa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* kufanya Ukaguzi wa Kiufanisi *(Performance Audit)* kuhusu uendeshaji wa Taasisi ya Ustawi wa Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bima ya Afya na Wateja. Malengo hasa ya kuanzisha Mfuko wa Bima ya Afya ilikuwa ni kuhakikisha mteja anapata huduma ya afya wakati wote bila shida yoyote. Hata hivyo, wanaonufaika na mfuko huu ni wale walio katika ajira rasmi ambao sehemu ya mishahara yao hukatwa na waajiri pia huwachangia katika Mfuko wa Bima ya Afya. Kambi Rasmi ya inataka kujua Mfuko huu wa Bima ya Afya unawasaidia vipi Watanzania walio wengi hasa waishio vijijini ambao hawako kwenye ajira rasmi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na malalamiko kwa wateja wa Mfuko huu kwamba kuna unyanyapaa kwa wateja wa *NHIF*. Hospitali zilizosajiliwa na Mfuko zinatoa upendeleo kwa wenye fedha taslimu/mkononi na wale wenye vitambulisho vya bima kuonekana kama vile ni wakopaji wa huduma. Ubaguzi huu upo sana hasa kwa hospitali zinazomilikiwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine katika Mfuko huu ni kwamba kuna baadhi ya huduma za afya na dawa ambazo hazilipiwi na Mfuko. Ili mteja

apate huduma au dawa hizo ni lazima alipie kwa fedha taslimu. Jambo hili limekuwa ni kero kubwa kwa wateja kwani mteja anaweza kupata tatizo la ugonjwa wakati hana fedha taslimu na anakosa huduma eti kwa sababu huduma hiyo haipo katika orodha ya huduma au dawa zinazolipiwa na Mfuko wa Bima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kurekebisha utaratibu huu wa sasa wa kulipia baadhi ya huduma na dawa na kulipia huduma zote na dawa zote ili kutowachanganya wateja. Utaratibu wa sasa wa kulipia baadhi ya dawa na huduma ni hujuma dhidi ya mteja kwa kuwa hakukuwa na makubaliano kati ya mteja na Bima ya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma ya afya ya mzazi kwa mama na mtoto. Kwa mujibu wa Lengo la 5 la Malengo ya Milenia (MDG 5) – ambalo ni "kupunguza vifo vya akinamama kutokana na matatizo ya uzazi", Tanzania inatakiwa kupunguza vifo hivyo kwa asilimia 75 ifikapo mwaka 2015. Kutokana na Ripoti ya Tathmini ya Malengo ya Milenia ya mwaka 2008 *(Mid-Way Evaluation Riport 2000- 2008)* ni kwamba, Tanzania imeonekana kuwa haifanyi vizuri katika kupunguza vifo hivyo vya kina mama. Ripoti hiyo inaonyesha pamoja na kuwa malengo yalikuwa kupunguza vifo vya akina mama kutoka 529 kwa kila idadi ya vizazi salama 100,000 mwaka 1990 hadi 244 kwa kila idadi ya vizazi salama 100,000 ifikapo mwaka 2008, vifo viliongezeka hadi kufikia 578 kwa kila idadi ya vizazi salama 100,000 kwa Tanzania Bara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Zanzibar matarajio ya Malengo ya Milenia yalikuwa kupunguza vifo kutoka 323 kwa kila idadi ya uzazi salama100, 000 mwaka 2000 hadi kufikia 173 kwa kila idadi ya uzazi salama 100,000 mwaka 2008. Lakini badala yake takwimu zinaonyesha kwamba vifo viliongezeka na kufikia 473 kwa kila idadi ya uzazi salama 100,000. Kutokana na takwimu hizi, ni dhahiri kwamba itakuwa vigumu sana kufikia lengo la Milenia la kupunguza vifo vya akina mama kwa asilimia 75 ifikapo mwaka 2015 kama jitihada za ziada hazitafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma ya afya ya mama na mtoto hapa nchini bado inakabiliwa na changamoto nyingi. Kwa mujibu wa Jarida la Utafiti wa Afya Tanzania, Juzuu 13, (2011) licha ya vifo vinavyotokana na uzazi kupungua kidogo na kufikia vifo 454 kati ya vizazi salama 100,000 na licha ya asilimia 96 ya wajawazito kuhudhuria walau mara moja katika kliniki ya wajawazito, bado karibu nusu wa wajawazito yaani 49% hawapati huduma ya kitaalamu ya uzazi *(skilled delivery)* na hivyo kupunguza usalama katika uzazi. Pamoja na idadi kubwa hivi ya wajawazito kutopata huduma ya kitaalamu ya uzazi salama ni asilimia 13 tu wanaojifungulia majumbani wanapata huduma ya afya katika vituo vya afya baada ya kujifungua *(postnatal check-up).*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Taarifa ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii (2007), inakadiriwa kuwa asilimia 80 ya watu hapa nchini wanaishi umbali wa takriban kilomita tano (5) kutoka

kwenye kituo cha afya. Hata hivyo, pamoja na mtawanyiko huu mzuri wa vituo vya afya bado vingi havina huduma za uzazi kwa wajawazito na vingine vimekosa wataalamu wenye sifa stahiki kwa ajili ya kutoa huduma hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na upungufu wa wahudumu katika huduma ya uzazi, ni kwamba hata wale wahudumu waliopo kuna baadhi ambao ni wazembe, huwanyanyasa wajawazito kwa kuwatolea maneno ya kejeli  na kusababisha vifo vya mama na mtoto kutokana na uzembe. Aidha, baadhi ya vifo vimetokea baada ya wahudumu kuomba rushwa kutoka kwa wajawazito na waliposhindwa kulipwa basi walitelekezwa bila huduma yoyote na hivyo kufariki wakati wa kujifungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa kutoka vyombo mbalimbali vya habari, kwa nyakati tofauti zimehusisha baadhi ya Wauguzi katika hospitali ya Amana, Mwananyamala na Temeke zilizopo Dar es Salaam, kuomba rushwa kutoka kwa wajawazito wanaopelekwa kwenye hospitali hizo licha ya Serikali kusema kuwa akina mama na watoto wapewe huduma bure wakati wa kujifungua. Matokeo yake ni kwamba wale wanaoshindwa kutoa rushwa huachwa bila msaada na ndio ambao hatimaye hufariki wakati wa kujifungua au watoto wanaozaliwa kufariki kwa kukosa huduma ya haraka. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kusema imewachukulia hatua gani Wauguzi ambao kwa uzembe au kutowajibika walisababisha vifo kwa wajawazito wanaojifungua na watoto wanapozaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vyanzo vingine vya vifo kwa akina mama wajawazito na watoto kwa mujibu wa Profesa Esther Mwaikambo, sababu zilizotajwa kusababisha vifo vya akina mama na watoto, kwa akina mama, vifo husababiswa na:-

(i) Kutokawa na damu nyingi wakati wa kujifungua (*Hemorrhage*)- 28%;

(ii) Utoaji mimba usio salama *(Unsafe abortion*) – 19%;

*(iii) Eclampsia* 17%;

(iv) Maambukizi (*Infections*) 11%; na

(v) Uzazi wenye matatizo (*Obstracted Labour*) 11%.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kwa upande wa vichanga, vifo vilisababishwa na:-

(i) Maambukizi (*Infections*) 29%;
(ii) Ukosefu wa hewa (*Asphyxia*) 27%;
(iii) Uzazi kabla ya umri wa kuzaliwa *(Low birth, Preterm*) 23%;
(iv) Kifo wakati wa kuzaliwa (*Congenital*) 7%;
(v) Kuhara (*Diarrhoea*) 3%;
(vi) Pepopunda (*Neonatal Tetanus*) 3%; na
(vii) Vyanzo vinginevyo 8%.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili kuwa imechukua

hatua gani hadi sasa kuboresha afya ya mama na mtoto na hivyo kupunguza vifo vya akina mama na watoto hapa nchini. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza imefanikiwa kiasi gani katika kufikia lengo la 5 la Malengo ya Milenia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango Maalum wa Afya ya Msingi (MMAM). Afya ya msingi ni muhimu sana kwa wananchi kwa kuwa huduma za afya husogezwa karibu zaidi na wananchi. Kwa mujibu wa Taarifa ya Hali ya Uchumi ya 2011, Serikali aliahidi kuendelea kutekeleza Mpango wa Afya ya Msingi ambao unalenga kusogeza karibu huduma za afya kwa wananchi kwa kuwa na zahanati katika kila kijiji na kituo cha afya katika kila kata. Aidha, Mpango huu unalenga pia kuboresha huduma za afya na ustawi wa jamii ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa dawa na vifaa tiba na kuongeza upatikanaji wa rasilimali watu. Kambi Rasmi ya Upinzani, inaitaka Serikali kueleza mbele ya Bunge hili imefikia hatua gani katika utekelezaji wa Mpango wa Afya ya Msingi hadi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukarabati na ujenzi wa vituo vya kutolea huduma ya afya. Taarifa ya Hali ya Uchumi 2011, inaonyesha kwamba Serikali ikishirikiana na wadau mbalimbali na mashirika ya umma, dini na watu binafsi, iliendelea kuboresha huduma za afya kwa kufanya ukarabati na ujenzi wa vituo vya kutolea huduma ya afya. Hata hivyo, taarifa hii haioneshi ni vituo vingapi vya afya na katika Wilaya zipi vilivyojengwa au kukarabatiwa. Taarifa hii imeishia kutoa idadi ya vitanda vilivyopo katika vituo vyote vya afya nchini. Kwa mujibu wa taarifa hii, idadi ya vitanda

katika vituo vyote vya afya nchini ni 48,480 ikilinganishwa na vitanda 45,241 mwaka 2010 ikiwa ni ongezeko la vitanda 3,239 sawa na asilimia 7.2. Hata hivyo, taarifa hii haioneshi ongezeko la vitanda 3,239 liligawiwa katika vituo gani vya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Chakula na Lishe. Kwa mujibu wa Taarifa ya Hali ya Uchumi, ni kwamba Serikali imethibitisha kwamba imekamilisha Mkakati wa Taifa wa Lishe wa Miaka Mitano (2011/2012 – 2015/16). Vipaumbele katika mkakati huu ni kuboresha ulishaji wa watoto wachanga na wadogo, kudhibiti upungufu wa vitamini na madini mwilini kwa watu wa rika zote, kudhibiti utapiamlo kwa wajawazito na watoto. Aidha, mkakati unalenga kutoa matunzo na huduma za lishe kwa watu wanaoishi na VVU, matunzo na huduma za lishe kwa wanawake na watoto na kaya zilizo katika mazingira hatarishi, udhibiti wa magonjwa sugu yasiyo ya kuambukiza yanayosababishwa na ulaji usiofaa na kuboresha uhakika wa chakula katika kila kaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza mbele ya Bunge hili, imetenga fedha kiasi gani katika mwaka huu wa fedha kutekeleza mkakati huu wa chakula na lishe? Aidha, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ilijulishe Bunge hili na wananchi kwa ujumla kwamba imefikia hatua gani ya utekelezaji wa mkakati huu wa chakula na lishe?

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa bajeti 2012/2013. Bajeti ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii inayoombewa idhini ya Bunge kwa mwaka huu wa

fedha 2012/2013 ni shilingi 576,674,066,000 ikiwa imepungua kwa asilimia 1.3 ukilinganisha na bajeti ya mwaka 2011/2012 ambayo ilikuwa ni shilingi 584,161,863,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, ingawa matumizi ya kawaida katika bajeti ya Wizara hii yameongezeka, bajeti ya maendeleo katika Wizara hii imepungua kwa asilimia 22.3 kutoka shilingi 364,794,487,000 mwaka 2011/2012 hadi kufikia shilingi 283,446,029,000 mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, mgawanyo wa fedha za maendeleo. Uchambuzi wa takwimu hizi unaonesha kuwa miradi ya maendeleo katika Wizara hii haujapewa kipaumbele kabisa. Bajeti ya maendeleo inayoombewa idhini katika Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa mwaka huu 2012/2013 ni shilingi bilioni 283. Kati ya fedha hizi shilingi bilioni 264 ni fedha za nje (mikopo/ufadhili) na shilingi bilioni 19 ni fedha za ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa takwimu hizi ni kwamba bajeti ya maendeleo ni tegemezi kwa fedha za nje kwa asilimia 93.2. Hii ni hatari sana kwa maendeleo ya sekta ya afya kwani fedha za ufadhili hazina uhakika, mara nyingi hufika kwa kuchelewa na wakati mwingine hazifiki kwa viwango vilivyotarajiwa. Aidha, kutegemea ufadhili kwa kiasi kikubwa hivi ni kuyaweka maisha ya wanachi chini ya mamlaka na udhibiti wa wahishani au wakopeshaji ambao hatuna mikataba nao ya kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya bajeti ya maendeleo kuwa tegemezi kwa fedha za nje kwa kiasi kikubwa sana lakini pia bajeti nzima ya Wizara ya Afya na Usitawi wa Jamii inakwenda kinyume na Malengo ya Milenia na Azimio la Abuja la mwaka la mwaka 2001 ambalo linataka kila nchi mwanachama wa Umoja wa Afrika walau inatenga asilimia 15 ya bajeti yake kwa ajili ya Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo nchi za Afrika zilizofikia na nyingine kupitiliza katika makubaliano ya Abuja. Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani *(WHO)* Afrika ya Kusini na Rwanda zimefikia kiwango cha 15% cha bajeti zao kwenye Sekta ya Afya. Aidha, Tume ya Umoja wa Afrika imeainisha nchi sita wanachama wa Umoja huo kufikia na kupitiliza kiwango cha Abuja cha 15% kama ifuatavyo: Rwanda (18.8%) Botswana (17.8%) Niger (17.8%) Malawi (17.1%) Zambia (16.4%) na Burkina Faso (15.8%) Kambi Rasmi ya Upinzani inaiuliza Serikali, je, imejitoa kwenye Azimio la Abuja? Kama sio, imepiga hatua kiasi gani katika kutekeleza Azimio la Abuja wakati bajeti ya Afya inazidi kupungua?

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya bajeti nzima ya Wizara hii kutofikia malengo ya Azimio la Abuja lakini pia kuna baadhi ya idara zimetengewa fedha kidogo tofauti na malengo ya "*Medium Term Expenditure Framework".* Kwa mfano, mahitaji halisi ya madawa na vifaa tiba muhimu kwa mujibu wa MTEF 2012/13 ni shilingi bilioni 198. Fedha zilizotengwa kwa ajili ya madawa na vifaatiba kwa mwaka huu wa fedha 2012/2013, ni shilingi bilioni 80 sawa na asilimia 40 ya mahitaji. Pamoja na upungufu huu, bado bajeti ya

ununuzi wa dawa ni tegemezi kwa shilingi bilioni 46.5 ikiwa ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuongeza fedha za ndani kwa ajili ya maendeleo ili kuinusuru sekta hii ya afya na utegemezi wa fedha za nje kwa miradi ya maendeleo. Aidha, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa kauli hapa Bungeni kuwa ni lini itatoa fedha zinazolingana na mahitaji halisi ya Bohari ya Taifa ya Madawa *(MSD)?*

Mheshimiwa Naibu Spika, mapambano dhidi ya UKIMWI. Maambukizi ya VVU na UKIMWI bado ni tishio kwa maisha ya wanachi na ni janga la Taifa. Hadi sasa hakuna taarifa rasmi za mafanikio ya upatikanaji ya chanjo za kutokomeza gonjwa hili tofauti na dawa za kupunguza makali ya UKIMWI *(ARVs*) na sasa kuna taarifa zilitolewa kuwa ugonjwa huu umeendelea kuwa sugu hasa Barani Afrika. Taarifa za maambukizi ya VVU kama zilivyoandikwa kwenye tovuti ya Tume ya UKIMWI (*TACAIDS)* ni za tangu mwaka 2008 na hivyo kutoweza kutoa picha halisi ya mwenendo wa maambukizi ya VVU kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kuna taarifa kwamba wanasayansi wamegundua chanjo ya UKIMWI. Kwa mujibu taarifa ya gazeti la Mwananchi la tarehe 25 Julai, 2012, nanukuu:-

*"Wanasayansi hao wamekuja na kauli hizo za matumaini wakati ambapo tayari wamefanya tafiti mbalimbali na kugundua tabia za VVU ikiwa ni pamoja na vitu ambavyo vinaviwezesha kushambulia seli*

*nyeupe za damu, maarufu kwa jina la CD4, ambazo ni sehemu ya kinga ya mwili wa binadamu".*

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya gazeti hili inaeleza kwamba licha ya tafiti mbalimbali kuonyesha kuwa kuna kila dalili ya kupatikana kwa chanjo, miaka michache iliyopita, waligundua moja ya dawa zinazotumika kupunguza makali ya VVU *(ARV)* ijulikanayo kama Truvada, yenye uwezo wa kumkinga mwathirika kumwambukiza mpenzi wanayeshiriki naye tendo la ndoa. Taarifa ya gazeti hili inaonesha kwamba wiki chache zilizopita, Mamlaka ya Chakula na Dawa ya Marekani *(FDA)* iliidhinisha Truvada, ambayo ilianza kutumika sehemu mbalimbali duniani tangu mwaka 2004, kuwa ni tiba ya kuzuia kuenea kwa Virusi Vya Ukimwi (VVU).

Mheshimiwa Naibu Spika, habari hizi zinazohusu uwezekano wa kupatikana dawa ya kutibu UKIMWI si jambo dogo kwa kuwa UKIMWI kwetu bado ni tishio kwa uhai wetu. Serikali haipaswi hata kidogo kupuuza taarifa kama hizi. Ni wajibu wa Serikali kufuatilia na kujua ukweli ni upi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kufanya mambo yafuatayo:-

(i) Kutoa takwimu halisi na sahihi za sasa za maambukizo ya VVU hapa nchini. Hii itawasaidia wananchi kujua mwenendo wa maambukizi ya gonjwa hili ili kujipanga vizuri kwa mapambano dhidi ya UKIMWI;

(ii) Kueleza kiwango cha mafanikio au kushindwa katika kupambana na UKIMWI na mwelekeo ukoje; na

(iii) Kueleza Bunge hili kama kuna watafiti kutoka Tanzania waliojiunga na watafiti wa kimataifa katika utafiti wa UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, walemavu. Walemavu katika nchi yetu wanakadiriwa kufikia asilimia 10 ya Watanzania wote milioni 42, hivyo kundi hili ni kundi muhimu sana kuliangalia kwa jicho la karibu. Kitendo cha Serikali kutenga jumla ya shilingi milioni 50 tu kwa ajili ya kundi hili inaonyesha dhahiri kuwa Serikali hailipi umuhimu kundi hili.

Mheshimiwa Spika, Bunge hili lilipitisha Sheria ya Walemavu, Na.9 ya mwaka 2010 na sheria hiyo ikasainiwa na Mheshimiwa Rais kwa ajili ya kuanza kutumika. Aidha, kifungu cha 8 cha sheria hiyo kinaanzisha Baraza la Ushauri la Taifa kwa watu wenye ulemavu. Sambamba na hilo, kifungu cha 11kinatoa mwongozo wa wajumbe watakaounda Baraza hilo. Kambi ya Upinzani inataka kuelewa kwa nini hadi leo Baraza hilo halijaundwa?

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 14 cha sheria hiyo kinataka kuundwa kwa Kamati za Ushauri za Vijiji, Wilaya na Mikoa lakini hadi sasa hakuna chochote kilichokwishafanyika. Kutokuundwa kwa Mabaraza hayo ngazi ya chini inatokana na kutokutungwa kwa kanuni za kusimamia sheria hiyo. Hivyo basi, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ilieleze Bunge hili ni kwa nini

toka Sheria hii itungwe kanuni zake bado hazijatungwa?

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Watu Wasioona-Manoleo cha Tabora. Chuo hiki kilijengwa kwa msaada wa watu wa Sweden kwa lengo la kuwafundisha stadi za maisha watu wenye ulemavu wa kuona na hivi sasa tangu kujengwa kwa chuo hicho ni miaka 16. Bajeti inayotengwa miaka yote ni kwa ajili ya kulipia mishahara ya watumishi wa Serikali lakini hakuna hata mwanafunzi anayesoma hapo. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali ilieleze Bunge hili na Watanzania wote fedha zinazoombwa za kukarabati chuo hicho ni kwa ajili ya nani na Serikali ina mpango gani na chuo hicho?

Mheshimiwa Spika, dawa kuharibika Bohari Kuu ya Dawa. Kumekuwa na ongezeko la dawa zilizoisha muda wake katika nchi yetu. Kwa mujibu wa Gazeti la Daily News la tarehe 4 Aprili, 2012 ni kwamba Serikali ilipata hasara ya shilingi bilioni 4.7 kutokana na dawa zilizoisha muda wake wa matumizi kwa mwaka wa fedha 2010/2011.

Mheshimiwa Spika, wakati dawa zinaharibika zikiwa Bohari ya Dawa, wananchi wetu wanaendelea kuteseka kutokana na dawa kutokupelekwa kwenye zahanati na vituo mbalimbali vya afya nchini. Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kuwa jambo hili halikubaliki hata kidogo kwani uzembe huu haupaswi kuvumiliwa tena na wahusika wote wanapaswa kuchukuliwa hatua mara moja.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) na mgogoro wa wamiliki wa Maduka ya Dawa Muhimu Dar es salaam. Pamoja na majukumu mengine, Mamlaka ya Chakula na Dawa ina jukumu la kuratibu maduka ya dawa hapa nchini. Katika kutekeleza Waraka wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii wa mwaka 2009 ambao ulisitisha Maduka ya Dawa Baridi na kutekeleza mpango wa Maduka ya Dawa Muhimu, Mamlaka ya Chakula na Dawa ilipiga marufuku Maduka ya Dawa Baridi na kuyabadili kuwa Maduka ya Dawa Muhimu. Matarajio ya waliokuwa wamiliki wa Maduka ya Dawa Baridi ni kwamba wangebadili maduka yao kuwa Maduka ya Dawa Muhimu na kuendelea na biashara ya dawa muhimu katika maduka yao katika maeneo yaleyale waliyokuwepo awali.

Mheshimiwa Spika, kinachoshangaza na kulalamikiwa ni kwamba Mamlaka ya Chakula na Dawa imewaamuru wenye maduka hayo kuondoa kabisa maduka hayo kutoka katika maeneo ya katikati jiji la Dar es Salaam na kuyahamishia maeneo ya pembezoni mwa Jiji kama ifuatavyo: Katika Wilaya ya Temeke maduka hayo yanatakiwa kufunguliwa katika maeneo ya Vijibweni, Kibanda, Kisarawe, Somangira, Kimbiji, Pemba, Mnazi, Mji mpya na Chamazi. Katika Wilaya ya Kinondoni, maduka hayo yanatakiwa kufunguliwa katika maeneo ya Kibwegere, Kwembe, Kisopa, Msumi, Msakuzi, Mavurunza, Changanyikeni, Makongo Salasala na Madale. Katika Wilaya ya Ilala, yanatakiwa kufunguliwa Kisukuru, Tembo, Vigwaza, Liwiti, Kinyerezi, Chanika, Msongola na Kitunda.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaamini kwamba kuwafukuza wamiliki wa maduka haya kutoka mjini kwenda pembezoni ni kuwanyima uhuru wa kujiajiri na kujipatia kipato halali na hivyo kudumaza uchumi wao na wa Taifa kwa jumla. Aidha, kitendo cha kuwafukuza wamiliki wa maduka hayo kuna sura ya ubaguzi na ufisadi kwani wanaofukuzwa ni wale wenye maduka madogo yenye mitaji midogo na wanaobaki ni wale wenye maduka makubwa yenye mitaji mikubwa. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza mbele ya Bunge hili kwamba Mamlaka ya Chakula na Dawa imetumia vigezo vipi kuwafukuza wamiliki wa maduka haya kutoka mjini kwenda pembezoni na kuwaruhusu wengine kuendelea kubaki mjini?

Mheshimiwa Spika, mahudhurio katika vituo vya afya kwa wagonjwa wa nje *(Out- Patient).* Taarifa ya Hali ya Uchumi, 2011 inaeleza kwamba mahudhurio katika vituo vya afya kwa wagonjwa wa nje yalikuwa ni 41,014,853 ikilinganishwa na 35,776,667 mwaka 2010 sawa na ongezeko la asilimia 14.6 Tafsiri sahihi ya ongezeko hili ni kwamba Taifa linaumwa. Idadi ya wagonjwa nchini inapoongezeka maana yake ni kwamba afya za wanachi ziko hatarini na kwa maana hiyo hata nguvukazi ya Taifa iko mashakani. Kwa vyovyote vile, ongezeko la wagonjwa si jambo la kufurahia hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inashangazwa na inalaani kitendo cha Serikali kufurahia ongezeko la wagonjwa hapa nchini kwa

maelezo kwamba ni mwamko wa jamii katika huduma za afya zitolewazo na vituo vya afya.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Rwamlanza, Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusiana na Wizara hii ya Afya na Ustawi wa Jamii.

## MWONGOZO WA SPIKA

**NAIBU SPIKA:** Naona Waheshimiwa wanataka Mwongozo, wako wangapi, mwendelee kusimama ili niwaone; Mheshimiwa Silinde, Mheshimiwa Mbatia na Mheshimiwa Lugola. Ahsante nadhani nimewaona wote, tuanze na Mheshimiwa Lugola.

**MHE. ALPHAXARD K.N. LUGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni zetu za Kudumu za Bunge 68(7), naomba Mwongozo wako. Juzi Jumamosi tarehe 28/7/2012 wakati Waziri wa Nishati na Madini anahitimisha hotuba yake aliliaminisha Bunge hili na kuwaaminisha Watanzania waliokuwa wanamtazama na kumsikiliza kwamba mgao huu wa umeme ulikuwa ni wa kubumba, ni wa kutengeneza na kwamba hatua ambazo ameanza kuchukua ni kwamba mgao wa umeme hautakuwepo na itakuwa ni historia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako kwa sababu matamshi haya yanahusu suala nyeti sana linalohusu uchumi na Watanzania kwa ujumla. Ni suala la muda mrefu kwa maana ya hujuma,

hujuma ambazo zimeota mizizi lakini suala la Mheshimiwa Spika la kuvunja Kamati ya Nishati na Madini, kwangu mimi bado siyo suluhisho la jambo hili, kwangu mimi kuwasimamisha Watendaji Wakuu wachunguzwe siyo suluhisho na suala la kusema Bodi inaweza kuvunjwa baadaye bado siyo suluhisho. Ninazo taarifa kuwa baada ya Waziri kwa kitendo chake na Manaibu wake pamoja na Katibu Mkuu ambapo ninawapongeza kwa kazi waliyofanya ya kuziba mianya na kusigina mirija ya mafisadi ndani ndani ya *TANESCO*, mafisadi hawa sasa baada ya kuona *Plan* A ya kulitumia Bunge lako Tukufu kama daraja la kuendeleza ufisadi ndani ya *TANESCO* imeshindwa, wanajipanga kufanya hujuma kwenye mitambo ya gridi ya Taifa na miundombinu ya *TANESCO*. *TANESCO* mpaka sasa inalindwa na kampuni binafsi, makampuni ambayo mengine yanaweza kuanzishwa jana tu, wakawapa virungu na filimbi Askari wao na wakaenda kulinda *TANESCO.* Katika nchi nyingine suala la umeme ni suala nyeti, linalindwa na Polisi na kwingine wanalinda Wanajeshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako kwa nini Serikali kupitia kwako usiitake itoe kauli hapa Bungeni ni kwa namna gani wataweza kudhihirisha kauli hii ya kutokuwepo mgao wa umeme kwa sababu kuna watu wamekuwa wakitaka suala la mgao wa umeme litangazwe kama janga la Taifa kwa maana kwamba nchi haitatawalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuomba uitake Serikali, kwa nini isije hapa Bungeni iseme sasa ina utaratibu gani katika kuwahusisha Watanzania wote

kwa sababu miundombinu ya *TANESCO* imepita kila mahali kwingine imepita maporini na kwingine vijijini, halafu na wao sasa wamejipangaje. Naomba Mwongozo wako juu ya suala hili.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutumia Kanuni za Bunge lako Tukufu, Kanuni ya 68(7) kuhusu jambo la dharura ambalo limetokea mapema ndani ya Bunge Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka niongezee tu pale alipozungumzia Mheshimiwa Mbunge wa Mwibara kwamba wahenga walisema heri kinga kuliko tiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii ambayo ni tete na ufisadi, ni mfumo ambao kuufumua kwa kauli hivihivi inakuwa ni shida na kwa kuwa Shirika hili la *TANESCO*, ni nyeti na muhimu kwa uchumi wa Taifa na kauli tu, tunafanya kazi huku, kwa sababu vita hivi vya ufisadi viko ndani ya Bunge lako Tukufu na nje ya Bunge lako Tukufu na kwa mtandao wa wafanyabiashara na Serikali haiwezi ikasema itatoa tu kauli kesho au wala nini, ni jambo la dharura sana na kwa kuwa Tanzania tuna Jeshi letu la Wananchi wa Tanzania na ndiyo kazi yao ya kulinda Taifa la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, liwe ni jambo la dharura, Serikali tuishauri iagize Jeshi liweze kulinda vyanzo vyetu vyote vya umeme wa *TANESCO* wakishirikiana labda na Jeshi la Kujenga Taifa na isitoshe hata Mawaziri wetu wenye dhamana na Wizara hii nao wapewe ulinzi wa uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tusije tukalia kesho au kesho kutwa kwa sababu hujuma hizi ambazo zinapangwa na hata baadhi ya vyombo vingine vya habari vinaweka wazi kwamba nchi itaingia gizani tupende tusipende ndani ya siku kumi na sita, *circumstantial evidence* za namna hii tusizidharau. Tunaomba tufanye maamuzi sasa na siyo kesho kwa ajili ya kuokoa maslahi ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tafadhali sana Mwongozo wako kuhusu jambo hili. *(Makofi)*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kanuni ya 68(7), muda mfupi uliopita kumewasilishwa taarifa mbili muhimu kuhusiana na suala la bajeti ya Wizara ya Afya. Taarifa ya kwanza ni taarifa ya Kamati ambayo kwenye ukurasa wa tano imesema kuhusu suala la utekelezaji wa madai ya Madaktari dhidi ya Serikali. Kamati imekuwa ikifuatilia kwa karibu na kutoa ushauri uliolenga kumaliza tatizo hilo na kwenye ukurasa wa saba wa maoni ya Kambi ya Upinzani umesema:-

*"Kuhusu Kamati ya Huduma za Jamii ilishashughulikia jambo hili na ikatuletea taarifa hapa. Sasa Kamati hii inarudi kufanya nini?"*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako, kwa mujibu wa Katiba ya nchi yetu, Ibara ya 63, Bunge ndilo lenye mamlaka ya kuishauri na kuisimamia Serikali. Sasa taarifa hii ya Kamati iliyowasilishwa hapa imesema tu kwamba Kamati ilitoa ushauri kwa Serikali juu ya ufumbuzi wa mgogoro kati ya Serikali na

Madaktari lakini huo ushauri wenyewe ambao Kamati imeutoa haujaletwa hapa Bungeni na taarifa ambayo Kamati ilikwenda kufanya kazi, kukutana na pande mbili mpaka sasa haijawasilishwa Bungeni. Kwa sababu hiyo, Wabunge tukiendelea kujadili, tutakuwa tunajadili taarifa za upande mmoja kwa mara nyingine tena bila ya kuwa na taarifa ya kina ya mambo yaliyojiri upande wa pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba Mwongozo wako kwa sababu hili jambo ni zito kidogo, bajeti iliyoko mbele yetu bado inautegemezi zaidi ya asilimia 90 kwa wahisani, *reallocation* iliyofanyika ni ndogo, hailengi kutatua matatizo ya msingi yaliyoko. Sasa ili kuliepusha Taifa kuingia tena kwenye mgogoro wa masuala ya Madaktari na watumishi wengine wa sekta ya afya, naomba Mwongozo wako ili ile Taarifa ya Kamati ya Huduma za Jamii iletwe hapa Bungeni tupate ushauri wa kina, mapendekezo, mawazo ya pande mbili ili Wabunge wakati wanajadili wayazingatie haya ili bajeti irekebishwe, iongezwe iweze kwenda kutatua tatizo la msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo kwa kutumia Kanuni ileile ya 68(7) kuhusu suala ambalo lilishatolewa Mwogozo lakini ninataka kuzumgumzia *angle* moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, asubuhi wakati Waheshimiwa wakiomba Mwongozo wa suala la

dharura kwa kutumia Kanuni ya 47 wakitaka jambo la mgomo wa Walimu lijadiliwe, katika Mwogozo wako ulisema kuwa suala hilo liko Mahakamani na tunasubiri majibu baada ya Mahakama, lakini ni kwamba hali baada ya Walimu kugoma mfano katika Jimbo la Mbozi Mashariki wanafunzi nao wameamua kugoma kwa kulala barabarani mfano katika eneo la Tunduma ambapo biashara za nchi za *SADEC* zimekuwa hazifanyiki lakini siyo katika eneo la Tunduma lakini pia katika maeneo mbalimbali nchini wamekuwa wakipigwa mabomu na sasa hivi wazazi wanashirikiana pamoja na wananchi wengine wakiamini kuwa Walimu wameonewa. Mfano mdogo katika eneo la Tunduma ofisi ya Halmashauri ya Mji imechomwa moto, magari yamepasuliwa na mambo mengine. Wakati tunasubiri hatma ya Mahakama, je, Bunge linachukua hatua gani ya dharura bila kuingilia uhuru wa Mahakama katika kuhakikisha tunalipatia suluhu suala hili? Naomba Mwongozo wako.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru. Hadi sasa tunaenda vizuri. Niwahakikishie kuwa kwa wale ambao wameomba Miongozo hii ya sasa hivi, yote mitatu, wawili walizungumzia Mwongozo mmoja; Mheshimiwa Lugola na Mheshimiwa Mbatia, nitatoa maelezo yake wakati wa *session* ya jioni, ni wakati muafaka, nitakuwa nimeshafanya *consultation* ya kutosha na kwa kuwa muda wetu wa kuendelea na shughuli hizi umebakia kidogo sana, naomba nimwite Mheshimiwa Magreth Mkanga awe mchangiaji wetu wa kutuanzishia zoezi hili.

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa mwanzo kwenye hoja hii iliyo mbele yetu. Kwanza, nimshukuru Mola kwa kunipa nafasi kusimama hapa leo na pia nitoe pole kwa yaliyotokea Zanzibar na hata msiba ambao bado ni mbichi kabisa ambao tunao hapa Bungeni. Niipongeze Wizara kwa hotuba nzuri tu ambao imetolewa na Wizara ambayo sasa inaongozwa na Waheshimiwa Madaktari wawili, Dkt. Mwinyi na Dkt. Suleiman na wenzao wote ambao wanaendesha jahazi hili muhimu kwa sababu ni uhai wa sisi sote binadamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mchango wangu pamoja na mengi yaliyoandikwa lakini bado ninasisitiza moja, uwepo wa huduma duni sana katika makao na vituo vinavyolea watu wenye ulemavu. Serikali inajitahidi lakini bado nimeona mfano Sukamahela juzi hapa, Mheshimiwa Dkt. Suleiman alikuwepo, hali ni mbaya. Kwa hiyo, bado tuongeze jitihada katika kuhudumia makundi haya na ieleweke siyo kwamba wanapenda kukaa kule lakini hali halisi ni kwamba wengine wamefukuzwa na jamaa zao kwa hiyo hawana mahali mbadala pa kwenda. Serikali kwa kweli ijitahidi kuokoa jamii hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ambacho napenda kuzungumzia, Kamati zote zimesemasema lakini wenzangu wa Upinzani hawa, hapa kidogo naweza kukubaliana nao, ulemavu hauna itikadi. Mlemavu anaweza kutoka popote, CHADEMA na kwingineko, hauna itikadi. Katika sehemu hii, masuala ya watu wenye ulemavu kwa upande wa tiba bado

kuna changamoto nyingi. Pamoja na kwamba Sera kwa Wazee imeweka wazi kuwa waliofikia miaka sitini hawalipishwi na Mheshimiwa Waziri Mkuu alishatoa maelekezo kwamba kuwe na Dirisha Maalumu kwa watu wenye ulemavu kuhusiana na masuala ya matibabu kwenye hospitali zetu na zahanati zetu, ni ngumu, wananyanyasika, bado akina mama wenye ulemavu wanapokwenda kujifungua wanasemwa vibaya. Wanaulizwa na wewe nawe umeshika mimba? Kana kwamba kushika mimba mtu mwenye ulemavu ni dhambi au haruhusiwi kuzaa. Haya mambo bado yapo! Wizara katika kushauriana na watendaji, naomba wakazanie mambo kama hayo. Umbali wa sehemu za kupata matibabu wengine hawawezi kufika huko na ununuzi wa dawa pia ni taabu. Kwa hiyo, naomba Sera izingatie kundi hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa kuna sheria ambayo ilishatungwa hapa ndani ya mwaka 2010, yazingatiwe yaliyomo kwenye sheria ile, mimi hilo ndiyo ombi langu na ndiyo msisitizo wangu. Sheria tuliitunga lakini sasa utekelezaji wake ni mgumu kwa sababu kanuni bado hazijatungwa. Juzi nilikuwa na Afisa Ustawi kutoka Wizarani, *VETA* walipokuwa na kikao cha viziwi, bado wanasema mchakato, sasa ni miaka miwili tangu sheria hii ipitishwe isije ikawa kama ile ya UKIMWI ambayo tulitunga toka mwaka 2007, lakini mpaka leo kanuni za utekelezaji hakuna, huku ni kuwakwamisha watu wenye ulemavu kuweza kupata haki zao kisheria zaidi kuliko kihurumahuruma kwa kuwa sheria ilipita tunahitaji kanuni ziwe tayari na kanuni hizi zitafsiriwe kwenye Kiswahili na wenyewe walengwa wafundishwe

ili waweze kuzitumia kikamilifu isiwe ni makabrasha tu masandukuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba nimeomba kanuni hizo zitafsiriwe kwa Kiswahili kama Serikali ilivyojitahidi kutafsiri Sheria kwa Kiswahili na kanuni hizi zitafisiriwe kwa Kiswahili, baadhi ziandikwe kwa maandishi ya *braille* ili wasiiona waweze kusoma na zitafsiriwe pia kwenye kanda za sauti angalau kuweza kuhimiza hata wasioona wasipokuwa na *braille* waweze kusikia ni nini kimesemwa ndani ya kanuni hizi. Haya ndiyo yatakayoweza kusaidia matumizi bora ya sheria hii na kanuni zake vizuri zaidi. Naomba Wizara hii ishirikiane na Wizara ya Utamaduni hata Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lugha ya alama bado zinalalamikiwa katika maeneo mengi. Kuna tangazo ambalo linaoneshwa sasa hivi kwenye luninga mimi kila ninapoliona huwa ninasikitika sana. Kwenye suala la tiba, tiba ni siri ya mtu, mgonjwa na Daktari lakini kwa viziwi inakuwa vigumu kwa sababu baadhi ya watekelezaji au wahudumu wengi lugha hiyo ya alama hawaijui na hii siyo kwa matibabu tu, kwenye elimu na kila mahali pia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lugha hii sasa na Katiba inapokuja, naomba wote kwa pamoja tusisitize lugha ya alama iwe ni lugha rasmi nchini ili kusudi kundi hili nalo liweze kujisikia linaeleweka kuliko hivi tunavyowaacha. Kiafya ndiyo hivyo, siri ya UKIMWI atajua na mwingine hata yule kiziwi akitoka hapo ana aibu, sasa tunafanyaje? Mawasiliano yanakuwa

magumu hapo. Mkifuatilia kwenye televisheni mnaweza mkaviona.

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama za kununulia vifaa bandia na dawa zake, kila siku ninasema. Pamoja na kwamba Serikali inasema wananunua vifaa hivyo, wanatoa ruzuku, lakini hata kwa wale wanaotengenezewa au wale watumiaji bei bado ni ghali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna *lotion* ya wenzetu walemavu wa ngozi ambayo kweli hiyo ukiitumia vizuri hata *cancer* ya ngozi yenyewe haikupati. Bei yake ni shilingi kumi na tano elfu mpaka ishirini na tano elfu. Ni walemavu wangapi wa ngozi (Albino) wanaweza kumudu? Kwa nini Halmashauri zetu zisitenge mfuko wa fedha ili kuweza kusaidia manunuzi ya vitu hivi bandia, wanasukumia Wizara. Naomba Wizara ya Afya ishirikiane kikamilifu kabisa na Halmashauri zetu. Sijui sasa Waziri Mkuu atatoa amri pawe na fedha maalum za kusaidia kwa sababu hata wenye ulemavu wenyewe wako kwenye Halmashauri zetu lakini wanahangaika na kusumbuka. Miwani, kofia, hata fimbo nyeupe kwa nini Halmashauri zetu zisiweze pia kufanya jitihada za kuweza kuhudumia watu wao katika maeneo yao?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Maafisa Ustawi wa Jamii, hii ni kada iliyotupwa, wapo wachache mno. Wizara imesema wanatakiwa elfu tatu na mia tatu, waliopo sasa hivi ni 437 tu, hivi tunafanya utani? Maafisa Ustawi wa Jamii ndiyo wanaoshughulika na makundi haya yenye matatizo jamani, sasa

wanapokuwa wachache tena wapo kwenye baadhi ya Mikoa, Wilayani sidhani kama hawa Maafisa wapo. Hata hawa wachache waliopo hali zao ni mbaya, ofisi ni za kupanga, mara wamefukuzwa, hazilipiwi kodi, hakuna *house rent* wala umeme, hivi ni nini sasa na hawa ndiyo watalaam waliosomea kushughulika na makundi haya magumu?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali hapa kwa kweli hamjatenda haki, walemavu, wazee, akina mama wanaozaa watoto saba, ni matatizo matupu kushughulikiwa, hali hii ni mpaka lini? Naomba Serikali ijitahidi kutimiza wajibu wake kikamilifu hapa. Fedha yenyewe wanaotengewa ndiyo hiyo wanashindwa kuhudumia hata wale wanaokaa kwenye vituo vya wazee. Ukienda Mkoani ukimwuliza mbona hapa Fungafunga hakuna kitu, wanakuambia kwanza hela zenyewe zinaletwa kidogo kutoka Makao Makuu, hivi ugatuaji wa Idara hii ya Ustawi wa Jamii kuileta chini ukoje mbona matatizo matupu?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Baraza la Ushauri la watu wenye ulemavu limesemwa kwenye sheria, hapa inasemekana limeundwa lakini mimi watu wangu wananiambia halijaundwa. Sasa tusielezane vitu ambavyo kidogo vinaleta wasiwasi moyoni, haipendezi, ukweli ni upi? Kama limeundwa limeshaanza kazi kweli? Mbona sielewi? Naomba hili nieleweshwe sawasawa kwa sababu ni muhimu ndilo litakalosaidia vyombo vingine kufanya kazi, kutoa huduma na kutetea watu wenye ulemavu kisheria zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kukumbusha, Mkataba wa Watu Wenye Ulemavu Duniani ulishaeleza kwamba kila baada ya miaka miwili nchi iliyoridhia ni lazima ipeleke ripoti watu hawa wanahudumiwaje, je, nchi yetu imeshapeleka ripoti hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ile Sheria ni tangu mwaka 2010 na Mkataba ule tuliupitisha hata kabla ya sheria, je, tumeshajiandaa kupeleka ripoti? Kama ni ripoti, tunaiandaa kwa jinsi gani, yasije yakaandikwa mambo ambayo si ya kweli hapa tukaonekana kule tunatia aibu kumbe huku mambo hayaendi kama yalivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kufahamu Baraza litaanza lini kazi na haya yote niliyoyasisitiza, Halmashauri zitenge pesa, Ustawi wa Jamii kama Watendaji jamani wapo hoi na waongezeke, wasomeshwe kwa bidii ili waweze kufanya kazi za kuhudumia makundi haya yaliyosahaulika vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja, lakini tusisahau pia mazingira ya kufikika kwa watu wenye ulemavu wa aina zote. Hata nyumba za Serikali, hospitali, zahanati mbona ni ngazi tu hata *wheel chair* haziwezi kupita, mnafikiri tutapataje hudumu ambazo tunapaswa kuzipata kama watu wengine? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana mama Margareth Mkanga, nafikiri dakika hizi zinatosha kabisa kwa

Mwenyekiti wa Kamati Mheshimiwa Mama Magreth Sitta kuweza kuchangia, karibu sana!

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nichangie hoja iliyoko Mezani, hoja ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru pia Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii ya kuwa hai siku ya leo. Wakati huohuo nawashukuru sana wanawake wa Mkoa wa Tabora, kwa kuwa bila wao nisingekuwepo hapa. Aidha, namshukuru sana Mheshimiwa Samuel Sitta, Kiongozi wa familia yetu ambaye ananisaidia sana kwa ushauri anaotupa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, natangulia kusema kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Huduma za Jamii na pia ni Mwenyekiti wa Kamati, kwa hiyo, namshukuru Dkt. Kebwe kwa kuwasilisha taarifa kwa niaba yetu sisi sote. Nawashukuru Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi na Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Dkt. Seif S. Rashid, kwa kazi nzuri ambayo wameanza kuifanya, nawatakia kila la kheri katika kazi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudi kubwa ya Serikali ya kuboresha utoaji wa huduma katika hospitali, bado sekta ya afya ina changamoto nyingi sana, lakini kutokana na muda nitazungumzia changamoto chache ambazo ni muhimu kufanyiwa kazi haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza kabisa katika Mpango wa MMAM ambapo wananchi wamehimizwa sana kujenga zahanati katika vijiji vyote na hakika wananchi wamejitolea kwa kusaidiana na Halmashauri na *TASAF* wamejenga zahanati nyingi sana, tunawapongeza sana wananchi. Lakini ni ukweli usiopingika kwamba hakuna wafanyakazi, majengo yaliyojengwa yamebaki wazi. Nitatoa mfano, ningeweza kutaja vijiji vingi tu ambavyo vimejenga zahanati ambazo hazina wafanyakazi na suala hili ni muhimu sana kutokana na juhudi kubwa ambazo wamefanya wananchi. Kwa mfano, ukichukua Wilaya ya Urambo katika Jimbo la Urambo Mashariki hivi sasa aende Afisa yeyote katika Kijiji cha Kasisi atakuta zahanati ambayo imeisha na nyumba za wafanyakazi lakini hazifanyi kazi kwa kuwa hakuna wafanyakazi. Hali kadhalika Nsogolo hakuna wafanyakazi, majengo yote yapo, pia aende Izengawatogilwe atakuta jengo halina wafanyakazi, akienda hali kadhalika Kiloleni. Hii ni mifano ya zahanati ambazo zipo tayari na nyumba za wafanyakazi lakini hakuna wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni suala la kusikitisha na kuwakatisha tamaa wananchi ambao wamejitolea kwa hali na mali. Naamini wapo Wabunge wengi tu ambao katika Majimbo yao zahanati zimejengwa na nyumba za wafanyakazi zipo lakini hakuna wafanyakazi. Hili ni jambo la kusikitisha wakati wananchi wanahitaji sana wafanyakazi wakiwemo Madaktari, Wauguzi, Manesi, Wafamasia na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili Wizara ya Afya ilichukulie kwa uzito unaostahili. Katika mwaka wa

fedha 2010/2011 na mwaka 2011/2012 walidahili watu, wakachukua kwanza watu zaidi ya 6000 pia wakadahili zaidi ya 7,000 lakini cha ajabu bado zahanati hazina watendaji kwa nini? Kama Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, wao waliomba kibali cha kuajiri na wakapewa kibali cha kuajiri wafanyakazi 9,391 lakini cha ajabu waliopatikana mpaka Desemba 2011 walikuwa ni 2,127, sasa wafanyakazi wako wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wasiwasi wangu ni kwamba wale wanaomaliza mafunzo iwe ya miaka miwili, mitatu na kadhalika wanaishia mijini na wakati mwingine wanaishia kuajiriwa na *NGO* na taasisi nyingine mbalimbali, zahanati zetu zilizojengwa kwa nguvu za wananchi zimebaki wazi. Ni lazima tujiulize huu ugonjwa tunautibu vipi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa pendekezo kwa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii jinsi ya kupata wafanyakazi haraka iwezekanavyo. Kwanza, napendekeza waangalie vijijini ambako wapo vijana waliomaliza Kidato cha Sita, wapo waliomaliza Kidato cha Nne na kuandaa mafunzo ya muda mfupi angalau wapate watu ambao watakwenda kukaa kwenye vituo vya afya na kusaidia maradhi kama vile malaria ambayo yanashambulia watu, kuharisha, homa za watoto na kadhalika. Kuliko kukaa tunasubiri hawa wanaochukua mafunzo ya miaka miwili na zaidi ambao itachukua muda mrefu sana mpaka kupata wafanyakazi wa kutosha. Naamini Wizara ya Afya inaweza kuandaa mafunzo maalum kama ya miezi sita au hata miezi minne ambayo yatasaidia kupata watu

wakaenda kwenye zahanati haraka iwezekanavyo. Wakishakupata waliopata mafunzo ya muda mrefu basi watakwenda pale na waliopata mafunzo ya muda mfupi wataongezewa ujuzi lakini kwa hali ilivyo wanapoomba vibali wanapewa 9,361 halafu wanaopatikana ni 2,127 hatufiki popote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba suala hili lifanyiwe kazi kwa kushirikiana na Halmashauri kupata vijana waliosoma vizuri huko vijijini na mafunzo haya wasiletwe Dar es Salaam wala wasipelekwe Tanga au wapi, wafundishwe hukohuko Mikoani kwa kutumia hospitali za Mikoani na kisha kupewa mkataba kwamba ukimaliza mafunzo haya utabaki kwenye Halmashauri hii ambayo imekusaidia kupata mafunzo haya. Lakini kwa kutumia utaratibu uliopo sasa hivi, vituo vyetu vya afya, hospitali zetu hata zahanati ambazo wananchi wamehimizwa na wamejenga zitaendelea kubaki wazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili nataka kuzungumzia suala la uzazi salama. Kwanza nawapongeza wanawake wote kwa kujitolea nafsi zenu kupata watoto ambayo siyo kazi rahisi, mnaweka roho zenu rehani, hongera sana akina mama wote. Tumepewa kazi hii na Mwenyezi Mungu lakini tuiombe Serikali yetu itusaidie tusiendelee kufa wakati wa kujifungua. Mpaka sasa hivi akina mama zaidi ya 454 kati ya wanawake wajawazito 100,000 wanafariki. Kwa nini watu 454 waendelee kufa vifo ambavyo vinaweza kuzuilika? Kwa hiyo, akina mama tuungane kuitaka Serikali iongeze bajeti, bajeti hii haitoshi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yetu ni nchi mwanachama wa Umoja wa Nchi za Afrika ambazo zilikubaliana mwaka 2001 kwamba bajeti ya Serikali angalau iwe asilimia kumi na tano. Jambo la ajabu sasa hivi bajeti yetu imeshashuka. Serikali ilijitahidi mwaka 2010/2011 mpaka ikafikisha asilimia 12, lakini ghafla imeshuka. *Graph* inashuka na tunaogopa kwamba sijui mwisho wake ni nini. Waliposema asilimia 15, hawasemi mpaka tuwe matajiri, wamesema hii asilimia kumi na tano ni kutokana na kile mlichonacho katika nchi yenu. Wanasema asilimia 15 ya hicho mlichonacho katika bajeti ya nchi yenu. Ili kudhibiti vifo vya akina mama wajawazito, kuna haja ya Serikali kuongeza bajeti ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja lakini kwa kuiomba Serikali iendeleze mazungumzo na Madaktari ili wamalize mgogoro wao lakini pia Wizara iangalie Ustawi wa Jamii ili nao watendewe haki kwa kupewa fedha za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta. Nami nakubaliana nawe kuwapongeza akina mama wote kwa kazi kubwa sana ya kuzalisha Taifa. Ananikumbusha safari moja niko Jimboni, nikakutana na mpigakura wangu mmoja, Mnyamwezi mmoja, ananiambia Mheshimiwa Mbunge afadhali tumekutana bwana, nina hali mbaya kweli. Nikamuuliza, nini tena rafiki yangu? Akaniambia bwana mke wangu ni mjamzito sasa ndiyo wamemuingiza

*theater,* sasa unanisaidiaje? Nikamuuliza sasa nikusaidie vipi kwani mwenzangu wewe umejiandaaje? Akaniambia mimi mwenzako hata thumni sina. Kwa hiyo, pamoja na kuitaka Serikali itenge fedha kwa ajili ya mambo haya, nami niwaombe wanaume wenzangu na sisi tujiandae jamani kuchangia kidogo. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, jioni tutakaporudi, ataanza Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye, atafuatiwa na Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Deogratius Ntukamazina na Mheshimiwa Azza Hillary Hamadi na wengine wataendelea kutajwa hapo baadaye.

Kwa namna hiyo, naomba kusitisha shughuli za Bunge hadi saa kumi kamili leo jioni.

*(Saa 7.15 mchana Bunge lilisitishwa mpaka saa 10.00 jioni)*

*(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea na nilikwishatangaza asubuhi kwamba mchangiaji wetu wa kwanza mchana huu atakuwa ni Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye na atafuatiwa na Mheshimiwa Lucy Owenya na Mheshimiwa Ntukamazina ajiandae.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya mwanzo kabisa mchana wa leo ili niweze kuchangia hoja ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naomba nimpongeze kwa kuleta mbele yetu hotuba ya kina ambayo imeainisha mambo mbalimbali ambayo amepanga katika kutekeleza wajibu wake katika Wizara yake hii mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja kwa moja, naomba nizungumzie suala la huduma ya afya ya uzazi na mtoto. *Program* hii ni ya miaka mingi sana. Imekuwa ikizungumziwa sana hapahapa Bungeni, lakini vilevile hata nje ya Bunge hili kuonyesha *concern* juu ya ukubwa wa tatizo hili hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu zinaonyesha kwamba kuna kupungua kwa vifo vya akina mama na vifo vya watoto wachanga. Takwimu hizi zinavyoonyeshwa kwenye vitabu, naomba nieleze wazi kwamba sivyo hali ilivyo huko vijijini. Ukichukua hatua ya kwenda vijijini mwenyewe ukaangalia hali halisi ya namna akina mama wanavyosumbuka katika kupata huduma za uzazi, kweli utasikitika. Mimi naamini kabisa kwamba kuna *factors* nyingi sana ambazo bila shaka hatujazi-*address* vizuri ikiwa ni pamoja kwenda *physically* vijijini na kuona hali halisi ya jinsi ambavyo akina mama, watoto wachanga wanavyopotea hapa duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kabisa katika bajeti ya mwaka huu, Wizara italiangalia suala hili kwa makini ili uchunguzi zaidi uweze kuelekezwa vijijini. Mwenyewe ameahidi kwamba hili litafanyika, sasa ninamuomba afanye uchunguzi zaidi katika maeneo

ya vijijini. Hapa nikizungumzia vijijini, naomba aanze na vijiji vya Mkoa wa Mbeya ambavyo mimi mwenyewe ni shahidi nimeona, nimetembea katika maeneo mengi nimeona jinsi akina mama wanavyotabika kule kwenye vituo vya afya, *dispensary,* hawana huduma yoyote, hamna vitanda hata vya kuzalia, naomba mabadiliko katika eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ambalo nataka nizungumzie ni suala la kinga ya malaria. Ni kweli kabisa kinga ni bora kuliko tiba. Hiyo ni wazi kabisa. Malaria kama tunavyofahamu umeendelea kuwa ni ugonjwa ambao unaua usiku na mchana. Hivi sasa tunavyozungumza kuna baadhi ya Wabunge wenzetu hawapo hapa wana matatizo ya malaria, malaria ni tatizo kubwa. Katika mkakati ambao unaelezwa hapa na Wizara, mkakati mmojawapo ni wa kinga. Mimi sina matatizo na usambazaji wa vyandarua kwa wananchi. Sina tatizo nalo kwa sababu na yenyewe ni sehemu ya kinga. Bahati nzuri vyandarua hivyo vinatiwa dawa ambayo inasaidia kuua mbu lakini ninafikiri kuna suala bado halijawa *addressed* vizuri nalo ni la kuua viluwiluwi, hilo ni la muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hiki Waziri ametuambia kwamba watajielekeza katika Mikoa mitatu ya Kanda ya Ziwa, sikuona Mkoa wa Mbeya lakini nataka niseme ukweli hata huo Mkoa wa Dar es Salaam, Wilaya zote tatu watakazojielekeza, bado kuna matatizo makubwa, ukipita kule Tandale utachukia kuishi Dar es Salaam. Mimi nawahurumia sana watu wanaoishi Dar es Salaam, maji machafu yanapita mbele ya makazi ya watu, hapo pembeni

unaona watu wanakaanga *chips*, wanakula mayai, wanafanya kila kitu wanachoweza kufanya lakini mbele yao maji ni machafu, meusi yamejaa takataka na utandu wa vidudu vya malaria vimejaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunafanya nini badala ya kusema tunajiekeleza kwenye Mikoa michache namna hii, mimi nashauri iwe ni *program* ya nchi nzima kwa sababu tatizo ni kubwa sana. Tatizo hili ni kubwa wala hatuwezi kulifumbia macho kwa sababu malaria mpaka sasa watoto wadogo ndio wanaoangamia zaidi, wanatia huruma sana. Kwa hiyo, naomba tujielekeze huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hili linapofanyika la kupulizia dawa kwenye maji machafu, liende sambamba na utunzaji na usafi wa mazingira. Katika miji yetu jamani bila ya kuingia kwenye mikataba kila mtu hapa anajua miji yetu ni michafu jamani, ni michafu sana, bila hata kwenda kuingia kwenye mikataba au kukodisha sijui taasisi za nje au nani, miji ni michafu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nataka kutoa pendekezo kwa sababu tunazo sheria na kwa sababu usafi ni tabia, naomba Wizara hii ikishirikiana na TAMISEMI, washirikiane kwa karibu sana kuhakikisha kwamba wale Wenyeviti wa Mitaa watusaidie kuli-*address,* hili suala Wenyeviti wa Mitaa wanaweza. Tuwape hata *motivation* kidogo, wapewe hela kidogo, kazi hii wangeweza kuifanya vizuri mno.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nina ushahidi wa mitaa kule Dar es Salaam na hata huko ninakoishi Rungwe na maeneo mengine niliyofanyia kazi Mkoa wa Kilimanjaro na kadhalika, ukitumia mitaa utapata mji ulio safi kabisa bila kungoja ufadhili wowote, bila kungoja hata fedha nyingi kutoka kwenye bajeti. Kwa sababu ile ni tabia, lakini ni tabia ambayo hivi sasa imekuwa ni tatizo. Watu hawajali kabisa kwamba wanatupa takataka wapi, wanatupa kwenye mfereji, wanatupa wapi, nyumbani kwake anatupa ovyo tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata zile sheria ndogo ambazo Halmashauri zimeweka zinatumikaje, kwa nini hazitumiki zile? Hapa tunazungumzia kinga maana yake hapo unazalisha magonjwa mengine pia siyo malaria peke yake ni pamoja na hayo tunayosema ya kuhara, yanaingia katika mfumo huuhuu ambao unatokana na kuzalisha uchafu ambao wananchi wa Tanzania tunaona kwamba ni haki yetu tuishi na uchafu. Si sahihi hata kidogo. Si tunatembea tunaona katika nchi za wenzetu, wenzetu wanavyojali suala la usafi, kwa nini sisi tunaona uchafu ni sehemu ya maisha yetu jambo ambalo halikubaliki na kwa sababu Wizara hii ndio inayohusika na masuala ya afya ya mwanadamu basi yenyewe iwe mstari wa mbele katika kuhakikisha kwamba Watanzania tunajenga tabia ya usafi na inakuwa kweli usafi wa kudumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi kuna mashindano ambayo Mheshimiwa Waziri ameyazungumzia, mashindano ya Wilaya kwa Wilaya, mashindano ya miji, mashindano ya Manispaa, yale

mashindano mimi naona yanasaidia kidogo sana kwa sababu wanachukua maeneo yale ambayo yanaonekana tu ndio ambayo yanakuwa *assessed* lakini maeneo ambayo ni ya porini, kule vitongojini, kule pembezoni kule hawayaangalii kabisa. Kwa hiyo, kule kunanuka, kuna uchafu, kuna nini, lakini utashangaa unaambiwa Wilaya hii ni ya kwanza, hii ya pili, hii ya tatu, nenda kajionee huko mitaani hali ni mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi nasema ili tujenge tabia ya wananchi twende huko kwenye vitongoji, kwenye mitaa, tukaangalie na tuwajengee tabia nzuri, tuwajengee mifumo mizuri Wenyeviti wa Mitaa ili waweze kuendelea vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka niliangalie na kulizungumzia kwa uzito tena suala la Idara moja katika Idara ya Afya, *Physiotherapies.* Hii Idara mimi naona watu wengi hawaizungumzii kabisa, wala hawaionei umuhimu wowote. (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu, kwa upendo wake, kwa kuweza kunipa pumzi na hatimaye kuweza kuchangia hotuba ya Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuanzia, naanza na bajeti ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, kwa ujumla wake ni ndogo sana. Kama hotuba ya Upinzani ilivyosema, Azimio la Abuja lilituhitaji kama Serikali tutenge asilimia 15 ya bajeti nzima ya Serikali ambayo bajeti nzima ya Serikali ni shilingi trilioni 15.1 kwa maana hiyo Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ingetakiwa iwe imetengewe shilingi trilioni 2.2 hii ikiwa ni pamoja na TAMISEMI, sekta nzima ya afya lakini bado hatujatimiza lengo hilo. Kwa sasa hivi kwa ujumla wamepata kitu kama trilioni 1.2, kwa hiyo, hatujatimiza lile Azimio la Abuja hata kwa asilimia 11. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jambo la kusikitisha tunashindwa kufikia Azimio la Abuja ukizingatia nchi kama Rwanda miaka ya hivi karibuni ilikuwa kwenye mauaji ya halaiki lakini wao wameweza kutimiza Azimio lile. Ni lazima tuhakikishe kwamba tunatimiza ahadi zetu kwa sababu sekta ya afya ina matatizo, wajumbe wengi wamelalamika zahanati hazina vitendea kazi, vifaa havipo, wahudumu hawapo, kwa mfano kwenye Jimbo la Moshi Vijijini, Kata ya Mbokomu kule vijijini wanaita *clinic*, kuna *clinic* moja ambayo inahudumia akina mama pale lakini *clinic* ile ina mhudumu mmoja na haifanya kazi masaa yote na hawana vifaa, akina mama wanakwenda kujifungua pale. Sasa *imagine* pale hakuna hata maji ndani ya *clinic*, mwanamke anakwenda kujifungua, Daktari atamhudumiaje yule mwanamke? Mwanamke yule inabidi aoge, anatoka nje, kuna kibafu tu cha bati lakini pia hakuna maji. Kwa hiyo, tunaomba mtusaidie jinsi gani mnaweza kuisaidia Wizara ili iweze kuwasaidia wagonjwa kwa sababu kila mtu anahitaji kuwa na afya nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kidogo kuhusu *preventive services*. Katika kitabu cha maendeleo *HIV and Aids* na *TB* kwenye hela za ndani hawajatengewa kitu chochote, tunategemea hela za nje. Sasa Ukimwi na TB bado ni ugonjwa ambao unaendelea, watu bado wanapata maambukizi. Kwa mfano, katika Jiji la Dar es Salaam lenye wakazi zaidi ya milioni nne, wakazi wale wanatumia zaidi usafiri wa daladala ambao huwa zinajaza watu wengi sana. Kwa maana hiyo, watu bado watakuwa wanapata *TB* na watu bado watahitaji elimu. Napenda kujua Wizara ya Afya mmejiandaaje? Je, wafadhili wasipoleta fedha zile na tunajua wafadhili wanaleta fedha wakiwa wamechelewa, mtapata wapi fedha kwa ajili ya kuweza kutolea elimu?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kidogo magonjwa ya *NCD (None Communicable Disease).* Haya ni magonjwa sugu ambayo hayaambukizi. Kwa bahati nzuri mume wangu ni Daktari alinialika kuhudhuria semina ya magonjwa haya. Kwa kweli nilijifunza mengi, ni kitu cha hatari, magonjwa kama kisukari, *pressure* ya kupanda na kushuka na magonjwa ya moyo, hatujapewa elimu ya kutosha kuhusu magonjwa haya. Magonjwa haya kama ilivyo UKIMWI ni kiasi tu cha kubadilisha mtindo wa maisha na mtindo wa vyakula. Nilijifunza kwa mfano wale wanywaji wa bia, naomba mnisikilize kwa makini, ukinywa bia moja ni sawasawa na umekula chapati nane. Sasa mtu mwingine anakuambia amekunywa bia 10, ina maana amekula chapati asilimia 80. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo bia tu kwa mtu anayekunywa soda, ukinywa soda moja umekula vijiko vya sukari 25. Sasa hii ni elimu ambayo kwa msaada wa Waziri, kwa sababu tuna bahati Mawaziri wetu ni Mabingwa, mmoja kama sikosei ni Bingwa wa Ugonjwa wa Kisukari, mwingine Bingwa wa Ugonjwa wa Moyo. Kwa hiyo, anaweza aka-*arrange* katika hizi siku tulizopo hapa, hata watenge masaa mawili, waweze kutupatia Waheshimiwa Wabunge elimu kwa sababu sisi ni wawakilishi wa wananchi tunaweza kwenda kutoa elimu hata kwenye Kata zetu na kuhamasisha kuwe na siku ya mazoezi kwenye Kata zetu kwa namna moja au nyingine inaweza ikatusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wizara kuna Kitengo cha Elimu ya Afya ya Msingi, tungeomba kitengo hiki kiwekewe Kurugenzi ili kiweze kupanga mipango madhubuti ya kuweza kuwaelewesha wananchi jinsi ya kuwa na maisha bora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nizungumzie kuhusu tatizo la upungufu wa Madaktari. Siyo jambo la kufichika sasa hivi tuna upungufu wa Madaktari kwa asilimia 68 na sasa hivi ma-*Intern* wale waliopunguzwa kwa maana hiyo kutakuwa na upungufu mkubwa zaidi. Naomba nitolee mfano kule *KCMC*, sasa hivi kuna *clinic* ambazo wagonjwa ambao huwa wanahudhuria, kwa mfano, *clinic* za visukari na kadhalika, lakini sasa hivi tusidanganye hali siyo nzuri, watu wanakwenda kwenye *clinics* unakuta *clinic* hazifanyi kazi, kwa hiyo, wanaoumia ni wale wananchi wa kawaida. Tunaiomba Serikali ijaribu kuwarudisha

wale ma-*Intern* waje wakafanye kazi kwa sababu wale ma-*Resident Doctors* wako kwenye mitihani na ma-*Intern* hawako wa kutosha kwa maana hiyo wale Madaktari Bingwa wanafanyakazi kwa muda mrefu sana, wanachoka hatimaye wanashindwa kuzifanya kazi zao vizuri kwa sababu hawana wasaidizi. Kwa hiyo, tunaomba mliangalie hili kwa uangalifu ili wananchi wasizidi kupata matatizo zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kidogo suala la malaria. Hapa naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa juhudi zake za kujaribu kutatua suala la malaria lakini inabidi Wizara zishirikiane kwa mfano Wizara ya Afya na Wizara ya Ujenzi kwa sababu mnaanzia katika Jiji la Dar es Salaam kule kwenye mitaro ya maji taka na maji machafu, watu wanatupa takataka na maji yanasimama panakuwa ni mazalia ya mbu. Kwa hiyo, tunaomba ile mifereji ya maji machafu waizibe, wakiziba ina maana tutakuwa tumezuia mazalio ya mbu, kwa kuanzia waanze kwa kuziba pamoja na kupiga dawa, nina hakika tutapunguza malaria kwa kiasi kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kidogo naomba nizungumzie kuhusu *TFDA*. Pamekuwepo na matatizo mengi ya dawa ambazo hazikidhi viwango na *TFDA* ndio mamlaka ambayo inapita na kuhakikisha kwamba dawa ambazo hazikidhi viwango zinaondolewa katika maduka na wanakwenda kuzichoma. Lakini mpaka sasa hivi bado kuna vipodozi ambavyo vinaharibu akina mama wengi na kwa kutumia vile vipodozi wanapata magonjwa ya ngozi na hatimaye wanapata kansa na kupelekea kifo. Sasa

sijui Serikali kwa kiasi gani mtaweza kusaidia hili pamoja na *TFDA* kukagua lakini bado *TFDA* inaonekana hamjawatengea fedha kwenye kitabu cha maendeleo. Sijui ni kwa jinsi gani wataweza kufanya ukaguzi huu bila kuwa na fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maamuzi ya UKIMWI, kwa mara nyingine tena nazungumzia suala la *saloon*. Kwenye *saloons* za wanaume kwa wanawake, wanatengeneza kucha lakini wanatumia hizi *nail cutters* na vitu vyenye ncha kali wanazifuta tu na *sprit* lakini wana-*share* vile vyombo vya kukatia kucha, pia kwa wanaume kunyolea nywele wanafuta vile vifaa kwa *spirit* lakini kutokana na majibu ya Mheshimiwa Waziri wakati mmoja alisema kwamba *spirit* haiui vijidudu vinavyoambukiza UKIMWI. Sasa naomba Wizara iende ikatoe elimu ili watu wasiweze kutumia vitu vile kwa sababu tunaweza kusema ni mambo ya kujamiana tu yanayoleta magonjwa ya VVU lakini kumbe watu *innocently* bila kujua wanakwenda kuambukizwa magonjwa ya VVU kupitia *saloon*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa *MSD*. Sasa hivi *MSD* imekuwa *monopoly* ndiyo wanaosambaza dawa tu kwenye Mahospitali yetu. Sasa ni ngumu, unakuta dawa nyingine wanakaa nazo kwenye *store* mpaka zinaharibika. Mimi niko kwenye Kamati ya *PAC,* ni kitu cha kusikitisha, madawa yanaharibika ndani ya *store* lakini ukienda Vijijini hamna dawa, hamna *(simple things)* vya kwenda kujisaidia kama sindano, hata pamba. Kuna wakati mwingine unakuta mama mjamzito anaambiwa

aende na pamba hospitalini, lakini *MSD* zipo. Dawa nyingine unakuta zina-*expire* ndani ya *MSD*. Kwa hiyo, naomba Serikali iruhusu kuwe na Mamlaka zaidi ya *MSD* kuweza ku-*supply* madawa katika Mahospitali yetu ili tuondokane na huu ukiritimba wa kuwa na *MSD* peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ni matumaini yangu kwamba utaruhusu Waheshimiwa Mawaziri wawasiliane na Wizara ya Afya waje watupe elimu kuhusu yale magonjwa ya *none communicable disease* na sisi tuweze kwenda kuwaelimisha wapiga kura wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, natumaini yote niliyoyasema mtayachukua na Mheshimiwa Waziri Mkuu usisahau vitanda nilivyokuomba kwa ajili ya Hospitali Teule ya Moshi ile ya St. Joseph. Ahsanteni kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kutoa mchango wangu katika hotuba hii muhimu ya Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii. Hotuba yangu dakika kumi hazitoshi. Katika dakika kumi naomba niigawe hotuba yangu katika sehemu tatu.

Moja, nitaanza kuzungumza kama Mbunge wa Ngara kuonyesha changamoto zilizopo za huduma za afya katika Wilaya yangu; pili, nitatoa ushauri wangu kwa Wizara; na tatu, nikipata nafasi nitazungumzia

mifuko hii muhimu miwili; Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya na Mfuko wa Afya ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri pamoja na timu yake inayoongozwa na Kaimu Katibu Mkuu – Ndugu Regina Kikuli akisaidiwa na Mganga Mkuu *(Chief Medical Officer)*. Hawa watu wawili mimi nawafahamu, nimefanyanao kazi. Mama Kikuli pamoja na *Chief Medical Officer* kama ningekuwa Mamlaka ya Uteuzi, ningewa-*confirm* katika kazi zao hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo ya nchi yoyote na nchi yetu yanategemea wananchi wenye elimu nzuri na wananchi wenye afya nzuri. Wananchi wenye afya nzuri, watashiriki katika uzalishaji mali na ndivyo nchi itakavyoendelea. Kwa hiyo, kwa upande wangu, afya na elimu ndiyo kipaumbele cha kwanza katika harakati zetu za kuelekea nchi ya ahadi *(the promised land)* au nchi yenye uchumi wa kati. Bila wananchi wa afya nzuri hatutafika. Nchi ya ahadi, tunazungumzia mwaka 2025, lakini sijui kama tutafika. Kwa nini nasema hivyo? ?Ni kwa sababu maneno yetu na mipango yetu hayaendani na vitendo na utekelezaji.

Kwa mfano, niende upande wa Ngara, mpango wa MMAM umeanza mwaka 2008 na utakamilika mwaka 2017. Lakini najua sisi Ngara utatuacha kwenye mataa. Kwa nini nasema hivyo? Tuna Kata 20, lakini tuna Vituo vya Afya vinne tu. Kwa hiyo, bado kujenga Vituo vya Afya 16. Tuna Vijiji 73, tunazo Zahanati 42,

tuna upungufu wa Zahanati 31, katika miaka mitano ijayo, hatutaweza kukamilisha kujenga Zahanati hizo pamoja na Vituo vya Afya. Kwa hiyo, naona kwamba tusipozingatia mpango huu wa MMAM, hatutafika huko tunapotaka kwenda. Najiuliza: Je, tulipokuwa tunajenga sekondari moja kwa kila Kata na tukamaliza katika muda mfupi, tulitumia uchawi gani au tulitumia mbinu gani? Kwa nini mbinu hizi zisitumike kujenga Kituo cha Afya kila Kata katika muda uliobaki?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nauona mpango wa MMAM na mpango wa kutokomeza Malaria na mpango wa uchangiaji wa wananchi kugharimia matibabu kwamba ni *strategic intervation* nzuri katika kuboresha huduma za afya na katika kuhakikisha kwamba huduma za afya zinawafikia wananchi.

Mheshimiwai Naibu Spika, Ngara tuna tatizo kubwa la dawa. Nimetembelea hospitali nzote, Vituo vya Afya, lakini nimekuta kwamba tatizo kubwa ni dawa. Nimeambiwa na Watendaji huko Ngara kwamba mwaka 2011/2012 tunaidai *MSD* madawa ya thamani ya zaidi ya Shilingi milioni 160. Fedha hizo zimeshalipwa na Wizara ya Afya, lakini hatujapata dawa hizo. Kwa hiyo, tatizo la dawa ni kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa nikizungumzia hospitali ya Nyamiyaga kwamba hospitali hii ilizinduliwa na Mheshimiwa Rais mwaka 2008, lakini bado Wizara ya Afya inafikiri kwamba hospitali hii ni Kituo cha Afya. Kwa hiyo, wanapeleka fedha kidogo *MSD* kwa ajili ya dawa. Naomba Mheshimiwa Waziri azingatie hilo kwamba Nyamiyaga ni hospitali kamili. Pia tuna tatizo

la upungufu wa vifaa tiba na rasilimali watu. Kwa mfano, mahitaji ya watumishi kule Ngara ni 651, waliopo ni 253, upungufu ni 298. Naomba Mheshimiwa Waziri alione jambo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni upungufu wa Madakitari Kitaifa. Kuna ripoti ambayo imetoka juzi juzi kwenye kikao cha wataalamu wa afya kule Arusha Makao Makuu ya *East African Community* yanaonyesha au yanajaribu kulinganisha uwiano kati ya Dakitari na idadi ya wananchi, kwa Kenya, Uganda na Tanzania. Ripoti hii inasema kwamba kwa upande wa Kenya, Madakitari 14 wanaweza kuwahudumia wananchi laki moja, Uganda Madakitari 12 kwa wananchi laki moja, na Tanzania Madakitari 2 tu kwa wananchi laki moja. Hii ina maana kwamba kwa Tanzania Dakitari mmoja anawahudumia wananchi 50,000, Kenya 7,000 na Uganda 8,000.

Kwa hiyo, unaona kwamba kuna tatizo kubwa sana. Lakini pia nina taarifa kwamba vijana wanaomaliza Vyuo vyetu Vikuu vya MUHAS, KAIRUKI, BUNGANDO, KCMC na IMTU sio wote wanaoajiriwa. Nimekuwa nikipigiwa simu na vijana waliomaliza MUHAS kwa sababu mimi ni Mwenyekiti wa *Council* ya MUHAS wananiambia, Mzee hatujapata ajira. Sasa sina hakika kama tatizo ni kibali kutoka Utumishi kwa ajili ya kuajiri Madakitari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tunajaribu kuwaajiri walimu wote wanaomaliza masomo, tufanye hivyo pia kwa Madaktari.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Wizara ya Afya imetoa tamko rasmi kwamba inataka hospitali zote za Mikoa ziwe Hospitali za Rufaa. Sasa hiyo ni changamoto kwa Waziri na timu yake kwamba: Je, tunao Madakitari Bingwa wa kutosha wa kuweza ku-*manage* hizo Hospitali za Rufaa au tunavyo vitendea kazi vya kutosha? Jambo lingine ni *training* ya Madaktari Bingwa. Sasa hivi Wizara ya Elimu ndiyo ina-*train* Madaktari kwa *Degree* ya Kwanza, Wizara ya Afya ina-*train* kwa *Masters Degree* ambao ndio Mabingwa, lakini kazi hiyo Wizara ya Afya pekee yake haiwezi.

Naishauri Wizara ya Afya ipanue wigo wa *sponsorship,* Taasisi za Dini pamoja na hospitali kubwa ziweze kuwasomesha Madaktari kwenye *Degree* ya pili, yaani wawe Mabingwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende kwenye hii Mifuko miwili. Kuna Mifuko hii miwili muhimu sana. Mfuko wa Taifa ya Bima ya Afya ambao ulianza mwaka 2001 na Mfuko wa Afya ya Jamii, Mifuko hii ni muhimu sana na ninaipongeza Serikali kwa kuanzisha Mifuko hii kwa sababu Serikali peke yake isingeweza kugharimia matibabu ya wananchi wote Tanzania, lakini kwa kutumia mifuko hii, tutafika.

Kwa mfano, nawaomba Waheshimiwa Wabunge pamoja na Viongozi wengine, tuwahamasishe wananchi wetu katika kaya mbalimbali wajiunge na Mfuko wa Afya ya Jamii. Kaya moja ni Sh. 10,000/= na wanatibiwa kwa mwaka mzima. Tukichangamka, tukawahamasisha wananchi, nadhani tutaweza kufikia

lile lengo la asilimia 30 ifikapo mwaka 2015. Nchi ya Rwanda yenye wananchi milioni 11, asilimia tisa ya Wanyarwanda wana Bima ya Afya, nchini nyingine ambayo imejitahidi ni Ghana ambayo asilimia 50 ya wananchi wa Ghana wana Bima. Sisi bado tuko kwenye asilimia 16. Kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge tuwahamasishe wananchi wetu katika kaya mbalimbali waweze kuingia katika Mfuko wa Afya ya Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaomba Waheshimiwa Wabunge wajiunge na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya. Naomba ni-*declare interest* kwamba mimi ni Mwenyekiti wa Mfuko wa Taifa ya Bima ya Afya. Waheshimiwa Wabunge mkijiunga na Mfuko huu, mtatibiwa mpaka kufa. Hata msiporudi mwaka 2015 wale ambao hawatarudi, wataendele kutibiwa mradi watachagia kidogo kidogo. Kwa hiyo, ni mfuko muhimu sana, kwani mnaweza mkatibiwa mahali popote katika nchi hii. Kwa hiyo, naomba mchangamkie Mfuko huu, mjiunge na Mfuko na Bima ya Afya.

Pia naomba mhamasishe watoa huduma mbalimbali. Katika hospitali mbalimbali tumeanzisha mikopo yenye unafuu ya aina mbili. Ya kununua vifaa tiba na ukarabati wa hospitali. Naomba mwahimize watoa huduma katika sehemu zenu waweze kuchangamkia mikopo hii, waweze kukopa mikopo ya vifaa tiba na mikopo ya ukarabati. Ombi kwa Wabunge nimeshalitoa kwamba mjiunge na Mfumo wa Taifa wa Bima ya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekwenda kwa spidi kali kwa sababu nilijua nina dakika kumi tu lakini nilikuwa na mambo mengi ya kuzungumza, lakini nadhani nimejitahidi kuyagusia yote. Nakushukuru sana.

**TAARIFA**

**MHE. ALPHAXARD K.N. LUGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 68(8) naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge aliyekuwa anasema kwamba Mfuko wa Bima ya Afya na Mfuko wa Afya ya Jamii una matatizo makubwa; dawa ni matatizo, lakini wakati huo tena anasema anahamasisha Wabunge na wananchi wajiunge. Sasa nilikuwa nampa hiyo taarifa kwamba katika mazingira yale ambayo hiyo Mifuko ina matatizo, siyo rahisi tena kuwahamaisha watu wakajiunga. Nilikuwa naomba nimpe hiyo taarifa. *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ntukamazina unaikubali hiyo taarifa?

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, siikubali kwa sababu nilikuwa nazungumzia matatizo ya dawa kutoka *MSD,* siyo kwenye Mifuko hiyo.

**MHE. ADAN I. RAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba Mwongozo wako. Kwa mujibu wa Kanuni namba 68(7), muda mfupi uliopita katika eneo la Bunge, Kiongozi mmoja wa Chama cha CHADEMA ameongea na Vyombo vya Habari na kutaja Mafisadi

kwa majina wa *TANESCO*, lakini jambo la kusikitisha amewataja wale wa CCM tu, hakuwataja wa CHADEMA. Je, huo ni utaratibu? Naomba tu Mwongozo wako.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana nitatoa ufafanuzi baadaye kidogo.

**MHE. AZZA H. HAMAD:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii. Kwanza, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya ya kutosha na hatimaye nimeweza kusimama ndani ya Ukumbi wako huu nikiwa nina nguvu ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kuwashukuru wanawake wa Mkoa wa Shinyanga kwa sababu bila wao nisingekuwepo ndani ya Ukumbi huu. Nawaahidi kwamba sitawaangusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, niseme naunga mkono hotuba ya bajeti ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii kwa asilimia mia moja. Kwa sababu nisipounga mkono bajeti hii, ina maana hata ile huduma ndogo inayotolewa haitapatikana kabisa. Kwa hiyo, sioni sababu ya kutokuunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze na huu mpango wa kuzifanya Hospitali za Mkoa kuwa Hospitali za Rufaa. Hospitali ya Mkoa wa Shinyanga ina msongamano mkubwa wa wagonjwa. Kinachosababisha msongamano huu, Halmashauri za

Wilaya tatu hazina Hospitali za Wilaya. Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu ina Vituo vya Afya vinne, lakini haina Hospitali ya Wilaya. Matokea yake wagonjwa wote wanakwenda Hospitali ya Mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Manispaa, leo ndiyo nimesikia kwamba kuna Korandoto, lakini nakumbuka hata mwaka 2011 kwenye bajeti ilisomwa kwamba Korandoto itahudumia Manispaa ya Shinyanga. Lakini mpaka hivi tunavyoongea hakuna mishahara wala dawa zilizopelekwa kwenye Hospitali ya Korandoto. Nakumbuka Mheshimiwa Maselle kabla hajawa Serikalini, amejaribu kulisemea sana hili. Nitamwomba Mheshimiwa Waziri anieleze: Je, mwaka huu Hospitali ya Korandoto, itapelekewa fedha, madawa na mishahara kwa watumishi?

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Kahama ina Kata 55, lakini inaVituo vya Afya vitano na Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye suala la Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga. Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga ina Kata 26, Vituo vya Afya vinne vinavyotoa huduma. Sasa hivi imeanzisha ujenzi wa Vituo vya Afya vingine vinne kwa nguvu za wananchi, lakini imeanzisha ujenzi wa Zahanati 22 kwa nguvu za wananchi. Kinachonisikitisha, ule mpango wa MMAM, mwaka wa fedha 2011/2012 tunaomaliza sasa, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga ilipangiwa Shilingi milioni 171, lakini mpaka hivi tunavyoongea, hakuna hata Shilingi moja ambayo imekwishafika Halmashauri.

Katika Zahanati 22 zilizopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga zilizoanzishwa kwa nguvu za wananchi, Zahanati mbili ziko tayari zimekwishakamilika ambayo ni Mwasingu na Mwajiji katika Kata ya Eselamagazi. Kibali kilishatolewa na Serikali, lakini mpaka hivi tunavyoongea, hakuna mtumishi hata mmoja aliyepangwa kwenye Zahanati hizo. Hivi hii Sera tunayosema kwamba kila Kijiji kiwe na Zahanati, tutaifikia kweli? Kwa sababu kwa *style* hii, tunawavunja moyo wananchi ambao wamejitoa pamoja na njaa kubwa iliyoko Shinyanga, lakini tumesema afya kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini bado hatuoni Serikali inatusaidia nini. Zile Zahanati 20 zote ni nguvu ya wananchi, fedha ya MMAM hakuna hata Shilingi moja. Namwomba Mheshimiwa Waziri aniambie ni kwa sababu gani zile fedha zilizotengwa mwaka 2011 hazikuweza kufika katika Halamahsauri ya Wilaya ya Shinyanga? Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga imeanzisha ujenzi wa Hospitali ya Wilaya kwa nguvu za wananchi mwaka 2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri iliamua kuandika ombi maalum kwa sababu ujenzi wa hospitali hii gharama yake ni Shilingi bilioni 15, lakini ombi lile maalum lilikataliwa, wakaambiwa Halmashauri wanatakiwa wajenge wenyewe. Kinachonisikitisha zaidi, fedha za maendeleo zinazopangwa kwenye Halmashauri, haziji kama zilivyopangwa. Nitoe mfano. Mwaka 2011, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga ilipangiwa Sh. 1,470,356,000/= lakini fedha ambayo Halmashauri imepokea ni Sh. 511,367,132/=. Hivi katika

hali hii, hii hospitali ya Wilaya tunaijenga kwa *style* gani? Kwa fedha hiyo ambayo mmetupa?

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Halmashauri wa Wilaya ya Shinyanga wameanzisha kwa nguvu zao misingi ya nyumba tano za watumishi katika Hospitali ya Wilaya, Wodi ya akina mama, Wodi ya watoto, Wodi ya wanaume, nyumba moja ya mtumishi tayari imeshajengwa, jengo la *OPD* limekwishakamilika, lakini bado hatujaona Wizara wanatusaiida nini kwa hili. Sijui labda Wizara wanapendelea kuona Halmashauri zote za Shinyanga zinakwenda kutibiwa katika Hospitali ya Mkoa, sielewi. Naomba sana Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga itazamwe kwa macho mawili kwa sababu tumeshaonyesha dhamira yetu ni nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga ina Vituo vya Afya vinne ambavyo vinafanya kazi. Katika Vituo hivyo vya Afya, kuna Kituo Kimoja cha Afya, kinaitwa Kituo cha Afya cha Nindo. Kituo hiki cha Afya cha Nindo, kina jengo la upasuaji na lina vifaa vyote. Kinachonishangaza ni zaidi ya miaka minne leo, hakuna kazi inayofanyika kwenye lile jengo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba sana Wizara, iangalie, kwa sababu, Kituo hiki cha Afya, kiko Kata ile ile ambayo tunajenga Hospitali ya Wilaya. Basi waweze kutoa kibali, ili Hospitali ya Wilaya, ianze kutoa huduma kwenye Kituo cha Afya cha Nindo kwa sababu jengo la upasuaji lipo na vifaa vipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, msahau kwao ni mtumwa. Nitakuwa sijawatendea haki wananchi wa Tinde, kwa sababu, ndipo nilipokulia na ndipo ninapoishi. Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, ina Kituo cha Afya kinaitwa Tinde. Kituo hiki, kiko njiapanda ya kwenda Burundi, Mwanza na Dar-es-Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maisha yangu mimi nimekulia kwenye kile Kituo cha Afya kwa sababu, mama yangu alikuwa Mtumishi, alishastaafu, lakini majengo yale toka mimi naanza chekechea mpaka hivi ninavyoongea, ndivyo yalivyo. Ukikiona kituo kile cha afya ni sawasawa na *Dispensary,* siyo Kituo cha Afya. Kituo kile cha Afya kina watumishi 11 tu, lakini Kituo kile cha Afya kwa mwezi kinatoa huduma ya kuzalisha akina mama wajawazito mpaka 120. Kwa siku moja akina mama wajawazito wanaokwenda pale kupimwa ni 50 mpaka 60. Huduma za *OPD* kwenye kile Kituo cha Afya ni watu 50 mpaka 60. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Huko kuna shughuli kubwa huko! Mheshimiwa, endelea kuchangia.

**MHE. AZZA H. HAMAD:** Mheshimiwa Naibu Spika, inanisikitisha sana vifaa vya Maabara hakuna na jengo la kuhifadhia maiti hakuna. Hicho kinaitwa Kituo cha Afya, na ule tunasema ni Mji Mdogo wa Tinde. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo hiki cha Afya kinahudumia majeruhi wengi kwa sababu ya ajali za barabarani. Lakini inanishangaza sana na inanisikitisha sana kuona kwamba, Wizara na Serikali kwa ujumla,

haikiangalii Kituo hiki cha Afya. Naiomba sana Wizara kwamba, Kituo hiki cha Afya kinahudumia zaidi ya Kata 10, lakini ukifika pale, ni sawasawa na Zahanati. Hivi hata yule Daktari au Nesi, akimjibu vibaya mgonjwa, utasema amemwonea? Wale ni binadamu, inafika mahali na wao wanachoka. Kwa sababu, mtu mmoja kuhudumia watu 60 kwa siku, ni kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana na ninaisihi sana Wizara, ikiangalie Kituo cha Afya cha Tinde. Lakini kinachonishangaza zaidi na kunisikitisha, mpaka Kituo kinafikia kuzimiwa umeme miezi mitatu au minne kwamba watu wa Afya hawawezi kulipa bili ya umeme. Akina mama pale wanajifungua kwa tochi. Tumefikia hapo Watanzania? Ni bora kungekuwa hakuna umeme. Lakini umeme upo, tatizo ni kwamba, Afya, hawaendi kulipa zile bili za umeme. Inanisikitisha sana na ninasikia uchungu kwa sababu, ndiyo eneo ninalotoka mimi Mbunge wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Afya ya Jamii. Hata ukiangalia kwenye Hotuba ya Waziri, kwa Mkoa wa Shinyanga, Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga inaonesha imechangia kati ya Kaya 55,000 na Kaya 33,000 ndizo ambazo zimejiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii. Kinachokatisha tamaa wananchi wetu, hata washindwe wengine kujiunga na Mfuko huu wa Afya ya Jamii, wanapokwenda kupewa huduma katika Vituo vyetu vya Afya, dawa hazipatikani. Sasa mwananchi wa kawaida anakuuliza, kama ninachangia hiyo Sh. 5,000/= au Sh. 10,000/= halafu

ninafika pale naambiwa dawa hakuna, kuna sababu gani ya kuchangia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili naomba tulitizame kwa makini, lakini tuone kama tunawatendea haki wananchi hawa ambao wanachangia fedha zao kwa moyo mmoja, halafu huduma hawapati.

*(Hapa, kengele ililia kuashiria muda wa Mzungumzaji kwisha)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, ni kengele ya pili.

**MHE. AZZA H. HAMAD:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Lakini namwomba Mheshimiwa Waziri atembelee Mkoa wa Shinyanga, ajionee mwenyewe hali halisi. Naunga Mkono Hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Azza Hamad Hillal. Tunakushukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa, nina mzigo mkubwa sana wa miongozo, naomba niipunguze kidogo, maana naona kuna dalili za kuongezeka, sasa huu mzigo utanielemea. Naomba niipunguze kama ifuatavyo. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, kuhusiana na Hoja mbalimbali ambazo zimetolewa leo asubuhi, mtakumbuka kwamba, niliagiza kwamba, Kamati ya Uongozi, iende kujadiliana na kumshauri Mheshimiwa Spika, namna bora ya kushughulikia mambo

yaliyokuwa yamejitokeza leo asubuhi. Kwa kuwakumbusha, kulikuwa na Hoja ya Kwanza, iliyotolewa na Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, kwa mujibu wa Kanuni ya 47, ya kutaka Bunge, liahirishe shughuli zake zilizopangwa kwa siku ya leo ili lijadili jambo la dharura kuhusu mgomo wa Walimu, uliotangazwa kufanyika nchi nzima na Wabunge wengine pia walisimama kutaka kuwasilisha Hoja hiyo hiyo.

Wahesimiwa Wabunge, kwa hiyo, kuhusiana na hoja hii, Kamati ya Uongozi imejadiliana kwa kina na imeshauri kama ifuatavyo:-

Kwamba, Bunge haliwezi kuahirisha shughuli zake zinazoendelea ili kujadili suala la mgomo wa Walimu kwa sababu, jambo hilo tayari liko Mahakamani.

Kuhusu Hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Joshua Nassari ya kutaka Mheshimiwa Spika azivunje Kamati za Kudumu za Bunge nyingine, ukiacha ile ya Nishati na Madini, ambazo zinatuhumiwa kujihusisha na vitendo vya rushwa; Kamati ya Uongozi imejadili pia hoja hii na kuhusiana na ombi la Mheshimiwa Salum Khalfan Barwany, nataka kuiunganisha hapa kuhusu uamuzi wa Mheshimiwa Spika wa Jumamosi tarehe 28 Julai, 2012 wa kuivunja Kamati ya Nishati na Madini kwa tuhuma za kujihusisha na vitendo vya rushwa, uamuzi huo uende sambamba na kuwataja Waheshimiwa Wabunge wanaohisiwa kufanya vitendo hivyo. Kuhusu Mlongozo ya Waheshimiwa hawa wawili; Mheshimiwa Nassari na Mheshimiwa Khalfani, Kamati imerejea kwenye *Hansard* kuhusu uamuzi uliotolewa na

Mheshimiwa Spika, siku hiyo ya Jumamosi, ambapo baada ya kulipeleka jambo lile kwenye Kamati ya Haki, Kinga na Maadili ya Bunge, alielekeza kuwa, Kamati hiyo ifanye uchunguzi na kubainisha Wabunge wanaohusika na vitendo hivyo.

Kwa hiyo, katika eneo hili, Kamati hiyo inapewa kazi ya kufanya uchunguzi. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge watakaoitwa mbele ya Kamati hiyo, wanakwenda kuisaidia Kamati, kuelewa zaidi na ku-*establish* kama kuna suala la kujibu au vinginevyo. Isichukuliwe kwamba Mbunge yeyote atakayeitwa kwenda kwenye Kamati hiyo, tayari ni mtuhumiwa kwa hatua hii ya mwanzo. Baada ya hatua ya mwanzo, sasa yakiwepo majina ambayo kunahitaji kutajana, na kadhalika, basi hatua hiyo itafuatia. Kwa hiyo, hatua ya mwanzo ni hatua ya kuisaidia Kamati kuweza kufika mahali pa kuweza kufanya uchunguzi ambao imeombwa na Mheshimiwa Spika ifanye. Sasa ninaiagiza Kamati hiyo kufanya kazi hiyo mara moja na kwa haraka iwezekanavyo.

Waheshimiwa Wabunge, niwaambie tu kwamba, katika Kamati ile, Mheshimiwa Spika ataiangalia vizuri zaidi Kamati ya Maadili, kama kuna Wabunge ambao wana *conflict of interest* kama ambavyo baadhi mlikwishaeleza huko nyuma, hatua zitachukuliwa za kuhakikisha kwamba hawashiriki katika mchakato wa zoezi hili. *(Makofi)*

Na pia, nilifahamishe tu Bunge kwamba, Taasisi ya *TAKUKURU* imekuwa ikijishughulisha katika kuwahoji baadhi yenu, mnafahamu, na zoezi hilo linaendelea.

Kwa hiyo, na yenyewe inaendelea kivyake. Tusidhani kwamba Taasisi za Serikali zimenyamaza kwa upande wake. Kwa hiyo, na yenyewe inaendelea kivyake na wakati utakapowadia, basi itafahamika ni nini kitakachojiri.

Kuhusu Mheshimiwa Spika kuwataja wala rushwa, kama alivyosema Mheshimiwa Barwany; Mheshimiwa Spika, hawajui. Hata mimi siwafahamu. Kwa hiyo, kupitia mchakato huu wa hii Kamati yetu itakayofanya uchunguzi, ndio itakayobainisha, basi tunaweza tukafikia huko kwenye kutajana, na kadhalika.

Waheshimiwa Wabunge, Mwongozo kuhusu hoja ilitolewa na Mheshimiwa Habib Mnyaa kwamba Kamati ya Uongozi izingatie upya Ratiba ya Shughuli za Bunge ili Bunge limalize shughuli zake kabla ya tarehe 18 mwezi wa Nane, kwa lengo la kutoa fursa kwa Waheshimiwa Wabunge ambao ni Waumini wa Dini ya Kiislamu kusherehekea Siku Kuu ya Iddi inayotazamiwa kuwa tarehe 19 mwezi wa Nane, wakiwa majumbani kwao. Kamati ya Uongozi imelitafakari jambo hili na imekubaliana kwamba itarekebisha Ratiba ya Bunge. Itakaporekebisha, mtaletewa Waheshimiwa Wabunge, kwamba ni kwa ajili ya kuzingatia maoni ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na miongozo hiyo iliyokuweko, mingine iliyoongezeka tena, wakati wa Kikao cha asubuhi, na yenyewe, mmoja ulikuwa ni wa Mheshimiwa Kangi Lugola, kuhusiana na hujuma ya mitambo ya *TANESCO,* ambayo huenda ikawa inapikwapikwa na baadhi ya watu.

Nichukue fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Kangi Lugola kwa kututonya na kutueleza hapa Bungeni kuhusu tishio hilo. Kwa hiyo, Mwongozo wangu ni kwamba, naiomba Serikali ilifanyie kazi jambo hili na kuchukua hatua za kiulinzi na kiusalama zinazostahili, na mkiona inafaa, basi mnaweza kuleta taarifa hapa Bungeni kuhusiana na nini kinaendelea. Lakini kwa vile huwa hatujadili mambo ya kiulinzi na kiusalama, matarajio yetu ni kwamba, mtalifanyia kazi zinazopasa.

Kuhusu hoja ya Mheshimiwa Mnyika, alitaka Taarifa ya Kamati ya Huduma za Jamii, kuhusu Mgomo wa Madaktari ya wakati ule iletwe hapa Bungeni kwa ajili ya mjadala. Mwongozo wangu ni kwamba, Taarifa ile ilipokelewa kutoka kwenye Kamati husika ya Huduma za Jamii na Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika, akaipeleka kwenye Kamati ya Uongozi, ambayo inajumuisha Wenyeviti wote wa Kamati za Bunge, ikachambuliwa mle ndani na yakaorodheshwa mambo ya utekelezaji na mambo yale ya utekelezaji yalipelekwa Serikalini, na baadhi ya hoja zile zimeshaanza kufanyiwa kazi. Kwa vile jambo hili liko Mahakamani, kama ambavyo nimeeleza mara zote, basi hatukusudii tena kulifungua mjadala wake hapa Bungeni.

Nyingine ni hoja ya Mheshimiwa David Silinde, kwamba, katika Jimbo lake, kutokana na Mgomo wa Walimu, kuna wanafunzi wanaolala barabarani na fujo na vurugu za aina nyingine. Kama nilivyoeleza awali, jambo hili la mgomo wa Walimu liko Mahakamani. Kwa hiyo, hatuna nia ya kuendeleza mjadala wake hapa.

La mwisho ni Mwongozo ambao ulikuwa umeombwa na Mheshimiwa Rage muda mfupi uliopita kwamba, kuna Kiongozi mmoja, sasa hakumtaja ni nani lakini wa humu ndani kutoka Chama cha CHADEMA, kwamba, alikuwa anawataja baadhi ya watu kujihusisha na masuala ya rushwa, lakini anaowataja ni wa upande wa Chama Tawala peke yake.

Sasa Mwongozo wangu ni kwamba, kwa kweli, mimi ningewashauri Waheshimiwa Wabunge, katika jambo hili tuwe na subira na utaratibu kidogo. Ukiamua kulizungumza, basi ulizungumze kwa haki. Kwa sababu, tukishalifanya jambo hili kuwa ni la siasa za kuonesha kwamba ni *CCM* au ni CHADEMA au ni *CUF, NCCR,* na kadhalika, hatuna Chama cha Siasa chenye Sera ya rushwa. Hakipo! Kama kuna mtu amejihusisha na mambo haya, ni yeye mwenyewe. Kwa hiyo, ni vizuri kama tunaamua kuwataja ili wachukuliwe hatua hawa watu ambao wanajiingiza katika mambo ya rushwa, tuwataje tukijua kabisa siyo kwa sababu, tunamkomoa kwa sababu ya Chama chake wala chochote, ni kwa sababu, ni tabia ambayo sisi wote tunaikemea kabisa hapa Bungeni. Kwa hiyo, huu ndiyo Mwangozo wangu. *(Makofi)*

Tunaendelea. Sasa namwita Mheshimiwa Zabein Mhita, na Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa ajiandae.

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Awali ya yote, namshukuru *Allah Subhanah-wataala*, kwa kunipa afya njema na kuweza kusimama hapa leo ili kuweza kuchangia Hoja iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, naomba nichukue nafasi hii nimpongeze kwa dhati kabisa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Kaimu Katibu Mkuu, Kaimu Mganga Mkuu wa Serikali na Viongozi wote wa Wizara, kwa kutayarisha bajeti nzuri ya kisayansi na inayoweza kutekelezeka. Ni matumaini yetu basi kwamba, pamoja na bajeti hii nzuri, utekelezaji wake nao utafuata maandalizi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Jimbo la Kondoa Kaskazini, wamechangia sana katika ujenzi wa Zahanati na Vituo vya Afya. Lakini pamoja na juhudi zote hizo ambazo wananchi wamezifanya wakishirikiana na Mbunge wao, kuna upungufu mkubwa sana wa Watendaji katika Zahanati hizo, Vituo vya Afya na Hospitali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze na Hospitali. Hospitali ya Wilaya ya Kondoa, mpaka hivi sasa inahudumia pia wananchi wa Jimbo la Chemba, kwa Mheshimiwa Nkamia.

Mahitaji ya Hospitali hii ni Madaktari saba, lakini mpaka sasa kuna Madaktari watatu tu, ikiwa na upungufu wa Madaktari wane, na hawa, ni Wataalamu wa magonjwa ya wanawake, Mtaalamu wa magonjwa ya watoto, upasuaji na mtaalamu wa utoaji wa ile tuliyokuwa tunasema tangu zamani, nusu kaputi; hawa hawapo. Sasa je, Serikali ina mpango gani wa dharura wa kujaza nafasi hizo muhimu kwa huduma muhimu na za lazima, kwa wananchi wa Wilaya ya Kondoa na Wilaya ya Chemba?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende kwenye Vituo vya Afya. Wilaya ya Kondoa, ina vituo vitatu vya Afya, navyo ni Busi, Kisese na Mnenya. Kituo hiki cha Mnenya, kimepandishwa hadhi tangu mwaka 2011, lakini mpaka sasa hakijaanza kufanya kazi kwa sababu, kina upungufu wa Madaktari katika Kituo hicho. Naomba nioneshe mahitaji. Madaktari Wasaidizi, mahitaji ni madaktari watatu katika Vituo vya Afya, hakuna hata mmoja. *Clinical Officers* mahitaji ni 12, mpaka sasa wako wawili tu, upungufu ni madaktari 10. Wauguzi ama *Nurses* mahitaji ni 18, wako wanne tu kwa maana upungufu ni 14. Hali siyo nzuri. Je, Serikali, Mheshimiwa Waziri, babie mwali, Serikali, ina mpango gani wa dharura kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa ili kupata Wataalamu hao?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niende nizungumzie kuhusu Zahanati. Kuna Zahanati 21. Katika Zahanati hizi katika Jimbo la Kondoa Kaskazini, katika hawa *Clinical Officers,* mahitaji ni 42, wapo saba tu, upungufu ni 35. Wauguzi mahitaji yao ni 42, lakini wako sita tu, upungufu ni 36. Hali ni mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Zahanati 10 nitakazozitaja, Zahanati ya Mongoroma, Kingale, Itaswi, Masawi, Kolo, Kwadeno, Hebijuu, Bukulu, Chololo na Ata, zinasimamiwa na Wahudumu wa Afya. Hao ndio wanaozisimamia hizo Zahanati. Baadhi ya hizi Zahanati, hakuna Wauguzi. Hali ni mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama hata Wauguzi hawapo, sasa fikiria mama mjamzito anapokwenda kule, anahudumiwa na nani? Hali siyo

nzuri, na mimi nikiwa mwanamke najisikia vibaya sana. Wanasema uchungu wa mwana aujuaye mzazi na hasa mama. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Eeeh!

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Eeh! Nimezungumzia kuhusu Watendaji, lakini sasa naomba nizungumze tena, nirudi kwenye Hospitali ya Wilaya. Hospitali ya Wilaya ina *ambulance* moja ambayo imechoka sana na gharama za matengenezo ni kubwa mno. Halmashauri inatumia pesa nyingi kwa matengenezo. Mheshimiwa Waziri mimi nakuelewa wewe ni mtu mwelewa, na ni mtu msikivu. Hospitali ya Kondoa tunahitaji *ambulance* kusaidia wagonjwa. Kwa sababu hii *ambulance* ya zamani mara kwa mara inaharibika, wakati mwingine inakuwa hata ikibeba wagonjwa inaharibika njiani. Tafadhali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile hii Zahanati, *I mean* Kituo cha Afya cha Mnenia, nacho pia hakina *ambulance*. *Ambulance* inayotumika ni hiyo ya hosptali ya Wilaya. Kituo cha Afya Kisese tunasema kina *ambulance* lakini siyo *ambulance,* ni gari tu ya kawaida tu, ambayo ina viti kwa pande zote mbili, yaani siyo *ambulances as such*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri hali ya Kondoa ndiyo hiyo, siyo nzuri. Mheshimiwa Waziri alipokuwa Naibu Waziri alifika Kondoa kuzindua Mfuko wa Afya, wananchi wale walimwomba urudi tena kutokana na kazi nzuri ambayo aliifanya pale Kondoa. Walimkaribisha wakati ule alikuwa Naibu Waziri, sasa amekuwa Waziri, ndiyo

wakati muafaka. Naomba niwaambie watu wa Kondoa kwamba yule Naibu Waziri mliyemwalika sasa ni Waziri eeh! Tafadhali nakuomba katika Mkutano huu tuongozane mimi na wewe twende Kondoa, baada ya Ramadhani. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Na baada ya kibali cha Naibu Spika. *(Kicheko)*

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Twende pamoja. Labda tu pengine ningeomba niseme kwamba pia sitakuwa peke yangu, nitakuwa na Mbunge wa Kondoa Kusini - Mheshimiwa Juma Nkamia tutakuwa wote. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Aah!

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Twende tukakague hii hospitali, uone hali yake ilivyo, twende kwenye baadhi ya Vituo vya Afya na twende kwenye baadhi ya Zahanati ukaone hali halisi iliyoko kule. Hali siyo nzuri. Ningeomba uone mwenyewe madhila. Narudia, naomba uende ukaone madhila yanayowapata wananchi wa Wilaya ya Kondoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kawaida, sipendi kupigiwa kengele. Kwa mara nyingine tena, nawatakia Watanzania wote Ramadhani Karim. Inshallah. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi

niweze kuchangia siku ya leo katika Wizara hii ya afya. Awali ya yote, naomba niwatakie Waislam wote nchini Ramadhani Karim. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, afya bora na elimu ya afya kwa binadamu yeyote ndiyo chimbo na gurudumu la maendeleo. Lakini afya hii ambayo ninaizungumzia, sielewi kama ni mojawapo ya vipaumbele vyetu kwa sababu binadamu yeyote huwezi kufanya kazi bila kuwa na afya bora. Lakini sielewi kama vipaumbele hivyo vipo Tanzania katika Sekta hii ya Afya. Kwanini nasema hivyo? Kwa sababu Wizara hii ya Afya imetengewa bajeti ndogo sana. Ninashangaa, kwanini bajeti hii inazidi kushuka? Kwa mfano, katika *total development budget,* Serikali yenyewe imetoa *6.3 percent* na wafadhili ni *93.7 percent,* sasa sielewi kwanini tunategemea wafadhili zaidi ya asilimia 90. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunategemea hawa wafadhili zaidi ya asilimia 90, hili Azimio la Abuja kweli tutalifikia la asilimia 15? Tumesema hii asilimia 15 Azimio la Abuja *by 2015* ambayo imebakia ni miaka mitatu tu. Sasa sijui kama tutafikia, ningeomba Wizara husika kwenye ile *finance bill* inapofikia hili tuliangalie kwa makini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la mpango wa afya ya msingi. Naomba niipongeze Serikali kwa kuanzisha mpango huu, na ni kweli hii iko katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi, Ilani ya Uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile naomba niishukuru Serikali kwa kupandisha Kituo cha Afya cha Igawilo kuwa Hospitali ya Wilaya kule Mbeya. Naomba vilevile nitoe rai kwamba kuna Hospitali ya Kamsamba katika Wilaya mpya ya Momba, kwa kweli Kituo cha Afya cha Kamsamba ningeomba, pamoja na Isoko kule Ileje, vipandishwe Isoko iwe Hospitali Teule, Kamsamba iwe Hospitali ya Wilaya kwa sababu unaweza ukatoka Kamsamba kwenda Tunduma ni zaidi ya kilomita 200. Unaweza ukatoka Kamsamba kwenda Vwawa, ni zaidi ya kilomita 150. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunapozungumzia MMAM, sijui maana yake ni nini? Kwa sababu hospitali ziko mbali, huduma inakuwa ni shida. Lakini vilevile tukumbuke kwamba katika Tanzania zaidi ya asilimia 70 wanaishi vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba tu pia kuzungumzia suala la pale ninapotoka kwangu Mbeya. Kuna Hospitali ya Mkoa, kuna Wodi ya Watoto pale, kwa kweli imepangiwa bajeti yake, ni Shilingi bilioni moja na milioni mbili. Lakini hela zilizopatikana ni Shilingi milioni 130 tu na hili ni jengo la gorofa. Sasa sijui litajengwa kwa miaka mingapi? Ningeomba hili liweze kuangaliwa. Nikiwa hapo hapo katika mpango wa MMAM, mwaka 2011 Vituo vya Afya havikuzidi 37, Zahanati hazikuzidi 200. Sasa sijui tuna Mikoa mingapi? Tuna Wilaya ngapi? Tuna Tarafa ngapi? Tuna Kata ngapi? Tuna Mashina mangapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo ni lazima tujiulize, kwa sababu tunapozungumzia MMAM tunaweza

tukajikuta kwamba tuna majengo mengi, lakini vifaa tiba hakuna, watumishi hakuna, damu salama inakuwa siyo salama, kule Mkoani kwangu Mbeya hawa *Assistant Medical Officers* hakuna, *registered nurses,* Wakunga kwa kweli hawatoshi. Nilikuwa naangalia kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 224, hata ukiangalia lile jedwali inatisha. Hakuna kabisa, hawa niliowataja kule kwangu Mbeya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nieleze suala la afya ya mama na mtoto. Nampongeza Mheshimiwa Rais ambaye ni Mwenyekiti wa Afya ya Mama na Mtoto wa Umoja wa Mataifa. Hii ni sifa nzuri kwa nchi yetu ya Tanzania. Lakini vilevile tukumbuke kwamba hii ni nyezo muhimu sana, maana bila mama, hakuna familia na humu ndani wote tumezaliwa na akinamama. Kwa hiyo, lazima tuwape heshima yao. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Ndiyooo!

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Lakini ajabu ni kwamba, mwaka 2011 zilitengwa Shilingi bilioni 71 katika hii afya ya mama na mtoto. Mwaka huu imeshuka mpaka kwenye Shilingi bilioni 33.8, yaani ni punguzo la asilimia 53. Sasa mimi nashindwa kuelewa, hawa akinamama wanapata shida sana. Mama zangu kwa mfano kule Mbeya wanasafiri kwa mwendo mrefu sana, kule vijijini wanapotaka kujifungua wengine wanazalia njiani. Sasa hivi inakuwa ni hatari sana kwa akina mama, na mimi ukizingatia ni mwanamke ambaye pia nina watoto, ninaelewa uchungu wa kuzaa unakuwaje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, akina mama hawa wakati wa kujifungua kuna tatizo tunaita *PPH,* kutokwa na damu nyingi wakati wa kujifungua, na hii ni njia mojawapo pia inayosababisha vifo vya mama na mtoto kwa ajili ya kutokwa na damu nyingi sana wakati wa kujifungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ningeomba, maana Wizara ilikuwa na mpango kupitia *MSD*, kusambaza zile *clean delivery kit*, ikiwemo na ile *misoprostal* ambayo ni dawa pamoja na zile *delivery kit* anazopewa mama anapojifungua kwa ajili ya kupunguza hili tatizo la kutokwa na damu wakati wa kujifungua. Ningeomba Mheshimiwa Waziri anapojumuisha hapa, atueleze, Wizara ina mkakati gani katika suala hili la *delivery kit* pamoja na hii *misoprostal* kwa Tanzania, siyo kwa Mkoa wa Pwani na Dodoma tu kama ilivyokuwa imepangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tena niipongeze Serikali. Ukweli ni kwamba, inafanya jitihada sana ya kuongeza udahili wa fani hii ya Madaktari, lakini vilevile tukumbuke kwamba kwa mwaka tunazalisha Madaktari *almost 1000,* wanaoajiriwa siyo zaidi ya 100. Sasa naomba kuuliza, hawa wengine wanakwenda wapi? Serikali yetu hii ndiyo inayowasomesha?

Je, naomba kuuliza, Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anajumuisha atueleze ana mkakati gani na huwa inawa-*retain* vipi hawa Madaktari? Vilevile huwa inawa-*absorb* vipi hawa Madaktari? Vilevile tujue mikataba yao inasemaje? Ifike mahali iwe ni *pay for*

*performance* na iwe ni *cash on delivery* maana hii itasaidia kuongeza huduma mahospitalini na vilevile kuongeza ufanisi wa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kuhusu UKIMWI. Tunapozungumzia kwamba UKIMWI ni janga la Taifa, mimi sielewi kama kweli UKIMWI ni janga la Taifa. Kwanini nasema hivyo? Iweje bajeti ya UKIMWI imetengewa *zero*? *Zero* bajeti! Hivi hii inakuingia akilini kweli! Hapo hapo bado tunaita UKIMWI eti ni janga la kitaifa. UKIMWI utatoweka vipi endapo sisi wenyewe tunaipangia bajeti hii *zero? (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anajumuisha atueleze, maana kuna *NSP* katika Wizara ya Afya, na vilevile tuna *TACAIDS* katika Ofisi ya Waziri Mkuu na zote hizi zinashughulikia masuala ya UKIMWI na kwa bahati nzuri mimi mwenyewe Sekta ya Afya nimetoka huko ni mdau. Kwa hiyo, ningeomba tuelezwe kwa sababu wote wanashughulikia UKIMWI, *TACAIDS* UKIMWI, *NASP* UKIMWI, lakini wakati huo unashangaa unakuta kwamba *NASP* inakuwa kama ni *dormant* hivi, *TACAIDS* ndiyo inakuwa *active.* Wote ni watoto wa baba mmoja, wa mama mmoja. Kwa hiyo ningependa nielezewe kwa faida pia na ya Watanzania wote, wajue kwamba suala la UKIMWI linashughulikiwaje na linapewa mikakati gani na suala la *NASP* na suala *TACAIDS* vilevile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa sijatenda haki nikikaa hapa bila kuzungumzia suala la *MSD.* Kabla sijawa Mbunge, na bahati nzuri nimetoka kwenye

Sekta ya Afya; suala la *MSD* limekuwa ni tatizo ambalo halina *solution* kwa miaka yote. Tangu nimekuwa Mbunge, suala la *MSD* ni tatizo. Wengi wamezungumza; tatizo ni mfumo au ni nini? Naomba hili jambo lifike mahali iwe ni mwisho hadithi za *MSD* na matatizo ya *MSD*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niunge mkono hoja kwa asilimia 100 nisingongewe kengele ya mwisho, lakini niliyozungumza yafanyiwe kazi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. CLARA D. MWATUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii nami angalau nichangie mawili, matatu. Sana itakuwa ni maombi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nizungumzie juu ya wafanyakazi wa hospitali ambao ni katika Wizara hiyo ya Afya. Ni jambo la kusikitisha kwamba kulikuwa na tamko la kusema kwamba kila kijiji kinatakiwa kiwe na Zahanati. Zahanati hizi zikijengwa, watahudumia akina nani? Kwa sababu mpaka hivi watumishi ni wachache. Sasa hawa watakaokaa katika vijiji watawahudumia nani? Haitakuwa tu kama Shule za Sekondari za Kata ambazo zimekuwa kama uyoga wakati wahudumu, Walimu mle hawatoshi, hawapo kwa ujumla. Sasa naomba Serikali iangalie hilo. Hivyo vijiji vitapata Zahanati? Hata kwa kujitolea wananchi wanaweza kujitolea, zikajengwa, lakini wafanyakazi basi wapelekwe, wasomeshwe wengi ili waende wakahudumie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, katika hospitali zetu, kero kubwa ni mambo ya madawa. Dawa hazipatikani kwa urahisi. Kwa asilimia 99, madawa ya magonjwa tukanunue madukani. Wakati huo ukiangalia hali zetu tulio wengi, maana katika nchi hii walio wengi ni wale walalahoi wenzangu na mimi. Uwezo wa kupata hela za kwenda kununua dawa hawana, au hatuna. Kwa sababu bei zenyewe za dawa ni ghali ambazo hazikamatiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali, hizi dawa wanazopata hawa wenzetu wanaouza, Serikali nayo ichukue jukumu hilo kuweka mahospitalini ili wanyonge wapate kutibiwa pale. Kwa sababu utakuta mgonjwa akienda hospitali, cheti achukue mwenyewe, atatoa gharama ya cheti, lakini wakati huo huo yatakayoandikwa pale kuchunguzwa na daktari, dawa nenda dukani. Sasa si afadhali basi iamuliwe watu mkiumwa nendeni madukani? Kwa sababu hakuna faida ya kupoteza senti tano yake kwenda kununua kwanza huduma ya kuandikiwa cheti wakati dawa hatapata pale. Serikali iliangalie hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli suala la UKIMWI, pamoja na kwamba wanasema ni janga la Taifa kama alivyosema mwenzangu, mimi sioni kwamba ni janga la Taifa. Maana lingekuwa ni janga la Taifa lingetiliwa maanani, Serikali ingeng'aza macho pale na kuona kwamba wagonjwa hawa wanaangaliwa vilivyo, wanapata huduma ambazo wanapaswa wazipate. Walio wengi wamekwenda kuharibikiwa katika kutafuta maisha. Hali ya uchumi ni ngumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa dawa zinapokwenda kule zikauzwa ghali, nimesikia juzi juzi kwamba dawa sijui inayoongeza muda zaidi kwamba zimepatikana, lakini bei siyo za kukamatika. Sasa sijui Serikali itachukua hatua gani kutatua tatizo hili ili wale wenye hali ya chini wapate matibabu hayo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile mwanzo ilipotolewa utaratibu wa ushauri nasaha kwa watu hawa, walikuwa wanapata huduma kwenye vituo vile, walikuwa wengine wanarudi na vijisenti vya kula walikuwa wanapewa, lakini siku hizi yale hayapo. Pesa zinazotolewa na wafadhili, sijui zinazotolewa nchini, zinaishia kwenye Masemina! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naiomba Serikali ione umuhimu wa kutumia pesa zile zinazotolewa kwa ajili ya kitengo, zitumike kwa ajili ya kuwasaidia hao wagonjwa. Pamoja na hayo, hawa wafanyakazi walio wengi hawana nyumba pale wanapofanyia kazi. Sasa mishahara yenyewe tunaijua, ndiyo hii inayoliliwa. Sasa unapompa kazi ya kusema apange nyumba kwa mshahara ule mdogo kwa kweli unampa mzigo mzito, kwani kuna tatizo gani wakijengewa nyumba hizi za kawaida walizozizoea ziwe za miti?

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu nyingi hivi sasa watu wameelimika kiasi kwamba wakiambiwa wafyatue matofali wananchi wenyewe, Serikali isaidie juu, ili mradi wameshapata majumba; kwa kweli wakipata nyumba angalau kidogo watafutia machozi kwamba tumepata nyumba, tunashukuru, waweze kuipenda kazi hii. Nafikiri siyo jambo geni hilo

kulalamikiwa juu ya nyumba za Serikali za wafanyakazi wa afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu nyingi katika hospitali au Zahanati, mpaka hivi sasa watumishi waliopo pale, yaani wengine ni wale ambao walisoma miaka ya arobaini na saba, wenzangu na mimi. Sasa madawa kila leo yanakuja aina nyingine mpya. Sasa kama hawapati elimu mara kwa mara, ina maana wanabaki pale pale. Zinavyokuja dawa mpya, ndiyo kule kwenye kuhatarisha maisha ya wagonjwa. Hivyo, naomba iangaliwe, wale walioanza kazi zamani au waliosoma zamani wapelekwe wakapate misasa ili waendane na wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua wazi kwamba mpishi anashiba jikoni. Hawa wahudumu walio wengi dawa hizi mimi naamini kabisa zinakwenda. Yaani hizi kidogo zinazokwenda, lakini zikifika, kwa mfano ukipeleka tarehe moja halafu ukienda tarehe tatu dawa hazipo, lakini wakati huo huo majumbani humo dawa zinatolewa. Sasa hawa, nasema hawafanyi makosa. Ndiyo ule ule utaratibu wa mpishi kushiba jikoni. Tutafute njia ya kukomesha hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli bado nalia na watu hawa. Nakumbuka siku moja nilielezea kwamba Hospitali ya Ndanda ni Hospitali ya *Mission,* na ni hospitali ambayo inashughulikia au inahudumia watu wengi karibu Mkoa mzima wa Mtwara, ni hospitali ya Ndanda na wengine wanakwenda Lindi katika Hospitali ya Bilgita, ya mtu binafsi. Sasa wafanyakazi wa Hospitali ya Ndanda ni wachache, kwani wengi

wametoka pale, wamekwenda Serikalini. Pale unavyojua, *mission* hawana pesa, kwa hiyo, mishahara inakuwa midogo, wanakimbia. Sasa naomba Serikali iangalie kuwapeleka watumishi pale watakaohudumiwa na Serikali kulipwa mishahara. Ninasikia waliambiwa ile hospitali, yaani Wamishenari waliambiwa kwamba itakuwa Hospitali ya Rufaa, lakini mpaka leo sijui utaratibu huu unakuwa upo au umekwenda vipi! Hapo sina uhakika. Hivyo naomba watazamwe.

Vilevile nilifikisha maombi ya waliofanya kazi mwaka 2004 kipindi cha kipindupindu kilichozuka wakaweka Makambi Ndanda na sehemu nyingine katika Tarafa ya Chikundi. Sasa watumishi wa Serikali walilipwa, lakini hawa Wamishenari hawakulipwa ipasavyo, yaani walilipwa sijui Sh. 50/= kutoka hapo waliahidiwa watapewa nafikiri litakumbukwa hilo. Sasa wamekuwa wanadai malipo yale mpaka leo wananichosha, mama lakini vipi huko? Unatufikishia ujumbe wetu? Narudia tena kuwasilisha hilo, mwaangalie wale walioshughulikia matibabu kuwatibu wagonjwa wakati wa kipindupindu. Tunawategemea sana. Sasa tukiwanyanyasa hivi sasa, maana wameshajiona kwamba wamenyanyaswa, kwa sababu watumishi wa Serikali wameshalipwa, lakini hawa mara utuletee *cheque number* na kadhalika lakini mpaka leo hakuna kinachoendelea. Naomba Serikali au Wizara iliangalie hilo.

Kwa kweli, sina mengi zaidi, labda niende kwenye huduma za wazee na akina mama wajawazito ambao waliahidiwa kwamba watatibiwa bure na watoto. Sijui

kama kuna zinakofanyika hizo, kwani tukisema tu kwamba tuache na watu waendelee kutibiwa kwa pesa hizo hizo si bora kuliko kuwadanganya na kuwapa matumaini kwamba wazee watakwenda kutibiwa? Naomba kama ilikuwa nia kweli ya kuwahudumia, basi tuanze hilo ili mambo yaende sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa na hayo machache, pamoja na mengi ya kusema pengine niwaachie na wenzangu, lakini mimi niishie hapo. Ila naomba Serikali iangalie haya niliyoyasema. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mama yetu Clara Mwatuka. Sasa namwita Mheshimiwa Malole - Mbunge wa Dodoma Mjini, hapa tulipo, atafuatiwa na Mheshimiwa Meshack Opulukwa.

**MHE. DKT. DAVID M. MALLOLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika hotuba ya Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wizara hii ninayo maagizo na maombi mengi ambayo nimepewa na wananchi wa Jimbo la Dodoma Mjini. Kadri Mji unavyozidi kupanuka, ndivyo idadi ya watu inavyozidi kuongezeka sana na msongamano wa wagonjwa unazidi kuwa mkubwa sana katika Hospitali ambazo zipo katikati ya Mji. Dodoma inategemea zaidi Hospitali tatu, yaani Hospitali ya *General* ambayo ndiyo Hospitali Juu, lakini pia ipo Hospitali ya Makole na tatu ipo Hospitali Teule ya St. Gema.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Hospitali ya *General,* watu wamezidi kuwa wengi na matatizo makubwa yamezidi kuwa mengi kwa upande wa akina mama. Kuna msongamano mkubwa sana wa akina mama. Hospitali ilijitahidi miaka ya nyuma kupanua huduma kwa kuweka sehemu ambayo wanaiita Chikande. Sehemu ya Chikande haina Madaktari wa kutosha, inapata matatizo makubwa, miundombinu yake ni mibovu sana, akina mama wakienda wanaambiwa wajitegemee wenyewe kwa chakula, hakuna majiko, hakuna bafu na wanapata taabu kubwa sana kwa upande wa vyoo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya *General* imejitahidi kwa upande mwingine kuanzisha majengo mapya, lakini wamefika hatua wamekwama, hawana fedha za kutosha za kuweza kumalizia majengo yao. Jambo hili ni la kusikitisha sana. Naomba sana Wizara yako ikae karibu sana kuweza kuiangalia hospitali hii kuu kwa sababu ndiyo hospitali pekee ambayo inategemewa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuona kwamba hawana miundombinu ya kutosha, tumeweza kupata Hospitali ya Makole. Hospitali ile hata yenyewe ina msongamano mkubwa sana wa wagonjwa. Bado hata hivyo matatizo makubwa yapo kwa upande wa akina mama. Halmashauri ya Dodoma Mjini imejitahidi sana kupanua Hospitali ya Makole, lakini kama mnavyofahamu, Halmashauri zetu sasa hivi hazina fedha za kutosha. Halmashauri imeshindwa kabisa kukamilisha upanuzi wa majengo ya Hospital ya

Makole. Msongamano ni mkubwa na wagonjwa wengi wanalala chini badala ya kulala kwenye vitanda kama inavyotegemewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuona matatizo makubwa ya upungufu wa hospitali katika Mji wa Dodoma, Mheshimiwa Rais wetu mpendwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete ametuonea huruma kuteua Hospitali ya Mtakatifu Gema iwe ndiyo Hospitali ya Wilaya, wakati huo tukiwa bado tunasubiri ujenzi wa Hospitali ya Ilazo ambayo ndiyo itakuwa Hospitali ya Wilaya. Hospitali ya Ilazo mpaka dakika hii bado haieleweki. Bajeti inavyokwenda, haionyeshi kuwa itajengwa lini ili kupunguza msongamano huo. Lakini pia katika Hospitali ya Mtakatifu Gema ambayo Mheshimiwa Rais ameitamka kuwa Hospitali Teule ina matatizo makubwa na mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo mojawapo ni kucheleweshewa mgawo wa dawa. Wagonjwa wanapokuwa wanakwenda hospitali, wakati mwingine dawa zinakuwa pungufu kwa sababu wanashindwa kuzipata kwa wakati. Lakini jambo lingine walikuwa wameomba waongezewe Madaktari. Madaktari bado ni matatizo. Zipo Idara nyingi na nzuri sana na watu wanajitahidi sana kufanya kazi usiku na mchana, lakini kuna upungufu wa wafanyakazi upande wa *X-ray* na upande wa Maabara. Hospitali ina mashine za kisasa hata za kupimia Saratani, lakini mpaka dakika hii mashine hizi zipo zimekaa hazifanyi kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna Wataalamu ambao wanaweza kupelekwa kisha wakasaidia ili

mashine ziweze kufanya kazi. Lakini cha kusikitisha zaidi ni kwamba, hata hospitali inapoweza kujitahidi kuweza kuwapa *training* watu wao wenyewe ikiwa ni pamoja na Masista, bado walipokuwa wamemaliza mafunzo yao Masista wale wamechukuliwa na kwenda kufanya kazi kwenye Hospitali za Serikali, hivyo kufanya hospitali hii wakati wote kuwa na upungufu mkubwa sana kwa upande wa wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiongozi wa Hospitali ya Mtakatifu Gema ambaye ni Sista Gema mwenyewe pamoja na Jumuiya ya Hospitali na wagonjwa mbalimbali ambao wamekwenda pale, mimi mwenyewe nimeweza kuwatembelea na kuwaona. Wana kilio kikubwa sana. Wanaomba hasa Madaktari ambao wamepewa mafunzo na hospitali, Serikali iwarudishe kwenye hospitali ya Mtakatifu Gema ambayo ni hospitali teule ili waendelee kutoa huduma nzuri na inayojitosheleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nalileta ombi hili kwenu na naomba kabisa mlizingatie na nitashukuru sana katika majumuisho yenu kama mnaweza kuweka wazi kwamba Wizara inafanya jitihada kiasi gani kuweza kuona kwamba Hospitali Teule ya Mtakatifu Gema inapewa huduma zote zinazostahili kwa sababu mpaka dakika hii ndiyo inayopokea mzigo mkubwa sana wa wagonjwa kutoka Hospitali Kuu ya *General*. Nafikiri *point* ipo wazi *rationale*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na yote hayo, kuna Kituo cha Afya ambacho kimejengwa hapa siyo mbali sana kutoka hapa kwenye eneo ambalo linaitwa

Kikombo. Watu wa Kikombo wanaishukuru Serikali kwa jitihada kubwa ambayo mmefanya ya kuwajengea Kituo cha Afya. Wanasema kwamba wanapenda kuwafahamu viongozi wao, yaani Mawaziri wao wa afya, angalau Waziri; aidha, wewe mwenyewe binafsi au Naibu wako, wanawaomba mwende mkafungue kile Kituo cha Afya ili wapate kuwashukuru kikamilifu kwa kazi nzuri ambayo mmewafanyia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa haya machache ambayo nimeyasema, lakini naomba tu niseme kwamba, kwa kazi nzuri ambayo mmeifanya na ili mambo yote haya yaweze kwenda vizuri, mwangalie hospitali ya *General*, Makole na St. Gema, kwani wananchi wote wamenituma kuwa ili mpate nguvu ya kutosha na kuweza kuona umuhimu, niunge mkono hoja ya Wizara hii katika bajeti yake ili iweze kupitishwa na ili muweze kuuangalia upungufu wote uliopo katika hospitali hizo tatu na muweze kuwasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waswahili huwa wanasema, mmulika nyoka huanzia miguuni. Kama lipo tatizo, uanzie mahali ambapo wewe upo. Lakini bado wengine pia wanasema ukarimu huanzia nyumbani. Natambua kwamba ninyi mnaongoza hospitali zote na maeneo yote ya afya nchi nzima mnayoongoza, na mmeombwa kwenda maeneo mbalimbali ili kwenda kuangalia hali ilivyo.

Kwa vile Serikali yote ipo hapa Dodoma Mjini, na hapa tunahesabu kama ndiyo nyumbani kwa wote, yaani Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Mawaziri na Serikali nzima ipo hapa, basi ninawaomba

mtengeneze karatiba kadogo tuweze kuzungukia Hospitali ya *General*, Hospitali ya Makole na Hospitali ya St. Gema na tuone upungufu wake. Maana watu wanasema, kuona ni kuamini au *seeing is believing*, muweze kuona upungufu uliopo na baadaye kwa vile hapa ndiyo nyumbani, muweze kuweka kipaumbele kikubwa katika kuona kwamba mnazihudumia hospitali hizi kwa ukaribu zaidi ili kweli tuweze kuona kuwa mmeona umuhimu huo, kabla hamjaanza safari za kwenda mbali sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru sana. Kwa haya machache, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia ili muweze kutuinua hapa Dodoma. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. David Malole Mbunge wa Dodoma Mjini.

Waheshimiwa Wabunge, nimeletewa ombi maalum hapa ambalo na mimi nitalipeleka kwa Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club* - Mheshimiwa Idd Azzan, kama akilikubali la kuomba mchezo huu ujumuishwe katika michezo ya *Bunge Sports Club*. Waombaji ni wawili, yaani Mheshimiwa Vincent Nyerere na Mheshimiwa Peter J. Serukamba.

Mheshimiwa Wabunge, wanaomba katika michezo ya *Bunge Sports Club* ujumuishwe na mchezo wa ngumi katika mapendekezo yao na wanapendekeza kwamba timu zitakazocheza ziwe ni pande mbili, yaani upande wa Upinzani na Chama Tawala na wanapendekeza wachezaji kama

ifuatavyo kwa mechi za mazoezi kwanza, Mheshimiwa Said Nkumba - Chama Tawala, atapambana na Mheshimiwa John Mnyika; Mheshimiwa Frederick Werema atapambana na Mheshimiwa Tundu A. M. Lissu; Mheshimiwa Jenista J. Mhagama na Mheshimiwa Rachel Mashishanga; Mheshimiwa Ally Mohamed Keissy na Mheshimiwa Mustapha Akunaay; Mheshimiwa Moses Machali na Mheshimiwa Sylvester M. Mabumba na wachezaji wengine wanapendekezwa. Kwa hiyo, Mwenyekiti ataangalia kama atakubali, basi atanishauri ipasavyo. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa namwita Mheshimiwa Meshack Opulukwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Tundu A. Lissu.

**MHE. MESHACK J. OPULUKWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza napenda sana kuchukua nafasi hii angalau nami niweze kuchangia kuhusu bajeti hii ya Wizara ya Afya. Pamoja na kufurahishwa sana na mechi zinazokuja, lakini ningependa pia na mimi niweze kupangiwa mtu wa kucheza naye katika mechi ya ufunguzi ili basi mambo yaweze kwenda vizuri. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kujikita sana kwenye Wilaya yangu ya Meatu kutokana na ufinyu wa muda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kuna Wilaya au Halmashauri ambazo zina upungufu sana wa Vituo vya Afya ni pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Meatu. Halmashauri ya Wilaya hii kama zilivyo Halmashauri

nyingi, ina hospitali moja, lakini Halmashauri ina Kata 25 na katika Kata hizi 25 kuna Vituo vya Afya viwili tu na kuna Zahanati 46 kwenye vijiji vinavyotengeneza Halmashauri nzima, yaani vijiji 100. Kwa hiyo, kuna upungufu wa Zahanati 54.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua kwamba kuna matatizo ya fedha katika bajeti tuliyonayo, lakini angalau kwa kuanzia tungeweza kuongeza Vituo vya Afya japo vingine viwili ili angalau tuweze kuongeza Kituo cha Afya kwenye Kata ya Mwabuzo na katika Kata ya Mwabuzo itaweza ku-*save* Kata ya Mwamalole, Kata ya Imalaseko pamoja na Kata ya Mwamanongo. Hizi Kata zipo mbali sana na kuhudumiwa na Hospitali ya Wilaya ni takribani kilomita 60. Sasa iwapo kama tutaweka Kituo cha Afya au kitaanzishwa au kitafunguliwa katika Kata ya Mwabuzo, basi angalau Kata nyingine ambazo nimezitaja zitafaidika na huduma hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naishauri Wizara ianzishe Kituo kingine cha Afya kwenye Kata ya Sakasaka kwenye Jimbo la rafiki yangu Mheshimiwa Mpina ili tuwe na Vituo vya Afya vinne ili angalau watu wetu waweze kupata huduma bora ya afya na afya zao ziimarike.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na uchache wa Vituo vya Afya lakini bado tuna upungufu wa watumishi. Watumishi tulionao wa Idara ya Afya au Sekta ya Afya, Meatu wapo 217 tu wakati mahitaji ni 722. Kwa hiyo, watumishi wanao-*save* katika Sekta hii

kwa Meatu ni 30% tu na 70% inakwenda bila kuwa na wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na dhamira nzuri ya Serikali kuajiri watumishi wengine katika Idara hii ya Afya, katika kitabu cha bajeti ukurasa wa 246 nilikuwa naangalia watumishi ambao tayari vibali vilikwishatoka na walikwishaajiriwa na Halmashauri. Inaonekana kwamba kuna watumishi 29 ambao waliajiriwa kuanzia mwaka 2011/2012 hawajaripoti na hawajulikani wako wapi mpaka sasa? Kwa kuwa sasa hawa watu wanahitajika ili kuweza kutoa huduma katika Wilaya ya Meatu, nilikuwa naishauri Wizara ili sasa iweze kutoa idhini, basi ikiwezekana kwa Halmashauri yenyewe ili iajiri hawa watu ili kuanza kazi na kupunguza lile pengo la watumishi ambapo ni asilimia 30 tu wanaofanya kazi katika Halmashauri ya Meatu.

Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri wakati anafanya majumuisho, alizungumzie hili, kama kuna uwezekano, kwa sababu watumishi wameajiriwa, lakini hawakuripoti zaidi ya watumishi 29, basi Halmashauri ipate hayo mamlaka ya kuweza kujaza zile nafasi ambazo zipo wazi ili angalau watu wetu waweze kuhudumiwa kama ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna tatizo lingine katika Hospitali yetu ya Wilaya ambapo kuna vifaa kama *X-ray* pamoja na *generator*. Wizara ya Afya ilianzisha utaratibu wa Mkandarasi kuhudumia vifaa vyote kama vile *X-ray* nchi nzima ambapo Kampuni hii inajulikana kama *MOCAS*. *Generator* letu katika Hospitali ya

Wilaya ya Meatu limeharibika tangu mwezi Aprili, 2012 na hao wapo *supposed* kutembelea hospitali zote au Vituo vyote vya Afya kufanya *services* kwa *quarter* angalau mara moja. Lakini tangu mwezi Aprili, 2012 wameitwa hawajafika, *generator* ni mbovu, hakuna kinachofanya kazi ipasavyo. Naiomba sana Wizara ili basi iweze angalau kutoa maelekezo kwa Kampuni hii ya *MOCAS* ije ku-*service generator* letu ambalo ni bovu tangu mwezi Aprili, 2012 ili wananchi wetu wapate huduma kama ambavyo wananchi wengine wanapata katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la *ambulance* ambazo zipo kwenye Wilaya ya Meatu. Sisi tumebahatika kuwa na *ambulance* tatu, na katika *ambulance* hizi tatu, na kwa kuwa tuna Vituo vya Afya viwili vinafanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa namshauri Mheshimiwa Waziri kwamba ni vizuri sasa Vituo vya Afya viwili ambavyo ni Bukundi pamoja Kituo cha Mwandoya vipewe angalau kila moja *ambulance* moja na ile moja iweze kubaki Makao Makuu ya Wilaya ambapo ndipo hospitali inapopatikana. Lakini tatizo ambalo limekuja ni kwamba *ambulance* haziwezi kupelekwa kwenye Vituo hivi vya Afya kwa sababu hakuna ulinzi wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Wizara na naishauri Serikali kwamba, kama *issue* ni ulinzi wa kutosha na wananchi wanahitaji kupata hii huduma ambayo ni muhimu sana ya *ambulance,* basi Wizara iangalia uwezekano wa kujenga uzio katika Vituo vya

Afya hivi viwili cha Mwandoya pamoja na cha Bukundi ili *ambulance* hizi ziweze kupelekwa na watu wasaidiwe kwa sababu ni huduma muhimu sana. Kwa mfano, kama *ambulance* itapelekwa kwenye Kata ya Bukundi itaweza kusaidia pamoja na Kata nyingine tano ikiwemo Kata ya Mwangudo, Kata ya Mwanjoro, Kata ya Nkoma, Kata ya Kimali, pamoja na Kata yenyewe ya Bukundi. Hawa wananchi wanahitaji hii huduma kwa sababu ni huduma muhimu sana. Huo ni upande wa *ambulance* kama chombo cha kuweza kusafirisha wagonjwa kwa *emergence*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kuna gari la chanjo ambalo lilinunuliwa mwaka 1996. Ni gari la zamani sana na ni gari ambalo limechakaa na utendaji wa kazi sasa unazidi kupungua. Lakini kwa kuwa sasa Wizara ina mpango wa kuweza kufikia watu wengi sana, kwa mfano, ukiangalia kwenye ukurasa 125 kwenye Kitabu cha Hotuba cha Bajeti ambayo imewasilishwa na Mheshimiwa Waziri, inasema ni mkakati wa kufikia kila Wilaya, kila mtoto hususan katika Wilaya zilizo na kiwango kidogo cha chanjo. Lakini sasa tukichukulia upungufu wa gari hili ambalo limekaa kwa muda mrefu limekuwa ni gari chakavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa namwomba Mheshimiwa Waziri ili basi kama kuna uwezekano wa kuangalia kwenye maeneo mengine iweze kupatikana gari kwenye hospitali yetu au kwenye Wilaya yetu au kwenye Halmashauri yetu ili basi angalau hili suala la chanjo lifike kwa watu wengi zaidi na watu wetu waweze kupata huduma hii ambayo wanahitaji sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna fedha ambayo ilitengwa kwenye bajeti ya mwaka 2011/2012 zilikuwa ni Shilingi milioni 165 ambayo ilikuwa ni kwa ajili ya MMAM, lakini bahati mbaya sana hii Shilingi milioni 165 haikuja hata Shilingi moja kwenye Halmashauri yangu ya Wilaya ya Meatu, na hii Shilingi milioni 165 ilikuwa imegawanywa katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza, ilikuwa kwa ajili ya *OPD* ambapo ilikuwa ni Zahanati sita ambapo ilikuwa inatakiwa kutumika kiwango cha fedha kutoka Shilingi milioni 165, lakini na fedha nyingine ilikuwa ni kwa ajili ya *solar system* kwenye Zahanati ambazo ni 24.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naiomba Wizara, hizi fedha ambazo hazikutolewa kwenye bajeti iliyopita, basi ziweze kutolewa ili Vituo hivi vya Afya kwenye *OPD* pamoja na *solar sytem* kwa ajili ya zahanati zetu ziboreshwe na huduma ziweze kupatikana na wananchi wengi waweze kupata huduma kulingana na mahitaji waliyonayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, napenda kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuanzisha utaratibu wa kucheki afya kwa hiari alipokuwa pale Jangwani kipindi kilichopita, aliweza kucheki afya yake kama ipo sawa au haiko sawasawa.

*(Hapa kengele ya pili iligongwa kuashiria muda wa Mzungumzaj kwishai)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nakushukuru sana. Mheshimiwa Tundu Lissu.

**MHE. TUNDU A. M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kupata nafasi hii ya kuchangia hoja hii ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijazungumza masuala yaliyopo mbele yetu, naomba tu niseme kwamba gazeti la Mwanahalisi limefungwa leo, na kwa wale ambao wanafahamu ujasiri *(investigation Journalism)*, wale ambao wamejihusisha na gazeti hili siku zote, leo ni siku ya giza katika suala la Uhuru wa Vyombo vya Habari. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tundu Lissu hoja iliyopo mbele yetu ni Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

**MHE. TUNDU A.M. LISSU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa hiyo, ninachotaka kusema ni kwamba kilichotokea kibatilishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nizungumze masuala ya afya. Suala la uwekezaji katika Sekta ya Afya ni suala la maendeleo. Hakuna Taifa linaloweza kuendelea kama haliwekezi katika Sekta ya Afya. Kiwango cha uwekezaji katika kutengeneza wataalam, katika kujenga hospitali, na miundombinu ya afya ni kiwango hicho hicho kitakachoamua kama mnasonga mbele kama jamii au la.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa katika bajeti yetu tunayoijadili sasa hivi, Serikali inapendekeza Bunge hili Tukufu litenge Shilingi bilioni 80.5 kwa ajili ya kununua madawa na vifaa vya tiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Medical Stores Department (MSD)* wamesema kwamba mahitaji halisi ya vifaa pamoja na madawa ni Shilingi bilioni 198, lakini Bunge hili Tukufu linaambiwa litenge Shilingi bilioni 80.5.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wazi kwamba kiwango kinachopendekezwa hakitatosheleza mahitaji ya afya ya nchi yetu. Lakini siyo hilo tu. Katika hizo Shilingi bilioni 80.5 ambazo zinapendekezwa kwa Bunge lako Tukufu, zaidi ya Shilingi bilioni 46.5 ni fedha za wafadhili, ni fedha ambazo hatuna uhakika kwamba zitakuja, kiasi kilichobaki, yaani Shilingi bilioni 34 ndiyo fedha za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kuna kelele sana na kumekuwa na kelele sana kwamba Serikali na Taasisi zake zipo dhati zinaposema kwamba zitashughulikia matatizo ya ukosefu wa vifaa na madawa. Kwa ushahidi huo, fedha zinazopendekezwa na Serikali, hizi kelele siyo sahihi. Kama Serikali inatenga Shilingi bilioni 34 ya fedha za ndani wakati mahitaji halisi ni Shilingi bilioni 198 ni wazi kabisa kwamba kiasi ambacho kinatengwa ni kidogo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwamba lugha tunayoizungumza haingani na matendo. *We are not walking the talk*, tunahitaji

kuzungumza kuendane kama tunavyozungumza. Hivyo na sivyo tunavyofanya kwa huu utaratibu wa afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la wafanyakazi wa Sekta wa Afya. Nizungumzie suala la Madaktari na wafanyakazi wengine wa Sekta ya Afya. Tuna matatizo makubwa sana ya Madaktari. Tuna upungufu mkubwa wa Madaktari wa ngazi mbalimbali wa Afya. Sasa wakati tuna upungufu wa Madaktari, wakati tunahitaji Madaktari wengi, sisi ambao tuna upungufu mkubwa kiasi hiki badala ya kuongeza Madaktari tunapunguza Madaktari kwa kuwafukuza baada ya kuwasomesha na kuwaacha waende wakasaidie nchi nyingine za nje kama Botswana na kwingineko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Madaktari wetu tunawahitaji baada ya kutumia fedha nyingi, kuhakikisha kwamba wanabaki katika nchi yetu ili watibu wagonjwa wetu. Ili wabaki katika nchi yetu, inabidi kwanza tuwalipe sawasawa, inabidi kwanza tununue vifaa vinavyotosheleza ili kuwawezesha Madaktari wetu kufanya tiba ya wagonjwa wetu na hivi sivyo tunavyofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie hili la Madaktari kwa jambo moja ndogo tu. Sheria yetu inayohusu maadili ya Madaktari imeundwa na kitu kinaitwa Baraza la Madaktari la *Tanganyika (Medical Council of Tanganyika)* na Sheria hiyo inasema kwamba panapo na suala linalohusu maadili ya Madaktari, ili Daktari achukuliwe hatua za kinidhamu inabidi kwanza ashtakiwe na apewe fursa ya kujitetea. Hao Madaktari

319 waliokuwa *deregistered* hawakupewa hiyo *due process*. Hawakupewa hiyo fursa ya kujitetea! Wameandikiwa tuhuma, wakaambiwa wajitetee, walipoonyesha kwamba wanataka kuweka Wakili kama inavyosema Sheria inayounda Baraza la Madaktari, uamuzi ukatolewa wa kuwafukuza bila hata kujitetea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii siyo namna ya kwenda! Kama tunaamini kwamba wamevunja sheria huwezi ukatibu uvunjifu wa sheria kwa kuvunja sheria. *Two wrongs never make one right.* Makosa mawili hayafanyi sahihi moja kama ambavyo uongo mara mbili hautengenezi ukweli mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, niongee masuala ya afya ya Jimbo langu la Singida Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilizaliwa kwenye Hospitali ya *Mission* ya Makiungu miaka 44 iliyopita. Hospitali ya *Mission* ya Makiungu leo ni Hospitali Teule ya Wilaya. Kwa uamuzi wa Serikali imekuwa *Designated District Hospital*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kabla sijawa Mbunge na mwaka huu ni wa pili tangu nimechaguliwa kuwa Mbunge, kuna malalamiko makubwa ya Madaktari na wafanyakazi wa Makiungu *Mission Hospital* ambayo ni *Designated District Hospital* kwamba yale mafao wanatakiwa wayapate kama tofauti ya malipo wanayolipwa na mwajiri wao, yaani

*mission* na ile *difference* inayotakiwa kulipwa na Serikali wamekuwa hawalipwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili limekuwa tatizo la muda mrefu sana. Naomba Wizara ya Afya kwanza ilizungumzie hili suala, na pili, ichukue hatua za kuondoa haya madeni ya wafanyakazi wa hospitali zetu kwa sababu wote tunafahamu jinsi ambavyo wanafanya kazi katika mazingira magumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, kwa vile muda unakwenda, hospitali zetu na Vituo vya Afya na *Dispensary* za vijijini zina shida kubwa sana ya madawa. Ni rahisi kusema kwamba wazee wakatibiwe bure. Hawawezi wakatibiwa bure kama hospitali hazina madawa!

Mheshimiwa Naibu Spika, ni rahisi kusema kwamba akina mama wajawazito wakatibiwe bure kwenye *Dispensary* zetu. Haiwezekani kama *Dispensary* hizo au Vituo vya Afya havina madawa. Ili hizi kauli ziende sambamba na vitendo, inabidi Wizara itoe kauli juu ya haya matatizo kwenye *Dispensary* zetu na kwenye Vituo vya Afya na vilevile ichukue hatua za kuhakikisha kwamba kweli kunakuwa na madawa, kweli kunakuwa na vitendea kazi katika Vituo vya Afya na katika *Dispensary* zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilisema haitakuwa vizuri, siku zote huwa ninagongewa kengele. Naomba nimalize hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tundu Lissu ahsante, ninakushukuru sana. Kwa muda wetu kama sote tutakavyokuwa mashahidi mtaona hauruhusu kuweza kupata mchangiaji mwingine.

Niseme tu kwamba nimezidi kupata vikaratasi vingi vinavyoshabikia ile mechi, vingi kweli! Lakini vinapendekeza baadhi ya maeneo mabadiliko ya wachezaji na mahali pengine wachezaji wapya. Basi nivipitie vichache.

Kimoja kinasema hapana, mechi iwe kati ya Mheshimiwa Stephen Wasira na Mheshimiwa Freeman Mbowe; Kingine kinasema Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu na Mheshimiwa Rose Kamili; kingine kinasema Mheshimiwa Halima Mdee yeye atatwangana na Mheshimiwa Job Ndugai; kingine kinasema Mheshimiwa Joshua Nassari na Mheshimiwa Livingstone Lusinde na orodha ni ndefu inaendelea. Basi Mheshimiwa Idd Azzan ana kazi kweli kuona kama mchezo huu kweli uruhusiwe au usiruhusiwe. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maelezo hayo, na kwa vile muda wetu haupo upande wetu, naomba sasa niahirishe Shughuli za Bunge hadi kesho Tatu asubuhi.

*(Saa 12.00 jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne,*
*Tarehe 31 Julai, 2012, Saa Tatu Asubuhi)*